**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**
**TUME YA TAIFA YA MIPANGO**

# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/2027






**JANUARI, 2026**

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ADC** | Aquaculture Development Centres |
| **ADEM** | Agency for the Development of Educational Management |
| **AFCON** | Africa Cup of Nations |
| **AFDP** | Agriculture and Fisheries Development Programme |
| **AHSP** | Annual Health Sector Performance Report |
| **AMIS** | Airport Management Information |
| **ASDP II** | Agricultural Sector Development Programme II |
| **ATCL** | Air Tanzania Company Limited |
| **ATE** | Association of Tanzania Employers |
| **AU** | African Union |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili Tanzania |
| **BBT** | Building Better Tomorrow |
| **BEVAC** | Beekeeping Value Chain |
| **CAMARTEC** | Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology |
| **CBE** | College of Business Education |
| **CBR** | Central Bank Rate |
| **CNG** | Compressed Natural Gas |
| **COSTECH** | Commission for Science and Technology |
| **DAWASA** | Dar es Salaam Water and Sewarage Authority |
| **DIT** | Dar es Salaam Institute of Technology |
| **DMDPII** | Dar es Salaam Metropolitan Development Project II |
| **DMGP** | Dar es Salaam Maritime Gateway Program |
| **DMI** | Dar es Salaam Maritime Institute |
| **DRC** | Democratic Republic of the Congo |
| **EAC** | East African Community |
| **EACOP** | East African Crude Oil Pipeline |
| **EASTRIP** | East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project |
| **EIA** | Environmental Impact Assessment |
| **EOCC** | Emergency Operations and Communication Centre |
| **EP4R** | Education Programme for Results |
| **EPZA** | Export Processing Zones Authority |

| | |
|---|---|
| **ETF** | Enhanced Transparency Framework |
| **FCC** | Fair Competition Commission |
| **FCT** | Fair Competition Tribunal |
| **FDCs** | Folk Development Colleges |
| **FOLUR** | Food Systems, Land Use and Restoration |
| **FORLAND** | Forestry, Land Use and Value Chains Development |
| **FYDP IV** | Fourth Five Year Development Plan |
| **FYDP III** | Third Five Year Development Plan |
| **GAVI** | Global Alliance for Vaccines and Immunization |
| **GPE** | Global Partnership for Education |
| **Ha** | Hectare |
| **HBF** | Health Basket Fund |
| **HEET** | Higher Education for Economic Transformation Project |
| **HEP** | Hamlet Electrification Project |
| **ICHF** | Improved Community Health Fund |
| **IJCs** | Intergrated Justice Centers |
| **ILFS** | Integrated Labour Force Survey |
| **IMF** | International Monetary Fund |
| **IWT** | Illegal Wildlife Trade |
| **JNHPP** | Julius Nyerere Hydropower Plant |
| **JNIA** | Julius Nyerere International Airport |
| **JPM** | John Pombe Magufuli |
| **KIA** | Kilimanjaro International Airport |
| **KM** | Kilometer |
| **KPI** | Key Performance Indicator |
| **KWh** | Kilowatt Hour |
| **LGAs** | Local Government Authorities |
| **LNG** | Liquefied Natural Gas |
| **LPG** | Liquefied Petroleum Gas |
| **LVD** | Lake Victoria to Dodoma |
| **MDAs** | Ministries, Departments and Agencies |
| **MICE** | Meetings, Incentives, Conferences and Exhibition |
| **MIT** | Ministry of Industry and Trade |

| | |
|---|---|
| **MoCU** | Moshi Co-operative University |
| **MW** | Megawatt |
| **NACTE** | National Council for Technical Education |
| **NCAA** | Ngorongoro Conservation Area Authority |
| **NCT** | National college of Tourism |
| **NDC** | National Development Corporation |
| **NDC** | National Development Cooperation |
| **NEMC** | National Environment Managament Council |
| **NHC** | National Housing Corporation |
| **NHIF** | National Health Insuarance Fund |
| **NIDA** | National Identification Authority |
| **NIT** | National Institute of Transport |
| **NMT** | National Museum of Tanzania |
| **NPMIS** | National Project Management Information System |
| **NPS** | National Prosecution Service |
| **NRW** | Non-Revenue Water |
| **PAMOJA** | Project for Advancing Gender Equality in Tanzania |
| **PCP** | Programme for Country Partnership |
| **PFMRP** | Public Finance Management Reform Programme |
| **PIM-OM** | Public Investment Management Operational Manual |
| **PPP** | Public-Private Partnership |
| **PPPC** | Public-Private Partnership Centre |
| **PSRP** | Public Service Reform Programme |
| **PSRS** | Public Service Recruitment Secretariat |
| **PSSN** | Productive Social Safetynet |
| **SADC** | Southern African Development Community |
| **SDGs** | Sustainable Development Goals |
| **SDL** | Skills Development Levy |
| **SEZ** | Special Economic Zones |
| **SGR** | Standard Gauge Railway |
| **SIDO** | Small Industries Development Organisation |
| **SMMRP** | Sustainable Management of Mineral Resources Project |
| **SPV** | Special Purpose Vehicle |
| **SRWSSP** | Sustainable Rural Water Supply and Sanitation Programme |

| | |
|---|---|
| **TaESA** | Tanzania Employment Services Agency |
| **TAFICO** | Tanzania Fishing Corporation |
| **TAISP** | Tanzania Agricultural Input Support Project |
| **TAKUKURU** | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| **TANAPA** | Tanzania National Parks |
| **TANIPAC** | Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination |
| **TANROADS** | Tanzania National Road Agency |
| **TANTRADE** | Tanzania Trade Development Authority |
| **TANZIS** | Tanzania Innovation Systems |
| **TASAF** | Tanzania Social Action Fund |
| **TaSUBa** | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo |
| **TATC** | Tanzania Automotive Technology Centre |
| **TAWA** | Tanzania Wildlife Management Authority |
| **TAWIRI** | Tanzania Wildlife Research Institute |
| **TAZAMA** | Tanzania Zambia Mafuta |
| **TAZARA** | Tanzania - Zambia Railway Authority |
| **TBC** | Tanzania Broadcasting Cooperation |
| **TBS** | Tanzania Bureau of Standards |
| **TDHS-MIS** | Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey |
| **TEA** | Tanzania Education Authority |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TEMDO** | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization |
| **TFSRP** | Tanzania Food Systems Resilience Program |
| **TGC** | Tanzania Gemmological Centre |
| **TIC** | Tanzania Investment Centre |
| **TIRDO** | Tanzania Industrial Research and Development Organisation. |
| **TIRP II** | Tanzania Intermodal Railway Project II |
| **TMCHIP** | Tanzania Maternal and Child Health Program |
| **TPSF** | Tanzania Private Sector Foundation |
| **TUCTA** | Trade Union Congress of Tanzania |
| **U&T** | Ufuatiliaji na Tathmini |
| **UDSM** | University of Dar es Salaam |
| **UNFPA** | United Nations Population Fund |

| | |
|---|---|
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund |
| **USD** | United States Dollar |
| **UVIKO – 19** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona – 2019 |
| **VHF** | Very High Frequency |
| **VVU** | Virusi Vya Ukimwi |
| **WMA** | Weight and Measurement Agency |
| **WRRB** | Warehouse Receipt Regulatory Board |
| **WSDP** | Water Sector Development Programme |

# YALIYOMO


**ORODHA YA VIFUPISHO**......i
**YALIYOMO**......vi

**SURA YA KWANZA**......1
**UTANGULIZI**......1
1.1 Usuli......1
1.2 Malengo ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27......1
1.3 Mawanda wa Mpango......2
1.4 Mbinu na Njia Zilizotumika Kuandaa Mapendekezo ya Mpango......2
1.5 Mpangilio wa Kitabu......3

**SURA YA PILI**......4
**HALI YA UCHUMI**......4
2.1 Utangulizi......4
2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda......4
2.2.1 Uchumi wa Dunia......4
2.2.2 Uchumi wa Kikanda......4
2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia......6
2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara......6
2.2.5 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki......7
2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa......8
2.3.1 Uchumi wa Taifa......8
2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini......11
2.3.3 Sekta ya Nje......12
2.3.4 Sekta ya Fedha......14
2.3.5 Deni la Serikali......15
2.3.6 Demografia na Maendeleo ya Watu......16
2.3.6.1 Demografia......16
2.3.6.2 Hali ya Umaskini Nchini......16
2.3.6.3 Maendeleo ya Watu......17
2.4 Mwenendo wa Sekta Binafsi......18
2.4.1 Ukuzaji wa Mitaji......18
2.4.2 Mitaji kutoka Nje......18
2.4.3 Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi......19
2.5 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2026/27......19
2.5.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla......19
2.5.2 Misingi ya Mpango kwa Mwaka 2026/27......20

**SURA YA TATU** .......... 21
**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO** .......... 21
3.1 Utangulizi .......... 21
3.2. Miradi ya Kielelezo .......... 22
3.2.1. Miundombinu ya Usafirishaji .......... 23
3.2.2 Miradi ya Miundombinu ya Nishati .......... 25
3.2.3 Miradi ya Kuongeza Uzalishaji Viwandani .......... 26
3.3 Mapitio ya Utekelezaji Kisekta .......... 30
3.3.1 Sekta ya Ujenzi .......... 30
3.3.2 Sekta ya Uchukuzi .......... 32
3.3.3 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari .......... 33
3.3.4 Sekta ya Nishati .......... 35
3.3.5 Sekta ya Kilimo .......... 37
3.3.6 Sekta ya Mifugo .......... 38
3.3.7 Sekta ya Uvuvi .......... 41
3.3.8 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani .......... 43
3.3.9 Sekta ya Madini .......... 44
3.3.10 Sekta ya Mazingira na Maliasili .......... 45
3.3.11 Sekta ya Utalii .......... 48
3.3.12 Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo .......... 49
3.3.13 Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara .......... 50
3.3.14 Uwekezaji wa Umma na Sekta Binafsi .......... 51
3.3.15 Sekta ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi .......... 52
3.3.16 Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi .......... 53
3.3.17 Sekta ya Afya .......... 57
3.3.18 Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira .......... 57
3.3.19 Sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi .......... 58
3.3.20 Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii .......... 60
3.3.21 Kuendeleza Ujuzi .......... 61
3.3.22 Utawala Bora na Utawala wa Sheria .......... 62

**SURA YA NNE** .......... 65
**VIPAUMBELE KWA MWAKA 2026/27** .......... 65
4.1 Utangulizi .......... 65
4.2 Maeneo ya Kipaumbele ya Mapendekezo ya Mpango .......... 65
4.2.1 Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji wa taasisi na kuimarisha utawala bora .......... 67
4.2.2 Kuimarisha miundombinu ya kidijitali, nishati, na usafirishaji fungamanishi .......... 67
4.2.3 Kuimarisha sekta zinazochochea uzalishaji, uongezaji wa thamani na ukuaji jumuishi. .......... 68

4.2.4 Kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii ... 68
4.3.5 Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ... 69

**SURA YA TANO** ... 70
**MAPENDEKEZO YA UGHARAMIAJI WA MPANGO** ... 70
5.1 Utangulizi ... 70
5.2 Mwelekeo wa Sera ya Fedha na Bajeti kwa 2026/27 ... 70
5.2.1 Mahitaji ya Fedha kwa mwaka 2026/27 ... 70
5.2.2 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2026/27 ... 71
5.3 Mikakati ya Ugharamiaji kwa 2026/27 ... 71

**SURA YA SITA** ... 73
**UFUATILIAJI NA TATHMINI** ... 73
6.1 Utangulizi ... 73
6.2 Misingi na Miongozo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Mwaka 2026/27 ... 73
6.3 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini ... 73
6.4 Mgawanyo wa Majukumu ... 74

**SURA YA SABA** ... 76
**VIHATARISHI VYA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27** 76
7.1 Utangulizi ... 76
7.2 Aina ya Vihatarishi ... 76
7.3 Mikakati ya Kudhibiti Vihatarishi ... 76
7.4 Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi. ... 77

Kiambatisho Na. 1: Mwenendo wa Viashiria vilivyotumika katika Upimaji wa Utekelezaji Wa Mpango kwa kipindi cha Miaka Mitano. ... 78
Kiambatisho Na. 2: Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ... 96

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Kwa miongo miwili na nusu, Tanzania imekuwa ikitekeleza mikakati ya maendeleo iliyoongozwa na Mpango Elekezi wa Muda Mrefu 2025 chini ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Katika kuelekea kufikia ukomo wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango Elekezi, Serikali imeandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) itakayotekelezwa kupitia Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51 (Mpango Elekezi). Mpango Elekezi unatoa tafsiri ya utekelezaji wa malengo, shabaha na matarajio yaliyoainishwa katika Dira 2050. Aidha, Mpango huu unajenga muunganiko madhubuti baina ya Dira 2050 na mipango ya muda wa kati na muda mfupi kwa kutoa mwelekeo wa kimageuzi na kubainisha maeneo ya kipaumbele na afua mahsusi za utekelezaji. Utekelezaji wa Mpango elekezi utakuwa katika vipindi vitano vya miaka mitano. Mipango ya miaka mitano hutekelezwa kupitia mipango ya maendeleo ya Taifa ya mwaka mmoja mmoja. Kwa msingi huo, Serikali imeandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ili kutimiza takwa la kuwa na mpango wa maendeleo wa muda mfupi.

Mapendekezo haya ni ya kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 - 2030/31) unaotekeleza Dira 2050 (FYDP IV) ambao una dhima ya "**Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira**". Mapendekezo ya Mpango yanabainisha maeneo ya kimkakati ambayo yametoholewa kutoka katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maeneo hayo ni pamoja na: Uchumi imara jumuishi na shindani; kuimarisha tija na kuleta mageuzi ya kiuchumi kwenye sekta za kimkakati; uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi; kutumia kikamilifu vichocheo vya maendeleo; kuimarisha misingi endelevu ya taifa; ujumuishaji wa mabadiliko na kuwekeza kwenye maeneo yanayoleta mageuzi.

## 1.2 Malengo ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 yanalenga kubainisha maeneo ya kipaumbele ambayo yanalenga kuhakikisha kuwa utekelezaji wa afua, programu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2026/27 unaendana na mwelekeo wa vipaumbele vya FYDP IV na matumizi bora ya rasilimali ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kwa msingi huo, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka

2026/27 yanatafsiri vipaumbele vya FYDP IV kwa kuviainisha katika hatua za utekelezaji zenye malengo, matokeo na viashiria vinavyopimika ili kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji na ufuatiliaji madhubuti. Utekelezaji wake unajielekeza katika kuhakikisha uendelevu wa utekelezaji wa afua za maendeleo ambazo hazikukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa Dira 2025 pamoja na kujenga msingi wa mageuzi ya kimfumo na kimuundo yanayolenga kuongeza tija, ushindani na ustahimilivu wa uchumi wa Taifa ili kufikia malengo ya Dira 2050.

### 1.3 Mawanda wa Mpango

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 yamejikita katika maeneo ya kipaumbele yafuatayo: Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji wa taasisi na kuimarisha utawala bora; kuimarisha miundombinu ya kidijitali, nishati, na usafirishaji fungamanishi; kuongeza tija na uwezo wa uzalishaji ili kuchochea mageuzi ya viwanda; kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii; na uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Maeneo haya ya kipaumbele yamelenga kuhakikisha Serikali inaweka msingi imara wa kuanza utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa muda wa kati ili kufikia malengo ya Dira 2050 na kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu ifikapo mwaka 2050. Uainishaji wa maeneo mahsusi ya vipaumbele yamezingatia mafanikio na muendelezo wa afua zilizotekelezwa ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano uliotekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, mipango ya kisekta; pamoja na kuzingatia mabadiliko ya mwenendo wa kiuchumi na kijamii.

### 1.4 Mbinu na Njia Zilizotumika Kuandaa Mapendekezo ya Mpango

Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 yamezingatia mbinu na njia shirikishi kwa kuhusisha wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi. Ushirikishwaji wa makundi tajwa ulifanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo vikao vya majadiliano, uandishi na uhariri.

Aidha, Mapendekezo ya Mpango huu yamezingatia Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa pamoja na ajenda za Kimataifa ikijumuisha Dira 2050 Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaotekeleza Dira 2050, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs 2030), Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika (Agenda 2063), na Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050 (Vision 2050). Aidha, Mapendekezo haya yamezingatia matokeo ya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yaliyotokea duniani, mabadiliko ya tabianchi na mageuzi

ya kidijitali yanayoendelea duniani. Lengo likiwa ni kuhakikisha kunakuwa na ulinganifu katika utekelezaji na ufuatiliaji.

Vilevile, maandalizi ya mapendekezo ya mpango huu yaliongozwa na uchambuzi wa kina wa takwimu za kitaifa na kimataifa, mapitio ya utekelezaji wa Mipango iliyopita pamoja na tafiti na taarifa za tathmini za taasisi za Serikali, Taasisi za Elimu na Tafiti na washirika wa maendeleo ili kuhakikisha usahihi, uhalisia na uzingatiwaji wa ushahidi. Pamoja na hayo, maandalizi ya mapendekezo ya mpango yamezingatia matumizi ya mfumo wa upangaji unaozingatia matokeo (results-based planning framework) kwa kuoanisha malengo na matokeo yanayopimika kupitia viashiria (Key Performance Indicators). Vyanzo vikuu vya taarifa na takwimu vinajumuisha Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Taarifa za Utendaji za Taasisi za Umma, na Benki ya Dunia (World Bank), Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), na mashirika ya Umoja wa Mataifa.

Ili kuhakikisha upatikanaji wa maendeleo jumuishi na endelevu, Mapendekezo ya Mpango yamezingatia masuala mtambuka katika maeneo yote ya kipaumbele. Masuala hayo ni pamoja na usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, ajira kwa vijana, mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira, mabadiliko ya kidigitali, sayansi, teknolojia na ubunifu, utawala bora, pamoja na usawa katika upatikanaji wa fursa.

Baada ya kukamilika kwa zoezi la uandishi na uhakiki mapendekezo ya mpango yaliwasilishwa katika vikao vya maamuzi Serikalini kwa ajili ya kuidhinishwa. Vikao hivi vilijumuisha vikao vya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Kikao Kazi cha Makatibu Wakuu, Baraza la Mawaziri na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 1.5 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango kimegawanyika katika sura saba (7): Sura ya Kwanza: utangulizi ambao unajumuisha usuli, malengo ya mapendekezo, mawanda na maandalizi; Sura ya Pili: inaelezea mapitio ya hali ya uchumi; Sura ya Tatu: inatoa uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa Mipango iliyopita katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III); Sura ya Nne: inaelezea vipaumbele kwa mwaka 2026/27; Sura ya Tano: inaelezea mapendekezo ya ugharamiaji wa Mpango; Sura ya Sita: inaainisha ufuatiliaji na tathmini; na Sura ya saba: Vithatarishi vya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/27.

# SURA YA PILI

# HALI YA UCHUMI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa tathmini ya mwenendo wa viashiria vya kiuchumi na kijamii katika ngazi ya dunia, kikanda, na kitaifa kwa mwaka 2024 na 2025, pamoja na matarajio kwa mwaka 2026. Uchambuzi huu ni sehemu muhimu ya mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka uliopita, kwa madhumuni ya kubaini mafanikio na changamoto, na kutumia mafunzo yake katika maandalizi ya Mpango unaofuata.

Uchambuzi wa viashiria hivi una umuhimu mkubwa katika kupanga maendeleo ya Taifa kwa kuwa unawezesha: Kufanya tathmini ya ufanisi wa sera za uchumi na kijamii; Kulinganisha mwenendo wa uchumi wa ndani na mazingira ya dunia na kikanda; Kubaini maeneo yenye changamoto na fursa; na Kutoa mapendekezo mahususi kwa ajili ya kupanga sera, mipango na mikakati. Viashiria vilivyofanyiwa uchambuzi ni pamoja na: Pato la Taifa; mfumuko wa bei; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Serikali; na demografia na maendeleo ya watu.

## 2.2 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

### 2.2.1 Uchumi wa Dunia

Uchumi wa Dunia umeendelea kuimarika licha ya changamoto mbalimbali, ikiwemo migogoro ya kikanda na kutokutabirika kwa sera za biashara. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba 2025, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajia kuendelea kupungua kufikia wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2025 na asilimia 3.1 mwaka 2026. Maoteo hayo yanatokana na matarajio ya utekelezaji wa sera za bajeti zinazolenga kuongeza fedha katika uchumi na kupungua kwa athari zitokanazo na utekelezaji wa sera za bajeti zinazolenga kuongeza ushuru kwa mataifa yaliyoendelea hususan nchi ya Marekanii.


### 2.2.2 Uchumi wa Kikanda

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2023. Kuongezeka kwa ukuaji kulichangiwa na kupungua kwa athari za majanga yanayokabili uchumi wa dunia, kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kufuatia ongezeko la uwekezaji katika sekta ya umma, kuimarika kwa mauzo ya bidhaa nje na utekelezaji mzuri wa sera za kupunguza mfumuko wa bei. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kubaki thabiti kwa asilimia 4.1 mwaka 2025 na

kuongezeka hadi kufikia asilimia 4.4 mwaka 2026, kutokana na juhudi za kuimarisha uchumi na mageuzi ya sera katika nchi za eneo hili.


Uchumi wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika - SADC ulikua kwa wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.4 na asilimia 3.7 mwaka 2025 na 2026, mtawalia. Katika ukanda wa uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ukuaji wa Pato la Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2023. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa ukanda wa EAC ilichangiwa na kuporomoka kwa uchumi wa nchi ya Sudani Kusini ambao ulikuwa na ukuaji hasi wa asilimia 26.1 mwaka 2024. Uchumi wa nchi za EAC unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2025 na mwaka 2026.

**Kielelezo Na. 2.1: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) Mwaka 2023 - 2024 na Matarajio mwaka 2025**




***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Oktoba 2025*

**Kielelezo Na. 2.2: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), 2023 – 2024 na matarajio 2025**




***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Oktoba 2025*

### 2.2.3 Mfumuko wa Bei wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF toleo la Oktoba 2025, mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi kutokana na utekelezaji wa sera za fedha zilizolenga kuwa na utulivu wa mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei wa dunia unatarajiwa kupungua kutoka wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2024 hadi asilimia 4.2 mwaka 2025 na asilimia 3.7 mwaka 2026.

Kwa upande wa makundi ya nchi, mfumuko wa bei kwa nchi zenye kipato cha chini uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2024, sawa na wastani wa mwaka 2023; kwa nchi zinazoibukia na zinazoendelea kiuchumi ulipungua hadi asilimia 7.8 mwaka 2024 kutoka asilimia 8.1 mwaka 2023; na kwa nchi zilizoendelea ulipungua zaidi, kufikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2023.

### 2.2.4 Mfumuko wa Bei wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Oktoba 2025, nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2024, ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2023. Kupungua kwa mfumuko wa bei katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kulisababishwa na kushuka kwa bei za kimataifa za chakula na mafuta baada ya mishtuko ya awali ya vita ya Ukraine

na COVID-19, utekelezaji wa sera thabiti za kifedha na bajeti na benki kuu kuongeza viwango vya riba ili kudhibiti mahitaji, utulivu wa sarafu katika baadhi ya nchi uliozuia

gharama za uagizaji, pamoja na kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa chakula na nishati.

Aidha, Mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) umefikia wastani wa asilimia 10.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 16.2 mwaka 2023 (Jedwali Na. 2.1).

**Jedwali Na. 2.1 :** Mwenendo wa Mfumuko wa Bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

| Nchi/ Miaka | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|
| Angola | 14.7 | 12.1 | 11.2 | 10.5 |
| Botswana | 12.0 | 7.9 | 4.6 | 3.8 |
| Comoros | 21.9 | 20.2 | 3.5 | 6.0 |
| Congo | 19.9 | 18.0 | 16.1 | 8.5 |
| Eswatini | 5.6 | 4.8 | 4.3 | 4.1 |
| Lesotho | 8.1 | 6.8 | 5.5 | 5.0 |
| Madagascar | 9.8 | 10.5 | 8.7 | 8.2 |
| Malawi | 25.9 | 28.0 | 23.5 | 20.1 |
| Mauritius | 10.8 | 7.0 | 4.8 | 4.2 |
| Mozambique | 10.3 | 9.8 | 6.5 | 6.0 |
| Namibia | 6.1 | 5.3 | 4.9 | 4.5 |
| Seychelles | 2.9 | 3.4 | 2.5 | 2.3 |
| South Africa | 6.9 | 6.0 | 5.3 | 5.0 |
| Tanzania | 4.3 | 3.8 | 3.1 | 3.9 |
| Zambia | 11.0 | 9.8 | 8.2 | 7.5 |
| Zimbabwe | 190.0 | 105.0 | 55.0 | 32.7 |
| Wastani kwa Ujumla | **22.5** | **16.2** | **10.5** | **8.3** |


**Chanzo:** Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi husika na Taarifa ya IMF ya Oktoba, 2025

### 2.2.5 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki

Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), mfumuko wa bei umeendelea kutofautiana kati ya wanachama, ambapo Sudan Kusini na Burundi walirekodi viwango vya juu zaidi vya wastani wa asilimia 16.1 na 16.0 mwaka 2024,

ikilinganishwa na asilimia 18.0 na 23.8 mwaka 2023 mtawalia. Nchi nyingine kama Kenya ikifikia asilimia 5.8, Uganda asilimia 7.2 na Rwanda asilimia 5.0 mwaka 2024. Tanzania imeendelea kudumisha utulivu wa bei, ambapo mwaka 2024 mfumuko wa bei umefikia wastani wa asilimia 3.1. Hii imetokana na utekelezaji wa sera thabiti za fedha, utulivu wa soko la chakula na kupungua kwa bei za bidhaa za kimataifa. Hali hii inaonyesha tofauti kubwa za kiuchumi ndani ya ukanda wa EAC, ambapo baadhi ya nchi zinakabiliwa na shinikizo kubwa la bei huku nyingine zikidumisha uthabiti wa kiuchumi.

**Kielelezo Na. 2.3: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2022 - 2024 na Matarajio mwaka 2025**




***Chanzo:*** *Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi husika na IMF*


## 2.3 Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

### 2.3.1 Uchumi wa Taifa

Kwa mujibu wa takwimu zilizokokotolewa kwa kuzingatia mwaka wa kizio wa 2019, Pato halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 5.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na: uwekezaji wa Serikali kwenye miradi ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji; kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere; kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi; usimamizi madhubuti wa sera za fedha; kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuimarika kwa huduma za fedha na bima; pamoja na uwekezaji wa Serikali katika huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, maji na hifadhi ya jamii.


Shughuli za kilimo zimeendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa kwa kuchangia asilimia 24.9, ikifuatiwa na shughuli za ujenzi (asilimia 12.5), madini (10.1), biashara na matengenezo (asilimia 8.6) na usafiri na usafirishaji (asilimia 8.1). Aidha, sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa Pato la Taifa ni sekta ya kilimo iliyochangia asilimia 20.8 ikifuatiwa na usafiri na usafirishaji (asilimia 10.4), fedha na bima (asilimia 9.3) na madini (asilimia 8.3) kama inavyooneka katika **Kielelezo Na. 2.4 na 2.5**

**Kielelezo Na. 2.4:** Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa




***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*


**Kielelezo Na. 2.5:** Mchango wa Sekta katika Ukuaji



***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Katika nusu ya kwanza (Januari - Juni) ya mwaka 2025, ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka wa kizio wa 2015 ulifikia wastani wa asilimia 5.8 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulitokana na: uwekezaji wa Serikali katika miradi ya kimkakati ya miundombinu ya nishati, maji, na usafirishaji; kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji hususan kilimo, viwanda na uchimbaji wa madini na mawe; pamoja na kuendelea kuimarika kwa sekta ya fedha na shughuli za usafirishaji nchini. Aidha, sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji ni sekta ya madini iliyochangia asilimia 15.4 ikifuatiwa na kilimo (asilimia 15.3), ujenzi (asilimia 11.7) na fedha na bima (asilimia 10.7) kama inavyooneka katika **Kielelezo Na.2.6**.


**Kielelezo Na. 2.6:** Mchango wa Sekta katika Ukuaji (Asilimia) katika kipindi cha nusu ya kwanza (Januari - Juni) ya mwaka 2025




**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Kwa kuzingatia mwenendo wa viashiria mbalimbali ikiwemo ukuaji halisi wa Pato la Taifa katika nusu ya kwanza na athari za matukio ya wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia 6.3 mwaka 2026. Aidha, katika kipindi cha muda wa kati (2025 – 2029) uchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.9. Ukuaji huu utategemea utekelezaji endelevu wa miradi mikubwa ya kimkakati inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji, jitihada za Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji, utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili – ASDP II na Mpango Kabambe wa Sekta ya Kilimo 2050, utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha pamoja na uwekezaji wa Serikali katika sekta ya huduma za kijamii. Mwelekeo wa uchumi katika kipindi cha muda wa kati ni kama unavyoonekana katika **Kielelezo Na. 2.7**

**Kielelezo Na. 2.7 : Mwelekeo wa Uchumi wa Tanzania**





Mwaka 2025 – 2030 ni maoteo

### 2.3.2 Mfumuko wa Bei Nchini

Mwaka 2024/25, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.1 kama ilivyokuwa katika mwaka 2023/24. Aidha, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.1 Juni 2025 ikilinganishwa na asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (**Kielelezo Na. 1.5**). Mwenendo wa mfumuko wa bei ulichangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti na kupungua kwa bei za mafuta katika soko la dunia. Kiwango hicho cha mfumuko wa bei kipo ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0, vigezo vya mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (usiozidi asilimia 8.0) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (wigo wa asilimia 3.0 hadi 7.0).

**Kielelezo 2.8: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini kwa mwaka 2024/25.**




**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

### 2.3.3 Sekta ya Nje

Mwaka 2024/25, sekta ya nje imeendelea kuimarika licha ya changamoto zilizotokana na migogoro ya kisiasa na mivutano ya kibiashara duniani. Urari wa malipo ya kawaida (current account) uliendelea kuimarika na kufikia nakisi ya dola za Marekani milioni 2,178.3 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,767.4 mwaka 2023/24. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ikilinganishwa na uagizaji wa bidhaa na huduma. Aidha, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma ilikuwa dola za Marekani milioni 16,923.8 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 14,410.5, sawa na ongezeko la asilimia 17.4. Kwa upande mwingine, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma ilikuwa dola za Marekani milioni 17,763.0 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 16,144.9 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 10.0.

Mwaka 2025/26 na katika kipindi cha muda wa kati, urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kupungua kutoka asilimia 2.5 ya pato la Taifa mwaka 2024/25 hadi wastani wa asilimia 2.0 katika kipindi cha muda wa kati. Hii ni kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa na huduma. Ongezeko la mauzo ya bidhaa na huduma ni kutokana na matarajio ya kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii, uuzaji wa bidhaa za asili na zisizo asilia ikiwemo dhahabu na bidhaa za maua na mbogamboga. Aidha, uagizaji wa bidhaa na huduma unatarajiwa kupungua kutokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi inayotekelezwa na Serikali

**a) Urari wa Biashara ya Bidhaa**

Thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 9,805.2 kwa mwaka 2024/25, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 7,831.8 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 25.2. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia, hususan korosho na kahawa, pamoja na mauzo ya nafaka, vyuma na bidhaa za mbogamboga. Aidha, thamani ya bidhaa asilia zilizouzwa nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 1,461.7 mwaka 2024/25 kutoka dola za Marekani milioni 1,066.3 mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 37.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya korosho na kahawa.

Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia ilikua kwa asilimia 24.6 na kufikia dola za Marekani milioni 7,937.7. Ongezeko hilo lilichangiwa na mauzo ya dhahabu kufuatia kupanda kwa bei katika soko la dunia. Kwa upande mwingine, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 14,706.2 mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 6.7 kutokana na kuongezeka kwa uagizaji wa vyombo vya usafirishaji, pamoja na malighafi za viwandani.

**b) Urari wa Biashara ya Huduma**

Katika mwaka ulioishia Septemba 2025, thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 17,728.7, ikilinganishwa na dola milioni 16,759.4 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Ongezeko kubwa lilionekana hasa katika uagizaji wa vifaa vya viwandani, vifaa vya usafirishaji wa viwandani, sehemu na vipuri, pamoja na mitambo na mashine za kimekanika. Hata hivyo, uagizaji wa mafuta, ambao unachangia asilimia 16.8 ya jumla ya uagizaji wa bidhaa, ulipungua kwa kiasi kikubwa hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,469.6, hasa kutokana na athari ya kushuka kwa bei.

**c) Akiba ya Fedha za Kigeni**

Akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,971.5, Juni 2025, kiasi cha kutosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.8. Kiwango hicho kipo juu ya lengo la nchi la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa angalau miezi minne (4) na kigezo cha mtangamano kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki cha angalau miezi 4.5. Kiwango hiki cha fedha za kigeni kimetokana na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na kuongezeka kwa bei ya dhahabu, mauzo ya mazao ya biashara ikiwemo korosho na kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini. Aidha, akiba ya fedha za kigeni inatarajiwa kuendelea kuimarika kutokana na matarajio ya kuendelea kukua kwa mapato ya fedha za kigeni na utekelezaji wa programu ya Benki Kuu ya ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani.

### 2.3.4 Sekta ya Fedha

Utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa wa kuridhisha, hivyo kuwezesha utekelezaji mzuri wa malengo ya uchumi kwa mwaka 2024/25. Aidha, Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate - CBR) ilibaki kuwa asilimia 6 katika robo zote nne za mwaka 2024/25 ili kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3.0 – 5.0 na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi.

**a) Viwango vya Riba**

Hadi Juni 2025, wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya benki iliongezeka na kufikia asilimia 7.93 ikilinganishwa na asilimia 7.98 kwa Juni 2024. Aidha, wastani wa riba za jumla za dhamana za Serikali za muda mfupi ziliongezeka hadi wastani wa asilimia 10.72 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na asilimia 9.14 mwaka 2023/24. Hali hii ilitokana na kupungua kwa ukwasi katika masoko ya fedha ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei, kama ilivyokuwa katika Benki Kuu za nchi nyingine katika kutekeleza sera ya fedha.

Riba za mikopo kwa ujumla zilipungua hadi wastani wa asilimia 15.42 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 15.47 mwaka 2023/24. Riba za amana ziliongezeka hadi kufikia asilimia 8.22 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na asilimia 7.32 mwaka 2023/24. Ongezeko hili lilitokana na kupungua kwa ukwasi katika benki.

**b) Mikopo kwa Sekta Binafsi**

Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 15.9 katika mwaka 2024/25, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 17.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Mikopo iliyotolewa kwa shughuli za kilimo ilikuwa na ukuaji wa juu zaidi wa asilimia 30.2, ikifuatiwa na sekta za ujenzi na ujenzi wa majengo pamoja na usafirishaji na mawasiliano, kila moja ikiwa na kiwango cha ukuaji cha asilimia 25.7.

Ukuaji wa mikopo ya kilimo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na mikopo inayotolewa kwa benki kupitia mkopo maalumu wa shilingi trilioni 1, na unafuu unaotolewa kwa kiwango cha amana zinazotakiwa kuwekwa kisheria Benki Kuu kwa benki zinazotoa mikopo kwa sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10. Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na kuimarisha huduma za ugani na tafiti. Hatua hizi zimeendelea kuhamasisha benki kuongeza mikopo kwa sekta hiyo na kuchochea ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya.

**c) Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki**

Sekta ya benki ilibaki kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha katika kipindi chote cha mwaka 2024/25. Uwiano wa mtaji wa msingi kwa jumla ya rasilimali ulifikia asilimia 18.8 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na asilimia 18.6 mwaka 2023/24 na asilimia 10.0

ambayo ni kiwango cha chini kinachokubalika kisheria. Aidha, rasilimali zimeendelea kuongezeka ambapo hadi Juni 2025, uwiano wa mali zinazobadilishwa kirahisi kuwa fedha na amana za wateja wa benki ulikuwa asilimia 27.7, kiwango ambacho ni zaidi ya ukomo wa chini wa kisheria wa asilimia 20. Vilevile, amana, rasilimali na mikopo iliendelea kuongezeka kutokana na matumizi ya huduma za uwakala wa benki na kuongezeka kwa utoaji wa huduma za fedha kwa njia ya kidijitali. Ongezeko la ukwasi lilikuwa sambamba na ukuaji wa mikopo iliyotokana na mazingira bora ya biashara na uwekezaji. **Jedwali Na. 2.2** linaonesha mwenendo wa amana, rasilimali na mikopo.

**Jedwali Na. 2.2: Mwenendo wa Amana, Rasilimali na Mikopo**
(Shilingi bilioni)

| **Aina ya Kiashiria** | **2023/24** | **2024/25** |
|---|---|---|
| Amana | 40,760.7 | 48,610.2 |
| Rasilimali | 59,045.1 | 69,077.0 |
| Mikopo (loans advances and overdraft) | 35,059.1 | 40,961 |

***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania*

### 2.3.5 Deni la Serikali

Hadi Septemba 2025, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 108.17 ikilinganishwa na shilingi trilioni 102.78 Septemba 2024, sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa shilingi trilioni 70.71 na deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 37.46. Hii ilitokana na kuendelea kutolewa kwa mikopo iliyosainiwa zamani pamoja na uwepo wa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kwa mujibu wa taarifa ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Julai 2025 kati ya IMF na Benki ya Dunia imebainisha kuwa deni la Serikali ni himilivu, ambapo viashiria vyote vikiwa ndani ya viwango vinavyokubalika kimataifa kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu. Aidha, tathmini hiyo inaonesha kuwa katika mwaka ulioishia Juni 2024, uwiano wa deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 40.5 ambao ni chini ya ukomo wa asilimia 55 wa Pato la Taifa na chini ya ukomo wa asilimia 50 unaotumika kama kigezo cha muunganiko wa viashiria vya uchumi jumla kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mwaka 2024/25, Tanzania ilifanyiwa tathmini ya kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa na kampuni za Moody's Investors Service na Fitch Ratings, ambapo matokeo yanaonesha nchi kuendelea kuwa na mwelekeo imara kwa kutunukiwa daraja B1 na B+ mtawalia. Matokeo mazuri ya tathmini hizo yanaakisi uhimilivu wa deni la serikali kutokana na ukuaji mzuri wa uchumi unaoweza kuhimili majanga ya kimataifa, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha

mazingira ya biashara, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma.

### 2.3.6 Demografia na Maendeleo ya Watu

#### 2.3.6.1 Demografia

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) idadi ya watu inakadiriwa kufikia milioni 66.1 mwaka 2025 na milioni 67.9 mwaka 2026 kwa Tanzania Bara. Kasi ya ongezeko la idadi ya watu inatoa fursa chanya zikiwemo uwepo wa nguvu kazi ya kutosha pamoja na misingi ya kuchochea mageuzi ya kidigitali katika shughuli mbalimbali za uzalishaji kutokana na uwepo wa kundi kubwa la vijana wenye umri wa miaka 15-35. Aidha, ongezeko hili linaashiria uhitaji wa kuwekeza zaidi katika huduma za kijamii pamoja na mageuzi katika mifumo mbalimbali ya elimu na utendaji pamoja na kutekeleza mikakati mahsusi ya kuwawezesha vijana kuzalisha kwa tija. Utekelezaji wa mikakati hii utawezesha rasilimali watu ya nchi kuwa shindani kimataifa hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kwa upande mwingine, kiwango cha utegemezi kimeendelea kuwa 0.87 mwaka 2025 na kinatarajiwa kupungua hadi 0.86 mwaka 2026. Hali hii inaakisi mzigo mkubwa kwa nguvu ngazi inayozalisha. Aidha, kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya watu na maendeleo ya kiuchumi, kuna haja ya kuetekeleza mikakati itakayochachua maendeleo ya kiuchumi kuwa jumuishi kwa kuhakikisha wadau wote muhimu wanashiriki katika kuleta maendeleo hususan katika sekta za huduma za kijamii na miundombinu ya kiuchumi. Hivyo kuashiria uhitaji wa mikakati ya makusudi ya kuwekeza katika sekta za elimu, mafunzo ya ujuzi, lishe bora, afya, maji, miundombinu ya barabara, nishati, mawasiliano na teknolojia, na uunganishaji wa maeneo ya mIjini na vijijini, sekta hizi zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi.

#### 2.3.6.2 Hali ya Umaskini Nchini

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuboresha ustawi wa jamii na kupunguza umaskini uliokithiri kwa kupeleka huduma za msingi karibu na wananchi hususan huduma za maji, elimu, afya pamoja na kutekeleza miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya nishati na barabara, na uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kumpunguzia mwananchi gharama za maisha na kupunguza umaskini. Hatua hizi zinatarajiwa kuchangia katika kufikia shabaha zilizoanishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ya kupunguza umaskini kufikia kiwango cha chini ya asilimia 15 mwaka 2030/31.

Aidha, kutokana na utafiti wa mapato na matumizi ya Kaya Binafsi wa 2017/18, taarifa ya hali ya umaskini nchini inaonesha kuwa, umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18 na kiwango cha umaskini wa chakula kimepungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011/12 hadi asilimia 8.0 mwaka 2017/18.

Vilevile, kulingana na utafiti wa *National Panel Survey* ya mwaka 2022 unaonyesha takribani asilimia 48.9 walitoka katika umaskini na asilimia 20.7 waliingia katika umaskini. Hii inamaanisha kuwa kati ya kila watanzania wanne waliotoka katika umaskini wawili ambao hawakuwa maskini waliingia katika hali ya umaskini. Aidha, kiwango cha utofauti wa matumizi (consumption inequality) kimeongezeka kutoka 0.416 mwaka 2015 kufikia 0.444 mwaka 2021. Hali hii inaonyesha uhitaji wa kuwa na mikakati ya makusudi ya kuhakikisha umaskini unapungua pamoja na kuhakikisha wale walio nje ya umaskini kutoaingia katika umaskini.

#### 2.3.6.3 Maendeleo ya Watu

Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha maendeleo ya watu kwa lengo la kuimarisha maisha ya watu ili kufikia matamanio yaliyoainishwa katika Dira 2050. Juhudi hizo ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu bila ada; kuendelea kuboresha upatikanaji wa maji mijini na vijijini; kuendelea kuboresha ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya hususan maeneo ya vijijini; kuendelea na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali; na kuendelea na ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo ya mijini na vijijini. Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo, kumekua na matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo:

i. Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 68.0 mwaka 2024 hadi miaka 68.3 mwaka 2025. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa kuzingatia jinsia, umefikia miaka 70.7 kwa wanawake na miaka 65.9 kwa wanaume mwaka 2025; Hii ni kwa mujibu wa makadirio yaliyotakana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022;
ii. Kuimarika kwa mwenendo wa vifo vya watoto wa umri chini ya miaka mitano na kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022 kutoka vifo 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20;
iii. Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20 hadi vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022;
iv. Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari kutoka asilimia 47.4 mwaka 2021 hadi asilimia 53.1 mwaka 2025;
v. Kuongezeka kwa idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba kama chanzo kikuu kutoka asilimia 72.3 mwaka 2020/21 hadi asilimia 83 mwaka 2024/25;
vi. Kuunganishwa na huduma ya umeme kwa vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara mwaka 2025/26;
vii. Fahirisi ya maendeleo ya watu imefikia 0.556 mwaka 2024 kutoka 0.529 mwaka 2019, fahirisi hii inaashiria kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za jamii za muhimu kama vile afya, elimu na maji pamoja na kuimarika kwa kiwango cha maisha. Hii ni kwa mujibu wa taarifa za UNDP

## 2.4 Mwenendo wa Sekta Binafsi

Malengo ya Tanzania ni kufikia hadhi ya nchi yenye kipato cha kati ngazi ya juu ifikapo mwisho wa utekelezaji wa Dira ya Taifa Maendeleo 2050, kupitia ukuaji endelevu wa uchumi unaochochewa na mageuzi ya kisera yanayotoa kipaumbele kwa ushiriki wa sekta binafsi. Tanzania imejipanga vyema kutumia utulivu wa kisiasa na uwepo wa maliasili ili kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi. Ushiriki wa sekta binafsi umeleta manufaa makubwa, ikiwa ni pamoja na kuongeza fursa za ajira, kuchochea shughuli za kibiashara, na kuboresha urari wa malipo. Manufaa haya yanachangia kufanikisha lengo la kujenga uchumi shindani na wa viwanda, kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

### 2.4.1 Ukuzaji wa Mitaji

Mwaka 2024, ukuzaji wa rasilimali  kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 76,301.64  kutoka shilingi milioni 69,226.05 mwaka 2023. Ongezeko hili lilichangiwa na ujenzi wa majengo, barabara, madaraja, na miradi mingine ya miundombinu. Katika kipindi hicho, uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika ulikuwa asilimia 37.1 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Mwaka 2024, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 77,126.78 kutoka shilingi bilioni 71,482.46 zilizokuwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.9.

Mwaka 2024, ukuzaji wa rasilimali  kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 76,301.64  kutoka shilingi milioni 69,226.05 mwaka 2023. Ongezeko hili lilichangiwa na ujenzi wa majengo, barabara, madaraja, na miradi mingine ya miundombinu. Katika kipindi hicho, uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika ulikuwa asilimia 37.1 kama ilivyokuwa mwaka 2023. Mwaka 2024, ukuzaji rasilimali za kudumu kwa bei za mwaka husika ulifikia shilingi bilioni 77,126.78 kutoka shilingi bilioni 71,482.46 zilizokuwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.9.

### 2.4.2 Mitaji kutoka Nje

Kwa mujibu wa Taarifa ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2024, uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje uliongezeka kwa asilimia 3.9 na kufikia dola za Marekani milioni 23,042.5 mwaka 2023. Kati ya uwekezaji huo, uwekezaji wa moja kwa moja ulikuwa dola za Marekani milioni 19,139.6, sawa na asilimia 83.1 ya uwekezaji wa sekta binafsi kutoka nje, uwekezaji wa hisa ulifikia dola za Marekani 204.3 (asilimia 0.9) na uwekezaji mwingine ulifikia dola za Marekani 3,698.6 (asilimia 16.1). Aidha, mitaji iliyowekezwa na sekta binafsi kutoka nje ya nchi kwa bei za miaka husika ilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 1,694.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,745.8 zilizowekezwa mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 2.9.

Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ulikuwa na thamani ya dola

za Marekani milioni 1,648.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,437.6 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 14.7. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato na muunganiko na ununuzi wa kampuni za kimataifa pamoja na kuimarika kwa ugharamiaji wa miradi ya kimataifa. Aidha, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliongezeka ambapo nchi za OECD zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wa asilimia 42.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 42.7 mwaka 2022. Vile vile, mchango wa uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje wa nchi za EAC na SADC ulikuwa asilimia 30.0 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 18.0 mwaka 2022. Nchi za Mauritius na Afrika Kusini zilichangia zaidi katika uwekezaji kutoka nchi za SADC na Kenya ilichangia zaidi katika uwekezaji kutoka nchi za EAC.

#### 2.4.3 Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Shughuli za Kiuchumi

Mwaka 2023, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje uliendelea kujikita zaidi katika shughuli za uchimbaji madini na mawe, fedha na bima pamoja na uzalishaji viwandani. Shughuli hizo zilichangia wastani wa asilimia 70.4 ya uwekezaji wote wa moja kwa moja kutoka nje. Aidha, shughuli za uchimbaji madini na mawe zilikuwa na uwekezaji mkubwa zaidi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 532.5, sawa na asilimia 32.3 ya uwekezaji wote, ikifuatiwa na uzalishaji viwandani wenye thamani ya dola za Marekani milioni 361 (asilimia 21.9) na shughuli za fedha na bima zenye thamani ya dola za Marekani milioni 267.6 (asilimia 16.2) mwaka 2023.

### 2.5 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2026/27

Tanzania inatarajiwa kuendelea kukua kiuchumi kwa kasi ya wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2026. Ukuaji huu unategemea uwekezaji mkubwa wa Serikali katika sekta za mageuzi na vichocheo vya kufikia malengo ya Dira 2050.

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27 yamejielekeza katika maeneo manne (4) mahsusi: (i) Kujenga Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani kwa Kufanya Mageuzi ya Mifumo ya Utendaji wa Taasisi na Kuimarisha Utawala Bora; (ii) kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii ili kuwa na watu wenye ujuzi, afya na wanaoweza kuhimili mabadiliko; (iii) kuimarisha miundombinu ya Kidijitali, Nishati, na Usafirishaji Fungamanishi; na (iv) kuimarisha Sekta zinazochochea uzalishaji, uongezaji thamani na ukuaji jumuishi.

#### 2.5.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla

Malengo na shabaha za msingi za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026 ikilinganishwa na matarajio ya ukuaji wa asilimia 5.9 kwa mwaka 2025;
ii. Kuimarisha mfumuko wa bei katika wigo wa asilimia 3.0 – 5.0 katika kipindi cha muda wa kati, ili kulinda uwezo wa wananchi kumudu mahitaji muhimu;
iii. Kuongeza mapato ya ndani kufikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27, kutoka matarajio ya asilimia 16.8 mwaka 2025/26;

iv. Kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya Pato la Taifa mwaka 2026/27, kutoka matarajio ya asilimia 13.3 mwaka 2025/26;
v. Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa mwaka 2026;
vi. Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na
vii. Kuongeza uzalishaji wa ajira kufikia 1,700,000 mwaka 2026 kutoka ajira 981,000 zilizozalishwa mwaka 2024

### 2.5.2 Misingi ya Mpango kwa Mwaka 2026/27

Ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2026/27 utajengwa katika misingi ifuatayo:

i. Kuendelea kuwepo kwa demokrasia, amani, usalama na utulivu wa ndani na katika nchi jirani, inayowezesha shughuli za kiuchumi na uwekezaji kustawi;
ii. Kudumisha misingi ya utawala bora na utawala wa sheria, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;
iii. Kuendelezwa kwa miundombinu ya nishati, bandari, barabara na reli kwa mujibu wa dira ya kuwa kitovu cha biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati;
iv. Kuendelezwa kwa miundombinu ya nishati, bandari, barabara na reli kwa mujibu wa dira ya kuwa kitovu cha biashara, viwanda na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati;
v. Kuimarika kwa ubunifu na matumizi ya teknolojia za kidijitali katika huduma za kijamii na uzalishaji;
vi. Utekelezaji wa mageuzi ya kitaasisi na kiutawala chini ya falsafa ya 4Rs, unaolenga kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji;
vii. Kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji kupitia mashirikiano ya sekta binafsi (PPP) na ushirikiano wa kikanda (EAC na SADC);
viii. Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, mafuriko, vita, milipuko ya magonjwa na misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa kupitia mikakati ya kukabiliana na kupunguza athari zake; na
ix. Kuweka misingi imara ya utekelezaji thabiti wa mipango iliyopangwa.

.

# SURA YA TATU

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea hatua za utekelezaji wa viashiria vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao utekelezaji wake utahitimishwa June 2025/26. Uchambuzi wa viashiria unaonesha kuwa utekelezaji umepiga hatua katika sekta mbalimbali, ingawa kasi ya mafanikio inatofautiana kati ya sekta na viashiria. Kwa ujumla, sekta za miundombinu, uchukuzi, nishati, maji, utalii, viwanda, kilimo, mifugo na madini zimeonesha mwelekeo chanya unaoendana na uwekezaji mkubwa wa serikali katika miundombinu ya uzalishaji wa umeme, usafirishaji na programu za kuimarisha uzalishaji. Mfano, uzalishaji wa umeme umeongezeka kutoka 1,602 MW hadi zaidi ya MW 4031.7 na uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini umeendelea kuongezeka, ikionyesha uendelezaji wa TEHAMA. Vilevile, idadi ya miradi ya uwekezaji imeongezeka kwa kiasi kikubwa, sambamba na kuimarika kwa mazingira ya biashara kupitia maboresho ya sheria na tozo.

Katika sekta za kijamii kama elimu, afya, maji, utawala bora na maendeleo ya jamii, kuna mafanikio makubwa katika upatikanaji wa huduma (mfano, ongezeko la huduma za afya ya uzazi, uandikishaji wa wanafunzi, na kupungua kwa vifo vya watoto). Hata hivyo, baadhi ya viashiria vya ubora kama vile uwiano wa wanafunzi kwa walimu, upatikanaji wa vitabu, na miundombinu ya vyoo vinaendelea kuhitaji jitiada za Serikali ili utekelezaji wake uweze kuimarika. Sekta ya maji imepiga hatua kubwa katika maeneo ya vijijini na miji midogo, ingawa upotevu wa maji bado ni changamoto katika baadhi ya maeneo.

Kwa upande mwingine, baadhi ya sekta zimeonesha mwenendo usioridhisha au usiotabirika, kama vile uvuvi ambayo ina ukuaji mdogo. Baadhi ya viashiria vya kama vile vya elimu ya juu kilimo cha mbegu, na baadhi ya viashiria vya ajira na mafunzo ya uanagenzi na utarajali vinaonesha kupungua. Vilevile, kuna viashiria vilivyo na mabadiliko yasiyo ya kawaida (outliers), hasa katika maeneo ya utamaduni, sanaa na ubunifu ambayo yanaweza kuwa yanasababishwa na mabadiliko ya mifumo ya ukusanyaji, kanuni, au ufafanuzi wa kiashiria.

Kwa ujumla, asilimia kubwa ya viashiria inaonyesha ongezeko, jambo linalodhihirisha kuwa utekelezaji wa Mpango umeleta matokeo chanya katika maeneo mengi ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, mwendelezo wa mageuzi, uwekezaji katika rasilimali watu, ubunifu na maboresho ya mifumo ya usimamizi ni muhimu ili kuongeza uthabiti na ubora wa huduma, pamoja na kufikia shabaha za

2025/26 kikamilifu. Mwenendo wa viashiria na shabaha umeainishwa kwa kina katika **kiambatisho I**.

### 3.2. Miradi ya Kielelezo

Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) 2021/22–2025/26 umezingatia miongozo na taratibu za mipango ya maendeleo ambapo serikali ilisisitiza ushirikishwaji wa wadau muhimu kutoka sekta za umma na binafsi. Utekelezaji huo uliongozwa na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka, ambapo msukumo zaidi uliwekwa katika kukamilisha na kutekeleza miradi ya kielelezo ili kuendana na vipaumbele vya kisekta na malengo ya taifa kwa ujumla. Mchakato wa maandalizi ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka uliendana na mchakato wa bajeti za serikali ili kuhakikisha vipaumbele vinaendana na sera na malengo ya mwaka husika.

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) ulijumuisha miradi 17 ya kielelezo, ambapo hadi Oktoba, 2025 miradi mitatu (3) ipo katika hatua za kukamilika kwa utekelezaji, ambayo ni Ujenzi wa Kiwanda cha sukari - Mkulazi, Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP). Miradi mitano (5) utekelezaji wake unaendelea vizuri, ambayo ni ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR), Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), ujenzi wa madaraja makubwa na barabara za juu, ununuzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu na ujenzi wa bandari ya uvuvi, pamoja na uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi kwa ajili ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZs) na Uwekezaji wa Kiuchumi (SEZs). Hata hivyo, miradi nane (8) ya kielelezo iliyopangwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) ipo katika hatua mbalimbali za awali za maandalizi ya utekelezaji. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na minne (4) inahusu uzalishaji wa umeme wa maji, mafuta na gesi asilia (kama vile miradi ya Ruhudji, Rumakali, Eyasi Wembere na Mnazi Bay), mmoja unahusu makaa ya mawe na chuma (Mchuchuma na Liganga), na mwingine unahusu uzalishaji wa Magadi Soda.

Baadhi ya miradi ya kielelezo iliyopangwa katika Mpango huo haijaanza kutekelezwa kutokana na changamoto mbalimbali za kifedha na kiutawala. Vile vile, mabadiliko ya hali ya masoko ya kimataifa pamoja na marekebisho ya sera yaliathiri maamuzi ya uwekezaji katika sekta muhimu kama makaa ya mawe, chuma na uzalishaji wa Magadi soda. Hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo ambayo imeanza kutekelezwa, sambamba na ile iliyo katika hatua za awali za kuanza utekelezaji, ni kama ifuatavyo:

### 3.2.1. Miundombinu ya Usafirishaji

Miradi ya miundombinu ya uchukuzi ni ile inayohusiana na ujenzi ikiwemo barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege kwa ajili ya kutolea huduma za uchukuzi. Katika eneo hili Serikali imetekeleza miradi ifuatayo:

**i. Ujenzi wa Madaraja ya Juu**

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDPIII), Serikali imetekeleza miradi ya ujenzi wa madaraja ya juu ambayo ujenzi wake utachochea shughuli za kiuchumi na kurahisisha usafiri na usafirishaji kwa kupunguza msongamano wa magari mijini.

Madaraja haya ni pamoja na: Kigongo – Busisi (JPM) lenye urefu wa km 3.2 na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66 lililopo Mwanza ambapo utekelezji wake umeshakamilika na daraja hili lilifunguliwa June, 2025. Kuanza kutumika kwa daraja hili kutachochea ukuaji wa uchumi kwa Ukanda wa Ziwa na nchi jirani za DRC, Uganda, Rwanda, Burundi na mikoa inayozunguka ukanda wa Ziwa kwa ujumla. Vilevile, mradi huu umerahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa zinazotoka na kwenda katika maeneo hayo.

Ujenzi wa daraja la Tanzanite lenye urefu wa km 1.03 lililopo jijini Dar es salaam limekamilika na kuzinduliwa 24 Machi, 2022 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Daraja hili limegharamiwa na Serikali pamoja na Serikali ya Korea Kusini kwa gharama ya billioni 243. Kukamilika kwa daraja hili kumesaidia kupunguza msongamano wa magari yanayopita katika daraja la selender, limepunguza ajali na kufanyika kama kivutio muhimu katika Jiji la Dar es Salaam.

Vilevile, Sekta ya Ujenzi imekamilisha Ujenzi wa barabara za juu Flyovers katika maeneo ya Uhasibu na Chang,ombe. Ukamilishaji wa barabara hizi umesaidia kupunguza msongamano jijini Dar es Salaam na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa kutoka viwandani pamoja na watu wanaotumia barabara hiyo.

Wizara ya Ujenzi imeanza rasmi ujenzi wa daraja jipya la kisasa katika eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kudumu wa kuondoa changamoto ya mafuriko ya mara kwa mara yanayoathiri jiji hilo. Daraja hilo litakuwa na urefu wa mita 390, na linajengwa kwa viwango vya juu vya kisasa ili kuhakikisha uimara na usalama wa muda mrefu, mkandarasi wa mradi amepokea malipo ya awali na ujenzi umeanza kwa kutengeneza barabara ya muda (diversion) itakayotumika kupitisha magari wakati wa ujenzi. Daraja hili ni la kimkakati, linalenga sio tu kupunguza madhara ya mafuriko bali pia kuboresha usafiri katika eneo hili muhimu, ujenzi huu unahusisha pia njia za maingilio na barabara za magari pamoja na njia salama za watembea kwa miguu kukamilika kwa mradi huu kutachangia

kuimarisha mfumo wa usafiri kutoka katikati ya jiji na maeneo ya Ilala, Buguruni, pamoja na sehemu nyingine zinazotegemea barabara ya Morogoro.

Vilevile, Serikali inaendelea kufanya jitihada za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam ambapo Serikali inaendelea na majadiliano na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) kwa ajili ya ujenzi wa makutano ya barabara kwenye maeneo ya Morocco na Mwenge. Kujengwa kwa Daraja hili kutapunguza msongamano katika makutano ya Mwenge na Morocco na kurahisisha usafiri na usafirishaji katika maeneo hayo.

**ii. Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa**

Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa ili kuinua na kuimarisha huduma za usafirishaji. Katika kipindi cha kufikia Septemba, 2025, utandazaji wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa umefikia km 729.75, ikilinganishwa na lengo la km 1,219 ifikapo mwaka 2025/26 ambapo ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro na Morogoro – Makutupora umekamilika, Makutupora – Tabora (asilimia 14.54), Tabora –Isaka (asilimia 7.41), Mwanza - Isaka (asilimia 64.16) na Tabora – Kigoma (asilimia 8.00).

Kuanza kwa huduma za usafirishaji wa abiria kutoka Dar es Saalam hadi Dodoma kumepunguza muda wa safari kutoka saa tisa (9) hadi saa tatu (3). Kwa ujumla, tangu kuanza kwa safari za treni ya SGR hadi Septemba, 2025, jumla ya abiria 3,932,265 wamesafirishwa na mizigo tani 24,300 imesafirishwa, na jumla ya watanzania 207,468 wamepata ajira katika utekelezaji wa mradi huu. Kati ya ajira hizo, watanzania 1,304 wameajiriwa katika kutoa huduma kwenye vituo vya SGR, watanzania 55,284 wamepata ajira za moja kwa moja na watanzania 150,880 ajira zisizo za moja kwa moja katika ujenzi wa reli ya SGR. Vilevile kumeongeza tija katika uchumi na biashara kwa ujumla.

**iii. Ununuzi wa Meli na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

Serikali imeendelea na ujenzi wa Bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa - Masoko ambao umefikia asilimia 86.64. Shughuli zilizotekelezwa ni; kukamilika kwa uongezaji wa eneo kutoka baharini ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu, ujenzi wa miundombinu nchi kavu na baharini; na kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala, jengo la kupoza na kusambaza umeme, jengo la nitrojeni, jengo la soko, jengo la kuhifadhia na kuchambulia samaki, chelezo, ghala la kuhifadhia zana, jengo la karakana ya meli.

Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha upatikanaji wa huduma zinazotolewa kwa meli za uvuvi; kuongezeka kwa uzalishaji na tija ya mazao ya uvuvi, katika Bahari Kuu; kuwezesha meli za uvuvi kushusha samaki wasiolengwa na kufanyika kwa shughuli ya kuaulisha (transhipment) mazao ya uvuvi; kuongeza fursa za ajira na

kipato; na kuongeza uwekezaji katika viwanda vya kuchakata samaki katika mnyororo wa uongezaji thamani ya mazao ya uvuvi.

**iv. Kuboresha Shirika la Ndege la Taifa**

Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha Shirika la Ndege la Taifa, ambapo jumla ya ndege 15 zimenunuliwa na kulifanya Shirika la Ndege la Taifa kuwa na jumla ya ndege 16 sawa na asilimia 84.2 ya lengo ifikapo 2025/26. Kuongezeka kwa idadi ya ndege kumepelekea kuongezeka kwa idadi ya abiria kutoka abiria 663,016 mwaka 2021/22 hadi abiria 1,178,025 mwaka 2024/2025, na kuongezeka kwa mizigo iliyosafirishwa kutoka tani 1,953 mwaka 2021/22 hadi tani 5,869.81 mwaka 2025/26. Ununuzi wa ndege hizo umechangia kuwa na huduma ya uhakika ya usafiri wa anga, kuongezeka kwa watalii wa ndani na nje ya nchi, na usafirishaji wa mazao na bidhaa za sekta kilimo na sekta ndogo ya mbogamboga na matunda.

### 3.2.2 Miradi ya Miundombinu ya Nishati

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ilipanga kutekeleza miradi Saba (7) ya kielelezo ya nishati inayojumuisha uzalishaji umeme wa maji, utafutaji mafuta, gesi asilia, na bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**i. Miradi ya Uzalishaji Umeme wa Maji**

Miradi ya kuzalisha umeme kwa njia ya maji inayotekelezwa ni: mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere (MW 2,115) ambapo mitambo yote tisa (9) imekamilika na umeme umeingizwa kwenye gridi ya Taifa kulingana na mahitaji. Vilevile, miradi miwili (2) ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) ipo katika hatua za maandalizi. Kukamilika kwa miradi hiyo kutachangia upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa viwandani, ongezeko la ajira kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji, kuchochea uwekezaji nchini, kupunguza matumizi ya mafuta kwa ajili ya uzalishaji wa umeme suala linalosababisha matumizi ya fedha nyingi za kigeni, na kukuza uchumi shindani na jumuishi.

**ii. Miradi ya usindikaji Gesi asilia na utafutaji mafuta**

Serikali imepanga kutekeleza miradi ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Eyasi – Wembere na Mnazi Bay, pamoja na mradi wa Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG). Kwa sasa, miradi hiyo ipo katika hatua za maandalizi ambapo kwa upande wa utafutaji mafuta, taratibu za kuwezesha uchimbaji wa visima vya majaribio na uhakiki zinaendelea. Kuhusu mradi wa LNG, majadiliano baina ya Serikali na Wawekezaji bado yanaendelea.

Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza uzalishaji wa gesi asilia nchini kwa ajili ya

matumizi ya ndani ikiwemo viwandani pamoja na kuuza gesi hiyo katika nchi jirani za Kenya, Uganda, Zambia na Malawi. Hatua hiyo itachangia katika ukuaji wa uchumi, ongezeko la fedha za kigeni, fursa za ajira na huduma za ugavi na biashara kwa Watanzania. Aidha, itachochea uchumi shindani na jumuishi, uwekezaji, kuongezeka kwa uzalishaji viwandani, kuchangia maendeleo ya watu na ujuzi.

**iii. Mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania *(EACOP)***

Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi lenye urefu wa km 1,443 kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) ambao umefikia asilimia 62.5 ya utekelezaji. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza ajira za kudumu na zisizo za kudumu; kukuza mapato ya Serikali; kuhamasisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini; kuongeza wigo wa shughuli za uwekezaji na biashara; kuchangia maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi; na kuchochea ukuaji wa uchumi shindani na endelevu.

**iv. Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma Liganga**

Katika jitihada za kuhakikisha mradi unganishi wa Mchuchuma na Liganga unaanza utekelezaji wake, Serikali imefanikiwa kulipa fidia ya shilingi bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142 wanaopisha utekelezaji wa mradi huo sawa na asilimia 99.8. Majadiliano na mwekezaji yanaendelea. Matarajio ni kukamilisha majadiliano na makubaliano ili kuruhusu kuendelea na utekelezaji wa mradi.

Matokeo ya mradi huu utakapokamilika ni pamoja na kupatikana kwa malighafi ya chuma na makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya viwanda nchini na nje; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kununua chuma nje; kuimarisha maendeleo ya watu kupitia ajira zitakazotolewa; na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kwa kuongeza mauzo chuma, makaa ya mawe na saruji nje. Mradi huu unatarajiwa kuchochea uchumi shindani na jumuishi, uwekezaji na biashara na kuongezeka kwa uzalishaji bidhaa viwandani.

### 3.2.3 Miradi ya Kuongeza Uzalishaji Viwandani

Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano iliainisha miradi mitatu ya kielelezo yenye kujielekeza moja kwa moja kwenye kuongeza uzalishaji viwandani. Miradi hiyo ni Magadi soda (Engaruka), kiwanda cha sukari Mkulazi na Kanda maalum za uchumi na uwekezaji.

**i. Mradi wa Magadi Soda ya Engaruka**

Katika kutekeleza mradi huu, Serikali imetumia shilingi bilioni 5.7 kulipa fidia kwa wananchi 528 kati ya 595 sawa na asilimia 89 ya wafidiwa wote. Zoezi la ulipaji fidia linaendelea kwa wananchi 67 waliobaki.Aidha, Serikali imekamilisha taratibu za kumpata mbia ambapo kampuni ya KEDA (Tanzania) Ceramics Company Limited

imeteuliwa kutekeleza mradi huu kwa njia ya ubia.

Matokeo ya Mradi huu ni pamoja na: kuongeza ajira; kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa ajili ya kuagiza magadi soda kutoka nchi za nje; na kuongeza mauzo nje ya nchi. Mradi utasaidia upatikanaji wa malighafi za magadi soda na kuanzishwa kwa viwanda vinavyotumia malighafi hizo.

**ii. Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi ni moja kati ya uwekezaji wa kimkakati wa Serikali kupitia ubia kati ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unaomiliki asilimia 96 na Jeshi la Magereza kupitia Shirika la Uzalishaji Mali linalomiliki asilimia 4. Utekelezaji wa mradi unajumuisha uendelezaji wa shamba la miwa lenye ukubwa wa hekari 3600, pamoja na ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha sukari katika eneo la Mbigiri wilaya ya Kilosa, Morogoro kwa gharama ya shilingi bilioni 354. Aidha, uendelezaji wa shamba la miwa ulianza tarehe 20 Septemba, 2016 na kukamilika 10 septemba, 2025. Ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha sukari ulianza tarehe 9 Julai, 2021 na kukamilika 31 agosti, 2024.

Utekelezaji wa mradi umekamilika na jumla ya shilingi bilioni 354 zimetumika. Aidha, usimikaji wa mitambo ya kuzalisha sukari ya matumizi ya nyumbani (brown sugar) umekamilika; na mitambo ya kuzalisha sukari ya viwandani (refinery) umefikia asilimia 98.7. Shughuli zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na ufungaji wa paneli mbili (2) za kuendesha mitambo na valvu kwa ajili ya mtambo wa kuzuia chembechembe ya sukari.

Kwa upande wa uendelezaji wa mashamba ya miwa umefikia asilimia 94 ambapo hekta 3,392 za shamba zimelimwa kati ya hekta 3,600 na kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 2,730 kati ya hekta 3,600 pamoja mabwawa mawili (2) yenye uwezo wa mita za ujazo milioni 1.6 na mita za ujazo 3.5 yamekamilika. Vile vile uendelezaji wa mashamba ya wakulima wadogo wadogo umefikia asilimia 80 ambapo hekta 1,384 kati ya 1,717 zimeendelezwa. Aidha, usimikaji wa mitambo ya kuzalisha megawati 15 za umeme umekamilika, ambapo megawati 8 zinatumika kiwandani na megawati 7 zinatarajiwa kuuzwa TANESCO kupitia njia ya usafirishaji wa umeme yenye urefu wa kilometa 56.439 ambayo ujenzi umekamilika.

Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza uzalishaji wa sukari ndani ya nchi kwa kufikia tani 50,000 ifikapo Juni 2028, hivyo kupunguza pengo la mahitaji ya sukari kutoka nje na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia ongezeko la thamani kwenye mazao ya kilimo. Aidha, mradi huu umesaidia kuimarisha ushirikiano na wakulima wadogo 304 wanaozalisha miwa kwa ajili ya kiwanda. Ushirikiano huo umechangia kuongeza kipato cha kaya, kukuza ajira za moja kwa moja kwa takribani

wafanyakazi 2,000, pamoja na ajira zisizo za moja kwa moja zinazokadiriwa 8,000.

**iii. Kanda Maalum za Uchumi na Uwekezaji**

Serikali ililenga kuendelea kuimarisha miundombinu katika kanda maalum za uchumi na uwekezaji pamoja na kuanzisha maeneo mapya katika mikoa ya Singida (Manyoni), Pwani, Kigoma, Tanga, Manyara, Mara, na Ruvuma. Maeneo mawili ya Benjamin William Mkapa SEZ na Mtwara yameanza uzalishaji. Aidha, uendelezaji wa eneo maalum la uwekezaji la Bagamoyo unaendelea ambapo uhuishaji wa mpango kabambe upo katika hatua za mwisho na majadiliano ya kutafuta wawekezaji yanaendelea.

Utekelezaji wa miradi katika kanda maalum imeongeza idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa kufikia 131 mwaka 2025/26 kutoka 7 mwaka 2019/20, kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji kutoka dola za marekani milioni 35.73 mwaka 2019/20 hadi dola za marekani milioni 430.62 mwaka 2024/25, kuongezeka kwa kongani za uwekezaji kutoka 10 mwaka 2019/20 hadi 32 mwaka 2025/26, na kuongezeka kwa ajira kutoka 1,684 hadi 73,124 mwaka 2025/26. Kukamilika kwa miradi ya maeneo maalum ya uchumi na uwekezaji kumeongeza ushindani katika soko la ndani na nje, uzalishaji viwandani na kuvutia uwekezaji nchini.

**Mafanikio, Changamoto, Hatua za kuboresha na Mafunzo yaliyopatikana katika utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo**

**i. Mafanikio**

Utekelezaji wa miradi ya kielelezo umefikia mafanikio makubwa, yakionesha maendeleo thabiti ya Tanzania katika kufikia malengo ya maendeleo na matarajio ya muda mrefu. Miradi hii imechangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha miundombinu nchini, kuongeza ajira na ujuzi; kuboresha huduma za usafiri wa anga; kukuza sekta za viwanda na nishati; na kuharakisha mabadiliko ya kiuchumi na kijamii nchini kote.

**ii. Changamoto**

Licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana, utekelezaji wa miradi ya kielelezo unakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimeathiri ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo. Changamoto zilizojitokeza mara kwa mara ni pamoja na upungufu na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika; mapungufu katika upangaji wa vipaumbele na mpangilio wa utekelezaji, hali iliyosababisha kujumuishwa kwa miradi mingi ya kielelezo katika mipango, na hivyo kupunguza ufanisi kwenye miradi yenye athari kubwa za mageuzi na kiuchumi. Vile vile, ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya kielelezo pia umechangiwa na mapungufu ya kiutawala, ukosefu wa wataalam wabobezi kwenye maeneo mbalimbali, majadiliano ya utekelezaji wa miradi kuchua muda mrefu, pamoja na

mapungufu ya kitaasisi na uratibu.

Changamoto nyingine ni pamoja na ucheleweshaji wa upatikanaji wa ardhi na mchakato wa ulipaji fidia; utegemezi wa teknolojia na zana kutoka nje ya nchi; pamoja na athari za misukosuko ya kiuchumi ya kikanda na kimataifa. Vile vile, utegemezi mkubwa wa bajeti ya Serikali katika kufadhili utekelezaji wa miradi ya kielelezo ambapo kuna ushiriki mdogo wa sekta binafsi na Ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP).

iii. **Hatua za Maboresho**

Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo, hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo zinatakiwa kuchukuliwa. Serikali kuimarisha ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha kwa kupanua vyanzo vya ugharamiaji kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP), mikopo yenye masharti nafuu na kuongezaa wigo wa vyanzo vya ndani, sambamba na kuimarisha udhibiti wa matumizi na kuhakikisha utoaji wa fedha kwa wakati ili kupunguza ongezeko la gharama za utekelezaji.

Vile vile, Serikali kuongeza jitihada za kuvutia uwekezaji na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi; kuimarisha taratibu za manunuzi na usimamizi wa mikataba ili kupunguza ucheleweshaji, kuimarisha mifumo ya uratibu na ufuatiliaji ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi wa utekelezaji. Kuhakikisha upatikanaji wa haraka wa ardhi pamoja na ulipaji wa fidia kwa wakati kwa wananchi wanaopisha maeneo ya miradi na kuhimiza uhamisho wa teknolojia ili kujenga uwezo na ujuzi wa ndani.

**iv. Mafunzo yaliyopatikana**

Uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Mwaka iliyopita umetoa mafunzo muhimu kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27. Mafunzo haya yamebainisha umuhimu wa kuimarisha mifumo ya utawala na uwajibikaji ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza hapo awali na kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi na tija katika miradi ya kielelezo. Mafunzo muhimu ni pamoja na yafuatayo:

(i) **Kuweka Vipaumbele na Mpangilio wa Utekelezaji:** Kujikita katika idadi ndogo ya miradi ya kielelezo yenye athari kubwa za kiuchumi na mageuzi, iliyopangwa kimkakati ili kuharakisha mageuzi ya Tanzania kuwa kitovu cha viwanda, biashara na usafirishaji, pamoja na rasilimali kuelekezwa katika sekta za mageuzi na uwekezaji wa kimkakati wenye manufaa makubwa kwa taifa.

(ii) **Mikakati Shirikishi ya Ugharamiaji**: Kuweka mkakati shirikishi wa ugharamiaji unaojumuisha vyanzo vya kawaida, vyanzo mbadala vya mapato na kushirikisha kikamilifu sekta za umma na binafsi, ikiwemo ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) ili kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za

kutosha na endelevu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo.

(iii) **Ufuatiliaji, tathmini, uwajibikaji na Uratibu:** Kuimarisha ufuatiliaji, tathmini, uwajibikaji na uratibu wa utekelezaji wa miradi ya kielelezo pamoja na kujenga uwezo unaohitajika katika upangaji, ufuatiliaji, tathmini na matumizi ya mifumo ya kidijitali kwa ajili ya upatikanaji wa takwimu kwa wakati. Vilevile, kuweka wazi majukumu na wajibu wa wadau wote muhimu ili kuimarisha ufanisi na kuepusha mwingiliano wa majukumu miongoni mwa taasisi.

(iv) **Ushirikishwaji wa Wadau:** Kuimarisha ushirikishaji wa wadau mbalimbali katika hatua zote za utekelezaji ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi, Asasi za kiraia, mamlaka za Serikali za mitaa (LGAs) na wadau wa maendeleo.

(v) **Dhamira ya Kisiasa na Uendelevu:** Kuhakikisha miradi ya kielelezo inalindwa dhidi ya ushawishi wa kisiasa ili ipate kipaumbele stahiki katika utekelezaji na kudumisha uendelevu wake, kwa lengo la kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya miradi husika kama ilivyopangwa na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

(vi) **Kuandaa mwongozo wa kitaifa wa upangaji:** Mwongozo huu utahakikisha sekta zinaandaa mipango mikakati yake kwa kuzingatia vipaumbele vya mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2026/27 – 2030/31.

## 3.3 Mapitio ya Utekelezaji Kisekta

Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliweka shabaha za utekelezaji zilizotakiwa kupimwa kupitia viashiria vya kisekta. Ufikiwaji wa shabaha zilizowekwa unategemea utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo ambazo zinachangia katika maendeleo ya sekta. Aidha, ili kuwa na tathmin mathubuti ya utekelezaji wa Mpango na kujenga msingi wa kuweka vipaumbele vya Mpango kwa mwaka 2026/27, sehemu hii imeainisha uchambuzi wa kila sekta na kuonesha hatua zilizochukuliwa, mafanikio yaliyopatikana na matarajio ya sekta ili kuimarisha utekelezaji. Mwendendo wa viashiria na shabaha za Mpango ni kama ifuatavyo**:**

### 3.3.1 Sekta ya Ujenzi


Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha miundombinu kwa kujenga barabara, madaraja na vivuko ili kuifungua nchi na kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa kwenda kwenye maeneo mbalimbali. Pia ulilenga kujenga Miundombinu imara ambayo ni kichocheo kikuu cha ukuaji wa uchumi, biashara na kuongeza ajira hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania ni lango kuu la biashara kwa nchi za Zambia, Malawi, DRC, Burundi, Rwanda na Uganda. Mpango pia ulilenga kushirikisha Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara, madaraja na majengo inayotekelezwa ambayo itachochea maendeleo ya sekta nyingine kama viwanda, huduma na maendeleo ya miji.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa mtandao wa

barabara zinazopitika wakati wote za kitaifa na za mikoa kufikia km 37,225.72 mwaka 2024/25 kutoka km 36,361.95 mwaka 2021/22 ; Kuongezeka kwa mchango wa kampuni za ndani katika soko la Ujenzi kutoka asilimia 35 ya jumla ya thamani ya miradi yote mwaka 2021/22 hadi kufikia asilimia 40 ya jumla ya thamani ya miradi yote mwaka 2024/25; kuongezeka kwa Miundombinu (Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa kutoka 60 mwaka 2022/23 hadi kufikia 50 mwaka 2024/25; ;Kufikia kiwango cha wastani wa ukuaji cha asilimia 4.1 mwaka 2024/25; Mchango katika pato la taifa kufikia asilimia 12.8 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa kwa ujenzi wa barabara za vijijini kwa kiwango cha changarawe kutoka km 35,476.59 mwaka 2021/22 hadi km 41,107 mwaka 2024/25 na kuchangia katika uzalishaji wa ajira 21,527 mwaka 2024.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua zilizowekwa ni pamoja na kuongezeka kwa mchango wa Kampuni za ndani katika soko la Ujenzi.

**Kielelezo Na. 3.1:** Mwenendo wa Mchango wa Kampuni za Ndani katika Soko la Ujenzi (Asilimia)





**Chanzo:** *Wizara ya Ujenzi*

Utekelezaji wa afua za Sekta ya ujenzi umebaini kuwa katika kipindi cha Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa maendeleo (FYDP III) Serikali imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa miundombinu imara na imechangia kwa asilimia 12.8 katika pato la taifa. Vilevile, Sekta ya Ujenzi imebaini ongezeko la mtandao wa barabara kutoka km 36,361.95 mwaka 2021/22 hadi kufikia km 37,225.72. Matarajio ya Sekta ya Ujenzi ni kuhakikisha kuongeza kasi ya kujenga miundombinu kwa njia ya ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi na kuondoa dhana kwamba miradi ya miundombinu ni jukumu la serikali peke yake. Sekta binafsi na mashirika ya kimataifa yanayo nafasi muhimu sana, siyo tu kwenye kufadhili bali pia kwenye utaalamu wa kiufundi,

ubunifu wa kiteknolojia na usimamizi. Sekta ya Ujenzi itahakikisha inajenga mazingira wezeshi ili wakandarasi, wawekezaji na washauri binafsi waone fursa katika kila hatua na kutoka usanifu hadi uendeshaji wa mradi.

**Kielelezo 3.2**: Mchango katika Pato la Taifa, Wastani wa Ukuaji wa Sekta ya Ujenzi kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26




**Chanzo:** *Wizara ya Ujenzi*

### 3.3.2 Sekta ya Uchukuzi


Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli, anga, maji na huduma za hali ya hewa; kuendeleza na kuboresha viwanja vya ndege; na kuimarisha huduma za mawasiliano katika viwanja vya ndege.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia kuongezeka kwa mchango wa sekta ya uchukuzi katika pato la taifa kufikia asilimia 7.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2021; kuongezeka kwa idadi ya abiria wanaosafirishwa kwa reli kutoka abiria 1,143,787 mwaka 2021/22 hadi abiria 7,851,127 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa wanaanga waliopatiwa mafunzo kutoka 279 mwaka 2021/22 hadi 1,123 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya meli zilizohudumiwa na bandari zote nchini kutoka 4,686 mwaka 2021/22 hadi 4,888 mwaka 2024/25; na kupungua kwa muda wa makasha kukaa bandarini kutoka wastani wa siku 9 mwaka 2021/22 hadi wastani wa siku 5 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua: kuimarika kwa huduma za reli kunasaidia kupunguza muda na gharama za safari, kuongeza usafirishaji wa abiria na shehena, na kuchochea uzalishaji mali katika mikoa inayounganishwa na

SGR; kuongezeka kwa wigo wa safari za ndege ndani na nje ya nchi, kumechochea utalii na kuongeza mapato yatokanayo na bidhaa za kilimo kupitia usafirishaji wa mazao yanayoharibika haraka kwa ndege maalumu ya mizigo; na kuongezeka kwa ufanisi wa kuhudumia meli na kupunguza muda wa meli kukaa bandarini hivyo kuongeza ushindani wa Bandari ya Dar es Salaam katika ukanda wa Afrika Mashariki.

**Kielelezo 3.3:** Idadi ya Abiria wanaosafirishwa na Reli




**Chanzo:** *Wizara ya Uchukuzi*

Utekelezaji wa afua za Uchukuzi unaonesha mafanikio makubwa kupitia kuimarika kwa ufanisi wa usafiri wa reli, anga na bandari, ikiwa ni pamoja na kupungua kwa gharama na muda wa usafiri na usafirishaji. Uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na usafirishaji umeongeza tija, kukuza biashara, utalii, na kuongeza ushindani wa kimataifa sambamba na kuimarisha ujuzi wa wataalamu wa ndani kupitia uhawilishaji teknolojia. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kukamilisha sehemu zilizobaki za SGR na kuongeza usafirishaji wa mizigo; kuongeza idadi ya ndege na kuongeza mtandao wa safari kimataifa; na kuendelea kuimarisha ufanisi wa bandari.

### 3.3.3 Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Sekta Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kuwa kichocheo muhimu cha shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia matumizi ya mtandao wa intaneti, hivyo kuchangia katika kufanikisha vipaumbele vya kuchochea ushindani, kuongeza uzalishaji viwandani, pamoja na kuimarisha uwekezaji na biashara, kama ilivyobainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III). Kwa muktadha huo Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuboresha mawasiliano , upatikanaji na utumiaji wa intaneti nchini, Hatua hizo ni pamoja na Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB); kuboresha mtandao wa intaneti katika minara 304 ya simu kutoka 2G hadi 2G/3G na 4G; kujenga minara


758 na kutekeleza Mfumo wa Utambuzi Anwani za Makazi katika maeneo yote nchini.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: Kuongezeka kwa; Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini kutoka asilimia 74 mwaka 2024 hadi asilimia 82 mwaka 2025; Uwiano wa watu waliofikiwa na mitandao ya simu za mkononi kutoka asilimia 94 mwaka 2024/25 hadi asilimia 98 mwaka 2025/26 na kuongezeka kwa majengo yenye anuani za makazi kufikia 18,558,268 mwaka 2025/26 kutoka majengo 18,186,0000 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: Kuongezeka kwa Upatikanaji wa Habari; Kuongezeka kwa Fursa za Kiuchumi;Uboreshaji wa Huduma za Serikali (e-Government); Kuchochea ubunifu na uwekezaji na kuboresha huduma za afya na kilimo. Pia kuongezeka kwa idadi ya majengo yenye anuani za makazi kumeleta maatokeo chanya kwa jamii ikiwemo kumuongoza (Navigation) mtu kutoka eneo moja ama anwani ya makazi moja kwenda eneo lingine; kutambua na kuyafikia maeneo ya utalii na vivutio; kuonesha huduma za karibu kama vile ATM, Hospitali, Hoteli na Stendi na kutoa barua ya utambulisho wa mkazi kidijitali kupitia mfumo wa kidijitali wa NaPA ambapo kwa sasa muda wowote na mahali popote, mwananchi ataweza kuomba na kupata barua ya utambulisho wa mkazi kupitia simu yake ya mkononi au kompyuta bila kufika ofisi ya Mtendaji wa Kata, Mtaa au Kijiji.

Utekelezaji wa afua za za sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari umebainisha kuongezaka kwa Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini, Uwiano wa watu waliofikiwa na mitandao ya simu za mkononi pamoja na kuboresha utoaji huduma wa Serikali.Aidha matarajio ya Sekta ya mawasiliano na Teknolojia ya habari ni kuwa na jamii iliyoimarishwa kidijitali inayoendeshwa na uchumi wa kidijitali kwa maendeleo endelevu.

**Kielelezo 3.4:** Kiwango cha watu wanaopata na kutumia Mtandao wa Internet pamoja na simu kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26





**Chanzo:** *Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari*

### 3.3.4 Sekta ya Nishati

Sekta ya Nishati ni sekta wezeshi inayochagiza na kuchochea shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha upatikanaji wa nishati ya umeme kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini; kujenga na kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia; kubuni vyanzo vya nishati jadilifu kwa ajili ya kupikia ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na kuendeleza shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa uwezo wa uzalishaji wa umeme kufikia MW 4,031.71 mwaka 2024/25 kutoka MW 1,605.86 mwaka 2021/22; kuongezeka kwa urefu wa Gridi ya Taifa kutoka km 6,423.53 mwaka 2021/22 hadi kufikia km 8,140 mwaka 2024/25 sawa na asilimia 87 ya lengo la kufikia urefu wa km 9,351 ifikapo mwaka 2025/26; kupungua kwa upotevu wa umeme kutoka asilimia 14.71 mwaka 2021/22 hadi asilimia 12.3 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya vituo vya CNG *(Compressed Natural Gas)* kutoka vituo 2 mwaka 2021/22 hadi vituo 9 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa kiwango cha matumizi ya umeme kwa mtu mmoja kutoka kWh 120.93 mwaka 2020/21 hadi kWh 170 mwaka 2024/25; na kuunganishwa umeme vijiji vyote 12,318 mwaka 2024/25 kutoka 9,112 mwaka 2021/22.

**Kielelezo 3.5:** Mwenendo wa Uzalishaji wa Umeme Nchini (MW) kuanzia mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26




***Chanzo:*** *Wizara ya Nishati*

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuboreshwa kwa upatikanaji wa nishati kwa wananchi, taasisi na viwanda; kuanzishwa kwa viwanda na biashara ndogo ndogo ambazo zinahitaji huduma ya nishati; kuongezeka kwa matumizi ya nishati safi ya kupikia kumechangia kuboresha maisha ya wananchi na kulinda mazingira; kuongezeka kwa ajira, ujuzi, na mapato ya Serikali. Mafanikio haya yameweka msingi thabiti wa uchumi wa viwanda, kuongeza ushindani wa taifa katika masoko ya kikanda na kimataifa, na kuimarisha usalama wa nishati kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Utekelezaji wa afua za sekta ya nishati umebainisha kuwa: uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimkakati kama Bwawa la Umeme la Julius Nyerere ni muhimu kwa kuongeza uzalishaji wa umeme na kuimarisha miundombinu ya viwanda; ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi umethibitisha kuwa ni njia bora ya kufanikisha miradi ya kimataifa kama EACOP; matumizi ya nishati safi kama gesi asilia, jua na upepo yameonekana kuwa na mchango mkubwa katika kulinda mazingira na afya ya jamii; takwimu sahihi na mifumo ya ufuatiliaji wa miradi ni muhimu kwa kuhakikisha utekelezaji bora; maendeleo ya rasilimali watu kupitia mafunzo ya kitaalamu yameongeza ufanisi wa sekta; na upanuzi wa mtandao wa usambazaji umeme vijijini umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuendelea: kuimarisha sekta ya nishati kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme hadi kufikia megawati 8,000 kupitia vyanzo mbalimbali; kuunganisha vitongoji vyote vilivyobakia, na kuboresha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme; kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia; na kuendelea na shughuli za utafiti, uchimbaji na usindikaji wa mafuta na gesi asilia. Hatua hizi zote zinalenga kuleta mageuzi ya kiuchumi,

kuboresha maisha ya wananchi na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati nchini.

### 3.3.5 Sekta ya Kilimo


Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuboresha mifumo ya umwagiliaji ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa ya maji, kuimarisha Utafiti na maendeleo katika mazao ya kimkakati; kuimarisha mnyororo wa uongezaji thamani ya mazao ya biashara pamoja na kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa vyama vya ushirika; kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwandani; uongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo; kuongeza usalama wa chakula na lishe; kuongeza thamani ya mauzo nje ya nchi; na kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa eneo la umwagiliaji kutoka hekta 695,000 mwaka 2021/22 na kufikia hekta 983,466.6 mwaka 2024/25 ikiwa ni lengo la kufikia hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021/2022 hadi tani 22,803,316 mwaka 2024/2025; kuongezeka kwa utoshelevu wa chakula nchini kutoka asilimia 124 mwaka 2020/21 hadi kufikia asilimia 128 mwaka 2024/25 ikiwa lengo ni kufikia asilimia 130 ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa uwezo wa miundombinu ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) kutoka tani 501,000 mwaka 2021/2022 hadi tani 776,000 mwaka 2024/2025 ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia tani 700,000 ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya bustani kutoka tani 7,304,723 mwaka 2021/22 hadi tani 7,518,560.84 ikiwa lengo ni kufikia tani 9,000,000 ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao asili ya biashara kutoka tani 898,000 mwaka 2021/22 hadi tani 1,487,364 ikiwa lengo ni kufikia tani 1,583,200 ifikapo 2025/26.

Vile vile, idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika imeongezeka kutoka milioni 5.1 mwaka 2021/22 hadi wanachama milioni 8.4 mwaka 2024/25 ikiwa lengo ni kufikia wanachama milioni 14.5 ifikapo mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika kutoka viwanda 267 mwaka 2021/22 hadi kufikia viwanda 331 mwaka 2024/25 ikiwa lengo ni kufikia viwanda 338 ifikapo 2025/26.


Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo; kuimarika kwa upatikanaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea, viuatilifu na zana za kilimo; kupungua kwa upotevu wa mazao baada ya kuvunwa; kuimarika kwa usalama wa chakula, kupungua kwa uagizaji wa sukari na mafuta nje ya nchi; kuongezeka kwa upatikanaji wa masoko ya mazao na kupanda thamani ya mauzo ya mazao nje ya nchi; na kuimarika kwa huduma za ugani katika kilimo.

**Kielelezo 3.6**: Hekta za Kilimo cha Umwagiliaji kwa kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025 /26




***Chanzo:** Wizara ya Kilimo*

**Kielelezo 3.7**: Uzalishaji wa Mazao asili ya biashara kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26




***Chanzo:** Wizara ya Kilimo*

Utekelezaji wa afua za kuendeleza kilimo umebainisha kuwa uwekezaji katika miundombinu ya umwagiliaji ni muhimu ili kuwezesha uzalishaji kufanyika kwa kipindi chote cha mwaka bila kutegemea mvua za msimu. Vilevile, matumizi ya teknolojia bora za kilimo husaidia kupunguza watu mashambani ili wajiajiri katika sekta za viwanda na huduma na huduma za ugani na ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya mbegu bora, mbolea, udhibiti wa visumbufu vya mazao na kilimo endelevu ni muhimu katika kuongeza uzalishaji na tija. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ya kilimo ni kuhakikisha sekta inakua kwa asilimia 10 kwa mwaka ifikapo mwaka 2030, na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini kwa kuongeza pato la mkulima.

### 3.3.6 Sekta ya Mifugo


Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuwezesha upatikanaji wa chanjo bora za magonjwa ya mifugo; kuimarisha mifumo ya kufuatilia na kudhibiti magonjwa ya mifugo; kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya mifugo ya udhibiti wa vimelea; kutenga, kupima na kuendeleza maeneo ya malisho; kuwezesha utambuzi, usajili na kuhamasisha mauzo ya bidhaa za mifugo nje; na kuongeza idadi na uwezo wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia kupungua kwa vifo vya mifugo kutoka asilimia 21 mwaka 2021/2022 hadi kufikia asilimia 16 mwaka 2024/25; kupungua kwa magojwa ya mifugo kutoka asilimia 4.5 mwaka 2021/2022 mpaka asilimia 2.5 mwaka 2024/2025; kuimarika kwa kiwango cha uogeshaji wa mifugo kutoka asilimia 74 mwaka 2021/2022 hadi kufikia asilimia 82 mwaka 2024/2025; kuimarika kwa kiwango cha utowaji wa chanjo ya mifugo kutoka asilimia 39.5 mwaka 2021/2022 hadi kufikia asilimia 53.01 mwaka 2024/2025; uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 3.4 mwaka 2021/2022 hadi kufikia lita bilioni 4.1 mwaka 2024/2025; na mauzo ya nyama nje ya nchi kuongezeka kutoka tani 10,415.00 mwaka 2021/2022 hadi kufikia tani 13,112.44 mwaka 2024/2025.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na; kuongezeka kwa tija na mnyororo wa thamani katika uzalishaji wa bidhaa za mifugo; kupungua kwa vifo na magonjwa ya mifugo; na kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi.


Utekelezaji wa afua za Sekta ya Mifugo unaonesha kuongezeka kwa matumizi ya chanjo na mwitikio wa uogeshaji wa mifugo pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya malisho, maji na huduma za ugani kulikopelekea ongezeko la uzalishaji wa mifugo na bidhaa za mifugo. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuongeza uwekezaji katika ufugaji wa kibiashara; kufanya mageuzi ya miundombinu ya malisho na maji; na kuimarisha teknolojia za udhibiti wa magonjwa ili kupunguza milipuko na kuongeza ubora wa mifugo.

**Kielelezo Na. 3.8:** Mlinganisho wa kiwango cha Magonjwa ya Mifugo na Uzalishaji wa Maziwa (Lita Bilioni)  kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26





***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

**Kielelezo Na. 3.9:** Mlinganisho wa Kiwango cha Vifo vya Mifugo, Uogeshaji Mifugo katika Josho na chanjo ya mifugo kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26




***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

**Kielelezo Na. 3.10**: Mauzo ya Nyama nje ya nchi (Tani) kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26




***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

### 3.3.7 Sekta ya Uvuvi


Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha ujenzi wa miundombinu na uwezo wa kitaasisi ili kuboresha usimamizi wa sekta ya uvuvi. Miongoni mwa afua zitakazotekelezwa zinajumuisha: ujenzi wa bandari ya uvuvi; kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa sekta binafsi; kuanzisha na kukarabati viwanda vya mazao ya uvuvi; ujenzi wa miundombinu ya uvuvi; ununuzi wa zana na vifaa vya uvuvi; na kuhamasisha ukuzaji viumbemaji kibiashara.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ya uvuvi kutoka asilimia 1.9 mwaka 2022/23 hadi asilimia 2.3 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa asilimia ya mchango wa sekta ya uvuvi kwenye mauzo nje kutoka asilimia 3.2 mwaka 2021/22 hadi asilimia 3.4 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki kutoka tani 502,305.34 mwaka 2021/22 hadi tani 575,000 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa viwanda vya uchakataji na usindikaji wa samaki kutoka 17 mwaka 2021/22 hadi 21 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongeza mchango wa sekta katika usalama wa chakula na lishe; kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja; na kuchangia upatikanaji wa fedha za kigeni.


Utekelezaji wa afua za sekta ya uvuvi umebainisha kuwa kuna fursa kubwa za uvuvi katika bahari kuu. Hivyo Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha kuwa ujenzi wa bandari ya uvuvi na ununuzi wa meli ya uvuvi vinakamilika ili kuweza kutumia fursa hiyo. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya uvuvi na ukuzaji viumbemaji; kuboresha miundombinu ya uvuvi; na kuimarisha tafiti za uvuvi na kutumia taarifa za tafiti.

**Kielelezo Na. 3.11**: Uzalishaji wa Samaki kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/26




***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

**Kielelezo Na. 3.12:** Uwiano wa Kiwango cha Ukuaji wa Sekta ya Uvuvi, mapato yatokanayo na Mauzo Nje, Mchango katika ulaji wa Protini ya Wanyama na Idadi ya Viwanda vya kusindika samaki




***Chanzo:*** *Wizara ya Mifugo na Uvuvi*

### 3.3.8 Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani

Sekta ya Viwanda ndio nguzo muhimu katika kuleta matokeo makubwa kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji malighafi nchini hususan sekta za kilimo, mifugo na uvuvi. Sekta hii inajenga msingi muhimu katika uongezaji wa Tija na thamani ya malighafi mbalimbali zinazozalishwa nchini. Sekta hii ni nguzo katika kuelekea katika kujenga uchumi imara unaendeshwa na viwanda na hivyo kuweza kufikiwa kwa malengo ya Dira 2025. Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka mitano, ulilenga: kuboresha mazingira uwekezaji nchini; kuwezesha wajasiriamali wadogo na wa kati; kuendelea kutenga na kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji; kuwezesha uanzishaji wa kongani za viwanda; kufanya uvumbuzi, utafiti na uendelezaji wa teknolojia; kuhamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani; kutafuta masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi; na utayarishaji wa viwango pamoja na utoaji wa leseni za ubora.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa idadi ya viwanda nchini kutoka viwanda 80,969 mwaka 2021 hadi kufikia viwanda 128,032 mwaka 2024, ukuaji wa sekta ya viwanda umeongezeka kutoka asilimia 4.5 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 4.8 mwaka 2024; mchango wa katika Pato la Taifa umeendelea kuimarika na kufikia asilimia 8.5 mwaka 2024 kiwa ni sawa na lengo lililowekwa kufikia mwaka 2025; kuongezeka kwa mauzo nje katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kutoka dola za Marekani milioni 1,161.2 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,163.8 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 0.22; na kuongezeka kwa mauzo katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kutoka dola za Marekani milioni 1,303.4 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,968 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 127.7.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua: Kuongeza kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani; kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje hivyo kuchangia kuongezeka kwa fedha za kigeni; kuongezeka kwa nafasi za ajira katika sekta ya viwanda; na kuongezeka kwa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwemo bidhaa za kilimo.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya uzalishaji wa bidhaa viwandani unaonesha, Mazingira wezeshi ya uwekezaji ni nyenzo muhimu. Aidha kukamilika na kuanza utekelezaji wa miradi ya kielelezo na miradi ya kimkakati kutaongeza kasi ya ukuaji wa sekta kwa kutoa ajira, kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kuongeza uzalishaji bidhaa viwandani.

Aidha, matarajio ya mwelekeo wa sekta kwa miaka mitano ijayo ni: kupanua na kuimarisha Masoko ya Kikanda na Kimataifa; kutekeleza mpango maalum wa kukuza viwanda nchini wa Dkt. Samia; kufanya Mageuzi ya Dijitali katika Viwanda na Biashara; kurasimisha shughuli za wajasiriamali wadogo na wa kati; na kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi viwanda na biashara nchini.

### 3.3.9 Sekta ya Madini

Sekta ya madini ni miongoni mwa sekta zinazokua kwa kasi na zenye mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi nchini hususani kwa miaka ya karibuni. Hali hiyo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa mikakati mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mikakati hiyo imeimarisha usimamizi na udhibiti wa rasilimali za madini kwenye mnyororo wa kuongeza thamani; kuwezesha wachimbaji wadogo na wa kati; kuimarisha taasisi za utafiti wa madini; kuhamasisha uongezaji thamani ndani ya nchi; na kuwezesha uchimbaji wa madini muhimu na ya kimkakati. Katika utekelezaji wa mikakati yote hii, Sekta binafsi inaendelea kupewa msukumo wa kipekee kama kiungo muhimu katika kufikia malengo hayo.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: ukuaji halisi wa Sekta ya Madini kufikia wastani wa asilimia 8.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 7.3 mwaka 2020; mchango wa sekta hii kwenye Pato la Taifa umeendelea kuimarika na kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024 ikiwa imevuka lengo la asilimia 10 mwaka 2025/26; Mchango katika mapato yote ya fedha za nje yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje ulifikia asilimia 57 mwaka 2024 ikiwa imevuka lengo la asilimia 51.7 ifikapo mwaka 2025; na jumla ya Mapato ya Fedha za Nje kutokana na mauzo ya dhahabu yalifikia dola za Marekani milioni 4,119.9 mwaka 2024/25 yakivuka lengo la dola za Marekani milioni 3,760.4 ifikapo mwaka 2025/26.


Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: ufanisi umeongezeka na kusababisha baadhi ya viashiria kuvuka malengo kwa kufikiwa kabla ya muda uliopangwa kukamilika. Mafanikio hayo yameongeza mapato ya Serikali, hatua inayowezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi. Vilevile, wadau wa madini wamenufaika kwa kiasi kikubwa kutokana na mazingira bora ya uwekezaji na ongezeko la shughuli za uzalishaji katika sekta hii. Mafanikio haya yamechangia kwa kiwango kikubwa kuongezeka kwa ajira, jambo linalotokana na wingi wa wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa waliojitokeza kushiriki katika shughuli za uchimbaji madini. Halikadhalika, kumekuwa na ongezeko la viwanda vya kusafisha na kuchenjua madini ndani ya nchi, hatua inayosaidia uongezaji thamani wa madini. Uwepo wa viwanda hivyo umeongeza fursa za ajira ikiwa ni pamoja na kuongeza ujuzi wa watalaamu ndani ya nchi. Kwa ujumla, mafanikio haya yameimarisha sekta ya madini na kuifanya kuwa chachu muhimu ya maendeleo ya kiuchumi nchini.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya madini unaonesha kuwepo kwa ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi, utekelezaji wa Sera kuhusu "Ushirikishwaji wa Watanzania katika shughuli za madini (Local Content)" na "Wajibu wa Kampuni kwa Jamii (CSR)" pamoja na Sera ya Madini ya Mwaka 2009 ni nguzo muhimu za ukuaji endelevu wa sekta hii. Kufikia asilimia 10.1 mwaka 2024 ya mchango wa sekta katika Pato la

Taifa mwaka mmoja kabla ya mwaka 2025 imethibitisha ufanisi mkubwa uliotokana na mageuzi yaliyofanyika katika Sekta ya Madini.

Matarajio ya mwenendo wa Sekta ya Madini ni kuendelea kuongeza mapato na mchango wake kwenye Pato la Taifa; kuendelea kudhibiti utoroshaji na biashara haramu ya madini kwa kuimarisha masoko na vituo vya ununuzi. Vilevile, itahamasisha uanzishaji wa migodi mipya ya madini muhimu na madini mkakati ili kuongeza uzalishaji wake. Katika suala la uongezaji thamani ya madini, sekta itavutia uwekezaji kwenye ujenzi wa *smelters* na *refineries* ili kupunguza mauzo ya madini ghafi nje ya nchi. Halikadhalika, Sekta itaendeleza minada na maonesho ya madini ya vito ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti za kina za madini kutoka asilimia 16 hadi kufikia angalau asilimia 50 ifikapo 2030 ili kuboresha taarifa za rasilimali na kuvutia wawekezaji. Kwa upande wa wachimbaji wadogo wakiwemo vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum, Sekta itaendelea kuwarasimisha na kuwapatia maeneo yenye taarifa za jiolojia, leseni na mafunzo ili kuongeza tija na kupunguza uchimbaji holela.

**Kielelezo Na. 3.13:** Mchango na Ukuaji wa Sekta ya Madini katika kipindi cha Mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26




***Chanzo:** Wizara ya Madini*

### 3.3.10 Sekta ya Mazingira na Maliasili


Sekta ya Mazingira na Maliasili Asilia imeendelea kutekeleza afua za Mpango wa wa tatu wa Taifa wa Maendeleo wa  miaka mitano ikiwemo kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu;kuimarisha usimamizi wa tathmini ya athari kwa mazingira na jamii;kuimarisha na kuhamasisha matumizi endelevu ya maliasili asilia kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii; kupunguza uchafuzi wa mazingira pamoja na athari zake; kuimarisha uwezo wa taifa kukabiliana na athari za mabadiliko ya

tabianchi; na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191. Afua nyingine ni pamoja na kuboresha miundombinu ya taasisi za mafunzo ya misitu na nyuki; kuongeza mchango wa sekta ndogo ya ufugaji nyuki kwenye uchumi; kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kupambana na ujangili na usafirishaji haramu wa wanyamapori; na kuendeleza mikakati ya kupambana na ujangili, biashara haramu, uvunaji haramu wa rasilimali za wanyamapori, misitu,nyuki, na malikale nchini. Lengo ni kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa mazingira, uhimilivu wa jamii dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi na matumizi endelevu ya rasilimali asilia.

Utekelezaji wa afua hizo umechangia: kuongezeka kwa idadi ya miti iliyopandwa na kustawi kutoka miti 159,282,897 mwaka 2021 hadi kufikia miti 223,716,211 mwaka 2024; kuongezeka kwa taasisi hadi kufikia 1,047 zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku kuanza matumizi ya nishati safi ya kupikia; kuongezeka kwa mashamba ya miti, uboreshaji wa miundombinu ikiwemo barabara; Kuongezeka kwa mazao mapya ya Utalii wa Nyuki (Api Tourism) katika hifadhi ya msitu;kuongezeka kwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji inayokidhi tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 kutoka asilimia 90 mwaka 2019/20 hadi asilimia 98 mwaka 2024/25; kutekelezwa kwa programmu na miradi inayohusu usimamizi jumuishi wa mifumo ikolojia, urejeshwaji endelevu wa mazingira na hifadhi ya bionuai; na kujengwa kwa vituo vya kuchakata na kurejeresha taka ozo katika majiji sita ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Tanga, Mbeya na Dodoma ili kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa uelewa na ushiriki wa jamii katika masuala ya hifadhi ya mazingira ambapo zaidi ya makundi 2,000 ya jamii yanashiriki kwenye upandaji miti; kupungua kwa uharibifu wa ardhi, bionuwai, na kuenea kwa hali ya jangwa kutokana na jitihada za uhifadhi wa misitu na upandaji miti; kuongezeka kwa uzalishaji wa malighafi mbao katika mashamba ya miti ya Serikali yanayolimwa miti kibiashara kutoka mita za ujazo 1,108,791 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 1,264,535 mwaka wa fedha 2024/2025; Kuongezeka kwa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu kutoka viwanda vya kati na vikubwa 636 mwaka 2020 hadi kufikia 1,671 mwaka 2025 na viwanda vidogo vidogo kama useremala zaidi ya 7,000 ambapo thamani ya mauzo ya mazao ya misitu nje ya nchi imeongezeka kufikia shilingi 458,474,543,027.45 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 333.8 ikilinganishwa na Shilingi 105,689,957,500.00 mwaka 2020/2021; kupungua kwa athari za kiafya na mazingira kutokana na ongezeko la matumizi ya nishati safi ya kupikia hususani kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku na kupekelea kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa; na kuongezeka kwa kipato kwa jamii na mapato ya Serikali kupitia utekelezaji wa miradi ya biashara ya kaboni ambapo jumla ya shilingi **bilioni 48** zimepatikana mwaka 2024/25.

**Kielelezo Na. 3.14:** Miradi Mikubwa inayokidhi Uchambuzi wa Athari kwa Mazingira na Kanuni za Ukaguzi kwa kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2024/25




***Chanzo:*** *Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira*

Utekelezaji wa afua za mazingira na Maliasili Asilia umebainisha kuhamasisha, kusimamia, na kufuatilia utekelezaji wa programu, kuhakikisha azma ya kitaifa ya upandaji miti na hifadhi ya mazingira; kuwekeza katika uhamasishaji wamatumizi ya nishati safi ya kupikia zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku, ili kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa; Kuwekeza katika utekelezaji wa miradi na programmu za biashara ya kaboni ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; kutekeleza programu za kurejesha ardhi, misitu, ardhioevu na nyanda za malisho zilizoharibiwa ili kuimarisha mifumo ikolojia na uhifadhi wa bionuwai; Kuwekeza katika usimamizi na udhibiti wa taka kwa kushirikiana Sekta binafsi; Kuendelea kupanda miti, kulinda vyanzo vya maji na kuhamasisha matumizi endelevu ya misitu; na Kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika juhudi za kuhifadhi mazingira.

Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni Kuongezeka kwa eneo lenye uoto wa asili lililoharibiwa ili kunusuru kuenea kwa hali ya jangwa na ukame; Kuimarika kwa mifumo-ikolojia (ardhi ya kilimo; nyanda za malisho na ardhi-oevu) na ongezeko la uzalishaji kwa baadhi ya sekta za kiuchumi ikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, maji, nishati, misitu na utalii; Kuongezeka kwa matumizi ya nishati safi ya kupikia katika taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 na kupunguza uharibifu wa misitu; Kuongezeka kwa mapato ya Serikali kupitia Biashara ya Kaboni katika sekta za misitu, nishati, uchukuzi na usimamizi wa taka ili kuimarisha jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; Kuongezeka kwa fursa za ajira kwa wanawake na vijana katika shughuli za uanzishaji wa vitalu vya miche, urejelezaji wa taka ngumu, biashara ya kaboni, nishati safi ya kupikia; Kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya elimu ya uhifadhi, upandaji miti, ufugaji nyuki mpango wa matumizi bora ya

ardhi; Kuongezeka kwa programu za upandaji miti katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo maeneo ya vyanzo vya maji;na Kuongezeka kwa tani za asali na nta zinazozalishwa kutoka katika maeneo mbalimbali nchini.

### 3.3.11 Sekta ya Utalii

Sekta ya utalii ni sekta inayotegemea uwepo wa vivutio endelevu vya watalii ikijumuisha misitu, Hifadhi za Taifa na wanyama Pori. Aidha, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umeainisha utekelezaji wa afua ya sekta hii kuwa ni: Kutangaza utalii ndani na nje ya nchi; kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati; kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi; na kuimarisha matumizi bora ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa uhifadhi.


Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: Kuongezeka kwa idadi ya watalii wa kimataifa kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 2,142,895 mwaka 2024 na idadi ya watalii wa ndani kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 3,217,352 mwaka 2024 hivyo kufanya jumla ya watalii wa Kimataifa na wa ndani kuwa 5,360,247 mwaka 2024 ikiwa ni zaidi ya lengo la kufikia watalii milioni tano (5) mwaka 2025/26; kuongezeka kwa mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa kutoka dola za Marekani bilioni 1.3 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024. Kwa upande wa utalii wa ndani, mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 46.3 mwaka 2021 hadi shilingi bilioni 209.8 mwaka 2024.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: Tanzania kuwa kinara Afrika kwa ongezeko kubwa la watalii mwaka 2024; ongezeko la ajira kwa wananchi kutokana na huduma za utalii; kuongezeka kwa idadi ya wanyama waliohatarini kupotea na kuimarika kwa ulinzi na usimamizi wa rasilimali za wanyama pori; na kuimarika kwa biashara ya mazao na misitu na nyuki.

Utekelezaji wa afua za sekta ya utalii umebainisha kuwa kuna ongezeko la kampeni za kuhamasisha utalii wa ndani; ongezeko la bajeti na juhudi za kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi; ongezeko la ushiriki wa Jamii katika masuala ya uhifadhi; na kuimarika kwa mifumo ya M&E kwa takwimu na taarifa za muda halisi.


Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuendelea kubuni vyanzo vya kuongeza mapato; kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapato ma utalii wa kidijitali; kuendelea kupanda miti; kulinda vyanzo vya maji na kuhamasisha matumizi endelevu ya misitu; kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika juhudi za kuhifadhi mazingira;kukabiliana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutumia vifaa vya kisasa;kuboresha miundombinu (barabara, viwanja vya Ndege, Mawasiliano n.k);na kubuni na kuendeleza mazao mapya ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe na malikale.

**Kielelezo Na. 3.15:** Mwenendo na Ulinganifu wa Idadi ya Watalii kwa kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2024/25




***Chanzo:*** *Wizara ya Maliasili na Utalii*

**Kielelezo 3.16 :** Mchango wa Sekta ya Utalii Katika Pato la Taifa na Mchango Wake Katika Mapato ya Fedha za Kigeni Katika Kipindi cha Mwaka 2019/20 hadi 2025/26




### 3.3.12 Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa, na Michezo

Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imetekeleza afua zilizoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Afua hizo ni pamoja na: Kukuza uwekezaji katika sekta ya ubunifu; kuimarisha ulinzi wa kazi za sanaa; kudumisha utamaduni, mila na maadili kwa lengo la kurejesha, kuendeleza na kuhifadhi kwa vizazi vya sasa na vya baadaye; kutambua na kuirejesha historia ya harakati za ukombozi barani Afrika; kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili

kikanda na kimataifa; kujenga viwanja vya mpira vya kisasa, maonyesho ya sanaa na maonesho ya michezo na sanaa za kimataifa; na kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kuhakikisha wananchi wanapata taarifa muhimu.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa idadi ya miundombinu ya michezo kutoka 64 mwaka 2020/21 kufikia 174 mwaka 2024/25 ikiwa ni zaidi ya lengo la miundombinu 72 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu kutoka wasanii 3,931 mwaka 2020/21 kufikia wasanii 7,310 mwaka 2024/25 ikiwa lengo ni kufikia wasanii 8,666 mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo kutoka wataalamu 450 mwaka 2020/21 kufikia wataalamu 11,500 mwaka 2024/25 ikiwa lengo ni kufikia wataalamu 4,297 mwaka 2025/26.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa fursa za ajira kwa vijana; kuongezeka kwa pato la taifa; kuimarika kwa ushirikiano wa kimataifa kupitia lugha ya kiswahili pamoja na kazi za sanaa na michezo; kuongezeka kwa ushindani katika michezo na kazi za sanaa; na kuimarika kwa upatikanaji wa habari kwa umma.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya utamaduni, Sanaa na michezo umebainisha kuwa sekta imeendelea si kuwa sekta ya burudani tu, bali ina nguvu ya kuendeleza uchumi, kuongeza pato la taifa na ajira kwa vijana hivyo ni muhimu iendelee kutambulika kama sehemu ya maendeleo ya kiuchumi. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni: kuendelea kuwekeza katika sekta za michezo kwa kuendeleza miundombinu ya michezo, kukuza vipaji kwa kujenga studio za kisasa na shule za michezo, na kuhakikisha shughuli za michezo zinapatikana ngazi ya mikoa na halmashauri; kuendeleza lugha ya Kiswahili ili kiweze kutumika kikanda na kimataifa na kuwa chombo cha utambulisho wa Taifa na utamaduni; na kuboresha miundombinu ya Habari na mawasiliano kwa umma kama sehemu muhimu ya kuboresha ufikikaji wa Habari na utangazaji wa shughuli za Serikali kwa umma.

### 3.3.13 Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kurahisisha michakato ya uwekezaji na biashara; kupunguza gharama za uwekezaji na biashara; na kupunguza gharama za biashara kwa kuimarisha ufanisi.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa kutoka 220 mwaka 2019/20 hadi 2,938 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa thamani ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa kutoka dola za Marekani milioni 1724.47 mwaka 2019/20 hadi kufikia dola za Marekani milioni 11,267.29 mwaka

2024/25; kuongezeka kwa ardhi ya uwekezaji iliyotengwa kutoka ekari 90,990 mwaka 2019/20 hadi 1,055,403 mwaka 2025/26.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa ushindani katika soko la ndani na nje; kuongezeka kwa uzalishaji viwandani; na kuongezeka kwa uwekezaji nchini.

Utekelezaji wa hatua madhubuti za uratibu na uhamasishaji pamoja na uendelezaji wa miundombinu wezeshi unaonyesha kuwa chachu ya kuongezeka kwa usajili wa miradi  mpya ya uwekezaji.

Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuendelea kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia Mpango wa Pili wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI II); kuimarisha uhamasishaji na utekelezaji wa programu ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya msingi ya ndani na kuzunguka maeneo husika ; kuainisha maeneo ya ardhi ya uwekezaji (Land bank); na kuweka mfumo madhubuti wa kisera, kisheria na kitaasisi wa kusimamia mashirika na taasisi za umma ili kuongeza tija katika uwekezaji wa umma ndani na nje ya nchi kwa kukamilisha utungaji wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma na Kanuni zake pamoja na kuanza uandaaji wa Sera ya Uwekezaji wa Umma.

### 3.3.14 Uwekezaji wa Umma na Sekta Binafsi

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi imetekeleza miradi na programu mbalimbali zenye lengo la kutoa huduma, kuongeza ufanisi katika sekta za miundombinu, na kuboresha mazingira ya biashara. Shughuli zilizotekelezwa katika kufikia malengo ya mpango ni pamoja na: kuratibu majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji; kupata washauri elekezi kwa ajili ya ufunguaji wa makampuni; na kufunguliwa kwa kampuni za uendeshaji (SPV). Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuanza kutekelezwa kwa miradi takribani mitano (5) ya ubia nchini; kuvutia uwekezaji kutoka nje; kuongeza mapato; kuongeza ajira; na kusaidia uendelezaji wa sekta nyingine.

Aidha, sekta binafsi imeendelea kushirikiana na Serikali ili kuwekeza katika miradi muhimu katika sekta za kilimo, viwanda, miundombinu, utalii, ujenzi, na mawasiliano. Jedwali 3.15 linaonesha orodha ya miradi ya PPP ambayo ipo katika hatua za utekelezaji.

**Jedwali 3.2 Orodha ya Miradi Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji**

| Na. | Jina la Mradi | Taasisi inayotekeleza | Mratibu | Thamani ya mradi (Dola za Marekani milioni) |
|---|---|---|---|---|

| Na. | Jina la Mradi | Taasisi inayotekeleza | Mratibu | Thamani ya mradi (Dola za Marekani milioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa jengo la kisasa la biashara la *Stop Business Complex*. | Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam | LGAs | 14.8 |
| 2 | Utoaji wa Huduma za Mabasi kwa Mradi wa *Dar Rapid Transit* Awamu ya Kwanza | Wakala wa Mabasi yaendayo kasi | LGAs | 81.4 |
| 3 | Utoaji wa Huduma za Mabasi kwa Mradi wa *Dar Rapid Transit* Awamu ya Pili | Wakala wa Mabasi yaendayo kasi | LGAs | 248.67 |
| 4 | Ujenzi wa barabara kipande cha kwaza kutoka Kibaha- Mlandizi hadi Chalinze – 78.9km | Wakala wa Barabara Tanzania | MDAs | 328 |
| 5 | Kuanzishwa kwa Vituo vya Ukaguzi wa Magari | Tanzania Police Corporation Sole | MDAs | 117 |

***Chanzo:*** *Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi*

### 3.3.15 Sekta ya Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi

Tanzania imeendelea kudumisha uhusiano na ushirikiano wa nchi mbalimbali kwa lengo la kuboresha taswira yake katika medani za kimataifa kupitia utekelezaji wa diplomasia ya kisiasa na kiuchumi. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, sekta ya ushirikiano wa kimataifa na diplomasia ya uchumi, ililenga: kuendelea kustawisha utekelezaji wa diplomasia ya siasa na uchumi kupitia ushirikiano wa uwili, kikanda na kimataifa; Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa kwa maslahi ya Taifa; na Kushiriki katika jitihada za upatikanaji wa amani, ulinzi na usalama kwa maendeleo jumuishi.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa balozi kutoka 43 hadi 45 na konseli kuu kutoka tatu (3) hadi tano (5); Tanzania kuwa mwenyeji wa vikao muhimu vya kimataifa na mikutano ya ngazi ya juu ikiwemo, Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC na EAC, pamoja na Mkutano wa Wakuu wa Nchi Barani Afrika kuhusu Nishati; na Tanzania imeshika nafasi ya 11 kati ya nchi 119 zinazochangia walinda amani katika misheni za ulinzi wa amani za Umoja wa Mataifa.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua yanajumuisha kuongezeka kwa biashara na uwekezaji kupitia EAC, SADC, AfCFTA, AU, intra Africa Trade; kuimarika kwa amani, usalama na utulivu kupitia jitihada za utatuzi wa migogoro kwa njia ya amani pamoja na kushiriki katika operesheni za kulinda amani; na kuwezesha uhaulishaji wa teknolojia nchini.

Utekelezaji wa afua za Ushirikiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi umebainisha kuwa Sera ya kutokufungamana na upande wowote imeendelea kuimarisha uhuru wa maamuzi kwa nchi suala lililofanya Taifa kuaminika katika diplomasia, ulinzi, usalama na utulivu wa kisiasa. Aidha, matarajio ya mwelekeo wa

sekta ni; kuimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Sera ya Nje 2001 (Toleo la 2025) ili kuimarisha diplomasia ya siasa, uchumi na uwekezaji; na kuendeleza ofisi na makazi ya balozi nje ya nchi.

### 3.3.16 Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi

Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika Sekta ya Elimu ulilenga kutekeleza afua zifuatazo: Kuboresha na kuwianisha mazingira jumuishi ya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote za elimu; Kuhuisha na kuandaa mitaala kulingana na mahitaji ya soko la ajira; kuimarisha mifumo ya ithibati na uthibiti ubora wa elimu; kuboresha umahiri wa walimu katika masomo ya hisabati na sayansi; Kuongeza upatikanaji wa mikopo ya wanafunzi katika elimu ya juu hasa kwa wanafunzi wa masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati, kada maalumu na adimu; kujumuisha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza katika ngazi zote za elimu; na kukuza na kuwezesha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza katika ngazi zote za elimu.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: Kujenga na kukarabati miundombinu ya Elimu Msingi na Sekondari, ambapo kumekuwa na ongezeko la vyumba vya madarasa kutoka 191,708 hadi 254,393, sawa na asilimia 32.69; shule za msingi kutoka shule 16,406 hadi 17,986 sawa na ongezeko la asilimia 9.63; shule za sekondari kutoka shule 3,863 hadi 4,894 sawa na asilimia 26.68; ongezeko la matundu ya vyoo kutoka 206,670 hadi 278,911 (shule za msingi) sawa na asilimia 34.95; na kutoka matundu 92,724 hadi 120,970 (shule za sekondari) sawa na asilimia 30.43; nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 58,637 hadi 60,429 sawa na ongezeko la asilimia 3.05; maktaba kutoka 1,537 hadi 2,665 sawa na ongezeko la asilimia 73.38; maabara kutoka 8,072 hadi 8,710 sawa na asilimia 7.90; mabweni kutoka 2,245 hadi 3,245 sawa na asilimia 44.54; na mabwalo kutoka 871 hadi 1,004 sawa na asilimia 15.26, Shule 868 zimekarabatiwa(msingi 794 na za sekondari 74); na, Ruzuku ya Elimu Bila Ada imeongezeka kutoka shilingi bilioni 249.66 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 484.27 mwaka 2024/25 kwa mwaka sawa na asilimia 93.97.

Aidha, vyuo vya elimu ya ufundi vimeongezeka hadi kufikia vyuo 512 mwaka 2025 kutoka vyuo 441 mwaka 2021, kuongezeka kwa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi (VET) kutoka vyuo 810 mwaka 2021 hadi kufikia Vyuo 905 mwaka 2025. Kwa upande wa elimu ya Juu, Bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 570 zilizotolewa mwaka 2021/22 hadi Shilingi bilioni 916.7 mwaka 2025/26 ambapo kati ya fedha hizi, ufadhili wenye thamani ya Shilingi bilioni 7.29 umetolewa kwa wanafunzi 7,534 wenye ufaulu uliojipambanua katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kupitia SAMIA Skolashipu.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: Kuongezeka

kwa kiwango cha uandikishaji rika lengwa (Net enrolment rate-NER) katika elimu ya awali kutoka asilimia 35.9 mwaka 2020 na kufikia asilimia 51 mwaka 2025; kiwango cha uandikishaji jumla (Gross enrolment rate-GER) elimu ya awali kutoka asilimia 76.9 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 84.5 mwaka 2025; na kupungua kwa uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa kutoka 1:151 mwaka 2020 na kufikia 1:94 mwaka 2025 katika elimu ya awali.

Aidha, kwa upande wa elimu ya msingi, ufaulu wa darasa la saba umeongezeka kutoka asilimia 77.55 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 81.8 mwaka 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa umepungua kutoka 1:56 mwaka 2020 hadi 1:55 mwaka 2025, uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa kutoka 1:75 mwaka 2020 hadi 1:60, uwiano wa idadi ya wanafunzi wa kike kwa tundu la choo kufikia1:39 mwaka 2025 kutoka 1:51 mwaka 2020.

Vilevile, katika Elimu ya Sekondari ya chini (Kidato cha I-IV), ufaulu wa kidato cha Nne umeongezeka kutoka asilimia 80.65 mwaka 2020 hadi asilimia 92.37 mwaka 2024; na kiwango cha uandikishaji wa jumla (Gross enrolment rate) umeongezeka kutoka asilimia 46.2 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 53.1 mwaka 2025. Aidha, Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) Sekondari ya juu (V-VI) kimeongezeka kutoka asilimia 6.9 mwaka 2020 hadi asilimia 9.8 mwaka 2025 ambapo uandikishaji wa wasichana kwa rika lengwa umeongezeka kwa asilimia 3.9. Kuimarika kwa matokeo ya mitihani ya kitaifa Kidato cha sita ufaulu umefikia asilimia 99.99 kutoka 99.90 mwaka 2021.

Katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET), Kiwango cha udahili jumla (%) kimeongezeka kutoka asilimia 5.8 mwaka 2025 hadi asilimia 10.4 mwaka 2025, idadi ya wahitimu imeongezeka na kufikia wahitimu 129,766 mwaka 2025 ukilinganisha na lengo la kuwa na wahitimu 120,000 mwaka 2025/26 ambapo asilimia ya wahitimu wa kike imeongezeka kwa asilimia 10 kufikia asilimia 42 mwaka 2025. Aidha, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya Ufundi Stadi - VET imefikia wanafunzi 58,912 (wanawake 12,022 na wanaume 46,890) ambapo kati yao wanafunzi wa kozi za muda mrefu 24,670 (wanawake 8,450 na wanaume 16,220) na wa kozi za muda mfupi ni 34,242 (wanawake 3,572 na wanaume 30,670).


Aidha, kwa upande wa elimu ya Juu, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu kutoka wanafunzi 295,919 mwaka 2020/21 hadi wanafunzi 361,257 mwaka 2024/25, idadi ya wanafunzi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka 145,000 mwaka 2020/21 hadi kufikia 248,331 mwaka 2024/25; na idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu imeongezeka kutoka 48,621 mwaka 2020 hadi 62,570 mwaka 2024.

Utekelezaji wa afua za elimu umebainisha uandikishaji, udahili na ufaulu kwa

wanafunzi katika ngazi zote za elimu umeendelea kuongezeka; Idadi ya wahitimu wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi bado ni ndogo ukilinganisha na idadi ya wahitimu katika vyuo vikuu nchini; Idadi ya wasichana na wanawake wanaosoma masomo ya Sayansi,Teknolojia,Uhandisi na Hisabati imeendelea kuongezeka; Idadi ya wasichana na wanawake wanaojiunga na vyuo vya Ufundi na Ufundi Stadi inaendelea kuongezeka; Idadi ya watoto wenye ulemavu wanaojiunga katika ngazi zote za elimu imeendelea kuongezeka; na ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji katika sekta ya elimu umechangia kuongeza fursa za elimu nchini.


Aidha, matarajio ya mwelekeo wa sekta ni kuendelea kuwekeza kwenye uboreshaji wa miundombinu katika ngazi zote za elimu hususani miundombinu ya vyuo vya ufundi na mafunzo ya Ufundi Stadi ili kuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi zaidi; Kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia hususani vifaa vya amali na vitabu vya wanafunzi kufikia uwiano 1:1; kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA na teknolojia za kidijitali katika ujifunzaji na ufundishaji kwa ngazi zote za elimu nchini; Kuimarisha elimu maalum na jumuishi ili kuhakikisha wanafunzi wenye ulemavu wanapata fursa ya elimu bora; kuendelea kutoa ruzuku ya Ada katika ElimuMsingi na Sekondari, Mikopo na ufadhili kwa wanafunzi wa elimu hasa wenye jinsia ya Kike ili kusoma masomo ya Sayansi,Teknolojia,Uhandisi na Hisabati (STEM); Kuwezesha wanafunzi wenye ufaulu wa juu wa masomo ya Sayansi katika matokeo ya Kidato cha Sita ili kujiunga na Shahada ya Kwanza katika vyuo bora vilivyo nje ya nchi kusomea masuala ya akili-unde (AI) na *Data Science* kupitia programu ya Samia Extended Scholarship (DS/AI +), na kuwezesha wanafunzi kusoma sayansi na teknolojia ya nyuklia kwa shahada ya umahiri; Kuendelea na maboresho ya mitaala ngazi ya elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi na Elimu ya juu kwa lengo la kuimarisha ujuzi kwa wahitimu wa ngazi hizo; kuendelea kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza uwekezaji katika sekta ya elimu; na kuimarisha ushiriki wa sekta ya umma na binafsi katika kuongeza mchango wa utafiti na ubunifu kwenye maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**Kielelezo Na. 3.17:** Mwenendo wa uandikishaji rika lengwa na uandikishaji jumla katika Elimu ya Awali kuanzia Mwaka 2021 hadi 2025




***Chanzo:*** *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia*

**Kielelezo Na. 3.18:** Mwenendo wa Kiwango cha uandikishaji jumla na uandikishaji rika lengwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, Elimu ya Sekondari (Kidato cha I-IV)




***Chanzo:*** *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia*

**Kielelezo Na. 3.19:** Idadi ya Wanafunzi waliopata Mikopo ya Elimu ya Juu katika kipindi cha mwaka 2020/21 hadi mwaka 2024/25




**Chanzo:** *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia*

**Kielelezo Na. 3.20:** Mwenendo wa Idadi ya wahitimu wa Vyuo Vikuu Tanzania katika kipindi cha mwak 2020  hadi mwaka 2024**.**

### 3.3.17 Sekta ya Afya

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha mifumo ya usimamizi, upatikanaji wa dawa, chanjo, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Afua zilizotekelezwa ni pamoja na: kujenga na kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote; kuajiri na kuendeleza wataalam wa sekta ya afya katika ngazi mbalimbali za utoaji wa huduma za afya nchini; kuhamasisha na kuongeza wigo wa matumizi ya bima ya afya; kuimarisha huduma za tiba za dharura; na kuimarisha huduma za kibingwa na kibingwa bobezi.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 kutoka 26 mwaka 2021/2022 hadi vifo 24 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 66 mwaka 2020 hadi makadirio ya miaka 68 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya Hospitali za Wilaya kutoka 148 mwaka 2020 hadi 361 mwaka 2025; kuongezeka kwa idadi ya Vituo vya Afya vya Serikali kutoka 1,205 mwaka 2020 hadi 1,254 mwaka 2025; kuongezeka kwa idadi ya Zahanati za Serikali kutoka 7,242 mwaka 2020 hadi 8,328 mwaka 2025; kuongezeka kwa idadi ya watumishi katika Sekta ya Afya kutoka 138,059 mwaka 2021/22 na kufikia 177,711 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu (382 tracers); huduma za afya kutolewa katika miundombinu bora; kupunguza muda wa mgonjwa kupata huduma; na kutolewa kwa huduma za kibingwa na ubingwa ubobezi.

Utekelezaji wa afua za afya umebainisha kuwa uwekezaji mkubwa ambao Serikali imewekeza katika Sekta ya Afya katika kipindi cha Miaka mitano (5) katika maeneo mbalimbali ya utoaji wa huduma za afya nchini ikiwemo miundombinu, upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu (Dawa, Vifaa, Vifaatiba, Vitendanishi pamoja na chanjo), ajira (Rasiliamali watu) na mafunzo kwa watumishi wa afya kumewezesha kuboreshwa kwa huduma za afya nchini ambapo matokeo yake yamejidhihirisha na kiashiria cha ongezeko la umri wa kuishi kufikia miaka 68. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya afya kwa wote kwa kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ya mwaka 2023.

### 3.3.18 Sekta ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuteleza afua zifuatazo: ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya maji; kuimarisha upatikanaji wa huduma za usafi wa mazingira; na kuendesha kampeni za kuhamasisha matumizi bora ya maji na usafi wa mazingira.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba kama chanzo kikuu kutoka asilimia 72.3 mwaka 2020/21 hadi

asilimia 83 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira kutoka asilimia 47.3 mwaka 2020/21 hadi asilimia 78.5 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa idadi ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba kutoka asilimia 85 mwaka 2020/21 hadi asilimia 91.6 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: kupungua kwa milipuko ya magonjwa yatokanayo na maji kutokana na kuimarika kwa upatikanaji wa maji ya bomba katika maeneo mbalimbali; kuongezeka kwa tija katika sekta za uzalishaji kutokana na upatikanaji wa maji ya uhakika; na kupunguza muda wa wananchi kutafuta maji kwa ajili ya matumzi ya majumbani kutokana na vituo vya kuchotea maji kupatikana umbali wa wastani usiozidi mita 400.


Utekelezaji wa afua za sekta ya huduma ya maji na usafi wa mazingira umebainisha umuhimu wa Serikali kuendelea kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira kupitia ujenzi wa mabwawa yanayohakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuandaa gridi ya Taifa ya maji ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama nchini.

### 3.3.19 Sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuongeza uwekezaji katika upangaji, upimaji na utoaji wa hatimiliki za ardhi; kuandaa mipango kabambe ya miji, visiwa na fukwe; kuimarisha uwekezaji katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu; kuboresha mfumo wa usimamizi wa taarifa za ardhi; kuwianisha mifumo ya usimamizi wa ardhi na mipango ya sekta nyingine; pamoja na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika upimaji wa ardhi na utoaji wa hatimiliki.


Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa viwanja na mashamba yaliyopimwa kutoka 2,391,366 mwaka 2021/22 hadi 3,097,455 mwaka 2024/25 ambapo jumla ya Hatimiliki (CROs) 406,503 na Hati za Hakimiliki za Kimila (CCROs) 432,821 zimetolewa kutokana na kuimarika kwa mfumo wa ILMIS/e-Ardhi; kuongezeka kwa uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi kutoka asilimia 20.9 mwaka 2021/22 hadi asilimia 34.5 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa makazi yaliyopimwa na kurasimishwa kutoka 2,207,627 mwaka 2021/22 hadi 2,668,236 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa leseni za makazi kutoka 23,862 mwaka 2021/22 hadi 26,646 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa eneo la ardhi lililotengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma kutoka ekari 858,665 mwaka 2021/22 hadi ekari 874,937 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa Mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya yanayotoa huduma kutoka 81 mwaka 2021/22 hadi 112 mwaka 2024/25; na kuongezeka kwa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kupitia Shirika la Nyumba la Taifa kutoka nyumba 187 mwaka 2020 hadi nyumba 802 mwaka 2025.

**Kielelezo Na. 3.21:** Ulinganifu wa Idadi ya Mali zilizorasimisha, Eneo la Ardhi lililotengwa na Idadi ya Viwanja vilivyotengwa




***Chanzo:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*

**Kielelezo Na. 3.22:** Mwenendo wa eneo la ardhi yenye makazi yasiyo rasmi, vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi na ardhi iliyopimwa katika kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2025/26




**Chanzo:** *Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuimarika kwa usalama na uhakika wa umiliki wa ardhi; kuwezesha urahisi wa ufikiwaji wa huduma za jamii na shughuli za uchumi; kuongezeka kwa upatikanaji wa makazi bora na ya gharama nafuu; kuongeza ufanisi katika utatuzi wa migogoro ya ardhi; na kuimarika kwa matumizi endelevu ya ardhi.

Utekelezaji wa afua za Sekta ya ardhi na Maendeleo ya Makazi umebainisha umuhimu wa kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, matumizi ya teknolojia za GIS na mifumo ya kidijitali ya usajili ili kuongeza uwazi na ufanisi. Vilevile, kuna umuhimu wa kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika maandalizi ya mipango kabambe na mipango ya matumizi ya ardhi katika miji na vijiji. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni: kuwa na miundombinu ya kisasa ya upimaji na ramani, kuimarisha mifumo ya umiliki wa ardhi; kupanga miji na vijiji; kuongeza ardhi ya akiba kwa ajili ya uwekezaji na matumizi mbalimbali nchini; na kukuza ushirikiano na Sekta Binafsi katika kupima ardhi na uzalishaji wa makazi ya gharama nafuu.

### 3.3.20 Sekta ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo, kuongeza kipato, kupunguza mzigo kwa Serikali wa matunzo kwa makundi maalum ikiwemo wazee pamoja na kupunguza umaskini. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, sekta ya ustawi na maendeleo ya jamii ililenga: Kupunguza uwepo wa mila na desturi kandamizi na zenye madhara; kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia mikopo yenye riba nafuu na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi; kuimarisha huduma za haki jinai kwa watoto na kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma walio kwenye mfumo wa haki jinai; kuimarisha matunzo, ulinzi na usalama wa mtoto; na kupunguza matumizi yasiyo sahihi ya teknolojia ikiwemo mitandao yanayosababisha ongezeko la mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: Kuongezeka kwa idadi ya vituo vya kulelea watoto wadogo mchana vilivyosajiliwa kutoka vituo 2,714 mwaka 2021/22 na kufikia vituo 4,104 mwaka 2024/25 ambavyo ni sawa na asilimia 55 ya lengo la kusajili vituo 7,500 ifikapo mwaka 2025/26,; kuboreshwa kwa upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee na wasiojiweza kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wazee na wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure kutoka 201,509 mwaka 2021/22 kufikia 1,256,544 mwaka 2024/25, sawa na asilimia 219 ya lengo la wazee 574,321 ifikapo 2025/26; kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo kufikia 113,015 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na wafanyabiashara wadogo 11,003 mwaka 2022/23.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: Kuongezeka kwa muda kwa wanawake kujishughulisha na shughuli za uzalishaji mali; upatikanaji wa huduma za afya kwa wazee na wasiojiweza; na upatikanaji wa ajira na mitaji kwa wafanyabiashara wadogo.

Utekelezaji wa afua za ustawi na maendeleo ya jamii umebainisha kuwa idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano umeongezeka ikimaanisha watoto kupata

huduma za malezi pindi migogoro ya kifamilia inapotokea. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni kuendelea kuimarisha malezi katika ngazi ya familia ili kuwa na jamii inayozingatia misingi ya usawa; kuhamasisha wananchi kuwa kitovu cha maendeleo na kutokomeza mila na desturi hasi ili kuwa na jamii yenye maadili; kuwezesha makundi maalum; pamoja na kusimamia mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuwa na maendeleo endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

### 3.3.21 Kuendeleza Ujuzi

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha huduma za kinga ya jamii, kuongeza ushiriki wa vijana na watu wenye ulemavu katika shughuli za jamii na kiuchumi, kuhamasisha ukuaji wa fursa za ajira na kazi za staha kwa vijana na kukuza ujuzi wa nguvu kazi iliyopo kwenye soko la ajira. Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, sekta ya kazi, vijana, ajira na wenye ulemavu ililenga: kuhamasisha uzalishaji wa fursa za ajira na kazi za staha; kuratibu utekelezaji wa mpango wa kitaifa wa kuendeleza ujuzi kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu; kuongeza wigo wa huduma za kinga ya jamii katika sekta rasmi na isiyo rasmi; kukuza uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana kupitia mikopo rafiki na mafunzo ya ujasiriamali; na kukuza ujumuishaji na uwezeshaji wa kiuchumi kwa watu wenye ulemavu.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa fursa za ajira kutoka 5,000,000 mwaka 2021/22 na kufikia ajira 8,084,204 mwaka 2024/25 ikiwa ni zaidi ya lengo la uzalishaji wa ajira 8,000,000 ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa wigo wa kinga ya jamii kutoka asilimia 24.0 mwaka 2021/22 hadi asilimia 26.9 mwaka 2024/25 ikiwa ni lengo la kufikia asilimia 30 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa watu waliopata mafunzo ya ujuzi kutoka 108,840 mwaka 2021/22 na kufikia watu 157,867 mwaka 2024/25 ikiwa lengo ni kutoa mafunzo ya ujuzi kwa watu 681,000 ifikapo mwaka 2025/26. Aidha, Serikali imeanzisha mfuko wa kutoa ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu; kutolewa kwa mafunzo kwa vijana 94,779 kuhusu ujuzi wa stadi za maisha, afya ya uzazi na uzazi wa jinsia, na elimu ya familia; na kutoa mikopo ya masharti nafuu ya jumla ya shilingi bilioni 3.2 kwa vikundi na makampuni 1,241 ya vijana kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa kipato cha wananchi kutokana na kuongezeka kwa fursa za ajira, kupungua kwa hatari za kijamii, kiuchumi na umaskini kutokana na kuongezeka kwa wigo wa huduma za kinga ya jamii; kuongezeka kwa nguvu kazi inayotakiwa kwenye soko la ajira; kuongezeka kwa ushiriki wa watu wenye ulemavu katika shughuli za kijamii na kiuchumi; na kuimarika kwa huduma za malezi, afya ya uzazi, ushauri nasaha na uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana.

Utekelezaji wa afua hizi umeonesha kuwa hatua zilizochukuliwa katika kukuza ujuzi

zimewezesha kukidhi mahitaji ya soko la ajira hivyo kuongeza fursa za ajira nchini. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza na kuongeza wigo wa programu ya kitaifa ya kuendeleza ujuzi kwa nguvu kazi ya Taifa kulingana na mahitaji ya soko; kufanya utafiti wa kina wa rasilimali watu; kuongeza wigo wa huduma za kinga ya jamii; kuboresha mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni; na kuendelea kuwawezesha kijamii na kiuchumi vijana na watu wenye ulemavu.

### 3.3.22 Utawala Bora na Utawala wa Sheria

Utawala bora na utawala wa sheria unahusisha utekelezaji wa programu na mikakati ifuatayo: programu ya maboresho katika utumishi wa umma; mkakati wa kitaifa dhidi ya rushwa na mpango wa utekelezaji ambapo awamu ya tatu imekamilika na kuzinduliwa kwa awamu ya nne; programu ya maboresho ya Mahakama; usalama wa raia na mali zao; uendelezaji wa nyumba za viongozi; na uendelezaji wa mji wa Serikali Dodoma.

#### i. Utumishi na Utawala Bora

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuboresha miundombinu mbalimbali ikijumuisha miundombinu ya kuimarisha utawala bora kwa kufanya maboresho katika utumishi wa umma kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: kuongezeka kwa idadi ya watumishi waliopatiwa mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa umma kutoka 3,124 mwaka 2019/20 hadi 46,500 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa taasisi zilizowezeshwa kutumia Mfumo wa e-Mrejesho kutoka taasisi 148 mwaka 2021/22 hadi 408 mwaka 2024/25; na kupungua kwa malalamiko yatokanayo na masuala ya utawala bora kutoka 156 mwaka 2020/21 hadi 138 mwaka 2024/25.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuongezeka kwa ari ya watumishi wa umma kutoa huduma bora; kuimarika kwa uwezo wa Taasisi za Umma kutoa huduma bora na zenye tija. Utekelezaji wa afua za kiutumishi na utawala bora umebainisha kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kujengea uwezo watumishi wa Umma pamoja na kuimarisha mifumo ya kielektroniki. Aidha, matarajio ya mwenendo wa sekta ni: kuweka mikakati itakayoongeza uwajibikaji wa Watumishi na Taasisi za Umma katika utoaji wa huduma pamoja na kuongeza ufanisi na tija katika utoaji huduma.

#### ii. Utawala wa Sheria

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuboresha mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki kwa: kuboresha mifumo na miundombinu ya mahakama pamoja na majengo jumuishi ya utoaji wa haki; kuhamasisha

matumizi ya TEHAMA katika utoaji na upatikanaji wa haki; kuimarisha huduma za usajili wa vizazi na vifo na kuimarisha mifumo ya utunzaji wa taarifa na kumbukumbu za mahakama.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia: Kuongezeka kwa idadi ya IJCs zilizojengwa kutoka 3 mwaka 2021/22 na kufikia 9 mwaka 2024/25; kuongezeka kwa idadi ya majengo ya mahakama ya mwanzo kutoka majengo 663 mwaka 2021/2022 hadi 740 mwaka 2024/2025; kuongezeka kwa raia wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi kutoka asilimia 77 mwaka 2021/2022 hadi asilimia 83 mwaka 2024/2025.


Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kupungua kwa muda na gharama wanazotumia wananchi kupata huduma za mahakama na msaada wa kisheria; na kurahishwa kwa upatikanaji wa huduma za usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Bodi za Wadhamini kidijitali kupitia eRITA.

### iii. Amani, Utulivu na Usalama

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulilenga kuimarisha usalama wa raia na mali zao nchini kwa kupunguza kiwango cha uhalifu; kuongeza utambuzi na usajili wa raia; na kupunguza kiwango cha ajali barabarani.

Utekelezaji wa afua zilizowekwa umechangia; kusajiliwa na kutambuliwa kwa jumla ya watu 34,080,610 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na watu 23,965,371 mwaka 2021/2022; kupunguza kiwango cha uhalifu nchini kufikia asilimia xx mwaka 2024/25 ikilinganishwa na asilimia xx mwaka 2021/22; na kuimarika kwa miundombinu ya uangalizi wa usalama barabarani ambapo jumla ya kamera xxx zimefungwa mwaka 2024/25**.**

**Kielelezo Na. 3.23:** Idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa na NIDA




**Chanzo:** *Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi*

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua ni pamoja na: kuimarika kwa hali ya amani, utulivu na usalama kutokana na kudhibitiwa kwa vitendo vya uhalifu; kurahisishwa kwa udhibiti wa uhalifu, utambuzi wa wahalifu, na kupungua kwa matumizi ya vitambulisho feki; na kuongezeka kwa ushiriki wa jamii katika shughuli za usalama.

**iv. Uendelezaji wa Mji wa Serikali Dodoma**

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeendelea kukamilisha ujenzi wa mji wa Serikali Mtumba. Utekelezaji wa afua iliyowekwa umechangia: Jumla ya Wizara 14 kati ya 25 zimehamia kufikia Septemba, 2025. Mafanikio yaliyopatikana kutokana utekelezaji wa afua ni pamoja na huduma za Serikali kupatikana katika eneo moja hivyo kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wananchi. Aidha, Serikali inatarajia kukamilisha ujenzi wa majengo yaliyobaki na kuweka miundombinu katika eneo hilo.

**v. Kukabiliana na Maafa**

Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kukabiliana na maafa kwa kutekeleza ujenzi wa Kituo cha usimamizi wa Maafa kwa Awamu ya pili katika eneo la Nzuguni B jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65. Mafanikio yatakayopatikana ni kuboreshwa kwa mazingira ya utoaji huduma katika kituo cha taifa cha menejimenti ya maafa pamoja na kuwezesha kutolewa kwa taarifa za tahadhari za mapema ambazo zitasaidia kupunguza athari zitokanazo na maafa.

# Sura ya Nne
# Vipaumbele kwa Mwaka 2026/27

## 4.1 Utangulizi

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2026/27 yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele yaliyoanishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaotekeleza Dira 2050. Lengo kuu la Dira 2050 ni kuifanya Tanzania kuwa **Taifa Jumuishi Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea**. Malengo mahsusi ya Dira 2050 ni pamoja na: (i) Kuiwezesha Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani; (ii) Maisha bora na ustawi kwa wote; (iii)Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija, na linalostahimili mabadiliko ya tabianchi; na (iv) Jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitali katika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake kimataifa.

Malengo ya Dira 2050 yatafikiwa kupitia utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51. Utekelezaji wake utazingatia kanuni ya kuanza kutekeleza maeneo ya msingi yenye uwezo wa kufungua fursa za maendeleo katika nyanja mbalimbali. Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51 utatekelezwa kupitia awamu tano (5) mfululizo za Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya ya Miaka Mitano. Utekelezaji wa mipango hii utaanza na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 unaotekeleza Dira 2050 (FYDP I) wenye dhima ya "**Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira**". Kwa muktadha huo, Mapendekezo ya Mpango ya mwaka 2026/27 yamezingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika FYDP IV.

## 4.2 Maeneo ya Kipaumbele ya Mapendekezo ya Mpango

Hatua za kimkakati za Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaotekeleza ya Dira 2050 zinajengwa juu ya nguzo tatu ambazo ni: (i) kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani unaoongeza tija na kubadili vyanzo vya ukuaji; (ii) kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii ili kuwa na watu wenye ujuzi, afya na wanaoweza kuhimili mabadiliko; na (iii) kukabiliana na athari za mazingira na ustahimilivu wa tabianchi ili ukuaji wa uchumi ujengwe katika misingi endelevu. Nguzo hizi zimejengwa kwenye msingi wa utawala bora, ugatuaji wenye ufanisi, mazingira yaliyoboreshwa ya uwekezaji na biashara, uongozi wa kidijitali, sayansi na teknolojia, ujumuishaji wa kikanda, na mabadiliko ya fikra.

Kutokana na mtazamo huu, vipaumbele vya mpango vinaeleza hatua za utekelezaji zinazolenga kuimarisha mazingira thabiti ya shindani wa uchumi mpana, uendelezaji wa viwanda, kilimo cha kisasa, madini na nishati, uimarishaji wa sekta ya ujenzi, maboresho ya biashara na huduma za usafirishaji, ukuaji wa uchumi wa buluu, ushiriki katika masoko ya kaboni, na upanuzi wa huduma zenye thamani kubwa. Vile vile, vipaumbele vilivyowekwa vinaelezea mahitaji ya kimkakati yanayohitajika ili kuziwezesha sekta kufikia viwango vya juu vya utendaji, kuwa na muunganiko katika

utendaji, kuongeza thamani, kuboresha matumizi ya teknolojia na kujenga ushindani wa muda mrefu. Aidha vipaumbele vya Mpango vinasisitiza umuhimu wa mageuzi ya kitaasisi, mifumo ya uratibu na maboresho ya kanuni kama hatua muhimu ya kubadili fursa kuwa matokeo ya kimabadiliko.

Kutokana na maeneo hayo, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 yamejielekeza katika maeneo matano (5) mahsusi ambayo ni: (i) Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji wa taasisi na kuimarisha utawala bora; (ii) kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii ili kuwa na watu wenye ujuzi, afya na wanaoweza kuhimili mabadiliko; (iii) kuimarisha miundombinu ya Kidijitali, Nishati, na Usafirishaji Fungamanishi; (iv) kuimarisha Sekta zinazochochea uzalishaji, uongezaji thamani na ukuaji jumuishi; na (v) uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

Uchaguzi wa maeneo hayo umelenga kujenga msingi wa utekelezaji wa FYDP I ili kufikia malengo ya Dira 2050. Vigezo vilivyotumika kuchagua maeneo ya kipaumbele ya Mpango kwa mwaka 2026/27 ni kama ifuatavyo:

i. **Uwezo wa kuleta mabadiliko ya kimfumo**: Kigezo hiki kinalenga kupima uwezo wa eneo la kipaumbele kuleta mageuzi ya kimfumo ili kuondoa urasimu na kuleta nidhamu ya matumizi ya fedha za umma;
ii. **Utayari wa kuanza utekelezaji:** Kigezo hiki kimelenga kuweka mazingira endelevu ya utekelezaji wa miradi inayoendelea ambayo haikukamilika wakati utekelezaji wa Mipango iliyopita pamoja na miradi iliyotayari kutekelezwa;
iii. **Kuchochea ukuaji wa sekta nyingine:** Kigezo hiki kimelenga kutoa kipaumbele kwa sekta zinazokua zenyewe na kuchangia ukuaji wa sekta nyingine;
iv. **Uwezo wa kuzalisha ajira kwa wingi**: Kigezo hiki kimelenga kutoa kipaumbele kwa sekta zinazozalisha ajira kwa wingi hususan kwa vijana;
v. **Uwezo wa kuleta mageuzi katika uchumi**: Kigezo hiki kimelenga kutoa kipaumbele kwa sekta zilizo na fursa ya kuleta mageuzi ya kimfumo ya uchumi na ushindani wa kimataifa ili kuondoa utegemezi ya mifumo ya zamani ya kiuchumi. Hii inajumuisha sekta zenye uwezo wa kuongeza thamani ya bidhaa na huduma, zinazochangia fedha za kigeni, na zinazoongeza mapato ya Serikali; na
vi. **Uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi**: Kigezo hiki kinalenga kutoa kipaumbele kwa miradi inayohimiza utunzaji wa mazingira na kuongeza uhimilivu ya mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, utekelezaji wake utajielekeza pia katika kuhakikisha uendelevu wa utekelezaji wa miradi ya kielelezo na afua za maendeleo ambazo hazikukamilika katika kipindi cha utekelezaji wa Dira 2025.

Hatua mahsusi katika kila eneo la kipaumbele ni kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji wa taasisi na kuimarisha utawala bora

Eneo hili limelenga kuimarisha utawala bora na ufanisi katika sekta ya umma ili kuleta uwajibikaji, uwazi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma huku ikilenga kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani na kuweka mazingira wezeshi kwa ustawi wa Taifa. Afua zitakazotekelezwa katika eneo hili ni:

i. Kufanya mageuzi katika mifumo ya utawala;
ii. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;
iii. Kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa shughuli za uchumi ili kuweka msingi thabiti wa utekelezaji wa Dira 2050;
iv. Kufanya maboresho ya sera, sheria, kanuni na taratibu ili kuleta ulinganifu wa sera na sheria na mikakati ya kisekta;
v. Kutenga maeneo ya biashara kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ili waweze kutambulika na kurasimishwa;
vi. Kusimamia utekelezaji wa sera zinazolenga kuboresha hali ya makazi kwenye maeneo yenye makazi duni;
vii. Kuimarisha na kuendeleza ushirikiano na nchi mbalimbali na mashirika ya kimataifa ili kukuza fursa za kidplomasia na kiuchumi; na
viii. Kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama ili kuhakikisha ulinzi wa mipaka, rasilimali na usalama wa raia na mali zao.

Hatua hizi zitawezesha kuwepo kwa sera zinazotabirika, kuvutia wawekezaji nchini, kupunguza urasimu pamoja na kuimarika kwa mifumo ya uwekezaji wa umma hivyo kujenga msingi imara wa uchumi jumuishi, uendeshaji wa mashirika ya umma kwa tija pamoja na kuongezeka kwa mapato ya ndani ili kugharamia utekelezaji wa Mpango.

### 4.2.2 Kuimarisha miundombinu ya kidijitali, nishati, na usafirishaji fungamanishi

Eneo hili limelenga kuongeza ushindani kimataifa kwa kuongeza tija, uwezo wa uzalishaji pamoja na kuongeza thamani ya bidhaa na huduma nchini, kuvutia uwekezaji wa kimkakati na kuchochea uzalishaji wa ajira zenye tija na staha. Maeneo yanayoweza kuleta mageuzi ni pomoja na: nishati; usafirishaji shirikishi; sayansi na teknolojia; utafiti na ubunifu; mifumo ya taarifa na takwimu; mabadiliko ya kidijitali; upanuzi wa TEHAMA na mazingira wezeshi ya kufanya biashara ili kuharakisha mabadiliko ya kimuundo na kuunga mkono matarajio ya taifa chini ya Dira 2050. Kuimarisha vichocheo hivi ni muhimu katika kuendeleza uzalishaji viwandani, kuboresha miundombinu, kuongeza uwezo wa kuuza nje, kuwezesha upokeaji wa teknolojia, kuboresha utoaji huduma na kuvutia uwekezaji wenye ubora wa juu. Hatua mahsusi za kufanikisha eneo hili zimelenga katika:

i. Kuwekeza kwenye miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme;
ii. Kuboresha miundombinu ya barabara, reli, meli, bandari na viwanja vya ndege;
iii. Kuboresha miundombinu ya kuhifadhi, kusafirisha na kusambaza bidhaa zinazohitaji hali ya ubaridi;
iv. Kuboresha miundombinu ya mabomba ya mafuta na gesi;
v. Kutekeleza Mfumo wa Kitaifa wa Ubunifu,
vi. Kuboresha maabara za utafiti pamoja na vituo vya teknolojia;

vii. Kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na TEHAMA pamoja na usalama wa mtandao ili kuchochea uchumi wa kidijitali; na
viii. Kufunganisha mifumo ya kidijitali ya utoaji huduma za Serikali ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo na kupunguza urasimu.

Kuimarisha miundombinu hiyo kutachochea dhamira ya Tanzania ya kukuza sekta ya viwanda, kuongeza thamani kwenye rasilimali za madini na mazao ya kilimo na kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI)**.**

### 4.2.3 Kuimarisha sekta zinazochochea uzalishaji, uongezaji wa thamani na ukuaji jumuishi.

Eneo hili limelenga kuchochea uzalishaji na uongezaji wa thamani katika sekta za uzalishaji ikiwemo: kilimo; viwanda; ujenzi, ardhi na maendeleo ya makazi; madini na uchimbaji wa mawe pamoja na mafuta na gesi. Aidha, sekta za utalii, michezo na burudani vinaongeza mauzo ya huduma nje na kuimarisha taswira ya kitaifa, huku sekta za fedha, biashara, huduma za kibiashara na ushirikiano wa kikanda zikiboresha ujumuishaji wa masoko, uwekezaji na ushindani. Hatua mahsusi zitahusisha:

i. Kuendeleza mnyororo wa thamani katika madini adimu na madini ya kimkakati;
ii. Kuwarasimisha na kuwaendeleza wachimbaji wadogo;
iii. Kuhimiza uwekezaji katika viwanda vya uchakataji wa mazao ya kilimo, uzalishaji wa dawa, mbolea na bidhaa za chuma;
iv. Kujenga miundombinu wezeshi katika maeneo maalum ya uwekezaji, kongani za viwanda na maeneo maalum ya uzalishaji kwa mauzo ya nje;
v. Kuwekeza na kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani katika Sekta ndogo za mazao, mifugo na uvuvi ili kuongeza tija na uzalishaji;
vi. Kutoa motisha kwa viwanda vya ndani ili viweze kuzalisha kwa gharama nafuu na kuviwezesha kushindana katika soko la ndani na nje;
vii. Kufungamanisha vivutio vya utalii na kuboresha vyuo vya utalii na ukarimu ili kuongeza idadi ya watoa huduma wenye weledi kwenye fani zote za utalii na ukarimu;
viii. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu, uongezaji thamani na utafutaji wa masoko; na
ix. Kuongeza uwekezaji kwenye tafiti za kina za madini (High Resolution Geophysical Survey).

Hatua hizi zinalenga kuimarisha nafasi ya Tanzania katika biashara ya kikanda na kimataifa, kuvutia uwekezaji wa kimkakati na kuongeza thamani ya uzalishaji wa ndani**.**

### 4.2.4 Kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya jamii

Eneo hili limelenga kuwekeza kimkakati katika masuala ya elimu, afya, huduma za maji safi na salama ili kupata nguvu kazi yenye afya, maarifa na ujuzi unaoendana na mahitaji ya soko. Uwekezaji huo utahusisha kufanya mageuzi kwenye utoaji wa huduma za kijamii na kuchochea sekta za uzalishaji . Hatua mahsusi zitahusisha:

i. Uboreshaji wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia ikiwemo matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu na kuwezesha maandalizi ya kundi rika mbili;
ii. Kuendelea na maboresho ya mitaala ngazi ya elimu ya amali (Ufundi na Mafunzo ya Ufundi stadi) na elimu ya juu kwa lengo la kuimarisha ujuzi kwa wahitimu wa ngazi hizo;
iii. Kuimarisha matumizi ya sayansi, teknolojia, tafiti na ubunifu ;
iv. Kuimarisha na kuongeza wigo wa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa nguvukazi iliyopo kwenye soko la ajira hususan ujuzi adimu;
v. Kuboresha vituo vya ubunifu na umahiri ili kukuza ubunifu na ujasiriamali;
vi. Kuboresha upatikanaji wa huduma ya usafi wa mazingira pamoja na maji safi na salama ili kuwa na gridi ya Taifa ya Maji;
vii. Kuimarisha uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji nchini;
viii. Kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya;
ix. Kuimarisha na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma jumuishi za kinga ya jamii kwa wananchi wote;
x. Ushirikishwaji wa vijana na watu wenye ulemavu katika masuala ya maendeleo ikiwemo kuwawezesha vijana wanaomiliki biashara ndogo kupata elimu ya biashara na kuweza kujisajili katika Mfumo wa Kielektroniki wa Manunuzi ya Serikali (NeST);
xi. Kuongeza kasi ya maandalizi ya mipango miji kwa maeneo ya miji na majiji;
xii. Kuendelea kuvutia michezo mbalimbali kufanyika hapa nchini ili kuongeza fursa zitokanazo na kuwa mwenyeji wa michezo hiyo; na
xiii. Kuleta maendeleo jumuishi maeneo ya vijijini kwa kuboresha uzalishaji, kupanua miundombinu ya vijijini, kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha, kuimarisha utawala wa ardhi, na kuendeleza shughuli mbalimbali za kujipatia kipato.

#### 4.3.5 Uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi

Eneo hili limelenga kuchochea uendelezaji endelevu wa viwanda, ukuaji wa miji, ustawi wa maisha ya watu na mifumo thabiti ya ikolojia. Vilevile, linajumuisha eneo la uhifadhi wa misitu na bioanuwai, nishati jadidifu na kuboresha mifumo ya utoaji tahadhari mapema. Hatua mahsusi zitahusisha:

i. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kibiashara yenye ustahimilivu wa tabianchi kwa kupanua umwagiliaji, na kuongeza matumizi ya pembejeo bora;
ii. Kuimarisha utunzaji wa mazingira kupitia usimamizi wa utekelezaji wa mkakati wa nishati safi ya kupikia pamoja na kuimarisha usimamizi wa biashara ya hewa ukaa;
iii. Kuongeza kasi ya urasimishaji wa maeneo ya makazi kwa kupima ardhi kwa teknolojia ya kisasa ya satelaiti; na
iv. Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa mazingira na kuweka misingi ya uendelevu katika sekta zote ili kuhakikisha usalama na ustawi wa ikolojia.

Maelezo ya kina ya afua zitakazotekelezwa kwa mwaka 2026/27 yameainishwa katika kiambatisho II. Utekelezaji wa afua hizo unalenga kuandaa mazingira ya kutekeleza

maeneo ya kielelezo yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31.

# SURA YA TANO

## MAPENDEKEZO YA UGHARAMIAJI WA MPANGO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mwelekeo wa ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/27 ambao ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa FYDP I. Katika mwaka huo, Serikali itaweka msingi wa kujenga mfumo thabiti wa ugharamiaji wa miaka mitano ya awali ya Dira 2050 kwa kutekeleza mabadiliko makubwa ya mifumo ya ugharamiaji, ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa fedha za umma, na uanzishaji wa mbinu bunifu za kufadhili maendeleo, kama ilivyoainishwa kwenye misingi ya DIRA 2050.

Kuanzia mwaka 2026/27, ugharamiaji wa Mpango unalenga kuimarisha mfumo wa ugharamiaji unaotumia mtazamo wa 70:30 (Sekta Binafsi: Serikali**)** ili kuongeza uwekezaji katika sekta za kipaumbele, kuongeza uwezo wa uchumi, na kuongeza ajira ili kuweka msingi wa uchumi wa kisasa, jumuishi na shindani.

### 5.2 Mwelekeo wa Sera ya Fedha na Bajeti kwa 2026/27

Katika mwaka 2026/27, Serikali itatekeleza sera za fedha na bajeti zinazolenga kulinda uthabiti wa uchumi, kuongeza uwezo wa ndani wa ugharamiaji, na kuweka misingi ya ushiriki mkubwa wa sekta binafsi katika kufadhili maendeleo. Mwelekeo huu unalenga:

i. Kuongeza uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa kwa kuimarisha mifumo ya kodi, kuongeza wigo wa kodi, na kuongeza ufanisi wa TRA.
ii. Kudhibiti nakisi ya bajeti ili kuhakikisha uhimilivu wa deni la Taifa sambamba na viwango vya kimataifa.
iii. Kuhamisha matumizi kutoka kwenye gharama zisizo za uzalishaji kuelekeza kwenye miradi ya kimkakati yenye tija na matokeo ya kitaifa.
iv. Kuongeza matumizi katika sekta zinazochochea ukuaji kama vile nishati, viwanda, TEHAMA, kilimo, miundombinu na ujuzi.
v. Kuongeza matumizi ya mifumo ya fedha ya kijani, kidigitali na mseto (blended finance) kama msingi wa fedha za miaka ijayo ya Dira 2050

#### 5.2.1 Mahitaji ya Fedha kwa mwaka 2026/27

Mahitaji ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 yanakadiriwa kufikia kiasi cha shilingi trilioni 84.9. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 19.3 ni kutoka kwenye bajeti ya Serikali sawa na asilimia 31.3 ya Bajeti Kuu ya Serikali, trilioni 5.5 ni kutoka katika mashirikia ya umma yanayojiendesha kibiashara na shilingi trilioni 60.1 ni kutoka sekta binafsi ikiwa ni makadirio ya kiasi kitakachotengenezwa katika ukuzaji wa mitaji. Kiasi hiki kinaendana

na mahitaji ya uchumi unaohamia katika uandaaji wa mazingira ya uwekezaji, mageuzi ya taasisi, na uimarishaji wa sekta za uzalishaji.Serikali itachukua hatua zifuatazo:

i. Kudhibiti nakisi ya bajeti isizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa;
ii. Kuhakikisha mapato ya ndani yanafikia asilimia 17.1 ya Pato la Taifa;
iii. Kuimarisha nidhamu ya matumizi kupitia usimamizi makini na ufanisi katika matumizi ya rasilimali za umma;
iv. Kuhakikisha miradi inayofadhiliwa kwa mikopo inaleta matokeo ya muda mrefu yenye manufaa kwa vizazi vijavyo; na
v. Mifumo ya ufuatiliaji wa fedha inaimarishwa kupitia Results-Based Monitoring, Evaluation, Accountability and Learning (RBMEAL) ili kuhakikisha uwajibikaji na ufanisi

### 5.2.2 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2026/27

Vyanzo vya mapato vinavyotarajia kuchangia katika utekelezaji wa Mpango 2026/27 vitatokana vyanzo vinne vikuu kama ifuatavyo:

i. Mapato ya Ndani: kodi, mapato yasiyo ya kodi, gawio kutoka kwa mashirika ya umma na mapato ya halmashauri;
ii. Rasilimali fedha za Nje: mikopo nafuu, misaada, na mikopo isiyo nafuu kwa miradi ya kibiashara;
iii. Mitaji ya Sekta Binafsi: kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP), uwekezaji wa moja kwa moja (FDI), na ushiriki wa sekta binafsi katika ufadhili wa miradi;
iv. Mbinu Bunifu ya Ufadhili: kama vile hati fungani za kijani, za miundombinu, na za halmashauri.

## 5.3 Mikakati ya Ugharamiaji kwa 2026/27

### 1 Serikali (MDAs & LGAs)

Kipaumbele ni kuongeza mapato, kuongeza wigo wa walipa kodi, na kuboresha usimamizi wa matumizi.

**Hatua kuu 2026/27:**

i. Kuendelea na kufanya PSCs kujitegemea (kupungua kwa ruzuku kwa ≥10% mwaka 2026/27).
ii. Kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji wa Taifa TZS 123 bilioni kwa vijana, wanawake, watu wenye ulemavu.
iii. Kuweka asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri kuanzisha Maeneo Maalum ya Kibiashara (Business Parks).
iv. Kuanza mchakato wa *Sovereign Wealth Fund (SWF)* kwa mapato ya madini na mafuta.
v. Kuanzisha *Sustainable Finance Taxonomy*.

### 2 Sekta Binafsi

Sekta binafsi ndiyo injini ya ugharamiaji wa 2026/27. Serikali inalenga:

i. Kuongeza FDI hadi ≥10% ya GDP kufikia 2030;

ii. Kuongeza uwekezaji wa ndani (DDI) kupitia kupunguza NPLs chini ya asilimia tano (5);
iii. Kufanya *capital account* liberalization ifikapo 2027.

**Mikakati ya 2026/27:**

i. Miradi ya PPP ≥6 kuingia hatua ya maandalizi ya miamala (bankability).
ii. Kuongeza ushiriki wa wawekezaji kupitia IFC-DSM.
iii. Kuimarisha Skimu ya Dhamana ya Mikopo (Credit Guarantee Schemes (CGC-T).

**3 Mashirika ya Umma na Taasisi za Kisheria (Public and Statutory Corporations (PSCs)**

PSCs zinatarajiwa kuchangia TZS 5.5 trilioni (2026/27).

**Mikakati ya 2026/27:**

i. Kuanza mchakato wa kuyapatia PSCs utaratibu wa kufadhili uwekezaji kupitia corporate bonds.
ii. Kuunganisha baadhi ya PSCs kwa "resource pooling" ili kuongeza tija.
iii. Kupunguza hasara kwenye PSCs kwa ≥15% mwaka 2026/27.
iv. Kuanzisha mpango wa PSC Asset Monetisation.

**4 Fedha Mbunifu na Masoko ya Kijani**

Mwaka 2026/27 inalenga kuanza utekelezaji wa:

i. Hati Fungani ya Kijani za Serikali
ii. Hati Fungani za Diaspora (Diaspora Bonds)
iii. Mfumo wa Uuzaji wa Hisa za Kaboni (Soko la Kaboni Tanzania) (Carbon Credit Trading Framework (Tanzania Carbon Exchange))
iv. Vyanzo Mseto vya Ufadhili katika sekta za nishati, kilimo na Uwezeshaji wa mikopo kwa Wafanyabiashara wa Kati na Wadogo; na
v. Sera ya Ugeuzaji Takwimu kuwa Chanzo cha Mapato (Data Monetization Policy)

# SURA YA SITA
# UFUATILIAJI NA TATHMINI

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kutoa maelekezo mahsusi ya ufuatiliaji na tathmini yatakayozingatiwa wakati wa uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/27. Malengo mahsusi ya sura hii ni kama ifuatavyo: Kuhakikisha kila shilingi inayotumika inaleta matokeo yanayoonekana na yanayopimika; kubaini changamoto za uratibu na utekelezaji mapema na kuzitatua ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya utekelezaji wa afua mbalimbali za maendeleo; na kuongeza uwajibikaji na uwazi wa Serikali kwa wananchi inaowahudimia.

## 6.2 Misingi na Miongozo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Mwaka 2026/27

Waratibu na watekelezaji wa afua mbalimbali za mpango wa maendeleo wanatakiwa kuzingatia masuala yafuatayo:

i. **Uwajibikaji wa Matokeo** – Kila taasisi itawajibika kwa matokeo yaliyoainishwa kwenye mpango wa mwaka.
ii. **Upangaji wa Bajeti Unaotegemea Matokeo** – Bajeti yoyote ya utekelezaji wa afua za maendeleo uzingatie mipango ya maendeleo na matokeo halisi yanayotarajiwa
iii. **Maamuzi Yanayotegemea Takwimu Rasmi** – taarifa za utekelezaji na takwimu sahihi vitakuwa msingi katika kufanya maamuzi.
iv. **Uwazi na Ushirikishwaji wa Wananchi** – Uibuaji na utekelezaji wa afua mbalimbali za maendeleo ushirikishe wananchi.
v. **Matumizi ya Teknolojia na Ubunifu** – uibuaji wa afua, uwasilishaji na upokeaji wa taarifa za utekelezaji wa afua mbalimbali za maendeleo utafanyika kupitia mifumo ya kielektroniki ikiwemo NPMIS

.

## 6.3 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Katika mchakato wa kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2026/27, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kama nguzo muhimu ya kuhakikisha utekelezaji bora wa miradi na programu za maendeleo. Ufuatiliaji na tathmini vinachangia katika kuongeza ufanisi, kuimarisha uwajibikaji, na kuwezesha maamuzi ya kisera yanayotegemea ushahidi. Ili kufikia matokeo tarajiwa ya Mpango, watekelezaji wa miradi na waratibu wa mipango wanapaswa kusimamia kikamilifu taratibu za ukusanyaji, uchambuzi, na uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji.

Katika muktadha huo, Mapendekezo ya Mpango 2026/27 yanaainisha matokeo mahsusi ya ufuatiliaji na tathmini kama ifuatavyo:

i. **Kuandaa mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini**: watekelezaji na waratibu wanaelekezwa kuandaa mipango ya ufuatiliaji na tathmini na kuitekeleza ipasavyo. Taarifa za utekelezaji wa mazoezi hayo zitawasilishwa kulingana na taratibu za Serikali;

ii. **Taarifa za ufuatiliaji na tathmini:** watekelezaji wa miradi ya kielelezo wataandaa taarifa za utekelezaji za kila wiki kwa kuzingatia mwongozo wa PIMG 2025. Aidha, watekelezaji wa miradi na mpango wataandaa taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka kwa kuzingatia mwongozo wa PIMG na miongozo mingine ya Serikali;
iii. **Uchambuzi na tathmini ya matokeo:** Taarifa zinazokusanywa zitachambuliwa ili kutathmini maendeleo ya miradi na programu kulingana na malengo yaliyowekwa. Uchambuzi huu unasaidia kubaini changamoto, mapungufu, na fursa za kuboresha utekelezaji wa Mpango;
iv. **Upatikanaji na usambazaji wa taarifa:** Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yatawasilishwa kwa wadau husika, ikiwemo Wizara, Mamlaka za Serikali za Kawaida, na wadau wa maendeleo, ili kuongeza uwazi, uwajibikaji, na kuhamasisha ushirikiano katika utekelezaji wa Mpango; na
v. **Kuendeleza maboresho na mafunzo:** Matokeo yatumike kama msingi wa mafunzo kwa watekelezaji na waratibu, kuboresha utendaji, na kuanzisha maboresho ya kimfumo katika mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Hii inalenga kuongeza ufanisi wa utekelezaji, kuhakikisha .; wa wadau wote, na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa maendeleo ya Taifa

### 6.4 Mgawanyo wa Majukumu

| Mdau | Wajibu wa Msingi | Muda wa Kutoa taarifa |
|---|---|---|
| **Tume ya Taifa ya Mipango** | Kusimamia NPMIS, kupokea na kufanya mapitio ya taarifa za utekelezaji kitaifa za kila wiki kwa miradi ya kielelezo, robo na mwaka, na kufanya ufuatiliaji na tathmini | Kila robo mwaka, nusu mwaka na mwaka |
| **Wizara / Idara Zinazojitegemea** | Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya kila mara na kutoa taarifa kulingana na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini; kuandaa na kuingiza taarifa za utekekelezaji na ufuatiliajina tathmini kwenye NPMIS. | Kulingana na mwongozo wa PIMG pamoja na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini. |
| **Sekretarieti za Mikoa** | Kusimamia utekelezaji wa mipango ya ufuatiliaji na tathmini za halmashauri; kufuatilia utekelezaji wa mpango wa maendeleo katika ngazi ya mkoa na halmashauri; kuandaa taarifa na kuwasilisha OR TAMISEMI. | Kulingana na mwongozo wa PIMG pamoja na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini |
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | Kusimamia utekelezaji wa mipango ya ufuatiliaji na tathmini; kufanya ufuatiliajina tathmini; Kutoa taarifa za utekelezaji wa mpango pamoja na miradi katika ngazi halmashauri kwenye mfumo wa NPMIS. | Kulingana na mwongozo wa PIMG pamoja na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tath;...........mini. |
| **Wakala na** | Kusimamia utekelezaji wa mipango | Kulingana na mwongozo |

| | | |
|---|---|---|
| **Mashirika ya Umma** | ya ufuatiliaji na tathmini; kufanya ufuatiliajina tathmini; Kutoa taarifa za utekelezaji wa mpango pamoja na miradi katika ngazi taasisi kwenye mfumo wa NPMIS. | wa PIMG pamoja na mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini. |
| **Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia** | Kushirikiana na Serikali katika kusimamia na kutoa taarifa sahihi wakati wa ufuatiliaji na tathmini; kuwasilisha maoni na ushauri wao moja kwa moja Tume ya Taifa ya Mipango ili kusaidia kuboresha utekelezaji wa mpango wa maendeleo | Inapohitajika. |

# SURA YA SABA

# VIHATARISHI VYA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27

## 7.1 Utangulizi

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 yatazingatia kubainisha vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wake, pamoja na kuainisha mikakati madhubuti ya kupunguza au kudhibiti vihatarishi hivyo. Lengo kuu ni kuhakikisha ustahimilivu, ufanisi, na uendelevu katika utekelezaji wa malengo na matokeo yaliyopangwa. Aidha, zoezi la utambuzi wa vihatarishi litatekelezwa kwa kuzingatia *Mwongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma, 2023*.

## 7.2 Aina ya Vihatarishi

Mpango utazingatia aina zifuatazo za vihatarishi:

i. Vihatarishi vya Kifedha na Uchumi ambavyo ni pamoja na mabadiliko yasiyotabirika ya uchumi wa dunia, mabadiliko ya ghafla ya viwango vya riba na ubadilishaji wa fedha za kigeni, na misukumo ya bei za bidhaa za msingi katika soko la kimataifa;
ii. Vihatarishi vya Kiutawala, ikijumuisha, uwiano hafifu na ukosefu wa nidhamu katika utekelezaji wa miradi; mifumo dhaifu ya ufuatiliaji, udhibiti na uwajibikaji; uhaba wa rasilimali watu wenye ujuzi na ustadi unaohitajika; na mapungufu katika utawala bora; na
iii. Vihatarishi vya Mazingira na Tabianchi, ambavyo vinajumuisha mabadiliko ya hali ya hewa, ukame, mafuriko, na matukio mengine ya asili yanayoweza kuathiri utekelezaji wa miradi.

Aidha, vihatarishi vitagawanywa katika makundi mbalimbali — vya kimkakati, kitaasisi, kiutendaji, kimazingira, kijamii na kiteknolojia — ili kurahisisha uratibu wa hatua za udhibiti katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali (MDAs), Sekretarieti za Mikoa (RSs), na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs).

## 7.3 Mikakati ya Kudhibiti Vihatarishi

Katika maandalizi ya Mpango, Sekta zitaelekezwa kubainisha mikakati ya kudhibiti vihatarishi kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

i. Kuhakikisha vipaumbele vinaandaliwa kwa kuzingatia DIRA 2050, Mpango wa Nne wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP IV) 2026/27–2030/31, na mikakati ya kisekta iliyoidhinishwa;
ii. Kudhibiti matumizi na kuimarisha akiba ya fedha za kigeni;
iii. Kuanzisha na kuimarisha mfumo wa uwajibikaji wa kisheria na kitaasisi;
iv. Kuongeza nidhamu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
v. Kuimarisha mazingira wezeshi kwa Sekta binafsi na Mashirika ya Umma katika kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
vi. Kuimarisha ufuatiliaji, udhibiti na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji;

vii. Kuimarisha utayari wa kukabili majanga na misukumo ya kiuchumi au kimazingira;
viii. Kuendelea kutunga na kusimamia sera thabiti za kifedha;
ix. Kuendeleza ubunifu na matumizi ya teknolojia mpya;
x. Kukuza ujuzi wa kidijitali na uongozi wa kiteknolojia katika taasisi za umma; na
xi. Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

### 7.4 Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi.

Ili kuhakikisha usimamizi endelevu na ufuatiliaji wa vihatarishi, maandalizi na utekelezaji wa Mpango yataimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi kwa kuchukua hatua zifuatazo:

i. Kufanya mapitio ya vihatarishi kila robo mwaka kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi (NPMIS);
ii. Kuandaa dashboards za ufuatiliaji kwa wakati ili kuwezesha maamuzi sahihi na ya haraka; na
iii. Kutoa mafunzo ya usimamizi wa vihatarishi kwa watendaji wa MDAs, RSs na LGAs, ambao ni watekelezaji wakuu wa miradi ya maendeleo

**Kiambatisho Na. 1:** Mwenendo wa Viashiria vilivyotumika katika Upimaji wa Utekelezaji Wa Mpango kwa kipindi cha Miaka Mitano.

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 1 | Ujenzi | Miundombinu (Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa | 0 | | | 60 | 55 | 50 | 45 | 111 |
| 2 | | Kiwango cha wastani wa ukuaji (%) | 9 | 9.1 | 4.3 | 4.4 | 3.9 | 4.1 | 9.9 | 100 |
| 3 | | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 13.9 | 14 | 13.8 | 14 | 14.1 | 12.8 | 16.7 | 100 |
| 4 | | Mchango wa Kampuni za Ndani katika Soko la Ujenzi (%) | 35 | 35 | 35 | 35 | 35 | 40 | 60 | 20 |
| 5 | | Idadi ya Ajira zilizozalishwa katika Miradi ya Maendeleo | 23,585 | 11,862 | 24,007 | 47,617 | 26,367 | 21,527 | 30,155 | -31 |
| 6 | | Nafasi ya barabara katika mpangilio wa kimataifa | 86 | | | 42 | 39 | 27 | 26 | 98 |
| 7 | Uchukuzi | Nafasi ya reli katika mpangilio wa kidunia | 83 | 83 | 83 | 78 | 58 | 58 | 70 | 192 |
| 8 | | Urefu wa reli ya kati kwa kiwango cha Standard Gauge (SGR) kwa kilometa | 395.2 | 451.43 | 487.9 | 553.03 | 625.84 | 780.38 | 1,219 | 47 |
| 9 | | Kiasi cha shehena kinachosafirishwa na reli (tani) | 1,569,536 | 2,374,969 | 3,217,620 | 3,941,229 | 4,541,731 | 4,788,764 | 5,162,258 | 90 |
| 10 | | Idadi ya abiria wanaosafirishwa na reli | 972,000 | 1,250,373 | 1,143,787 | 1,394,058 | 1,213,225 | 1,931,045 | 2,272,682 | 74 |
| 11 | | Muda wa meli kurejea kituoni kwake (siku) | 3 | 8.8 | 9.7 | 8.7 | 13.1 | 11.2 | 8 | 164 |
| 12 | | Idadi ya meli zinazoingia bandarini kwa mwezi | 210 | 353 | 391 | | | 411 | 254 | 457 |
| 13 | | Muda wa makasha kukaa bandarini (siku) | 7 | 7 | 9 | 9.2 | 6.7 | 5.3 | 5 | 85 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 14 | | Muda wa meli kukaa bandarini (siku) | 2 | 3.7 | 4.6 | 4.4 | 4.1 | 3.7 | 2 | -85 |
| 15 | | Idadi ya bandari kavu | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 3 | 0 |
| 16 | | Idadi ya meli zinazohudumiwa | 3,704 | 4,241 | 4,686 | 5,675 | 4,487 | 2,471 | 4,000 | -417 |
| 17 | | Mizigo inayotoka nje kuelekea nchi za jirani (tani milioni) | 15 | 17.2 | 19.9 | 22.6 | 30.1 | 34.7 | 18 | 676 |
| 18 | | Mizigo ya kwenda nje toka kwa nchi jirani (tani milioni) | 6.3 | 9.8 | 14.9 | 20.6 | 26.8 | 27.9 | 10 | 584 |
| 19 | | Idadi ya ndege zilizonunuliwa | 11 | 11 | 11 | 13 | 15 | 16 | 19 | 63 |
| 20 | | Idadi ya ndege za mizigo zilizonunuliwa | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 100 |
| 21 | | Idadi ya ndege za abiria za masafa marefu zilizonunuliwa | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 3 | 3 | 100 |
| 22 | | Idadi ya ndege za abiria za masafa ya kati (kanda) zilizonunuliwa | 2 | 2 | 4 | 4 | 6 | 6 | 8 | 67 |
| 23 | | Idadi ya ndege za ATCL zinazofanya kazi | 10 | 10 | 12 | 13 | 14 | 15 | 19 | 56 |
| 24 | | Idadi ya wanaanga waliofunzwa | 61 | 99 | 279 | 320 | 567 | 1,088 | 1,359 | 79 |
| 25 | | Idadi ya Viwanja vya ndege vyenye mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege (AMIS) | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 10 | 14 | 69 |
| 26 | | Idadi ya mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege (X-ray machines) | 46 | 80 | 83 | 83 | 85 | 101 | 71 | 220 |
| 27 | | Viwanja vya ndege vyenye uzio kuzunguka kiwanja | 9 | 9 | 11 | 16 | 16 | 18 | 27 | 50 |
| 28 | | Idadi ya rada za hali ya hewa zilizonunuliwa | 5 | 3 | 5 | 5 | 5 | 7 | 7 | 100 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 29 | Nishati | Uzalishaji wa Umeme (MW) | 1,602.30 | 1,605.86 | 1,694.55 | 1,872.05 | 2,138 | 4,031.00 | 4,915 | 73 |
| 30 | | Idadi ya Mikoa Iliyounganishwa na Gridi | 23 | 23 | 23 | 24 | 24 | 24 | 26 | 33 |
| 31 | | Urefu wa Gridi ya Taifa (km) | 5,896.30 | 6,423.53 | 6,423.53 | 6,363.27 | 7,745 | 8625.4 | 9,351 | 79 |
| 32 | | Kupungua kwa Upotevu wa Umeme (%) | 16.19 | 15.16 | 14.71 | 14.62 | 14.56 | 12.3 | 7.9 | 47 |
| 33 | | Asilimia ya Watu waliofikiwa na Umeme | 78.5 | - | - | - | - | 78.4 | 85 | -2 |
| 34 | Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | Uwiano wa watumiaji wa intaneti nchini (%) | 47 | 49 | 48 | 54 | 59.3 | 74.3 | 80 | 84 |
| 35 | | Idadi ya Majengo yenye Anwani za Makazi | 450,980 | - | - | 18,000,000 | 18,000,000 | 18,186,000 | 18,250,000 | 99.6 |
| 36 | | Idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi (Milioni) | 26.7 | 29,5 | 31.2 | 75.2 | 80.8 | 81.2 | 83.9 | 95.3 |
| 37 | | Idadi ya Anwani zilizosajiliwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi | | - | - | 12,385,956 | 12, 891,392 | 13,200,000 | 15,231,392 | 87 |
| 38 | | Idadi ya Huduma zilizosajiliwa kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi | | - | - | 800,000 | 831,436 | 1,000,000 | 1,100,000 | 91 |
| 39 | | Idadi ya Barua za Utambulisho zilizotolewa kupitia Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi | | - | - | 800 | 848 | 15,000 | 15,500 | 97 |
| 40 | | Uwiano wa watu waliofikiwa na mitandao ya simu za mikononi (%) | 94 | - | | | 98 | 94 | 100 | 0 |
| 41 | | Kaya zenye angalau mwenye mwanakaya mmoja anayemilik simu ya mkononi (%) | 82.7 | | | | 98 | 87.6 | 87.8 | 96 |
| 42 | Kilimo | Hekta za Umwagiliwa | 694,715 | 695,005 | 695,005 | 727,280.6 | 727,280.6 | 727,280.60 | 1,200,000 | 6 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| | | | | | | | | | | |
| 43 | | Mbegu zilizoidhinishwa na zilizozalishwa | 76,285.56 | 44,581.08 | 50,747 | 58,807.61 | 71,356 | 44,630.74 | 1,040,000 | -3 |
| 44 | | Akiba ya taifa ya chakula (tani) | 52,724.73 | 107,384.06 | 141,575.902 | 46,893.983 | 785,003.02 | 662,151.27 | 1,140,000 | 56 |
| 45 | | Kiasi cha mazao ya bustani yaliyozalishwa (tani) | 6,597,863 | 7,304,723 | 7,304,723 | 7,723,116 | 7,518,560.84 | 7,518,560.83 | 14,600,000 | 12 |
| 46 | | Kiasi cha uzalishaji wa mazao ya biashara ya asili (traditional)(tani). | 1,144,631 | 898,967 | 898,967 | 973,436 | 1,201,832.65 | 1,300,000 | 1,583,200 | 35 |
| 47 | | Idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika | 113 | 183 | 267 | 267 | 267 | 329 | 338 | 96 |
| 48 | | Idadi ya vyama vya ushirika vinavotumia mfumo wa soko rasmi | 1202 | 1302 | 1402 | 1573 | 2,231 | 4,060 | 2,782 | 181 |
| 49 | | Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika (milioni) | 4.2 | 4.5 | 5.1 | 6.2 | 6.9 | 8.4 | 14.5 | 41 |
| 50 | Mifugo | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 4.9 | 5 | 5 | 5 | 5 | 5.5 | 6.5 | 38 |
| 51 | | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 6.4 | 7.1 | 7.2 | 6.7 | 6.2 | 6.2 | 7 | -33 |
| 52 | | Kiwango cha Vifo vya Mifugo (%) | 27 | 24 | 21 | 18 | 16 | 16 | 12 | 73 |
| 53 | | Kiwango cha Magonjwa ya Mifugo (%) | 6 | 5 | 4.5 | 3.5 | 2.5 | 2.5 | 3 | 117 |
| 54 | | Kiwango cha Uogeshaji Mifugo katika josho (%) | 70 | 72 | 74 | 75 | 78 | 82 | 85 | 80 |
| 55 | | Kiwango cha Chanjo ya Mifugo (%) | 25 | 37 | 39.5 | 40 | 42 | 42 | 50 | 68 |
| 56 | | Wastani wa uzalishaji maziwa, Ng'ombe wa Asili (Lita) | 2 | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.8 | 0.85 | 4 | -58 |
| 57 | | Ngozi bora iliyochakatwa (%) | 10 | 15 | 20 | 25 | 30 | 40 | 50 | 75 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 58 | | Uzalishaji wa Nyama (Tani) | 702,000 | 738,165.99 | 769,966.65 | 803,264.30 | 963,856.55 | 1,124,449 | 951,700 | 169 |
| 59 | | Uzalishaji wa Maziwa katika (Lita bilioni) | 3.01 | 3.1 | 3.4 | 3.6 | 3.97 | 4.1 | 4.3 | 84 |
| 60 | | Asilimia ya Maziwa yaliyochakatwa | 5 | 2 | 2 | 2 | 2.2 | 2.2 | 14 | -31 |
| 61 | | Ngozi na ngozi Zilizochakatwa (Tani) | 1,190 | 143 | 146 | 2,250 | 2,385 | 2,900 | 9,210.60 | 21 |
| 62 | | Mauzo ya nyama nje ya nchi (Tani) | 692 | 1,774.00 | 10,415.00 | 12,243.79 | 14,701.10 | 14,900 | 7,200 | 218 |
| 63 | | Usafirishaji wa Ngozi (Tani) | 6,747 | 7,951 | 7,371 | 4,491 | 5,778 | 7,200 | 8,000 | 36 |
| 64 | Uvuvi | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 6.3 | 6.7 | 2.6 | 1.9 | 1.4 | 4.5 | 8.4 | -86 |
| 65 | | Asilimia katika Pato la Taifa (Bei za sasa) | 1.8 | 1.7 | 1.8 | 1.8 | 1.7 | 1.9 | 1.9 | 100 |
| 66 | | Asilimia katika Mapato yatokanayo na Mauzo Nje | 3 | 3.4 | 3.2 | 3.3 | 3.4 | 3 | 4.5 | 0 |
| 67 | | Ulaji kwa kila Mtu | 8.5 | 7.8 | 8.22 | 7.8 | 7.9 | 8.5 | 10.5 | 0 |
| 68 | | Mchango katika Ulaji wa Protini ya Wanyama Kitaifa | 30 | 30 | 30 | 30 | 30 | 33 | 35 | 60 |
| 69 | | Uzalishaji wa samaki (tani) | 497,567.28 | 493,850.24 | 502,305.34 | 513,218.90 | 530,379.66 | 575,000 | 600,000 | 76 |
| 70 | | Idadi ya viwanda vya kusindika samaki | 12 | 15 | 17 | 20 | 21 | 21 | 17 | 180 |
| 71 | | Idadi ya vituo vya Ukuzaji Viumbe Maji (Aquaculture Development Centres - ADC) | 9 | 9 | 9 | 9 | 9 | 12 | 12 | 100 |
| 72 | | Uzalishaji wa chakula cha samaki (tani) | 276.7 | 472.47 | 1,615.50 | 3,012.70 | 3,455.40 | 5,000 | 8,000 | 61 |
| 73 | | Idadi ya Maafisa Ugani wa Uvuvi | 657 | 657 | 657 | 657 | 657 | 700 | 1,850 | 4 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 74 | Viwanda na Biashara | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 8.2 | 8.4 | 7.8 | 7.1 | 7 | 8.5 | 8.5 | 100 |
| 75 | | Kiwango cha ukuaji halisi wa Pato la Taifa (%) | 5.2 | 4.7 | 4.5 | 4.2 | 4.3 | 6.8 | 6.8 | 100 |
| 76 | | Mchango katika Ajira Zote (%) | 7.4 | 8.5 | 8 | 8 | 8.1 | 12.8 | 12.8 | 100 |
| 77 | | Mchango katika Mapato ya Mauzo Nje (%) | 17.1 | 17.7 | 22.9 | 26.9 | 17.7 | 19 | 19 | 100 |
| 78 | | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya kati katika mauzo nje (%) | 28 | 29.2 | 21.1 | 0 | 25 | 36 | 39 | 73 |
| 79 | | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje (%) | 8 | 8.8 | 8.9 | 0 | 25 | 42 | 10 | 1700 |
| 80 | | Mchango katika Mauzo yote nje (%) | 16.9 | 17.7 | 22.9 | 26.9 | 21.6 | 39 | 24 | 311 |
| 81 | Madini | Wastani wa Ukuaji (%) | 17.7 | 7.3 | 9.4 | 10.8 | 11.3 | 8.3 | 11.6 | 154 |
| 82 | | Mchango kwenye Pato la Taifa (%) | 5.3 | 6.8 | 7.3 | 9.0 | 9.1 | 10.1 | 11.2 | 81 |
| 83 | | Jumla ya Mapato ya Fedha za Nje (Dola za Marekani milioni) | 2,326.7 | 3,375 | 3,116.4 | 3,395.30 | 3,551.40 | 4,119.9 | 3,760.40 | 125 |
| 84 | | Mauzo ghafi nje (%) | 15 | 15 | 1.6 | 0.45 | 9 | 9 | 7 | 75 |
| 85 | | Bidhaa zilizoongezwa thamani (%) | | | | | | 93 | 95 | 98 |
| 86 | | Mchango katika mapato yote ya fedha za nje yatokanayo na mauzo ya bidhaa nje (%) | 61.4 | 64.2 | 54.1 | 56 | 56.2 | 57.1 | 51.7 | 44 |
| 87 | Utalii | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 17.5 | 14.9 | 10.1 | 13 | 17.2 | 17.5 | 18.9 | 0 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 88 | | Idadi ya Watalii kutoka nje ya nchi | 1,527,230 | 620,867 | 922,692 | 1,454,920 | 1,808,205 | 2,141,895 | 5,000,000 | 18 |
| 89 | | Idadi ya Watalii ndani ya nchi | 959,831 | 788,933 | 2,363,260 | 1,084,737 | 1,976,009 | 2,102,371 | | -119 |
| 90 | | Wastani wa idadi ya siku za kulala mtalii. | 13 | 10 | 10 | 9 | 10 | 10 | 14 | -300 |
| | | Wastani wa Matumizi ya Mtalii kwa Siku (USD) | 0 | 321 | 364 | 367 | 419 | 416 | 260 | 160 |
| 91 | | | | 115 | 141 | 166 | 178 | 172 | 260 | 66 |
| 92 | | Mchango katika Mapato ya Fedha za Kigeni (%) | 25 | 5.3 | 21 | 25 | 25 | 26 | 26 | 100 |
| 93 | | Mapato yatokanayo na Watalii (Dola za Marekani bilioni) | 2.6 | 0.7 | 1.3 | 2.5 | 3.9 | 4.1 | 3.9 | 115 |
| 94 | Michezo | Idadi ya miundombinu ya michezo na iliyoboreshwa nchini kote | 63 | 64 | 64 | 66 | 68 | 174 | 72 | 1233 |
| 95 | | Idadi ya miundombinu iliyojengwa/kukarabatiwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamaoyo (TaSUBa). | 35 | 48 | 50 | 52 | 53 | 58 | 40 | 460 |
| 96 | | Idadi ya filamu na muziki zilizoidhinishwa, kusambazwa na kutumika | 15,303 | 2,962 | 3,763 | 3,201 | 4,070 | 4,342 | 25,735 | -105 |
| 97 | | Idadi ya wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu | 3,462 | 3,931 | 4,299 | 5,254 | 6,473 | 7310 | 8,666 | 74 |
| 98 | | Idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo | 2,852 | 450 | 442 | 500 | 10,837 | 11,500 | 4,297 | 598 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 99 | | Idadi ya michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa na Tanzania kushiriki | 178 | 0 | 98 | 135 | 157 | 110 | 350 | -40 |
| 100 | | Idadi ya vibali vilivyotolewa kwa vyama vya michezo na wanamichezo binafsi | 178 | 0 | 57 | 45 | 194 | 110 | 400 | -31 |
| 101 | | Idadi ya wanariadha wanaocheza nje ya nchi | 54 | - | 21 | 31 | 17 | 62 | 150 | 8 |
| 102 | | Idadi ya wageni wanaoendesha shughuli za kuzalisha filamu nchini Tanzania. | 359 | 60 | 87 | 100 | 64 | 70 | 1,059 | -41 |
| 103 | | Idadi ya wasanii/wataalamu katika tasnia ya ubunifu/makundi yanayofanya maonesho yao nje ya nchi | 1,620 | 330 | 430 | 461 | 467 | 61 | 1,755 | -1155 |
| 104 | | Idadi ya wasanii wa nje/wataalamu katika tasnia ya ubunifu wanaofanya maonesho yao nchini Tanzania | 720 | 142 | 153 | 162 | 167 | 2 | 2,312 | -45 |
| 105 | | Idadi ya wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania | 56 | 64 | 71 | 95 | 111 | 384 | 656 | 55 |
| 106 | | Idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi | 200 | 252 | 2189 | 1640 | 242 | 502 | 700 | 60 |
| 107 | | Idadi ya tuzo za kimataifa zilizoandaliwa na kutolewa kwenye utamaduni, sanaa na tasnia ya ubunifu | 47 | 38 | 41 | 188 | 62 | 68 | 130 | 25 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 108 | | Idadi ya vikundi vya utamaduni na sanaa kutoka nje ya nchi vilivyoshiriki katika matamasha ya Kimataifa yanayoandaliwa kila mwaka na TaSUBa. | 5 | 4 | 4 | 6 | 23 | 11 | 20 | 40 |
| 109 | | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya | 300 | 439 | 533 | 684 | 758 | 503 | 1,300 | 20 |
| 110 | | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa TaSUBa | 350 | 439 | 533 | 684 | 758 | 947 | 1,200 | 70 |
| 111 | | Idadi ya wilaya zinazofikiwa na matangazo ya TBC (TBCFM na TBCTaifa) | 102 | 119 | 121 | 134 | 137 | 138 | 139 | 97 |
| 112 | Uwekezaji | Idadi ya Miradi ya Uwekezaji iliyosajiliwa na TIC na EPZA | 227 | 251 | 290 | 385 | 723 | 640 | 600 | 111 |
| 113 | | Thamani ya Miradi ya Uwekezaji (Dola za Marekani) | 1760.2 | 3404.6 | 2351.34 | 5497.61 | 6663.87 | 8,813 | 8,500 | 105 |
| 114 | | Idadi ya Ajira kutokana na Miradi ya Uwekezaji | 33509 | 39170 | 46246 | 56192 | 228906 | 280,000 | 250,000 | 114 |
| 115 | | Idadi ya Kongano za Uwekezaji | 10 | 12 | 13 | 14 | 27 | 21 | 5 | -220 |
| 116 | | Idadi ya Miongozo ya Uwekezaji ya Mikoa (Kila mkoa) | 13 | 7 | 0 | 2 | 0 | 26 | 26 | 100 |
| 117 | | Idadi ya Ofisi za Utoaji Huduma Mahala Pamoja | 11 | 13 | 13 | 13 | 14 | 15 | 18 | 57 |
| 118 | | Kiasi cha Ardhi ya Uwekezaji iliyotengwa (ekari) | 90,990 | 98,861 | 99,735 | 159,813 | 214,972.94 | 391,030.94 | 528917 | 69 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 119 | | Idadi ya Makongamano ya Uwekezaji Kimataifa | 21 | 49 | 63 | 89 | 204 | 180 | 150 | 123 |
| 120 | | Idadi ya Maboresho ya sheria na kanuni za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | | 35 | 42 | 55 | 66 | 80 | 88 | 91 |
| 121 | | Idadi ya maboresho ya kufuta au kupunguza tozo, ada na ushuru katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji yaliyofanywa | | 218 | 232 | 307 | 374 | 383 | 388 | 99 |
| 122 | Mambo ya nje | Idadi ya mikutano kati ya Tanzania na nchi moja moja, ya kikanda na kimataifa iliyoshiriki | 30 | 32 | 80 | 90 | 101 | 110 | 250 | 36 |
| 123 | | Idadi ya watanzania walioshiriki katika ulinzi wa amani nje ya nchi | 0 | 0 | 1401 | 1401 | 1532 | 1500 | 3,500 | 43 |
| 124 | | Idadi ya ofisi na nyumba za kuishi zilizokarabatiwa | 0 | 4 | 4 | 4 | 4 | 4 | 14 | 29 |
| 125 | | Idadi ya Hati za Makubaliano ya Pamoja zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine | 12 | 32 | 33 | 66 | 78 | 84 | 80 | 106 |
| 126 | Elimu | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 38.7 | 35.9 | 34.2 | 37.4 | 40.5 | 51.2 | 51 | 80 |
| 127 | | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu mwenye sifa | 0.145139 | 0.131944 | 0.127083 | 0.122917 | 0.129861 | 0.146528 | 0.106944 | 1:50 |
| 128 | | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 110.6 | 110.6 | 109.7 | 108.5 | 98.2 | 84.2 | 80.6 | 283 |
| 129 | | Kiwango cha uandikishaji wa rika lengwa | 95.7 | 95.7 | 95.3 | 94.4 | 86 | 79.6 | 76.8 | -439.5 |
| 130 | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya msingi kwa Mwalimu | 1:54 | 1:51 | 1:56 | 1:57 | 1:55 | 1:56 | 1:55 | -25 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 131 | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi kwa Kitabu | 1:04 | 1:03 | 1:02 | 1:02 | 1:02 | 1:02 | 1:02 | 66.7 |
| 132 | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi kwa Darasa | 0.09375 | 0.09375 | 0.093056 | 0.090278 | 0.088889 | 0.085417 | 0.084722 | 86.7 |
| 133 | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Kiume kwa Tundu la Choo | 1:54 | 1:54 | 1:51 | 1:52 | 1:46 | 1:43 | 1:40 | 50.1 |
| 134 | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Kike kwa Tundu la Choo | 1:51 | 1:51 | 1:48 | 1:48 | 1:43 | 1:47 | 1:39 | 33.7 |
| 135 | | Uwiano wa Idadi ya wanafunzi kwa Dawati | 1:04 | 1:04 | 1:04 | 1:04 | 1:04 | 1:04 | 1:04 | 100 |
| 136 | | Asilimia ya Shule za msingi zenye umeme | 43.5 | 42.2 | 48.8 | 56 | 61.9 | 68 | 73.5 | 181.8 |
| 138 | | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) | 46 | 46 | 47.4 | 48.2 | 52.7 | 51.7 | 53.1 | 48 |
| 139 | | Asilimia ya Uandikishaji wa Watoto Wenye Umri wa Rika lengwa Ikilinganishwa na idadi ya watoto wote wenye umri wa kwenda shule | 36 | 36 | 37 | 38.3 | 41.8 | 40.6 | 40 | 42 |
| 140 | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Sekondari kwa Mwalimu | 23:01 | 23:01 | 24:01 | 25:01 | 26:01 | 26:01 | 20:01 | -100 |
| 141 | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Sekondari kwa Darasa | 1:41 | 1:40 | 1:42 | 1:36 | 1:37 | 1:34 | 1:34 | 100 |
| 142 | | Uwiano wa Idadi ya Wanafunzi wa Sekondari kwa Tundu la Choo | 1:27 | 1:20 | 1:27 | 1:28 | 1:34 | 1:28 | 1:26 | -100 |
| 143 | | Asilimia ya Shule za Sekondari Zenye Umeme | 69.8 | 69.8 | 73.9 | 77.2 | 77.5 | 81.4 | 97.8 | 85 |
| 144 | | Asilimia ya kundirika la wanafunzi waliofaulu mtihani wa Elimu ya Sekondari ya Chini | 80.65 | 85.84 | 87.3 | 87.79 | 89.37 | NA | 90 | 90 |
| 145 | | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya | 6.9 | 6.9 | 6.7 | 7.6 | 7.7 | 9.1 | 9.8 | 75 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| | | Wanaostahili) | | | | | | | | |
| 146 | | Kiwango cha uandikishaji rika lengwa (% ya wanaostahili) | 3.3 | 3.3 | 3.4 | 4 | 4.1 | 5.2 | 6.7 | 55.9 |
| 147 | | Uandikishaji halisi wa wanafunzi wa kiume (%) | 3.3 | 3.3 | 3.4 | 3.9 | 4.1 | 5 | 6.3 | 56.7 |
| 148 | | Uandikishaji halisi wa wanafunzi wa kike (%) | 3.2 | 3.2 | 3.4 | 4.1 | 4.1 | 5.4 | 7.1 | 56.4 |
| 149 | | Asilimia ya wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kidato cha VI | 99.51 | 99.5 | 99.6 | 99.9 | 99.9 | 99.9 | n/a | 100 |
| 150 | | Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo ya elimu ya juu | 132,392 | 145,000 | 149,472 | 177,925 | 197,469 | 227,998 | 248,331 | 82.4 |
| 151 | | Idadi ya wahitimu wa vyuo vikuu | 60,940 | 48,621 | 54,810 | 57,742 | 56,520 | 62,570 | N/A | 17.8 |
| 152 | | Idadi ya wahitimu kwa wanafunzi wa kiume | 34,513 | 34,513 | 29,780 | 30,375 | 27,574 | 31,919 | N/A | -50.1 |
| 153 | | Idadi ya wahitimu kwa wanafunzi wa kike | 26,427 | 26,427 | 25,030 | 27,367 | 28,946 | 30,651 | N/A | 23.1 |
| 154 | | Kiwango cha udahili jumla (%) | 4.5 | 5.8 | 7.4 | 6.9 | 8 | 8 | 6 | 233 |
| 155 | | Idadi ya wanafunzi wanaohitimu kwa mwaka | 86,547 | 146,671 | 154,800 | 140,014 | 89,967 | 89967 | 120,000 | 10.2 |
| 156 | | Asilimia ya wanafunzi wanaohitimu masomo ya sayansi na uhandisi kwa mwaka | 36 | 18.1 | 17.3 | 16.2 | 17.2 | 17.2 | 40 | -470 |
| 157 | | Asilimia ya Wanafunzi wa kike wanaohitimu kwa mwaka | 42 | 32.6 | 33.2 | 33.21 | 35.7 | | 43 | -630 |
| 158 | Afya | Idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 | 26 | 25 | 24 | 24 | 24 | 24 | 15 | 18 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 159 | | Idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1000 | 81 | 67 | 43 | 43 | 43 | 43 | 40 | 93 |
| 160 | | Uzazi uliohudumiwa na mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi | 80 | 92.3 | 93.6 | 94.4 | 94.6 | 94.7 | 85 | 294 |
| 161 | | Wastani wa umri wa kuishi (miaka) | 66.1 | 66.7 | 65.4 | 67.6 | 67.8 | 68 | 68 | 100 |
| 162 | | Kiwango cha maambukizi ya VVU kitaifa (%) | 4.7 | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 4.4 | 4.4 | 3.1 | 19 |
| 163 | | Matumizi ya Serikali katika huduma za afya (%) | 10 | 10.6 | 10 | 9 | 9.1 | 10.3 | 12.2 | 14 |
| 164 | | Idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa kila vizazi hai 100,000 | 454 | 530 | 220 | 220 | 104 | 104 | 180 | 128 |
| 166 | Maji | Asilimia ya idadi ya watu wa vijijini wanaopata maji ya bomba au maji yalivyolindwa kama chanzo kikuu | 70 | 72.3 | 74.5 | 77 | 79.6 | 83 | 85 | 87 |
| 167 | | Uwiano wa kaya za vijijini zenye miundombinu iliyoboreshwa ya usafi wa mazingira | 36 | 47.3 | 60.4 | 73.5 | 77.5 | 78.5 | 60 | 177 |
| 168 | | Asilimia ya watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba au maji yaliyolindwa | 84 | 85 | 86.5 | 88 | 90 | 91.6 | 95 | 69 |
| 169 | | Asilimia ya kaya katika makao makuu ya mikoa iliyounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 13 | 11 | 13 | 13 | 14 | 13 | 30 | 0 |
| 170 | | Asilimia ya upotevu wa maji (NRW) katika makao makuu ya mikoa | 30 | 36.8 | 35.7 | 35.3 | 35.3 | 33.4 | 20 | -34 |
| 171 | | Asilimia ya watu katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 70 | 67 | 72 | 73.4 | 74.5 | 74.5 | 85 | 30 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 172 | | Asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu | 85 | 87 | 89 | 90 | 92.5 | 93 | 95 | 80 |
| 173 | | Asilimia ya kaya katika jiji la Dar es Salaam waliounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 13 | 13 | 11 | 13 | 12.4 | 13 | 30 | 0 |
| 174 | | Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) katika jiji la Dar es Salaam | 35 | 38.3 | 39.2 | 41.5 | 39.5 | 43.2 | 20 | -55 |
| 175 | | Idadi ya vyanzo vya maji vilivyotengwa na kutangazwa kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi | 18 | 18 | 34 | 34 | 59 | 68 | 80 | 81 |
| 176 | Ardhi nyumba na maendeleo ya makazi | Idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi | 1,496,357 | 1,754,822 | 2,207,627 | 2,469,686 | 2,602,711 | 3,102,715 | 3,402,715 | 84 |
| 177 | | Asilimia ya eneo la ardhi yenye makazi yasiyo rasmi | 70 | 70 | 69 | 67.3 | 67.3 | 67.3 | 60 | 27 |
| 178 | | Eneo la ardhi lilitengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma (ekari) | 858,665 | 858,665 | 858,665 | 865,337 | 870,437 | 874,937 | 1,452,415 | 3 |
| 179 | | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa | 24 | 25 | 27 | 28 | 28 | 28 | 54 | 13 |
| 180 | | Idadi ya viwanja vilivyotengwa | 1,551,716 | 2,015,532 | 2,391,366 | 2,706,343 | 2,967,753 | 3,097,455 | 4,051,716 | 62 |
| 181 | | Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo | 1 | 19 | 62 | 84 | 86 | 88 | 26 | 348 |
| 182 | | Uwiano wa vijiji vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi (%) | 19.3 | 19.3 | 20.9 | 23.2 | 33.5 | 34.5 | 52.7 | 46 |
| 183 | | Idadi ya mabaraza ya ardhi yanayofanya kazi | 57 | 68 | 81 | 93 | 105 | 112 | 139 | 67 |
| 184 | | Asilimia ya ardhi iliyopimwa | 25 | 25 | 25 | 25 | 26 | 26 | 37 | 8 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 185 | | Idadi ya leseni za makazi zilizotolewa katika makazi yasiyo rasmi | 1,738 | 1,738 | 23,862 (2021/22) | 23,862 (2021/22) | 23,862 | 23,862 | 20,000 | 121 |
| 186 | | Idadi ya ramani za msingi zilizohuishwa kwa eneo | 1 | 19 | 62 | 84 | 86 | 88 | 26 | 348 |
| 187 | | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa | 24 | 25 | 27 | 28 | 28 | 28 | 54 | 13 |
| 188 | Maendeleo ya jamii | Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa | 1,543 | 1,543 | 2,714 | 3,233 | 4,068 | 4,800 | 7,500 | 55 |
| 189 | | Idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure | 166,866 | 166,866 | 201,509 | 262,513 | 365,284 | 432,642 | 574,321 | 65 |
| 190 | | Idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano | 12,068 | 12,068 | 26,903 | 32,905 | 46,473 | 48,051 | 50,000 | 95 |
| 191 | | Idadi ya watu wenye mafunzo ya uanagenzi | 46,200 | 14,440 | 22,200 | 11,973 | 6,300 | 8,250 | 46,300 | -37950 |
| 192 | | Idadi ya watu wanaotumia teknolojia ya kisasa kwenye kilimo | 40,000 | 8,980 | 4,480 | - | - | 4480 | 41,000 | -3552 |
| 193 | | Idadi ya watu walioshiriki mafunzo ya utarajali (Internship) | 30,000 | 4,118 | 2,490 | 1,888 | 3,085 | 1,861 | 31,000 | -2814 |
| 194 | Utumishi | Idadi ya Watumishi waliopatiwa mafunzo ya maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma | 3,124 | 4,248 | 4,518 | 15,372 | 15,010 | 4,228 | 15,000 | 9 |
| 195 | | Idadi ya taasisi zilizofundishwa matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho (ili kuongeza uwajibikaji na mapambano dhidi ya rushwa katika utumishi wa umma na nchi kwa ujumla) | 0 | 0 | 148 | 100 | 120 | 40 | 121 | 33 |
| 196 | | Kupungua kwa malalamiko yatokanayo na utawala bora na masuala ya utawala bora | 123 | 156 | 158 | 152 | 147 | 138 | 100 | -65 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 197 | Katiba na sheria | Asilimia ya raia wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi | 69 | 77 | 77 | 83 | 83 | 83 | 100 | 45 |
| 198 | | Asilimia ya kesi zilizohudumiwa na watoa msaada wa huduma za kisheria | 0.13 | 8.2 | 11.4 | 13.97 | 13.97 | 15 | 20 | 75 |
| 199 | | Idadi ya IJCs zilizojengwa na zinazofanya kazi katika maeneo yaliyo chaguliwa | 10 | 16 | 19 | 19 | 28 | 28 | 28 | 100 |
| 200 | | Idadi ya majengo ya mahakama ya wilaya yaliyojengwa | 64 | 82 | 94 | 101 | 107 | 114 | 139 | 67 |
| 201 | | Idadi ya majengo ya mahakama ya mwanzo yaliyojengwa | 649 | 656 | 663 | 667 | 668 | 740 | 791 | 64 |
| 202 | | Idadi ya ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizojengwa mikoani | 0 | 0 | 1 | 2 | 5 | 8 | 10 | 80 |
| 203 | | Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa mikoani | 1 | 1 | 1 | 5 | 11 | 15 | 7 | 233 |
| 204 | | Idadi ya ofisi za NPS zilizojengwa wilayani | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 5 | 11 | 40 |
| 205 | | Idadi ya wilaya zenye watoa msaada wa huduma za kisheria waliosajiliwa | | | | | | 116 | 138 | 84 |
| 206 | | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu | 390 | 312 | 166 | 239 | 242 | 78 | 350 | 780 |
| 207 | | Asilimia ya watu walioridhishwa na huduma za mahakama | 78 | 78 | 78 | 88 | 88 | 88 | 80 | 500 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | Utekelezaji wa Shabaha | | | | | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 208 | | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa kesi na kutolewa hukumu katika Mahakama ya Biashara | 480 | 390 | 365 | 324 | 231 | 231 | 350 | 192 |
| 209 | | Asilimia ya mlundikano wa kesi, kwa jumla ya kesi zote zinazosubiri maamuzi | 5 | 13 | 9 | 3 | 5 | 4 | 2 | 33 |
| 210 | Mambo ya Ndani | Kiwango cha kupungua kwa uhalifu nchini (%) | 5.2 | -7.5 | -1.9 | 4.3 | 3.2 | 35 | 35 | 100 |
| 211 | | Idadi ya watu waliosajiliwa na kutambuliwa na NIDA | 22,194,288 | 23,185,729 | 23,965,371 | 24,897,459 | 27,286,749 | 34,080,610 | 34,100,000 | 100 |
| 212 | | Idadi ya kampeni za amani zilizofanyika | 50 | 60 | 70 | 90 | 110 | 130 | 150 | 80 |
| 213 | | Kiwango cha ushiriki wa jamii katika shughuli za usalama (%) | 30 | 35 | 40 | 45 | 50 | 55 | 60 | 83 |
| 214 | | Idadi ya ajira zilizozalishwa katika miradi ya maendeleo | 23,000 | 25,000 | 27,000 | 28,000 | 30,000 | 31,000 | 33,000 | 80 |
| 215 | | Mchango katika ajira (%) | 14.7 | 15.2 | 15.8 | 16.3 | 17.2 | 18.1 | 18.8 | 83 |
| 216 | | Kiwango cha kupungua kwa ajali za barabarani (%) | 45 | 48 | 50 | 52 | 54 | 58 | 60 | 87 |
| 217 | Mazingira | Wastani wa Ukuaji (%) | 4 | 2.7 | 2.6 | 2.7 | 2.5 | 6 | 7 | 67 |
| 218 | | Mchango katika Pato la Taifa kutokana na matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari | 4 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.3 | 6 | 7 | 67 |

| Na. | Sekta | Kiashiria | Kiziomsingi | | | | | Utekelezaji wa Shabaha | Shabaha | Utekelezaji wa Shabaha (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | |
| 219 | | Kiwango cha kupungua kwa uharibifu wa misitu (Reduced Deforestation Rate) (Ha.) | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 469,420 | 234,710 | 0 |
| 220 | | Maeneo ya misitu ya kibishara (commercial forest Plantation) yaliyoanzishwa (Ha) | 500,000 | 507,274 | 507,274 | 507,274 | 507,274 | 550,000 | 550,000 | 100 |
| 221 | | Asilimia ya miradi mikubwa inayokidhi uchambuzi wa athari kwa mazingira (EIA) na kanuni za ukaguzi | 90 | 100 | 100 | 100 | 100 | 93 | 65 | -12 |

**Maelezo**

Utekelezaji wa kiashiria upo juu ya asilimia 60 ya ufikiwaji wa shabaha

Utekelezaji wa kiashiria upo kati ya asilimia 35 na 59 ya ufikiwaji wa shabaha

Utekelezaji wa kiashiria upo chini ya asilimia 35 ya ufikiwaji wa shabaha

Ujazaji wa kiashiria haukufuata mtiririko unaotakiwa au uwekaji wa shabaha haukuzingatia hali halisi

## Kiambatisho Na. 2: Afua za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| **Nguzo 1: Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani** | |
| **1.1.Uchumi Jumla Tulivu na Unaotabirika** | |
| **Lengo 1: Kuwa na uchumi jumla imara kwa ajili ya kukuza uwekezaji na uchumi unaotabirikika.** | |
| 1. Ukuaji wa uchumi kufikia asililimia 6.3 ifikapo 2026/27 | Kutoa vivutio kwa kuzingatia utendaji wa wauza mauzo nje ya nchi, ikiwemo punguzo la ushuru wa umeme kwa viwanda vilivyothibitishwa kuongeza mchango wa ukuaji wa mauzo nje ya nchi kwa kila mwaka. |
| | Kuzindua mpango wa ruzuku ya ulinganifu (matching grant scheme) kwa SMEs na viwanda katika sekta zisizo asilia (mfano. Uchakataji mazao, na huduma za kidijitali) ili kukabiliana na vikwazo vya kuingia sokoni na kuchochea vyanzo vipya vya uchumi. |
| 2. Mfumuko wa bei kuwa ndani ya wigo wa asilimia 3-5 kwa mwaka | Kuimarisha utekelezaji wa sera ya fedha kwa kuidhinisha utaratibu wa kulenga mfumuko wa bei (inflation-targeting). |
| | Kuimarisha usambazaji wa chakula na bei kwa kuongeza uzalishaji, kuboresha mnyororo wa thamani wa kilimo, na kutoa vocha za kidijitali za pembejeo za kilimo kwa wakulima wadogo |
| | Kuweka mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa ufuatiliaji wa bei kufuatilia bei za bidhaa muhimu kwa wakati halisi (real-time) na kuongeza uwazi katika masoko. |
| | Kuwa na akiba ya chakula na mafuta inayotosha matumizi ya angalau miezi sita ili kupunguza athari za mitikisiko ya bei kutoka nje |
| | Kuimairisha uratibu kati sera za fedha na kibajeti kila mwaka ili kuhakikisha ulinganifu na utulivu wa sera. |
| **1.2. Uendelevu na Utabilifu wa Sera za Kibajeti** | |
| **Lengo 1:** Kuweka mfumo endelevu wa sera za kibajeti kwa kuongeza mapato ya ndani, kupunguza hatari ya deni la serikali na kuimarisha matumizi endelevu, kuhakikisha ufadhili wa kutosha wa miundombinu na huduma za jamii kwa kudumisha nidhamu ya fedha. | |
| 1. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kutoka asilimia 16.8 hadi asilimia 17.1 ya Pato la Taifa (GDP). | Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya kodi kwa kutumia mifumo ya kidijitali, ankara za kielektroniki, na teknolojia za kisasa za kikodi. |
| | Kuboresha mifumo ya urasimishaji wa sekta isiyo rasmi kupitia michakato rahisi ya utekelezaji wa kanuni na motisha za kikodi. |
| 2. Kuongezeka kwa makusanyo ya kodi hadi asilimia 13.7 ya Pato la Taifa (GDP) kwa mwaka 2026/27. | Kutekeleza maboresho ya mageuzi ya kikodi na misamaha ya kodi ili kuleta usawa na ufanisi. |
| | Kuimarisha na kuendeleza makubaliano na wadau wa biashara wa kimataifa kwa ajili ya kubadilishana taarifa za kikodi ili kudhibiti mtiririko haramu na ukwepaji kodi katika biashara ya kidijitali. |
| 3. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato yasiyo ya kikodi hadi asilimia 3.4 ya Pato la Taifa (GDP) kwa Mwaka 2026/27. | 3.1 Kufanya mapitio ya kina na kuandaa utaratibu wa ukusanyaji wa vyanzo vikuu vya mapato yasiyo ya kodi |
| | Kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kufanya mapitio ya kina ya mifumo ya udhibiti na kuboresha mifumo kidijitali ili kuongeza ufanisi. |
| | Kuongeza kasi ya upangaji wa ardhi, upimaji na urasimishaji kwa kutumia teknolojia mpya (mfano, picha za satelaiti, ndege zisizo na rubani) ili kuongeza wigo wa mapato yasiyo ya kodi. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 4. Deni la Serikali kuwa ndani ya asilimia 50–55 ya kiwango cha DSA ifikapo Juni 2031. | Kuimarisha mikakati ya usimamizi wa deni la serikali kila mwaka, kwa kulenga mikopo nafuu na kupunguza utegemezi wa mikopo ya kibiashara yenye gharama kubwa. |
| | Kufanya ufuatiliaji wa mapato ya uwekezaji kutokana na fedha za mikopo, unaolenga ukuaji mkubwa na athari za pana katika miradi yote inayofadhiliwa kwa mikopo ili kuhakikisha matumizi yenye tija ya mtaji. |
| 5. Kuhakikisha nakisi ya fedha inakuwa chini ya asilimia 3 ya Pato la Taifa (GDP) kila mwaka. | Kuandaa bajeti kwa kuzingatia matokeo na urasimishaji wa matumizi katika wizara zote za serikali. |
| | Kuimarisha mifumo ya uwajibikaji ya fedha ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya serikali. |
| | Kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Dharura na Mfuko wa kukabiliana na majanga ili kusimamia kikamilifu vihatarishi vya kifedha pale athari zinapojitokeza. |
| 6. Matumizi ya Maendeleo kudumu katika asilimia 31-35 ya matumizi yote ya Serikali. | Kuboresha ufanisi katika manunuzi ya umma na utoaji huduma kupitia mifumo ya kidijitali na kuimarisha matumizi ya migao ya fedha. |
| | ii. Kutumia mifumo ya kidijitali kuboresha ufanisi katika utoaji huduma na matumizi ya fedha. |
| **1.3. Sekta ya Nje iliyo Himilivu na Mseto** | |
| **Lengo 1:** Kukabiliana na athari za nje kwa kuainisha mauzo nje mbalimbali, kupunguza utegemezi wa uagizaji bidhaa nje na kuimarisha mizania ya malipo, hivyo kuongeza biashara inayotabirika na uchumi himilivu. | |
| 1. Kuongezeka kwa mchango wa mauzo nje ya bidhaa za viwandani kutoka asilimia 12 hadi 16.5 ya jumla ya mauzo nje ya bidhaa kufikia Juni 2027. | 1.1 Kutekeleza sera za viwanda zinazochochea ongezeko la thamani katika sekta za kilimo, uchimbaji wa madini na viwanda |
| | i. Kuweka mfumo wa utoaji wa motisha katika biashara za viwandani (mfano, punguzo la kodi, ufadhili nafuu) ili kusaidia ongezeko endelevu la mauzo ya nje ya bidhaa zilizozalishwa viwandani na kusindikwa |
| | ii. Kuwezesha upanuzi wa viwanda vya uzalishaji na usindikaji mazao ya kilimo ili kupunguza mauzo nje ya madini ghafi na rasilimali nyingine muhimu za asili. |
| | iii. Kuwekeza katika miundombinu wezeshi ya biashara, ikiwemo, kuboresha bandari, kuendeleza vituo vya usafirishaji, na kuongeza ufanisi wa forodha |
| 1. Kupungua kwa utegemezi wa uagizaji nje kwa asilimia 4 ifikapo 2026/27 | i. Kuongeza uzalishaji wa pembejeo muhimu na kupanua uwezo wa viwanda vya ndani katika sekta muhimu kama vile dawa, usindikaji mazao ya kilimo, na mavazi kupitia katika viwanda vinavyolengwa na uwekezaji katika Tafiti na Maendeleo (R&D) |
| | ii. Kuanzisha utoaji wa ruzuku kwa viwanda vya kimkakati vilivyolengwa ili kuongeza ushindani na bidhaa zinazoagizwa kila mwaka |
| 2. Nakisi ya Urari wa Malipo kuwa/ sio zaidi ya asilimia 6 ya Pato la Taifa (GDP) | i. Kuboresha ukusanyaji wa akiba ya fedha za kigeni kuweza kukidhi mahitaji ya uagizaji nje wa bidhaa na huduma kwa angalau kipindi cha miezi minne na nusu |
| | ii. Kuhamasisha mauzo nje ya huduma, ikiwemo utalii na huduma za fedha, ili kubainisha vyanzo mbalimbali vya mapato ya fedha za kigeni |
| | iii. Kuimarisha jumuiya za biashara za kikanda ili kupunguza utegemezi kwenye masoko yaliyoendelea na kuongeza uhimilivu wa athari kutoka nje |
| **1. Sekta za Kimageuzi:** | |
| **1.1. Sekta ya Kilimo.** | |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| Lengo 1: Kuwa na biashara ya kilimo cha mazao himilivu na faida kibiashara ili kuchochea ukuaji wa uchumi na maisha vijijini ifikapo mwaka 2050 | |
| 1.1.1. Biashara ya Kilimo cha mazao | |
| 1 Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 7 za juu katika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara (SSA) katika ushindani wa kilimo cha mazao ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuimarisha mamlaka za udhibiti ili kuongeza faida na ushindani katika kilimo cha biashara |
| | Kuimarisha wadhibiti kutekeleza viwango vya kimataifa, na kupunguza bidhaa zilizo kataliwa katika mauzo nje kwa asilimia 50 |
| | i. Kufungamanisha viwango vya mazao vya kitaifa na itifaki za EAC, SADC, na AfCFTA |
| | ii. Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa ufuatiliaji wa mazao kwa ajili ya mauzo ya mazao makuu nje |
| | 1.2 Kufanya mapitio, kurekebisha na kupendekeza sheria mpya ili kuondoa urasimu usio wa lazima na kuboresha urahisi wa kufanya biashara |
| | i. Kufanya ukaguzi wa kisheria wa sheria za biashara na uwekezaji |
| | ii. Kufungaminsha sheria za nchi na mifumo ya AfCFTA, WTO na hali ya hewa (Climate Smart Agriculture - CSA). |
| | 1.3 Kupanua ufadhili (patient finance) kutoka vyanzo vya ndani na kimataifa ili kuboresha upatikanaji wa fedha kwa wakulima wa biashara na wadogo kila mwaka. |
| | i. Kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (ADF) ili kupunguza vihatarishi katika uwekezaji wa muda mrefu wa kilimo kila mwaka |
| | ii. Kuandaa mifumo ya fedha kwa kushirikiana na taasisi za kifedha za ndani ili kuongeza utoaji wa mikopo kwa SME za kilimo na wakulima wadogo kila mwaka. |
| | iii. Kupata mikopo mahsusi yenye riba nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya wakulima wakubwa wa biashara na kilimo biashara kila mwaka |
| | iv. Kuanzisha mpango wa kitaifa wa dhamana ya mikopo ili kufungua upatikanaji wa ufadhili wa benki za biashara kwa wakulima vijana na wanawake kila mwaka |
| | 1.4 Kupanua wigo wa upatikanaji wa ruzuku za serikali na mbinu za kukabiliana na vihatarishi ili kuimarisha usalama wa fedha na kuwawezesha wakulima |
| | i. Kutekeleza mpango mahsusi wa ruzuku kwa pembejeo muhimu za kilimo |
| | ii. Kuanzisha jukwaa la kitaifa la kidijitali la taarifa za masoko ili kutoa taarifa za bei na mahitaji kwa wakati halisi |
| | iii. Kuanzisha utaratibu wa kukabiliana na vihatarishi, ikiwemo kuweka vivutio vya kodi katika ununuzi wa mashine na kuwezesha vituo kwa kukodisha vifaa |
| | iv. Kupanua mbinu za kupunguza vihatarishi vya kifedha ikiwemo kuimarisha matumizi ya bidhaa za bima ya kilimo, dhamana ya mikopo, na mifumo imara ya fedha ya ushirika |
| | v. Kukuza mashamba makubwa (block farming), kuongeza tija, kupunguza gharama za pembejeo, kuboresha miundombinu na huduma ya usafirishaji, na kuimarisha majadiliano kwa kupanga wakulima katika makundi yaliyoratibiwa na yenye ufanisi mkubwa kila mwaka. |
| | 1.5 Kuanzisha mfumo wa kilimo cha mkataba, kuwezesha wakulima binafsi kwa kuwapatia masoko ya uhakika, upatikanaji wa pembejeo bora, msaada wa kiufundi na bei thabiti kupitia makubaliano ya moja kwa moja na wanunuzi kila mwaka |

| Shabaha | Afua |
| --- | --- |
| | i. Kuandaa mfumo wa kawaida wa kilimo cha mkataba ili kulinda wakulima na wanunuzi kila mwaka |
| | 1.6 Kuimarisha mnyororo wa thamani wa pamba kwa kuzalisha nyuzi (lint/fibre), uzi, vitambaa vilivyofumwa (denim, poplin), bidhaa zenye rangi na zilizokamilika, pamoja na nguo (apparel) |
| | i. Kuanzisha msingi wa uzalishaji wa nguo za kisasa, unaotumia nishati kwa ufanisi kuboresha viwanda vya kuchambua pamba (ginneries) na kuanzisha angalau kongano zilizofungamanishwa mbili za viwanda vya nguo. |
| | ii. Kuiwezesha Tanzania kuwa katika nafasi ya kitovu cha ushindani cha kuuza nguo na mavazi nje ya nchi kwa kuweka motisha maalumu ya uwekezaji na kuanzisha kampeni katika masoko ya kimataifa ya Made in Tanzania |
| | iii. Kuzalisha nguvu kazi yenye ujuzi katika sekta ya nguo kwa kutengeneza programu za mafunzo ya ufundi katika usanifu na utengenezaji, na kutoa vyeti kwa vijana na wanawake 5,000 katika ajira za viwanda |
| | 1.7 Kufufua viwanda vya kilimo vilivyobinafsishwa ambavyo vimekufa, hasa viwanda vya zamani vya nguo – kwa mfano Urafiki, MWATEX n.k., ili kuongeza thamani ya bidhaa |
| | i. Kuanzisha mkakati wa kitaifa wa kufufua sekta ya nguo, na kutoa kipaumbele cha uwekezaji kwa viwanda muhimu vya pamba(mills) |
| | ii. Kuhamasisha uhuishaji wa uwekezaji binafsi kupitia motisha maalumu na ushirikiano wa kimkakati |
| | iii. Kuweka ushindani kwa kuweka ulazima wa matumizi ya pamba ya ndani na kuanzisha vituo vya teknolojia na mafunzo ya ujuzi |
| 2. Angalau asilimia 45 ya wakulima kupatiwa pembejeo bora za kilimo ifikapo Juni 2030 | i. Kuimarisha mifumo ya matumizi ya mbegu zenye uzalishaji wa juu, zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na mwingiliano kati ya utafiti, ugani na sekta ya viwanda |
| | ii. Kuimarisha kanuni za ubora wa pembejeo na mifumo ya uthibitishaji ili kupambana na bidhaa bandia ifikapo 2029 |
| Kuongezeka kwa ardhi ya kilimo iliyolimwa kwa kutumia mbinu za kilimo zinazozingatia mabadiliko ya hali ya hewa hadi asilimia 40 ifikapo Juni 2031 | i. Kutumia mbinu za kilimo zinazozingatia mabadiliko ya hali ya hewa kwa ardhi yote ya kilimo |
| | ii. Kutumia kilimo bora na majukwaa jumuishi ya kilimo cha kidijitali |
| Uwiano wa maafisa ugani na wataalamu wa kilimo kuboreshwa kutoka 1:20,000 hadi 1:10,000 ifikapo Juni 2031. | i. Kuanzisha na kuimarisha mifumo endelevu kwa matumizi ya majukwaa ya ugani yanayotumia TEHAMA (e-extension) kufikia wakulima kwa ufanisi |
| | ii. Kuboresha mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ili kupanua wigo na ubora wa utoaji wa huduma za ugani |
| Lengo 2: Sekta ndogo za mifugo na uvuvi zilizo imara na zenye ushindani kibiashara, zinazochochea ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha vijijini | |
| **1.1.2. Mifugo na Uvuvi** | |
| 1. Angalau asilimia 50 ya mazao ya mifugo na uvuvi yaongezwe thamani ifikapo 2030 | i. Kuimarisha ufugaji wa mifugo na uvuvi na uwezo wa vinasaba |
| | ii. Kuendeleza makundi ya viwanda vya mifugo na uvuvi na miundombinu ya uchakataji |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 2. Kuongezeka kwa asilimia 50 ya uzalishaji wa ndani wa pembejeo ifikapo 2030 | i. Kuboresha uzalishaji wa pembejeo za mifugo na uvuvi |
| 3. Kuingia katika masoko ya kikanda na kimataifa kwa asilimia 50 ya bidhaa za samaki na ufugaji wa samaki kufikiwa ifikapo 2030. | i. Kujenga na kuboresha bandari za uvuvi, mialo na miundombinu ya uhifadhi baridi katika pwani ya Bahari ya Hindi |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya viwandani ya uidhinishaji na ili kuwezesha kwa mauzo nje ya bidhaa za Samaki na ufugaji wa samaki |
| **Lengo 3:** Uboreshaji wa uzalishaji na uchakataji jumuishi katika sekta ya kilimo, ili kuongeza ongezeko la thamani, kupunguza hasara baada ya mavuno na kuongeza kipato kwa wakulima wadogo ifikapo 2030 | |
| **1.1.3. Mnyororo wa thamani wa chakula na isiyo chakula** | |
| 1. Kuanzisha makundi ya ukuaji wa kilimo katika korido 2 ifikapo Juni 2031. | i. Kuanzisha makundi jumuishi ya chakula, vinywaji/visivyo chakula, na mnyororo wa thamani wa mifugo |
| | ii. Kuendeleza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya uchakataji wa mazao ya kilimo na mnyororo wa thamani jumuishi |
| **Lengo 4: Kuboresha ugharamiaji** bunifu wa kilimo kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya kilimo kwa kuboresha upatikanaji wa mikopo nafuu, kuhamasisha uwekezaji na kuwezesha mnyororo wa thamani himilivu | |
| **1.1.4. Ugharamiaji Bunifu wa Kilimo** | |
| 1. Kiwango cha wajasiriamali wa kilimo wanaopata huduma za fedha kuongezeka kutoka asilimia 15 hadi asilimia 30 ifikapo Juni 2031 | i. Kuanzisha vyanzo bunifu vya ugharamiaji (soko la mitaji, na benki za maendeleo,) kwa ajili ya uwekezaji wa muda mrefu wa kilimo |
| | ii. Kuanzisha mbinu za kukabiliana na vihatarishi ili kuvutia uwekezaji binafsi katika maeneo ambayo hayajapata huduma |
| 2. Asilimia 5 ya Bajeti ya Taifa iliyotengwa ipelekwe kwenye maendeleo ya kilimo kila mwaka | Kuanzisha mgao wa kimkakati wa bajeti kwa ajili ya kilimo na kilimo jumuishi katika mpango wa LED |
| **1.1.5. Misitu ya Biashara** | |
| **Lengo 5:** Kuhakikisha usambazaji endelevu wa mazao na huduma za misitu kwa kudumisha eneo la misitu la kutosha chini ya usimamizi madhubuti, na hivyo kuboresha mfumo wa ikolojia, kuimarisha maisha vijijini na uhakika wa usambazaji wa malighafi kwa viwanda vinavyotegemea misitu | |
| 1. Kuongeza eneo la biashara kwa ajili ya mashamba ya misitu na vitalu vya miti ya jamii kufikia hekta milioni 1.5 ifikapo Juni 2031 | i. Kuongeza na kuimarisha mashamba ya biashara na vitalu vya miti ya jamii |
| | ii. Kufungamanisha mbinu za usimamizi wa misitu zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi. |
| | iii. Kuweka ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya upanuzi wa misitu ifikapo |
| **Lengo 6:** Kukuza maendeleo endelevu ya viwanda vinavyotegemea misitu biashara na kuwa na mchango wenye tija katika kuongeza thamani ya bidhaa za misitu, kupanua wigo wa bidhaa, kuongeza mauzo nje na kutumia bidhaa za ndani badala ya kuagiza | |
| 1. Kuongeza mchango wa mazao ya misitu katika pato la Taifa kutoka asilimia 3 - 4 na mauzo nje kufikia Dola milioni 150 – 200 kufikia June 2031 | i. Kuendeleza ubiasharishaji wa bidhaa za misitu kupitia ongezeko la thamani, kupanua wigo wa bidhaa, na matumizi ya teknolojia ya kisasa katika usindikaji. |
| | ii. Kukusanya fedha za mabadiliko ya tabianchi na uwekezaji unaojali mazingira ili kusaidia ubiasharishaji endelevu kwa mwaka. |
| | iii. Kuimarisha sera wezeshi kwa viwanda vya mazao yatokanayo na misitu, ikijumuisha kufuata kanuni, taratibu, na ujumuishwaji |
| **1.1.6. Ufugaji nyuki** | |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| **Lengo 1:** Kufanya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara wa nyuki na uzalishaji wa asali ili kukidhi mahitaji kwa njia endelevu, kukuza biashara inayolinda mazingira, na kuongeza ushindani katika masoko ya nje kupitia uboreshaji wa ujuzi, ukuzaji wa teknolojia, na ujumuishaji wa masoko | |
| Kuongeza uzalishaji wa asali na mazao ya nyuki kitaifa kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa ifikapo Juni 2031 | i. Kuimarisha mifumo ya udhibiti, miundombinu na viwango vya uzalishaji ili kuweka mazingira wezeshi kwa uzalishaji na ubiasharishaji wa mazao ya nyuki |
| | i. Kuboresha mbinu za uzalishaji wa mazao ya nyuki na kuwezesha mabadiliko kutoka mizinga ya jadi kwenda kwenye vifaa vyenye viwango vya kisasa |
| | ii. Kutekeleza programu kubwa ya kupanda na kuhifadhi mimea rafiki kwa nyuki katika kanda muhimu za ufugaji nyuki, na kujumuishwa na juhudi za kitaifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na upandaji miti |
| | iii. Kuandaa na kusambaza mtaala wa kisasa wa ufugaji nyuki utakaozingatia hali ya hewa kikanda na kujumuishwa katika huduma za ugani za kilimo |
| Kuongeza uwekezaji unaoongozwa na sekta binafsi katika mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki kwa asilimia 50 ya kiwango cha sasa na kuanzisha angalau shughuli 5 kubwa za ufugaji nyuki zinazolenga mauzo ya nje ifikapo Juni 2031**.** | i. Kuunda chapa ya kitaifa ya hadhi ya juu (premium) yenye mfumo wa ufuatiliaji kidijitali na kusaidia wazalishaji kupata vyeti vya kimataifa. |
| | ii. Kuwezesha uundaji wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na mikataba ya wakulima wakubwa itakayounganishwa na shughuli kubwa za kibiashara na mitandao ya wafugaji wadogo wa nyuki, kuhakikisha upatikanaji wa malighafi bora, masoko ya uhakika na msaada wa kitaalamu |
| | iii. Kuandaa na kuimarisha mipango ya biashara iliyofanyiwa mapitio ya awali na iliyo tayari kwa ajili ya uwekezaji katika shughuli kubwa za ufugaji nyuki, viwanda vya usindikaji na mazao yake, vinavyoweza kuuzwa kwa wawekezaji wa ndani na nje |
| | iv. Kuandaa na kutekeleza viwango vya kitaifa vya ubora kwa bidhaa zote za msingi za nyuki, zilizoongezewa thamani, ili kuhakikisha usalama, upatikanaji wa masoko yote na kujenga imani ya watumiaji wa kimataifa |
| **1.2. Sekta ya viwanda na uzalishaji viwandani** | |
| **Lengo Kuu 1:** Kuwezesha Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji viwandani katika kanda ya Afrika Mashariki kwa kufikia kiwango cha ukuaji wa wastani asilimia 9 kwa mwaka na kuwa na mchango endelevu wa sekta wa asilimia 15 katika Pato la Taifa (GDP). | |
| 1. Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 50 bora duniani kulingana na Farihisi ya Benki ya Dunia cha Urahisi wa Kufanya Biashara (Business Readiness Index), kufikia Juni 2031.. | 1.1 Kuandaa Sera ya Kitaifa ya Viwanda na Mkakati wa uendelezaji viwanda 2050 unaohamasisha biashara mseto na uzalishaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani |
| | i. Kuunda mfumo wa kitaasisi wa udhibiti utakaosaidia kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa sera mpya ya viwanda |
| | ii. Kuweka kipaumbele cha minyororo ya thamani kwa viwanda kama mwelekeo wa kitaifa wa maendeleo ya viwanda chini ya sera mpya |
| | 1.2 Kuandaa sera mahsusi ya kibajeti na marekebisho ya kisheria ili kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) na kuhuisha teknolojia na maendeleo katika viwanda vya ndani |
| | i. Kuweka mfumo shindani wa kifedha unaotoa motisha maalum kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni unaolenga katika uhawilishaji wa teknolojia na maendeleo ya viwanda vya ndani |

| Shabaha | Afua |
| --- | --- |
| | ii. Kuweka mfumo rahisi kisheria ikiwemo kituo jumuishi cha huduma za uwekezaji, ili kupunguza muda na gharama za kuanzisha na kuendesha biashara za viwanda |
| | 1.3 Kuandaa mpango ulioratibiwa wa kuhamasisha uwekezaji ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi katika viwanda vya madini |
| | i. Kuandaa Mpango wa uwekezaji wa viwanda vinavyotegemea madini, ikijumuisha utoaji wa motisha, matumizi ya rasilimali za ndani, na fursa za Utafiti na Maendeleo (R&D) |
| | ii. Kuzindua kampeni mahsusi ya uwekezaji wa kimataifa kwa kutumia mfumo ulioboreshwa wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Viwanda (NIIMS) na maonyesho ya kimataifa ili kuvutia wawekezaji wenye sifa katika mnyororo wa thamani wa awali wa madini |
| | iii. Kuanzisha dawati maalum la uwezeshaji wa uwekezaji katika uzalishaji wa Madini |
| | 1.4 Kuweka kipaumbele kwa bidhaa za ndani katika manunuzi ya serikali na kuhakikisha wazalishaji wa ndani wanapata uhakika wa mahitaji ya bidhaa zao kila mwaka. |
| | i. Kutekeleza kiwango cha lazima cha Matumizi ya Rasilimali za Ndani katika manunuzi ya umma, kikihifadhi angalau asilimia 30 ya matumizi kwa bidhaa zinazokidhi vigezo kwa wazalishaji wa ndani walioidhinishwa |
| | ii. Kuanzisha mpango wa maendeleo ya wasambazaji ili kudhibitisha na kuongeza uwezo wa viwanda vidogo vya ndani kufikia viwango vya manunuzi ya serikali |
| 2. Kuongeza wigo wa mauzo nje yatokanayo na Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje - EPZ na Maeneo Maalumu ya Uwekezaji -SEZ kufikia asilimia 22 ya jumla ya mauzo ya nje ya sekta ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuanzisha vituo vya ubunifu na teknolojia ili kuvutia uwekezaji katika utafiti, maendeleo na uzalishaji, hasa katika viwanda vya teknolojia ya juu |
| | Kuanzisha mfumo maalum wa kisheria wa vituo vya ubunifu na teknolojia, unaotoa taratibu rahisi na motisha mahsusi |
| | 2.2 Kuanzisha vituo vya kisasa vya uzalishaji katika maeneo maalumu ya uwekezaji na Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje |
| | i. Kuweka miundombinu ya kidijitali ya msingi (mfano: intaneti ya kasi, majukwaa ya *IoT*) katika maeneo yote maalumu ya uwekezaji na Kanda zote za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje ili kusaidia utekelezaji mapinduzi ya nne viwanda |
| | ii. Kuandaa vivutio maalum kwa ajili ya viwanda na kuanzisha vituo vya mafunzo ya ujuzi ndani ya maeneo maalumu ya uwekezaji ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi katika matumizi ya mitambo inayojiendesha |
| | 2.3 Kuanzisha asilimia 50 ya Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje zenye vivutio na masharti maalum kwa ajili ya teknolojia ya juu ya uzalishaji wa viwanda na viwanda vinavyotegemea madini |
| | i. Kuweka mfumo maalum wa teknolojia ya juu na motisha ya ongezeko la thamani ya Madini kwa Kanda za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje |
| | ii. Kuainisha na kuziongezea viwango asilimia 50 ya Kanda zote za Uzalishaji Bidhaa za Kuuza Nje kuwa kanda za kisasa ya uzalishaji ifikapo Juni 2031, zikiwa na miundombinu muhimu ya kidijitali na nguvu kazi yenye ujuzi inayohitajika kwa viwanda vya teknolojia ya juu ya viwanda . |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 2.4 Kuhamasisha mbinu za uzalishaji nishati safi na rafiki kwa mazingira, zikizingatia viwango vya kimataifa na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa mwaka |
| | i. Kutekeleza mfumo wa lazima wa ukaguzi wa nishati na mazingira kwa viwanda vyote vya uzalishaji, na taasisi zilizothibitishwa zinazofanya ukaguzi kwa kufuata sheria na kanuni |
| | ii. Kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje wa kijani kwa kutoa vivutio maalum kwa kampuni za kigeni zinazohawilisha teknolojia za juu za nishati safi teknolojia safi za viwandani kwa mwaka |
| | iii. Kuanzisha Mpango wa motisha kwa viwanda rafiki kwa mazingira, unaotoa punguzo la kodi kwa kampuni zinazopata vyeti vya kimataifa vya mazingira (mfano: ISO 14001) |
| | 2.5 Kuhakikisha wazalishaji wa ndani wanakidhi viwango vya ubora vya kimataifa ili kuwa na ufanisi katika ushindani wa masoko ya kimataifa, hasa kwa bidhaa zenye thamani kubwa kwa mwaka**.** |
| | i. Kuanzisha mtandao wa kitaifa wa vituo vya ukaguzi na uthibitisho vya kimataifa ili kuwezesha wazalishaji wa ndani kuthibitisha bidhaa zenye thamani kubwa kufikia viwango vya kimataifa ndani ya nchi kwa mwaka. |
| 3. Kuongezeka kielezo cha mauzo nje ya bidhaa mseto kutoka 0.4 hadi 0.52 kufikia Juni 2031 | 3.1 Kuanzisha na kuvutia hisa za uzalishaji wa bidhaa za thamani ya juu (elektroniki, dawa, mitambo na vipuri vya magari) |
| | 3.2 Kuanzisha na kuongeza wigo wa uzalishaji wa ndani wa chuma, magari, makaa ya mawe na uzalishaji wa bidhaa za kielektroniki hadi kufikia angalau asilimia 40 na asilimia 1 katika mnyororo wa mauzo ya nje wa kikanda na kimataifa, mtawalia |
| | i. Kuendeleza maeneo maalumu ya kongane za viwanda kwa ajili ya chuma, magari na vifaa vya elektroniki, kuweka wazalishaji viwandani pamoja na vituo vya mafunzo ya ujuzi na vitovu vya mnyororo wa ugavi |
| | ii. Kuandaa vivutio katika maeneo ya uzalishaji ya kimkakati, ikijumuisha punguzo maalum la kodi, ruzuku ya viwango vya umeme, na vipaumbele vya ufadhili kwenye miradi itakayozingatia matumizi ya rasilimali za ndani na malengo ya mauzo ya nje. |
| | 3.3 Kuandaa na kuuza nje bidhaa za viwandani za teknolojia ya juu katika masoko ya kimataifa (Ulaya, Asia, Amerika) |
| | i. Kuanzisha mtandao wa kitaifa wa vituo maalumu vya ubunifu vinavyolenga akili unde na uzalishaji wa viwango, vilivyo na viwango vya kimataifa ili kuwa injini ya ukuzaji wa bidhaa za teknolojia ya juu |
| | ii. Kuanzisha kituo au mpango maalum wa kuwezesha utafiti pamoja na kutoa ruzuku kwa tafiti na maendeleo na unafuu wa biashara, na motisha maalum kwa wawekezaji. |
| | iii. Kuandaa Mpango wa Kimataifa wa uuzaji wa teknolojia ya juu ili kusajili bidhaa za teknolojia ya juu kwa viwango vya kimataifa na kuzindua kampeni maalum za kufuzu masoko ya Ulaya, Asia na Amerika |
| **Lengo 2:** Kuimarisha matumizi ya rasilimali za ndani na kukuza uchumi jumuishi unaolenga biashara ndogo ndogo, ndogo na za kati | |

<table>
<tr><th>Shabaha</th><th>Afua</th></tr>
<tr><td rowspan="13">1. Ongezeko la thamani katika uzalishaji (MVA) kwa biashara ndogondogo na za kati kutoka asilimia 12 hadi asilimia 22 kufikia Juni 2031</td><td>1.1 Kufanya mapitio na kuanzisha mifumo ya udhibiti kwa ajili ya kurasimisha biashara ndogondogo na za kati, kuongeza upatikanaji wa fedha, kujenga uwezo na upatikanaji wa masoko ya kikanda na kimataifa</td></tr>
<tr><td>1.2 Kuandaa mpango wa kusaidia biashara ndogondogo na za kati za uzalishaji kupitia ruzuku/mikopo</td></tr>
<tr><td>i. Kuanzisha kituo maalum cha kuwezesha biashara ndogondogo na za kati za uzalishaji, kutoa ruzuku na mikopo nafuu kwa ajili ya kuboresha teknolojia na kupanua biashara</td></tr>
<tr><td>ii. Kuanzisha mpango maalumu wa dhamana ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati ili kuwezesha benki za kibiashara kutoa mikopo kwa biashara ndogondogo na za kati za uzalishaji</td></tr>
<tr><td>1.3 Kuanzisha angalau eneo moja rafiki la viwanda kwa wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs) lenye miundombinu ya pamoja (huduma za msingi, usafirishaji na hifadhi) ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuimarisha ushirikiano katika kila jiji</td></tr>
<tr><td>i. Kuanzisha mfumo madhubuti wa usimamizi wa maeneo ya wajasiriamali wadogo na wa kati, ikijumuisha urahisishaji wa ugawaji ardhi na taratibu za usajili wa biashara</td></tr>
<tr><td>ii. Kuandaa usanifu wa gharama nafuu na kuanza ujenzi wa maeneo rafiki ya viwanda kwa wajasiriamali wadogo na wa kati katika miji ya majaribio kufikia</td></tr>
<tr><td>iii. Kujumuisha huduma muhimu za kuwezesha biashara, zikiwemo upatikanaji wa fedha na utalaamu wa kiufundi, katika maeneo yote ya viwanda ya wajasiriamali wadogo na wa kati yanayofanya kazi</td></tr>
<tr><td>1.4 Kuwezesha ujumuishaji wa wajasiriamali wadogo na wa kati wa ndani katika minyororo ya thamani ya uzalishaji kwa lengo la kuboresha viwango vya ubora, uwezo wa kiutendaji na upatikanaji wa masoko</td></tr>
<tr><td>i. Kuanzisha mpango wa kitaifa wa kusaidia kudhibiti ubora wa viwanda vidogo ili kufikia viwango vya kimataifa vya uzalishaji</td></tr>
<tr><td>ii. Kuzindua mpango wa kitaifa wa kuunganisha minyororo ya ugavi, utakasaidia kuoainisha biashara na makubaliano ya kandarasi kati ya biashara ndogondogo na za kati zilizothibitishwa na wazalishaji wakubwa</td></tr>
<tr><td>iii. Kuandaa mtaala wa mafunzo ya utayari wa kushiriki katika mnyororo ya usambazaji na kuupeleka kwa viwanda vidogo, kwa ajili ya taratibu za manunuzi, usafiri na usafirishaji na kuongeza uzalishaji</td></tr>
<tr><td></td></tr>
<tr><td colspan="2">1.3. Sekta ya Ujenzi</td></tr>
<tr><td colspan="2">Lengo 1: Kuanzishwa kwa sekta ya ujenzi endelevu, jumuishi, shindani kikanda, inayoongozwa na wakandarasi wa ndani, inayochochea ukuaji wa uchumi, kuendeleza ubiasharishaji, kuboresha viwango vya maisha, na kuhimiza maendeleo ya teknolojia na ubunifu</td></tr>
<tr><td rowspan="2">1. Kuongezeka kwa thamani ya hisa za wakandarasi wa ndani wanaoshiriki katika miradi mikubwa ya ujenzi hadi asilimia 50 kufikia Juni 2031.</td><td>Kuandaa mwongozo wa ugharamiaji kwa wakandarasi ambao utaimarisha upatikanaji wa fedha kwa kampuni za ndani na kuimarisha ushiriki wao katika miradi mikubwa</td></tr>
<tr><td>Kutekeleza mwongozo wa uwezeshaji wakandarasi wa ndani utakaoelekeza malipo ndani ya siku 30, kutoa kipaumbele kwa rasilimali za ndani katika manunuzi, na utekelezaji wa vifungu vya ubia vyenye viashiria vya uhawilishaji teknolojia kwa miradi yote ya umma.</td></tr>
</table>

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | Kuzindua mkakati wa utayari wa kimataifa ili kuthibitisha kampuni za ndani katika viwango vya kimataifa, na kuimarisha uwezo na ushindani katika miradi ya kikanda |
| 2. Asilimia 60 ya miradi mikubwa ya ujenzi kutekelezwa kupitia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa kushirikiana na wakandarasi wa ndani kufikia Juni 2031. | i. Kuimarisha na kutafsiri miongozo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa kuwezesha kuandaliwa kwa miradi inayotekelezeka na inayoweza kupata ufadhili. |
| | ii. Kuimarisha utekelezaji wa mifumo iliyopo ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kwa kuandaa orodha ya miradi inayoweza kupata ufadhili |
| | iii. Kuimarisha na kuendeleza majukumu ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ndani ya Wizara, Idara, Taasisi (MDAs) na Serikali za Mitaa (LGAs) ili kuwa na miradi inayoweza kupata ufadhili |
| 3. Asilimia 50 ya kampuni za ujenzi za ndani zitatumia teknolojia za kisasa na mbinu endelevu katika miradi mikubwa ya ujenzi kufikia Juni 2031. | 3.1. Kuimarisha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) kati ya na kampuni za ujenzi za ndani na watengenezaji wa vifaa vya ujenzi pamoja na kampuni za kimataifa. |
| | i. Kuweka sharti la ushiriki wa angalau asilimia 30 hadi 50 wa kampuni za ndani ili kuwa na uhawilishaji teknolojia katika miradi yote mikubwa ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) |
| 4. Asilimia 80 ya kazi za kitaalamu na zenye ujuzi zinazopatikana katika sekta ya ujenzi kufanywa na wakandarasi wa ndani kufikia Juni 2031. | 4.1.Kuimarisha uwezo wa kiufundi na ujuzi wa kiutawala kwa wataalam wa ujenzi wa ndani ili kuongeza ushiriki wao katika nafasi za kiutawala. |
| | i. Kuanzisha chuo cha kisasa cha mafunzo ya ujenzi kufikia 2028 ili kuweka viwango na kutoa mafunzo katika nyenzo za kidijitali (BIM),utakaozingatia ujenzi rafiki wa mazingira, na usimamizi wa miradi ya kimataifa. |
| | ii. Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Mafunzo kwa Vitendo katika Sekta ya Ujenzi (National Construction Apprenticeship Scheme), utakaowataka washiriki wa miradi mikubwa kushiriki kikamilifu na kushirikiana na taasisi za mafunzo ya ufundi ili kuwezesha vyeti kwa mafundi wenye ujuzi wa kisasa wa ujenzi kila mwaka. |
| 5. Asilimia 40 ya miradi ya ujenzi iwe imejumuisha miundo yenye ufanisi wa matumizi ya nishati na mbinu za ujenzi rafiki kwa mazingira ifikapo Juni 2031. | 5.1 Kuboresha ufanisi wa matumizi ya nishati na kuhimiza matumizi ya mbinu za ujenzi rafiki wa mazingira ifikapo Juni 2031. |
| | i. Kuanzisha na kutekeleza Kanuni ya Ujenzi Rafiki wa Mazingira (Green Building Code) pamoja na Sera ya Ununuzi wa Umma Rafiki wa Mazingira (Green Public Procurement – GPP) kwa miradi yote mipya ya Serikali |
| | ii. Kuanza mpango wa kutoa motisha kwa matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, utakaotoa msamaha wa kodi na ruzuku kwa miradi inayotumia nishati mbadala, teknolojia za ujenzi wa sehemu zilizotengenezwa awali (prefabrication), na ubunifu wa matumizi ya malighafi za ndani. |
| | iii. Kuanzisha na kuthibitisha wataalamu wa ujenzi katika usanifu, usimamizi na uthibitishaji wa majengo rafiki wa mazingira kupitia programu ya kitaifa ya kuongeza kasi ya ujuzi |
| **1.4. Sekta ya Madini na Uchimbaji wa Mawe.** | |
| **Lengo 1:** Kuendeleza sekta shindani na jumuishi ya madini inayotegemea viwanda na inayotumia kwa ufanisi rasilimali za madini huku ikidumisha na kuimarisha minyororo ya thamani ya ndani. | |

| Shabaha | Afua |
| --- | --- |
| 1. Asilimia 25 ya wataalamu wa sekta ya madini kupewa mafunzo ya umahiri, unaoendana na uongezaji thamani wa madini na uchumi wa viwanda ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuhakikisha upatikanaji wa nguvu kazi yenye ujuzi wa kutosha kusaidia uongezaji thamani wa madini na shughuli za uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na madini |
| | 1.2 Kupanua na kuboresha taasisi za mafunzo ya kiufundi (mfano, *Moshi Integrated Mining Technical Training*) ili kukuza nguvu kazi ya uchimbaji wa madini na uongezaji thamani |
| | 1.3 Kuanzisha vyuo vya mafunzo ya madini na ufundi vilivyofungamanishwa kwa lengo la kujenga mfumo endelevu wa kuzalisha wataalamu wenye ujuzi na utayari wa kufanya kazi katika sekta ya madini |
| 2. Kuongeza kiwango cha ufanisi wa usimamizi wa sekta ya madini kutoka kiwango cha sasa hadi angalau asilimia 65 ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuandaa na kutekeleza mfumo jumuishi wa utawala wa kidijitali (e-governance system) kwa sekta ya madini. |
| | 2.2 Kuimarisha uwezo wa taasisi kuu za udhibiti (Tume ya Madini na taasisi nyingine) ili kuboresha utawala, ukaguzi, ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria, na usimamizi wa sera |
| 3. Kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini kutoka asilimia 19 hadi asilimia 40 ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kuimarisha mifumo ya udhibiti ili kuhakikisha ushiriki sawa wa wanawake katika mnyororo mzima wa thamani wa sekta ya madini |
| | 3.2 Kuanzisha programu na viwango vya kitaifa vya kuongeza uwezo na ushiriki wa wanawake katika nyanja za kiufundi, kiuongozi na ujasiriamali katika sekta ya madini. |
| | 3.3 Kuanzisha mifumo maalum ya ufadhili na motisha, ikijumuisha upatikanaji wa mtaji, teknolojia na vifaa, ili kuendeleza biashara za madini zinazoongozwa na wanawake. |
| 4. Kuongeza ushiriki wa vijana katika uchimbaji mkubwa wa madini kwa angalau asilimia 10 ya jumla ya nguvu kazi katika sekta ya madini ifikapo Juni 2031. | i. Kuanzisha programu na motisha za kitaifa zinazohamasisha ubunifu wa kiteknolojia kwa vijana na masuala ya kidijitali katika sekta ya madini |
| | ii. Kuandaa mfumo wa kitaifa wa kukuza umahiri kwa ajili ya kuboresha taaluma endelevu ya vijana wanaofanya kazi katika sekta ya madini, unaoendana na mabadiliko ya kidijitali ya sekta na teknolojia mpya |
| | iii. Kuanzisha mifumo ya udhibiti na ununuzi inayoweka masharti au kutoa motisha kwa zabuni ndogo (subcontracts) kwa biashara zinazomilikiwa na vijana katika nyanja mbalimbali za mnyororo wa thamani wa madini |
| **Lengo la 2:** Kuongezeka kwa uanzishaji wa miradi mipya ya uchimbaji wa madini na kufunguliwa kwa miradi ya utafiti na uchimbaji wa madini iliyokwama, kuweka mazingira wezeshi na urahisishaji wa taratibu kwa wawekezaji wa ndani na wa nje (FDI) katika utafiti na maendeleo ya madini. | |
| 1. Kuongezeka kwa Utoaji wa huduma za ramani za kijiolojia, kifizikia na kikemikali unaofanywa na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2030. | 1.1 Kufanya mapitio ya kina na kuoanisha mifumo ya udhibiti ya sekta za madini, viwanda, fedha na kodi ili kuharakisha utafiti wa madini, kuhimiza maendeleo ya uchimbaji na kuunga mkono uchumi wa viwanda unaotegemea madini ifikapo mwaka 2027. |
| | 1.3 Kuipatia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) teknolojia za kisasa za uchoraji ramani za kijiolojia, kifizikia na kikemikali pamoja na miundombinu ya uchambuzi, ili kuwezesha upatikanaji kamili wa taarifa za kitaifa |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 2. Kulibadilisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kuwa kampuni ya umma ya kibiashara inayokidhi viwango vya kimataifa vya utawala bora na uendeshaji wa mashirika, ikiwa na cheti cha ubora cha ISO 9001 na taarifa za fedha zilizokaguliwa kila mwaka ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuifanya STAMICO kuwa kampuni ya kimkakati ya kitaifa ya uchimbaji madini ambayo Serikali ina umiliki mkubwa wa hisa ili kuweka msingi wa mageuzi ya utawala bora wa makampuni. |
| | 2.2 Kuiwezesha kifedha (mtaji) na kutoa mafunzo kwa watendaji na wafanyakazi, katika nyanja za ujuzi wa kiufundi, kifedha na kiutendaji, sambamba na kuboresha miundombinu na mifumo ili kukidhi viwango vya kimataifa vya uendeshaji. |
| | 2.3 Kuiwezesha STAMICO kupata haki za uchimbaji wa madini na kuongeza shughuli za utafiti na uchimbaji kutoka migodi 3 hadi 7 na kuwa na ukuaji unaopimika na uzingatiaji wa viwango vya kimataifa |
| 3. Kuongeza idadi ya ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi katika migodi yenye tija kutoka idadi ya sasa hadi kufikia angalau 10 ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kuanzisha mfumo wa kimuundo wa kurahisisha uwekezaji kwa ajili ya kuvutia na kurasimisha ubia kati ya Serikali na wawekezaji binafsi katika miradi yenye tija ya uchimbaji wa madini ifikapo mwaka 2028. |
| | 3.2 Kuandaa mipango ya pamoja ya maendeleo ya miundombinu (barabara, umeme, maji, na vituo vya usafirishaji) kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi ili kufungua fursa za madini na kuongeza tija ya sekta |
| | 3.3 Kuanzisha vivutio vya kisheria, kiudhibiti na kifedha ili kuongeza mvuto wa ubia na uwekezaji wa muda mrefu katika sekta ya madini. |
| 4. Kuidhinisha, kupata uwekezaji, na kuanza utekelezaji wa angalau miradi 5 ya kimkakati ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini ifikapo Juni 2031. | 4.1 Kutoa kipaumbele na kuharakisha utoaji wa leseni na vibali vya udhibiti kwa miradi ya madini ya kimkakati na maeneo muhimu ya ili kuvutia wawekezaji wa kimkakati ifikapo mwaka 2028. |
| | 4.2 Kuanzisha ubia wa kimkakati kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPPs) kwa ajili ya miradi mikubwa kama vile Liganga–Mchuchuma (chuma na chuma cha pua), viwanda vya uchenjejuaji nikeli, *cobalt* na shaba, pamoja na mitambo ya usindikaji wa madini adimu (Rare-Earth Minerals – REE), ili kuhakikisha upatikanaji wa fedha, uhamisho wa teknolojia, na maandalizi ya uendeshaji. |
| | 4.3 Kuendeleza miundombinu jumuishi na maeneo ya viwanda (nishati, usafiri, maji, na vifaa/logistics) ili kusaidia utekelezaji wa miradi ya madini na uchenjuaji wa madini. |
| **Lengo la 3:** Kuhamasisha uwekezaji wa ndani na wa kigeni (FDI) katika usindikaji, uchenjuaji, usafishaji, na utengenezaji wa madini ya viwandani na madini muhimu, kwa lengo la kuchochea ukuaji wa viwanda na uchumi. | |
| 1. .Mchango wa madini ya viwandani na madini muhimu (critical base metals) kupitia uongezaji thamani na uzalishaji wa viwandani uongezeke hadi angalau asilimia 3 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuhakikisha kuanzishwa kwa viwanda vya kimkakati vya uzalishaji wa bidhaa kama vile *vigae (ceramics)*, *mbolea (fertilizers)*, *glasi (glass)*, *saruji (cement)*, *kemikali (chemicals)*, *dawa (pharmaceuticals)*, na *betri (battery manufacturing)* vinavyotumia madini ya viwandani (mfano feldspar, jasi, dolomiti, fosfati, kaolini, soda ash, chokaa n.k.) na madini muhimu (mfano REE, grafiti, kobolti, nikeli, titani, lithiamu n.k.) vinaanzishwa |
| | 1.2 Kuanzisha *Kituo cha Teknolojia ya Madini Muhimu* (*Critical Minerals Technology Hub*), kinachojulikana kama "*Silicon Valley ya Dodoma*," kwa ajili ya kuendeleza viwanda vya ndani vya betri za lithiamu-iron na teknolojia nyingine rafiki kwa mazingira (mradi wa kimkakati) ifikapo Juni 2031. |
| | 1.3 Kuwekeza katika uanzishaji wa mitambo ya kuyeyusha na kusafisha metali za msingi (kama vile shaba, zinki, bati, alumini, risasi, nikeli n.k.) ifikapo Juni 2031. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| **Lengo la 4:** Kuongeza uzalishaji na mauzo ya nje ya dhahabu na vito vya thamani, ili kuimarisha nafasi ya Tanzania katika soko la kimataifa la madini. | |
| 1. Kuongeza uzalishaji na mauzo ya nje ya dhahabu na vito kwa angalau asilimia 30 kupitia ushirikishwaji wa wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo (ASM), urasimishaji wa shughuli zao, na upatikanaji wa fedha na teknolojia ifikapo Juni 2031. | **1.1** Kuandaa na kutekeleza mfumo wa kitaifa wa urasimishaji wa wachimbaji wadogo na wa kati (ASM), utakaowawezesha kuwaunganisha katika minyororo rasmi ya ugavi, uzingatiaji wa sheria, na masoko ya kuuza nje. |
| | **1.2** Kuanzisha ubia wa kimkakati kati ya Serikali na sekta binafsi (PPPs) pamoja na ubia wa pamoja (joint ventures) ili kuvutia uwekezaji katika utafiti na uchimbaji mkubwa wa dhahabu na vito ifikapo |
| | **1.3** Kuanzisha jukwaa la kitaifa la fedha na teknolojia kwa wachimbaji wadogo (ASM) na wachimbaji wakubwa, likijumuisha mikopo yenye riba nafuu, ukodishaji wa vifaa, na msaada wa kitaalamu ili kuboresha ufanisi wa uzalishaji na ubora wa bidhaa |
| | **1.4** Kuimarisha mifumo ya data za kijiolojia (geological) na kijiografia (geospatial) ili kuelekeza utafiti wa madini kwa malengo mahususi na kuwezesha uchimbaji endelevu wa dhahabu na vito vya thamani |
| 2. Kuongeza mchango wa dhahabu katika mapato ya fedha za kigeni ya Tanzania kwa angalau asilimia 30 ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuongeza uwezo wa uchimbaji mkubwa wa dhahabu kwa kutoa leseni mpya za kimkakati kwa migodi mipya na kuboresha ufanisi wa migodi iliyopo, ili kufikia angalau migodi 7 inayofanya kazi kikamilifu |
| | 2.2 Kuimarisha akiba ya dhahabu ya taifa na usimamizi wa dhahabu ghafi kwa kuongeza kiwango cha dhahabu kinachomilikiwa na Benki Kuu ya Tanzania kutoka tani 3.7 hadi tani 20 |
| | 2.3 Uongezaji thamani wa bidhaa za dhahabu kwa ajili ya mauzo ya nje kupitia usafishaji, uthibitishaji, na uundaji wa chapa, ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni na ushindani wa kimataifa |
| | 2.4 Kuwezesha ubia wa kimkakati kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPPs) ili kuvutia uwekezaji wa ndani na wan je (FDI) katika utafiti, uchenjuaji, na miundombinu ya uchimbaji wa madini yenye malengo ya kuuza nje |
| **Objective**: Kuifanya Tanzania kuwa kitua cha madini ya vito cha Afrika ifikapo 2050 | |
| 1. Sekta ya vito yenye ushindani na inayodhibitiwa vizuri, yenye angalau asilimia 40 ya biashara iliyorasimishwa na miundombinu ya uongezaji thamani kuanzishwa ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuandaa mfumo wezeshi wa kiudhibiti na kifedha kwa ajili ya utafiti, uchimbaji, uongezaji thamani, na biashara ya vito unaovutia wawekezaji wa ndani na wa kigeni. |
| | 1.2 Kuimarisha programu za kukuza uwezo kwa ajili ya kujenga ujuzi, maarifa, na rasilimali kwa watu binafsi na taasisi katika sekta ndogo ya vito |
| | 1.3 Kuanzisha miundombinu ya kimkakati ya uongezaji thamani wa vito (gemstones) ikiwemo ukataji, ung'arishaji, utengenezaji wa mapambo ya vito, na vituo vya viwanda vya *lapidary*, ikijumuisha kituo kikuu (flagship centre) jijini Dodoma. |
| | 1.4 Kuanzisha Eneo Maalum la Kiuchumi (SEZ) kwa ajili ya biashara na maonesho ya kimataifa ya vito jijini Dodoma kama mradi wa mfano (flagship project). |
| 2. Kituo cha biashara ya vito kilichothibitishwa kuanzishwa nchini Tanzania, chenye uhusiano rasmi na masoko makuu ya kimataifa ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kujenga miunganisho ya masoko ya kimataifa kupitia ushirikiano na taasisi za kimataifa za vito vya thamani, mashirika ya biashara, na taasisi za elimu |
| | 2.2 Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa uundaji wa chapa ya vito vya thamani, kwa kulenga kuvitambulisha vito vya Tanzania (ikiwemo tanzanite) kama bidhaa za ubora wa juu, zinazochimbwa kwa uadilifu, na za kipekee katika masoko ya kimataifa |

<table>
<tr><th>Shabaha</th><th>Afua</th></tr>
<tr><td></td><td>2.3 Kuzitumia fursa za ushiriki katika maonesho ya kimataifa ya vito vya thamani na maonesho ya vito vya mapambo ili kuongeza utambulisho, kuvutia wanunuzi, na kuimarisha fursa za mauzo ya nje</td></tr>
<tr><td colspan="2">1.5. Sekta ya Mafuta na Gesi</td></tr>
<tr><td colspan="2">Lengo 1: Kuongeza utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi, ili kufungua kikamilifu fursa za rasilimali za nishati za taifa kwa ajili ya kuendeleza nishati endelevu na kukuza uchumi.</td></tr>
<tr><td rowspan="4">1. Kutekeleza mpango wa motisha mahsusi (targeted incentives) kwa ajili ya kuvutia uwekezaji katika utafiti wa mafuta na gesi, unaolenga kufikia angalau asilimia 50 ya mabonde ya mashapo (sedimentary basins) ya Tanzania ifikapo Juni 2031</td><td>1.1 Kufanya mapitio ya sera, sheria na kanuni zinazohusiana ili kuimarisha mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji katika utafiti wa mafuta na gesi asilia</td></tr>
<tr><td>i. Kuimarisha mfumo wa kifedha na udhibiti wa utafiti wa mafuta na gesi asilia, kwa kukuweka wazi masharti, na vivutio mahsusi vya kuvutia mitaji yenye hatari (risk capital)</td></tr>
<tr><td>ii. Kuzindua mkakati maalum wa uhamasishaji wa utafiti wa mafuta na gesi asilia na kituo cha wazi cha taarifa (data room) kwa ajili ya kuonesha fursa za kijiolojia za Tanzania</td></tr>
<tr><td>iii. Kuanzisha Kituo Kimoja cha Huduma kwa Wawekezaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa leseni, vibali, na idhini za udhibiti, na kupunguza muda wa uidhinishaji maombi</td></tr>
<tr><td rowspan="3">2. Kulifanya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuwa Kampuni ya Kibiashara inayokidhi viwango vya kimataifa ifikapo Juni 2031.</td><td>2.1. Kuanza mchakato wa kulibadilisha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuwa kampuni ya umma inayokidhi viwango vya kimataifa</td></tr>
<tr><td>i. Kuiwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuongeza mara mbili wigo wake wa utafiti kwa kupewa vitalu vya ziada vilivyo na leseni</td></tr>
<tr><td>ii. Kuimarisha uwezo wa kibiashara wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kupata mtaji, kuunda timu ya usimamizi ya kiwango cha kimataifa, na kuboresha mifumo yake ya kiufundi</td></tr>
<tr><td colspan="2">Lengo 2: Kuongeza uzalishaji na matumizi ya ndani ya gesi asilia nchini, ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa nishati kwa ajili ya viwanda vya ndani na ukuaji wa uchumi</td></tr>
<tr><td rowspan="4">3. Uzalishaji wa gesi asilia ya nchi kavu (onshore) uongezeke kutoka MMSCFD 320 (futi za ujazo za kawaida milioni kwa siku) hadi MMSCFD 1,000 ifikapo Juni 2031</td><td>3.1. Kukuza na kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kwa matumizi ya ndani</td></tr>
<tr><td>i. Kuongeza kasi ya majadiliano ya mikataba ya uwekezaji kwa mradi wa LPG wa Mtwara.</td></tr>
<tr><td>ii. Kuimarisha mnyororo wa thamani wa gesi asilia ya ndani kwa kuanzisha ushirikiano wa kimataifa wa uhamishaji wa ujuzi na kuboresha mtandao wa usambazaji wa gesi wa nchi kavu ili kupunguza upotevu wa usafirishaji (transmission losses) .</td></tr>
<tr><td>iii. Kuongeza uzalishaji wa gesi nchi kavu kwa kuanzisha kisima kipya cha gesi.</td></tr>
<tr><td rowspan="4">4. Matumizi ya gesi asilia nchini kuongezeka kutoka futi za ujazo kwa siku tani 290 hadi 800 y kufikia Juni 2031.</td><td>4.1. Kuongeza matumizi ya gesi asilia nchini</td></tr>
<tr><td>i. Kuanzisha mfumo wa motisha ya matumizi ya gesi, ukitoa motisha za kifedha na zisizo za kifedha kwa viwanda na kaya zinazotumia gesi asilia</td></tr>
<tr><td>ii. Kuzindua mpango wa matumizi ya gesi hadi viwandani, na utakaolekeza kongane kuu za viwandani kutumia gesi asilia kwa kuunda mahitaji ya msing</td></tr>
<tr><td>iii. Kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Taifa cha Gesi, kwa ajili ya kujenga uwezo wa kitaalamu wa ndani, kuendeleza utafiti na ubunifu (R&D) katika matumizi ya gesi, na kutoa mafunzo kwa nguvu kazi maalumu katika sekta ya gesi.</td></tr>
</table>

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| Lengo la 3: Tanzania kuwa kituo kinachoongoza cha uzalishaji na usafirishaji wa gesi barani Afrika, kwa kupanua ushawishi katika masoko ya kikanda na kimataifa, na kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi wa Taifa. | |
| 5. Kuongeza Usambazaji wa gesi katika Kituo cha Biashara ya Gesi cha Kikanda kutoka milioni 290 za futi za ujazo kwa siku hadi milioni 3,500 za futi za ujazo kwa siku ifikapo Juni 2031 | 5.1. Kuanza mchakato wa kuibadilisha Tanzania kuwa miongoni mwa wauzaji wakuu wa gesi barani Afrika |
| | i. Kuhakikisha upatikanaji wa mikataba ya muda mrefu ya mauzo ya gesi na nchi muhimu ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) |
| | ii. Kujenga kituo cha biashara ya gesi cha kikanda, chenye mabomba ya kuvuka mipaka na miundombinu ya kuhifadhia gesi, kwa ajili ya kusambaza gesi katika masoko ya EAC na SADC. |
| | iii. Kujenga ushirikiano wa kimkakati katika sekta ya nishati na kuoanisha sera za biashara ya nishati za kuvuka mipaka na nchi wanachama wa EAC na SADC, ili kuwezesha biashara ya gesi katika ukanda huu . |
| 6. Uzalishaji wa gesi baharini (Offshore Gas) utakaowezesha biashara ya mauzo ya LNG kufikia tani milioni 15 kwa mwaka (MTPA) ifikapo Juni 2031. | 6.1. Kukuza uzalishaji na mauzo ya gesi asilia nje ya nchi LNG ifikapo Juni 2031. |
| | i. Kujenga mfumo thabiti wa udhibiti na kifedha unaohakikisha mazingira rafiki kwa uwekezaji katika mradi wa LNG na uthabiti wa mikataba ya mauzo ya gesi (off-take commitments) |
| 1. Sekta za Huduma: | |
| 2.1. Sekta ya Utalii. | |
| Lengo la 1: Kuimarisha shughuli, bidhaa, mbinu na uzoefu wa utalii ili kukuza uendelevu, ujumuishi na uimara, sambamba na kupanua fursa za ushiriki kwa jamii za wenyeji na kuhakikisha ukuaji wa muda mrefu wa sekta. | |
| 1. Kuboresha nafasi ya Tanzania katika Usafiri na fahirisi ya maendeleo ya utalii (Travel and Tourism Development Index )kutoka nafasi ya 81 hadi 60 kati ya nchi 119 duniani ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kusaidia maendeleo ya bidhaa na masoko mapya ya utalii |
| | i. Kuandaa na kuzindua bidhaa mpya za utalii zilizo tayari kuingia sokoni kwa kuzingatia tathmini ya kina ya vivutio vya utalii. |
| | ii. Kuandaa mkakati wa kitaifa wa utofauti wa utalii unaolenga kuvutia watalii wa thamani ya juu kutoka masoko mapya |
| | 1.2 Kuhamasisha uwepo na upatikanaji na fedha za gharama nafuu kwa ajili ya utalii kwa kila mwaka |
| | i. Kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Utalii ili kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa wawekezaji wadogo na wa kati katika sekta ya utalii, na kuwezesha uundaji wa bidhaa na masoko mapya ya utalii kila mwaka. |
| | ii. Kuanzisha mpango wa dhamana ya mikopo ya utalii ili kupunguza hatari kwa benki za biashara na kuwezesha upanuzi wa mikopo kwa sekta binafsi kila mwaka |
| | iii. Kuanzisha Mfuko wa Ustahimilivu na Urejeshaji wa Utalii kwa ajili ya kutoa fedha za dharura na msaada kwa sekta ya utalii wakati wa misukosuko ya kiuchumi au majanga, kila mwaka. |
| | 1.3 Kuimarisha uwezo wa maendeleo ya miundombinu ya utalii. |
| | i. Kuwezesha Wizara ya Utalii na Taasisi kuu za Serikali kuwa na mifumo ya kisasa ya usimamizi wa miradi na fedha, ili kupanga, kununua, kufadhili, kutekeleza na kusimamia miradi mikubwa ya miundombinu ya utalii kwa ufanisi |
| | 1.4 Kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za utalii |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | i. Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa kitaifa wa uthibitishaji wa utalii endelevu, unaowataka waendeshaji wote wa shughuli za utalii katika maeneo yaliyohifadhiwa kufuata viwango vya kimazingira na kitamaduni. |
| | ii. Kuweka sharti la utekelezaji wa mikataba ya mgao wa mapato kwa jamii katika miradi yote mipya ya utalii ifikapo Juni 2031, ili kuhakikisha jamii za wenyeji zinapata sehemu ya moja kwa moja ya mapato ya utalii. |
| | 1.5 Kuimarisha uwezo wa uratibu wa shughuli za utalii |
| | i. Kuanzisha na kuendesha mfumo wa kitaasisi na sera kwa sekta ya utalii. |
| | ii. Kuharakisha utekelezaji wa mifumo shirikishi ya kidijitali na majukwaa ya uratibu wa wadau. |
| | iii. Kuimarisha uunganishaji na uhamasishaji wa pamoja wa maeneo yaliyohifadhiwa katika Kanda za Utalii za Mashariki na Kusini |
| | iv. Kuoanisha na kuunganisha hifadhi za taifa za Kanda ya Ziwa katika mizunguko ya utalii ya kikanda (Uganda na Rwanda) |
| | 1.6 Kufanya uwindaji wa kitalii (Tourism Trophy Hunting) kuwa wa ushindani. |
| | i. Kuimarisha utawala na uwezo wa kiutendaji wa sekta ndogo ya uwindaji wa kitalii. |
| | ii. Kuimarisha mifumo ya udhibiti na sera ili kuhakikisha uwindaji wa kitalii unakuwa endelevu na wenye ushindani |
| | iii. Kukuza masoko na kuboresha ongezeko la thamani katika mnyororo wa uwindaji wa kitalii. |
| | iv. Kuanzisha na kuimarisha maeneo ya usimamizi wa wanyamapori katika vijiji vinavyozunguka hifadhi, ili kuongeza jitihada za kupambana na ujangili na kushirikisha jamii katika uhifadhi |
| | 1.7 Kuanzisha taasisi ya Urithi wa Asili na Maeneo ya Kale chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii |
| | i. Kufanya ukaguzi wa Urithi wa Asili na Maeneo ya Kale yote yaliyopo nchini ifikapo |
| | 1.8 Kujenga imani zaidi kwa watalii na wageni wanaotembelea Tanzania |
| | i. Kuanzisha na kutekeleza ratiba ya uhakika ya kupitia kodi, ada na tozo zinazohusiana na utalii kila baada ya miaka mitatu |
| | ii. Kuweka utaratibu wa lazima wa uanachama kwa wawekezaji wa utalii katika vyama vinavyotambulika vya sekta ya utalii |
| | 1.9 Kutumia fursa za mikataba ya ushirikiano wa nchi na nchi, wa kikanda, na wa kimataifa kwa ajili ya kukuza na kuendeleza utalii wa ukanda wa pwani na baharini kila mwaka. |
| | i. Kukuza na kuendeleza bidhaa za utalii rafiki wa mazingira katika fukwe (Beach Eco-Tourism Products – BETP) katika maeneo ya pwani yenye kipaumbele |
| | ii. Kuanzisha Taasisi ya Hifadhi za Pwani na Maeneo ya Baharini Tanzania (Tanzania Coastal and Marine Parks – TCMP) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii |
| 2. Kuendeleza Maeneo manne (4) maalum ya kiuchumi ya utalii (Tourism | 2.1 Kuongeza idadi ya Halmashauri za Serikali za Mitaa (LGAs) zinazoandaa na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya utalii kutoka 13 hadi 26. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| SEZs) na kuanza kufanya kazi ifikapo Juni 2031. | i. Kuhalalisha na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Halmashauri zote (LGAs) ili kuzuia mabadiliko ya matumizi ya ardhi yasiyopangwa ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya utalii |
| | 2.2 Kujenga mifumo ya kifedha, kisheria na udhibiti ili kuvutia uwekezaji na kukuza biashara katika sekta ya utalii. |
| | i. Kufanya mapitio na mageuzi ya mifumo iliyopo ya kifedha, kisheria na udhibiti inayosimamia uwekezaji katika sekta ya utalii |
| | 2.3 Kuanzisha Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya Utalii (Special Tourism Economic Zones – STEZ). |
| | i. Kujenga na kuendesha vituo vya meli za kitalii (cruise ship terminals) katika bandari zilizopo (Dar es Salaam, Tanga, Mtwara) na maeneo mapya (Kilwa, Bagamoyo, Mafia) |
| | ii. Kuanza na kuendesha huduma ya meli za kitalii katika Ziwa Victoria itakayounganisha Speke Bay, Mwanza, Musoma, Geita, Serengeti, Burigi–Chato, Kisumu na Entebbe. |
| | iii. Kujenga na kuendesha vituo vya mikutano vya kimataifa (International Convention Centres) katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma |
| | iv. Kuendeleza Kisiwa cha Mafia kuwa kituo maalum cha kutia nanga meli za kitalii (cruise ships). |
| | 2.4 Kuandaa sera na mifumo shindani ya kuhimiza ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) katika maendeleo ya utalii, kwa kuzingatia miundombinu, ubora wa huduma, na utalii endelevu. |
| | i. Kuimarisha na kuoanisha mifumo ya kisera, kisheria na ya udhibiti inayosimamia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) katika sekta ya utalii. |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya utawala na usimamizi wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) ili kuhakikisha maendeleo ya kimkakati ya miundombinu na ubora wa huduma. |
| | iii. Kuoanisha sera na mifumo ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) na malengo ya utalii endelevu na jumuishi. |
| 3. Kuongezeka kwa Ushiriki wa wazawa (local content) katika sekta ya utalii hadi kufikia asilimia 10 ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kurahisisha kanuni na taratibu za kiutawala ili kuwezesha wajasiriamali wa ndani kuingia kwenye soko la utalii |
| | i. Kurahisisha taratibu za utoaji wa leseni na vibali kupitia uanzishaji wa jukwaa la kidijitali lenye huduma zote. |
| | ii. Kufanya mapitio, kurahisisha na kuoanisha kanuni za utalii ili kuwezesha wajasiriamali wa ndani kutimiza matakwa ya kisheria kwa urahisi. |
| | iii. Kuanzisha mifumo ya usaidizi kwa wajasiriamali wa ndani wa sekta ya utalii, ikijumuisha huduma za ushauri wa kisheria, kifedha na kitaalamu. |
| | 3.2 Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa biashara na ujasiriamali ili kuwawezesha wananchi, wakiwemo wanawake na watu wenye mahitaji maalum, kuanzisha na kuendeleza biashara zinazohusiana na utalii kila mwaka. |
| | i. Kuanzisha mifumo jumuishi ya mafunzo na usaidizi wa ujasiriamali kwa biashara ndogo na za kati (SMEs) katika sekta ya utalii |
| | ii. Kuimarisha mifumo ya kisheria na udhibiti ili kuwezesha upatikanaji wa fedha na rasilimali kwa wajasiriamali wa ndani wa sekta ya utalii. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 3.3 Kuanzisha mfuko wa utalii ili kuwaezesha kampuni chipukizi na biashara ndogo na za kati kwa wajasiriamali wa ndani |
| | i. Kuanzisha na kuweka mifumo ya kisheria na kimuundo na miongozo ya kiutawala ili kuendesha mfuko wa Utalii |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya kutoa msaada wa kifedha na kitaalamu kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati kupitia mfuko wa watalii |
| | 3.4 Kuanzisha majukwaa kwaa wafanyabiashara wa ndani kushirikiana waendesha utalii wakubwa na masokomya kikanda na kimataifa |
| | i. Kuanzisha majukwaa ikiwemo ya kidigitali naili kuwezesha ushirikiano na upatokanaji wa masoko kwa biashara ya utalii wa ndani |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya kujenga uwezo na upatikanaji wa soko kwa biashara za kitalii za ndani |
| | iii. Kutengeneza bomba la mradi lililodhibitiwa na taratibu za lazima kuwezesha usawa wa ushiriki wa wazawa katika umiliki wa shughuli za utalii. |
| | iv. Kuhuisha usajili wa kampuni za utalii na hali ya uendeshaji wa kampuni za utalii zinazomilikiwa na wageni na sera zinazokuza ushiriki wa ndani |
| 4. Zaidi ya asilimia 12 ya maeneo ya vivutio vya utalii yamehifadhiwa na kuunganishwa kufikia Juni 2031. | 4.1 Kuongeza ufikiaji wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa usafiri wa anga |
| | i. Kuboresha na kusimamia njia za kurukia ndege za viwanja vyote 39 vya ndege vilivyopo vinavyohudumia maeneo yaliyohifadhiwa |
| | ii. Kuanzisha viwanja vya ndege vipya na kuimarisha viwanja vya ndege vya kanda vilivyopo karibu na maeneo muhimu yaliyohifadhiwa |
| | iii. Kupitia na kuhusisha kodi, ada na ada zinazohusiana na usafiri wa anga ili kuimarisha muunganisho wa watalii |
| | 4.2 Kuongeza vifaa vya malazi vyenye nyota moja hadi tano kutoka 315 hadi 508 |
| | i. Kuanish ana kuweka kipaumbele maeneo yenye mapungufu ya malazi na kuanzisha mfumo wa kuwezesha mwongozo wa uwezeshaji wa ardhi na miundombinu |
| | ii. Kuanzisha na kuainisha viwango vya malazi, mifumo ya uainishaji, na miundo ya motisha |
| | 4.3 Kuhakikisha ufunguaji upya wa kudumu na ulinzi wa shoroba zote za wanyamapori nchini kote |
| | i. Kuanzisha na kuainisha mfumo wa kisheria wa urejeshaji na ulinzi wa ukanda wa wanyamapori |
| | ii. Kuimarisha sera, miundombinu, na mifumo ya ufuatiliaji ili kusaidia ukanda wa wanyamapori |
| | iii. Kurasimisha mifumo ya ushirikishwaji wa jamii na utatuzi wa migogoro ili kusaidia ulinzi wa shoroba za wanyamapori. |
| | 4.4 Kuongeza vituo vya malazi ya gharama nafuu katika hifadhi za taifa kwa ajili ya watalii wa ndani kutoka 10 hadi 22. |
| | i. Kuandaa na kurasimisha mpango wa taifa wa upanuzi na uboreshaji wa vituo vya malazi ya gharama nafuu kwa watalii wa ndani. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 4.5 Kuanzisha mfumo wa kidijitali wa kufanya miamala na kutoa huduma za kitalii . |
| | i. Kuandaa na kutumia sanifu, viwango na mfumo jumuishi ya kidijitali kwa ajili ya kurahisha matumizi ya mfumo wa taifa wa maombi ya uwekaji nafasi za utalii. |
| | 4.6 Kuandaa fursa za kuvutia uwekezaji kwa wawekezaji wa kimataifa zinazolenga hoteli za kifahari, vivutio vya utalii na miundombinu ya utalii inayolenga masoko ya kimataifa. |
| | i. Kupitia na kuimarisha sera za kutenga, kuandaa, na kugawa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa kigeni katika miundombinu ya utalii wa daraja la juu. |
| | 4.7 Kutoa motisha za kila mwaka kwa biashara za utalii ili kuchochea utekelezaji wa mbinu endelevu, ikiwa ni pamoja na upunguzaji wa taka, matumizi bora ya nishati, na uhifadhi wa mazingira. |
| | i. Kuandaa na kutumia mfumo wa motisha za kifedha na utambuzi kwa ajili ya mbinu endelevu za utalii. |
| 5. Angalau asilimia 40 ya biashara za utalii ziwe zimeimarishwa kidijitali kufikia Juni 2031. | 5.1 Kuendeleza vituo vitano vya utalii wa kidijitali (Smart Tourism Destinations) vilivyowezeshwa na teknolojia ya Intaneti ya Vitu (IoT), Akili Unde (AI), na uchambuzi wa takwimu mchanganyiko (Big Data) ili kuboresha uzoefu wa wageni. |
| | i. Kuandaa na kutumia mifumo ya miundombinu ya utalii wa kisasa inayounganisha teknolojia ya Intaneti ya Vitu (IoT), Akili Unde (AI), na uchambuzi wa Big Data . |
| | 5.2 Kuzindua majukwaa ya mafunzo ya mtandaoni kwa wataalamu wa utalii ili kuimarisha ujuzi katika ukarimu, huduma kwa wateja, na uelewa wa kidijitali. |
| | i. Kuandaa na kutumia usanifu, viwango, na mfumo wa maudhui kwa ajili ya majukwaa ya mafunzo ya utalii kwa njia ya mtandao. |
| | 5.3 Kuanzisha kituo cha taifa cha takwimu za utalii (National Tourism Data Hub) kwa ajili ya kukusanya, kuchambua, na kusambaza takwimu za wakati halisi kuhusu mienendo ya watalii, mapendeleo yao, na mchango wa kiuchumi. |
| | i. Kuandaa na kurasimisha usanifu, utawala, na mfumo wa uendeshaji wa kituo cha taifa cha takwimu za utalii. |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya kujengea uwezo na saidizi ili kuhakikisha uendelevu katika kujifunza na ushiriki wa sekta nzima. |
| | iii. Kusawazisha na kurasimisha matumizi ya mfumo wa malipo ulioumganishwa kwenye mashirika yote ya Mali asili na utalii. |
| | 5.4 Kulea bunifu za utalii zinazolenga kuleta majibu ya bunifu za kidijitali, kama vile programu endelevu za usafiri na uzoefu wa kitamaduni. |
| | i. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya uvumbuzi na mifumo ya ufadhili kwa uanzishaji wa bunifu za utalii |
| 6. Kufikia kiwango cha matumizi ya mfumo jumuishi wa utalii wa kisasa (smart tourism ecosystem) nchini kwa asilimia 33, unaoendeshwa na majukwaa | 6.1 Kuanzisha huduma za uonaji wa uhalisia (Virtual Reality – VR) katika maeneo ya kitamaduni na urithi ili kuvutia watalii wanaopenda teknolojia na kutoa uzoefu wa kina kwa wageni. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| ya kidijitali, miundombinu na uboreshaji wa matumizi ya rasilimali kwa kutumia teknolojia za kidijitali kufikia Juni 2031. | i. Kuandaa na kutumia teknolojia fungamani na viwango vya maudhui kwa uzoefu wa uonaji wa uhalisia. |
| | 6.2 Kuanzisha mfumo thabiti wa ubunifu kwa ajili ya matumizi ya teknolojia bunifu katika sekta ya utalii. |
| | i. Kuendeleza miundombinu ya ubunifu pamoja na mifumo ya utawala inayounga mkono. |
| | 6.3 Kuimarisha nguvu kazi kwa ujuzi unaohitajika kwa teknolojia za kisasa. |
| | i. Kuanzisha programu za mafunzo endelevu na uboreshaji wa ujuzi katika mifumo ya kitaifa ya ujuzi wa utalii. |
| | ii. Kuendeleza na kurasimisha ushirikiano na mifumo ya uthibitisho kupitia ushirikiano kati ya sekta, vyuo vya elimu na serikali kila mwaka. |
| | 6.4 Kuunda mazingira yanayotabirika na yanayofaa kwa utalii, ubunifu wa ki teknolojia na maendeleo ya rasilimali watu. |
| | i. Kuimarisha mifumo ya sera, miundombinu, na ufadhili ili kuunga mkono ubunifu katika utalii. |
| 7. Kuifanya Tanzania kuwa kituo kikuu cha utalii wa matukio, utamaduni, na ikolojia kufikia Juni 2031. | 7.1 Kuendeleza uzoefu wa kina wa utalii wa kitamaduni (mfano: Maeneo ya Urithi wa Dunia ya UNESCO, ziara za jamii za asili, sherehe za kitamaduni) unaovutia wasafiri wa kimataifa wanaopenda historia na utamaduni. |
| | i. Kuanzisha mifumo ya masoko ya kidijitali na mitandao ya kijamii. |
| | ii. Kuweka mifumo ya kitaasisi ya ushiriki na ushirikiano wa kimkakati katika maonyesho ya kimataifa ya utalii. |
| | 7.2 Kufanya kampeni ya utambulisho wa kimataifa kupitia majukwaa ya kidijitali, mitandao ya kijamii na maonyesho ya kimataifa ya utalii ili kuongeza uelewa wa huduma za utalii za Tanzania. |
| | i. Kuweka mifumo ya masoko ya kidigitali na mitandao ya kijamii. |
| | ii. Kuweka mifumo ya kitaasisi ya ushiriki na ushirikiano wa kimkakati katika maonyesho ya kimataifa ya utalii. |
| | 7.3 Kuandaa dhana za ukusanyaji na uchakataji wa takwimu pamoja na kufuatialia utendaji wa sketa ya utalii, demographia ya watalii na masoko yanayoibukia ili kuoainisha huduma za utalii wa Tanzania na mahitaji ya kimataifa. |
| | i. Kuanzisha na kuhalalisha jukwaa la kituo shirikishi cha uangalizi wa takwimu za utalii. |
| | ii. Kupitisha na kusanifisha uchambuzi wa kina wa takwimu na teknolojia zinazoibuka ndani ya kitovu cha takwimu. |
| | 7.4 Kuanzisha vituo vya mafunzo ya ufundi stadi kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kutoa programu maalum za mafunzo zinazoendana na viwango vya kimataifa vya utalii na mienendo inayoibuka. |
| | i. Kuandaa mitaala na kurasimisha mifumo ya kukuza uwezo. |
| | ii. Kuendeleza miundombinu ya kisasa na kuoanisha viwango vya kiteknolojia katika vituo vya mafunzo. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 7.5 Kuhamasisha mikakati ya kukuza bidhaa za utalii za Tanzania, kuvutia watalii wa kimataifa wanaotumia kiasi kikubwa cha fedha na kutumia sehemu zinazokua kwa kasi katika sekta ya utalii duniani. |
| | i. Kuweka mifumo ya kitaasisi ya ukuzaji, uendelezaji, na utofautishaji wa bidhaa za utalii. |
| | ii. Kuimarisha miundombinu ya kiwango cha juu na upatikanaji wa masoko kupitia mifumo ya uwekezaji wa kimkakati. |
| | iii. Kuandaa na kurasimisha utambulisho wa chapa duniani, kampeni za masoko, na mifumo ya ushirikiano wa kimkakati. |
| | 7.6 Kuendeleza ushirikiano na mashirika ya ndege ya kimataifa na waendeshaji wa safari za utalii ili kuanzisha njia mpya za usafiri, pamoja na kuitangaza Tanzania katika maonesho ya kimataifa ya utalii na majukwaa ya kidijitali. |
| | i. Kuandaa na kuweka mifumo ya uunganishaji wa safari za anga na ufunguaji wa njia mpya za ndege. |
| | ii. Kuwa na ushirikiano rasmi na wa kimkakati na waendeshaji wa safari za utalii wa kimataifa. |
| | iii. Kuimarisha mifumo ya masoko ya kidijitali na ushiriki katika majukwaa ya kimataifa. |
| | 7.7 Kuendeleza miundombinu ya utalii, ikijumuisha makazi ya kisasa, vituo vya mikutano, mapumziko rafiki kwa mazingira, na mitandao ya usafiri (mfano: viwanja vya ndege, barabara na reli) ambayo inaunga mkono mnyororo wa thamani wa utalii. |
| | i. Kuandaa mifumo endelevu ya utalii wa hadhi ya juu na miundombinu ya utalii wa mikutano. |
| | ii. Kuweka mifumo rafiki na ya kisasa ya maendeleo ya miundombinu ya usafirishaji. |
| | 7.8 Kuanzisha Mamlaka ya Taifa ya Utalii na Ukarimu (NTHA). |
| | 8.3 Kuweka programu za mafunzo kwa wataalamu wa utalii ili kuboresha ubora wa huduma za ukarimu, uongozaji watalii na huduma kwa wateja wa kiwango cha juu. |
| | i. Kuandaa mitaala inayolingana na viwango vya kimataifa. |
| | ii. Kuanzisha mifumo ya kisasa ya utoaji mafunzo na kujenga uwezo. |
| | iii. Kuanzisha miongozo ya ushirikiano kati ya sekta ya utalii na uendelezaji kitaaluma. |
| | 8.4 Kujenga hoteli, migahawa na kutoa huduma za utalii zenye hadhi ya juu katika maeneo tengefu |
| | i. Kuandaa viwango vya miundombinu na vituo vya huduma za utalii |
| | ii. Kuandaa miongozo ya kuboresha na kusimamia uzoefu wa wageni. |
| | 8.5 Kukuza utalii endelevu ili kuvutia watalii wa kipato cha juu na wanaojali mazingira |
| | i. Kuandaa na kuanzisha viwango vya kijani (green standards) pamoja na mifumo ya uthibitisho. |
| | ii. Kuanzisha miongozo ya kukuza miundombinu na uendeshaji endelevu. |
| | iii. Kuanzisha miongozo ya ushirikishwaji wa jamii. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | iv. Kuanzisha miongozo ya kimataifa ya masoko na uhamasishaji wa utalii endelevu. |
| **2.2. Sekta ya Fedha** | |
| Lengo la 1: Kuimarisha utawala bora, ufanisi wa uendeshaji na uthabiti wa kifedha ili kuhakikisha ushindani na uimara wa sekta ya benki za biashara | |
| 1. Kuongeza kiwango cha uwiano wa utoshelevu wa mtaji (CAR) kufikia zaidi ya asilimia16.5 ifikapo Juni 2031 | i. Kuimarisha udhibiti na usimamizi wa vihatarishi kwenye mahitaji ya mitaji |
| | ii. Kuwezesha kuunganisha na kununuliwa kwa benki dhaifu ili kuimarisha mitaji. |
| | iii. Kuanzisha na kuendesha uwekezaji wa muda mrefu wa sekta ya umma na binafsi katika benki za biashara. |
| 2. Kuongeza kiwango cha amana dhidi ya Pato la Taifa (Deposit-to-GDP ratio) kufikia angalau asilimia 40 ifikapo Juni 2031 | i. Kuimarisha mfumo wa fedha wa kidijitali unaoongozwa na matumizi ya takwimu. |
| | ii. Kuweka mifumo ya kitaifa ya kuweka akiba inayotumia motisha zinazohusishwa na amana. |
| | iii. Kuongeza kiwango cha ujumuishaji wa huduma za kifedha kupitia mawakala wa benki na upanuzi wa huduma za kidijitali nchi nzima. |
| 3. Kudhibiti mikopo chechefu (NPLs) kubaki chini ya 5% ifikapo Juni 2031 | i. Kuanzisha mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa vihatarishi vya mikopo unaotumia AI na uchambuzi wa takwimu (big data) |
| | ii. Kuweka sharti la matumizi ya mifumo madhubuti ya urejeshaji na ufuatiliaji wa mikopo. |
| | iii. Kuunganisha sera za utoaji mikopo zinazozingatia mazingira, jamii na utawala (ESG) katika kanuni za sekta ya benki. |
| 4. Kuongeza kiwango cha mikopo kwa sekta binafsi kufikia 25% ya Pato la Taifa ifikapo 2030 | i. Kuimarisha sera za ugawaji mtaji kulingana na vihatarishi kwa ajili ya kuhamasisha mikopo kwenye sekta zenye tija kubwa. |
| | ii. Kuimarisha mifumo ya dhamana ya Serikali kwenye mikopo ili kupunguza vihatarishi vya utoaji mikopo kwa SMEs na sekta za kimkakati. |
| | iii. Kuanzisha jukwaa la kidijitali la kupima uwezo wa mkopaji (credit scoring) kwa kutumia fintech na takwimu (big data). |
| 5. Kuongeza idadi ya watu wazima wanaotumia huduma rasmi za kifedha kufikia 90% ifikapo Juni 2031 | i. Kuanzisha programu za elimu ya fedha za kidijitali. |
| | ii. Kutoa motisha kwa benki za biashara kuanzisha akaunti na waleti za gharama nafuu kwa wananchi wa vijijini na makundi yaliyotengwa |
| | iii. Kuunganisha majukwaa ya pesa za simu na benki ili kutoa huduma jumuishi. |
| **Lengo la 2:** Kuimarisha mtaji wa Taasisi za Kifedha za Maendeleo (DFIs), na kuwezesha uwekezaji wa sekta binafsi, mifuko ya hifadhi ya jamii na makampuni ya bima ili kuwa na ukuaji na uendelevu | |
| 1. Kuongeza mtaji wa DFIs kufikia angalau asilimia 1.25 ya Pato la Taifa ifikapo Juni 2031 | i. Kuanzisha mpango wa hatua kwa hatua wa Serikali kuongeza mtaji wa DFIs. |
| | ii. Kuongeza vyanzo vya fedha kupitia hati fungani za ndani na ushirikiano na mifuko ya pensheni, makampuni ya bima na wawekezaji wengine wa taasisi. |
| | iii. Kutumia aina tofauti za miongozo ya fedha (blended finance) na kupata ufadhili kutoka AfDB, Benki ya Dunia, EIB na washirika wengine wa kimataifa. |
| 2. Kufikia uwiano wa chini wa mtaji wa umma na binafsi wa 1:1.14 katika DFIs kufikia | i. Kuimarisha mifumo ya udhibiti ili kuruhusu ushiriki wa usawa wa ndani na nje ya nchi kwa wawekezaji binafsi wa ndani na nje, ikijumuisha ubinafsishaji kwa sehemu. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| Juni 2031. | ii. Kuwezesha ushiriki wa IFC, AfDB, EIB, na taasisi kama hizo ili kuchochea mapato ya mtaji wa binafsi. |
| | iii. Kuongeza uwekezaji wa sekta ya kibinafsi, ikijumuisha makampuni, biashara za ndogo na za Kati na wawekezaji wa taasisi. |
| **Lengo 3:** Kuboresha mwongozo wa maendeleo ya Taasisi za Fedha kwa kuimarisha usimamizi wa vihatarishi na kuboresha michakato ya tathmini ya mikopo na kuhakikisha ufanisi katika ufuatiliaji na urejeshaji. | |
| 1. Kusimamia kwa mikopo chechefu na DFIs kuwa chini ya asilimia 5 kufikia Juni 2031. | i. Kuimarisha mifumo ya usimamizi na udhibiti wa vihatarishi kupitia nyenzo za AI, viwango vya usimamizi wa sekta binafsi, ugawaji wa mikopo, na zana zinazozingatia usawa. |
| | ii. Kuongeza ufadhili wa miundombinu, uzalishaji na kilimo. |
| | iii. Kuongeza wigo wa ufadhili kwa biashara za ndogo na za kati na kampuni chipukizi kwa kitaji ya ubia and mikopo ya kidigitali. |
| | iv. EKuanzisha dirisha la ufadhaili kwa teknolojia ya masuala ya fedha na makampuni yanayoendeshwa kiteknolojia. |
| | v. Kutumia mfumo wa block chain kufadhili wa mnyororo wa thamani wa kilimo na ufadhili endelevu wa modeli za kijani. |
| **Lengo 4:** Sekta ndogo ya bima iliyoimarishwa inayoongozwa na sekta binafsi ambayo huchochea ukuaji endelevu wa uchumi kwa kuongeza uwepo wa bima, kuimarisha uthabiti wa soko na kutoa matoleo mbalimbali ya bidhaa. | |
| 1. Kuongeza matumizi ya bima (jumla ya malipo kwa Pato la Taifa) hadi asilimia 2.6 ifikapo Juni 2031 | i. Kuimarishwa kwa mifumo ya udhibiti, kukuza bima ndogo, na kuendesha programu za uhamasishaji nchi nzima. |
| | ii. Kukuza ubunifu kupitia bima ya kidijitali, kilimo mahsusi na bidhaa za afya, na kuboresha ujuzi wa kufikiri. |
| | iii. Kuongeza ushiriki wa soko la bima ya kikanda na kimataifa kupitia viwango vya kimataifa vya uandishi, uhakikisho wa bima na madai. |
| Lengo 5: Kukuza mtaji na kuwezesha udhibiti wa kanuni, kuhuisha na viwango vya UMIC ili kukuza ukuaji wa uchumi na uhimilivu. | |
| 1. Kufikia asilimia 33 ya ufadhili wa mtaji na ujumuishaji kamili wa huduma ndogo za kifedha vijijini ifikapo Juni 2031. | i. Kuimarisha mifumo ya udhibiti na kuanzisha MSMEs- na mbinu za kifedha zinazofaa vijijini, ikijumuisha dhamana ya mikopo ya mikopo midogo midogo na miamala ya kidijitali |
| | ii. Kuwezesha uthabiti na ujumuishwaji wa sekta ndogo ya fedha na ushirikishwaji wa sekta ya mikopo midogo midogo kupitia uwekaji rekodi za biashara zisizo rasmi kidijitali, kandarasi mahiri, na ufadhili unaozingatia ESG. |
| 1. Asilimia 25 ya huduma za kifedha kupatikana kupitia mfumo wa kidigitali ifikapo Juni 2031. | i. Kutekeleza huduma za benki ndogo za kidijitali na huduma za simu/kidigitali katika maeneo ya vijijini ambayo hayana huduma ya kutosha. |
| | ii. Kuandaa majukwaa ya ukopeshaji yanayoendeshwa na akili mnemba (AI) pamoja na sera zinazosaidia teknolojia ya kifedha (fintech) |
| | iii. Kuunganisha mifumo ya kidijitali ya mikopo midogo midogo na suluhu za fedha zisizodhibitiwa na mamlaka kuu (DeFi). |
| 2. Kubadilika kuelekea mfumo unaoendeshwa kikamilifu na sekta ya mikopo midogo midogo kwa Biashara Ndogo na za Kati (SME), ukiwa na ujumuishi wa | i. Kuimarisha mifumo ya udhibiti ili kuboresha ujumuishaji wa kifedha wa SME na vijijini, na kukuza uwekezaji wa vijijini. |
| | ii. Kuendesha programu za kitaifa za elimu ya kifedha kwa MFIs na SMEs. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| maeneo ya vijijini kwa asilimia 20–25 ifikapo Juni 2031. | |
| **Lengo 6:** Kuongeza mikopo na kuboresha udhibiti wa kanuni ili kuhakikisha unaendana na viwango vya UMIC ili kuchochea maendeleo endelevu na uthabiti wa kifedha**.** | |
| 1. Punguza kutengwa kwa kukosa huduma za kifedha hadi chini ya asilimia 10 ifikapo Juni 2031. | i. Kuongezaji upatikanaji wa huduma za kifedha kwa watu wasio na huduma nzuri, ikijumuisha maeneo ya vijijini, kupitia benki, MFIs, na ushirikiano wa fintechs Kupanua upatikanaji wa huduma za kifedha kwa makundi yaliyokosa fursa, ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijijini, kupitia ushirikiano kati ya mabenki, taasisi za mikopo midogo midogo (MFIs), na kampuni za teknolojia ya kifedha (fintechs) |
| | ii. Kuwezesha ujuzi wa masuala ya kifedha nchini kote ili kuongeza ufahamu wa manufaa ya akaunti |
| | iii. Kuboresha huduma za sekta ya kifedha chini ya NFIF, ikijumuisha majukwaa kimtandao na kidigitali kupitia mabenki. |
| 2. Kuongeza ukopaji rasmi hadi asilimia 31.2 ifikapo Juni 2031. | i. Kufanya mageuzi ya mifumo ya mikopo ili kuwezesha MSMEs, makampuni ya biashara ya vijijini, na sekta isiyo rasmi. |
| | ii. Kuboresha huduma za sekta ya kifedha chini ya NFIF, ikijumuisha majukwaa kimtandao na kidigitali kupitia mabenki. |
| 3. Kuongeza umiliki wa akaunti za benki hadi asilimia 33 na akiba hadi asilimia 35 ifikapo juni 2031. | i. Kuongeza miundombinu ya huduma za fedha kidigitali na kuhuisha ubunifu wa teknolojia ya masuala ya kifedha ili kuipa nafasi Tanzania kuongoza kikanda. |
| | ii. Kutekeleza programu ya kitaifa ya ujuzi na utaalamu wa masuala ya fedha ili kuongeza imani na ushiriki wa watumiaji |
| **Lengo 7:** Kuboresha mazingira ya biashara kwa ajili ya ukuaji wa mtaji wa biashara Tanzania na mfumo wa uwekezaji binafsi kwa kuongeza upatikanaji wa fedha kwa kampuni chipukizi na Makampuni makubwa. | |
| 1. Kuongezeka uwekezaji wa mtaji na uwekezaji binafsi kwa kampuni chipukizi kutoka dola za Marekani milioni 52 hadi zaidi ya dola za Marekani milioni 242 kwa mwaka ifikapo Juni 2031. | i. Kuanzishwa Mtandao wa Kitaifa wa Wawekezaji wa binafsi wa kampuni chipukizi na kurekebisha kanuni za uwekezaji binafsi (PE) na uwekezaki wa mtaji (VC). |
| | ii. Kuanzisha mfuko wa kitaifa kwa ajili ya kampuni chipukizi ili kuwezesha mitaji ya awali, ruzuku ya R&D kutoka Serikalini, na kuimarisha Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kwa IPOs na M&A. |
| | iii. Kuwezesha ushirikiano wa AfCFTA ili kuvutia uwekezaji wa kikanda. |
| **Lengo 8:** Kuongezeka kwa mtaji wa ubia na mikataba wawekezaji binafsi utakaowezesha ustawi wa mfumo wa kampuni chipukizi na ukuaji wa biashara unaoongozwa na ubunifu. | |
| 1. Kuongeza mikataba ya uwekezaji binafsi na uwekezaji kwa kampuni chipukizi kutoka dola za Marekani milioni 10 hadi 30 kwa mwaka ifikapo Juni 2031. | i. Kuanzisha Programu ya Kitaifa ya Hatimiliki ili kulinda uvumbuzi wa kampuni chipukizi. |
| | ii. Kuendeleza Hifadhi za Teknolojia na Vituo vya Ubunifu na Ubia wa Kibiashara ili kuchochea mageuzi ya kidijitali na ujasiriamali. |
| **Lengo 9:** Kukuza ujasiriamali jumuishi na endelevu, utakaowezesha ushiriki katika ukuaji wa kiuchumi na kuleta athari chanya katika mazingira. | |
| 1. Kuongeza nafasi kiashiria cha uvumbuzi kwa Tanzania duniani hadi 90 ifikapo Juni | i. Kuanzisha kongane za kiteknolojia na vituo vya ubunifu na mfuko wa uwekezaji wa kibiashara uliokusudiwa wa kutumia akili unde( AI), teknolojia ya kibiologia (biotech) na technolojia za kimazingira. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 2031. | ii. Kuanzisha masoko ya upili ya kikanda, kuwezesha kampuni chipukizi 5 na kuwezesha mifuko ya fidia kuwekeza kwenye makampuni chipukizi. |
| | iii. Kuanzisha programu za ufadhili wa tafiti na maendeleo (R&D) pamoja na ushirikiano wa kibiashara na kampuni chipukizi za kimataifa. |
| **2.3. Tasnia ya Michezo na Ubunifu.** | |
| **Lengo 1.** Kuimarishwa kwa ushindani wa ndani, kikanda na kimataifa wa tasnia ya michezo na ubunifu, kukuza ukuaji, na fursa za uwekezaji<br>. | |
| 1. Ukuaji kwa mwaka wa sekta kwa asilimia 20 ifikapo Juni 2031 | i. Kujenga na kuboresha miundombinu ya michezo (viwanja, vituo vya mafunzo na viwanja) kote nchini kwa kuanzisha angalau vituo 5 vya ubora wa kimataifa. |
| | ii. Kuzindua programu za kila mwaka za ufadhili wa masomo ili kufadhili angalau vijana 100 wenye vipaji wa shule na vyuo kwenda nje ya nchi kusomea tasnia ya ubunifu. |
| | iii. Kuanzisha sera na vifurushi vya motisha ili kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika miundombinu ya michezo na sekta za ubunifu. |
| 2. Kuvutia watalii zaidi 100,000 wa michezo kila mwaka ifikapo Juni 2031 | i. Kuanzisha mfumo/utaratibu wa biashara ya michezo ili kukuza utalii wa michezo. |
| | ii. Kuandaa kalenda ya kila mwaka ya matukio ya michezo na utamaduni ya kitaifa, kikanda, na kimataifa. |
| 3. Wasanii wa Tanzania kutambulika kimataifa katika angalau nyanja moja kuu ya ubunifu ifikapo Juni 2031. | Kujenga mfumo endelevu wa utengenezaji wa filamu, usambazaji na kurekodi muziki. |
| | i. Kuanzisha majukwaa ya kikanda kwa wasanii wa Tanzania kuonesha kazi zao za ndani na nje ya nchi. |
| 5. Mashirika yote ya wabunifu na michezo ya Tanzania yawezeshe wasanii kupokea mirahaba kwa kazi zao kila mwaka ifikapo Juni 2031. | Kuimarisha Mifumo ya Hakimiliki na Hatimiliki (IP) |
| | i. Anzisha mfumo bora wa usajili wa hakimiliki na IP ili kulinda wasanii wa ndani dhidi ya matumizi yasiyoidhinishwa na uharamia |
| **2.4. Sekta ya Majengo/ milki kuu** | |
| **Lengo 1:** Kuboresha mazingira ya ushindani, uwazi na rafiki ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje katika sekta ndogo ya majengo, kukuza ukuaji wake na kuongeza mchango wake katika uchumi. | |
| Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya majengo katika Pato la Taifa kutoka asilimia 4 hadi asilimia 5 ifikapo Juni 2031. | i. Kuimarisha mifumo ya udhibiti inayohusiana na maendeleo ya ardhi na miji ili kuchochea maendeleo ya soko la mali isiyohamishika |
| 2. Kuendeleza jumla ya nyumba milioni 2 ili kukidhi ongezeko la idadi ya watu mijini ifikapo Juni 2031<br>. | i. Kuanzisha na kuhamasisha ubia kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuongeza upatikanaji wa nyumba za bei nafuu chini ya Mpango wa Nyumba za bei nafuu Tanzania (TAHP) |
| | ii. Kuanzisha mfumo wa motisha kwa nyumba za utaratibu wa Ubia kati ya sekta binafsi na umma |
| | iii. Kuendeleza teknolojia za ujenzi wa gharama nafuu na endelevu ili kuharakisha ujenzi na kupunguza gharama<br>iv. |
| | v. Kuwezesha kuhamisha teknolojia na maendeleo ya ujuzi |
| | vi. Kuwapa motisha wazalishaji wa ndani wa vifaa ya ujenzi |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 3. Kuongeza Uwiano wa dhamana kwa Pato la Taifa kutoka asilimia 0.5 hadi asilimia 2 ifikapo Juni 2031 | 3.1. Kuanzisha na kuendesha dirisha/taasisi za fedha za nyumba kama TMIRC/TIB zenye angalau TZS bilioni 100 |
| | 3.2. Kufanya marekebisho ya udhibiti ili kupunguza viwango vya riba ya mikopo ya nyumba kutoka wastani wa asilimia 15 hadi asilimia 12 |
| | 3.3.Kuanzisha na kuwezesha upatikanaji wa ardhi zenye huduma kwa waendelezaji binafsi na umma |
| | i. Kuhuishwa na kuanzisha benki kwa ajili ya miradi na mali zisizohamishika |
| 4. Uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs), Miji Mahiri, Kongane za biashara za kimataifa na vitovu vya usafirishaji kufikia jumla ya Dola za marekani bilioni 3 ifikapo Juni 203. | Kuanzisha miji mahiri mitatu (3) yenye mpango wa kujiendesha kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya usimamizi wa miji kwa ufanisi |
| | i. Kuanzishwa kwa miji mahiri |
| 5. Jumla ya thamani ya mali inayosimamiwa katika REIT na TAHF kuongezeka hadi dola za marekani bilioni 1.5 kufikia Juni 2031 | i. Kuongeza mtaji wa masoko ya mitaji kupitia uandikishaji wa REITs na TAHF kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) |
| | ii. Kufadhiliwa kwa nyumba za bei nafuu kupitia mipango mahususi na zana bora za usimamizi kwa REITs na TAHF |
| | iii. Kuimarisha maendeleo yanayolenga Usafiri wa Umma (ToD) iliyoanzishwa kwa kujumuisha upangaji mchanganyiko wa matumizi ya ardhi na mifumo bora ya usafiri wa umma |
| | iv. Kuandaa mpango wa usimamizi wa ToD, zana, na mbinu za ufadhili |
| 4. Kufanyika kwa jumla ya asilimia 50 ya miamala ya milki kuu | i. Kuanzisha miundombinu ya kidijitali ya dhamana za kielektroniki, uhamishaji wa mali kidijitali, na mifumo ya upangaji miji inayoendeshwa na AI |
| | ii. Kuanzisha mfumo rafiki wa usajili wa mali kwa watu wasio raia kupitia marekebisho ya udhibiti |
| | iii. Kutekeleza mikakati ya usimamizi wa milki kuu inayostahimili mabadiliko ya tabianchi, ikijumuisha kanuni za ujenzi na viwango, ili kuimarisha uendelevu katika ujenzi |
| | iv. Kuanzisha viwango vya miundo na zana zinazostahimili mabadiliko ya tabisanchi |
| | v. Kupitishwa kwa kanuni za ujenzi unaostahimili mabadiliko ya tabianchi |
| **2 Sekta ya Biashara.** | |
| **Lengo 1.** Kuimarishwa kwa sekta ya biashara yenye ushindani wa kimataifa, sekta ya biashara ya kidijitali, kuwezesha mauzo ya nje, kukuza ukuaji jumuishi kwa SME na kuimarisha ushirikiano na masoko muhimu ya kikanda na kimataifa. | |
| 1. Bidhaa zilizoongezwa thamani katika mauzo ya nje kuongezeka kwa asilimia 10 kufikia Juni 2031 | i. Kuanzisha vituo vya usindikaji wa mazao ya kilimo katika maeneo ya mauzo ya nje, kuongeza mifumo ya umwagiliaji, na kusambaza pembejeo bora kwa wakulima |
| 2. Farihisi ya utendaji wa usafirishaji (LPI) kuboreshwa kwa asilimia 10 na kufikia nafasi ya 50 Bora duniani kufikia Juni 2031. | i. Kuboresha miundombinu ya bandari na kuhuisha barabara muhimu na maungio ya reli kwenye bandari na bohari za nchi kavu |
| | ii. Kutengeneza mifumo ya usimamizi wa bandari inayoendeshwa na AI na mifumo ya kidijitali, kujenga maghala mahiri, na kutumia mifumo ya satelite kufuatilia shehena za mizigo |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | iii. Kuunganisha na kuhuisha michakato yote ya forodha katika maeneo makuu ya biashara ya kuingia na kutoka |
| | iv. Kunzisha vituo maalum vya mafunzo ya ugavi ili kujenga wafanyakazi wenye ujuzi kwa ajili ya mlolongo wa ugavi wa kisasa |
| 3. Kuongezeka kwa biashara ya kidijitali kufikia kuchangia asilimia 50 ya biashara yote ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kuanzisha na kuzindua majukwaa ya biashara ya kielektroniki yanayoendeshwa na AI kwa soko la Afrika na kuanzisha mfumo wa malipo ya kidijitali wa *blockchain* |
| | 3.2 Kutekeleza ya masuala ya usafirishaji wa masuala ya IoT na Kuanzisha vitovu vya biashara kikanda vya kielektroniki ili kuongeza ufanisi |
| | 3.3 Kuhuisha kanuni za kitaifa za biashara ya kidigitali na mbinu bora za kimataifa ili kuweka mazingira thabiti na yanayoweza kutabirika |
| **3. Sekta ya Biashara.** | |
| **Lengo 1:** Kuongezeka kwa uwekezaji binafsi unaochochea ubunifu, kukuza ushindani na ujumuishaji,unaoshughulikia mahitaji ya ndani na kuunganisha Tanzania katika minyororo ya thamani ya kimataifa ili kusaidia ukuaji endelevu wa uchumi. | |
| 1. Uwekezaji binafsi kuongezeka hadi angalau asilimia 5 ya Pato la Taifa ifikapo 2030.<br>. | 1.1 Kuweka mfumo thabiti wa utoaji wa motisha na usaidizi unaolengwa kwa wawekezaji wa kimkakati, uanzishaji wa teknolojia ya juu na biashara za kidijitali ili kukuza ubunifu, ujasiriamali na miundo ya biashara inayotegemea teknolojia |
| | i. Uhakiki wa kina wa kanuni za biashara ili kuboresha urahisi wa kufanya biashara |
| | ii. Kupitia mifumo ya udhibiti ya Mashirika ya Umma ili kuhakikisha uwazi na uwekezaji wenye faida |
| | iii. Kuanzisha mwongozo mahsusi unaozingatia vigezo vya kutoa motisha iliyopangwa kwa uwekezaji wa kimkakati na makampuni chupukizi ya teknolojia ya juu |
| | iv. Kuhuisha michakato yote ya uwekezaji na kuimarisha uwezo wa mashirika ya kukuza uwekezaji kutatua migogoro |
| | v. Kuwezesha ukuaji wa viwanda unaotegemea kongane na uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi |
| | vi. Kuongeza wigo wa huduma za kifedha na kuboresha miundombinu ili kuwezesha ukuaji wa biashara |
| 2. Ushiriki wa mnyororo wa thamani duniani kuongezeka hadi angalau asilimia 25 ya Pato la Taifa ifikapo 2030 | 2.1 Kutekeleza mabadiliko ya kimkakati kuelekea mageuzi ya sekta ya uzalishaji wa ndani kuwa viwanda shindani, vinavyoelekeza mauzo ya nje |
| | i. Kutekeleza programu ya kitaifa ya kuunganisha MSME za ndani na kampuni kubwa za kimataifa ili kuongeza ushiriki wa mnyororo wa thamani |
| | ii. Kutumia nafasi ya Kijiografia ya Kimkakati ili kuunganishwa kwa ufanisi zaidi na masoko ya kikanda na kimataifa |
| | iii. Kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa kuwezesha biashara ili kunufaisha eneo la Tanzania na kuunganishwa vyema na masoko ya kikanda na kimataifa |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | iv. Kutoa kipaumbele kwa maendeleo ya sekta za kimkakati (k.m., usindikaji wa mazao ya kilimo, nishati) kwa ajili ya mabadiliko ya kimuundo na mwelekeo wa mauzo ya nje |
| 3. Utofauti ya kipato baina ya watu pamoja na tofauti za maendeleo kijiografia kuendelea kubaki katika viwango vya sasa ifikapo 2030 | i. Kuimarisha sera za fedha zenye usawa, ikiwemo wigo wa kodi unaoendana na programu za kijamii |
| | ii. Kutoa kipaumbele kwa viwanda vinavyohitaji nguvu kazi kubwa na usindikaji wa mazao ya kilimo katika maeneo ya vijijini na baadhi ya maeneo mijini ili kutengeneza ajira nyingi |
| | iii. Kuwekeza katika miundombinu ya usafiri, nishati na mindombinu ya kidijitali katika mikoa yote ili kupunguza tofauti za mijini na vijijini |
| | iv. Kuhakikisha ubia na ushiriki wa lazima wa mtaji wa ndani katika miradi ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje |
| **4. Ushirikiano Baina ya Nchi mbili, Kikanda na Kimataifa** | |
| **Lengo 1.** Kuimarishwa kwa uwezo wa nchi ili kukuza vyema maslahi ya kiuchumi na kuinua ushawishi wa Tanzania duniani, kuchangia maendeleo endelevu na ushirikiano imara wa kimataifa. | |
| 1. I Kutekeleza majukumu ya kidiplomasia ya kiuchumi kikamilifu ili kukuza uwekezaji kwa asilimia 40 ifikapo 2030. | 1.1 Kufafanua na kuchapisha vipaumbele na maslahi ya kimkakati ya Tanzania katika nyanja ya kimataifa |
| | 1.2 Kuimarisha uwezo wa majadiliano kitaifa na kuanzsiaha mfumo wa taarifa wa kisasa kati ya wanadiplomasia waliopo nje na wa ndani |
| | 1.3 Kuboresha upangaji wa watumishi na muundo wa balozi na uwakilishi wa kidiplomasia ili kujielekeza katika matokeo ya kiuchumi |
| | 1.4 Kuimarisha Kituo cha mahusiano ya kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim kwa ajili ya kuwajengea uwezo kizazi kijacho cha wanadiplomasia wa kiuchumi |
| | 1.5 Kuzindua na kutekeleza mkakati wa utambulisho wa kimataifa ili kuboresha taswira ya Tanzania kama kituo cha uwekezaji |
| | 1.6 Kuongeza upatikanaji wa huduma za kibalozi katika miji ya kiuchumi na kuimarisha ushirikishwaji wa diaspora ili kuvutia uwekezaji na ujuzi |
| | 1.7 Kuimarisha ulinzi wa haki miliki na ushindani kwa kuzingatia viwango vya kimataifa |
| | 1.8 Kuhakikisha ujumuishaji wa masuala ya jinsia na fursa za vijana katika maeneo yote ya ushirikiano wa kimataifa |
| **5. Mwenendo wa Kimataifa.** | |
| **Lengo la 1:**Kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu imara cha nguvu za kiuchumi katika ngazi ya kikanda na kimataifa ifikapo Juni 2031, kupitia biashara ya kimkakati, uwekezaji na ushirikiano wa kidiplomasia, kuongeza ustahimilivu, ushindani na ustawi endelevu. | |
| 1. Tanzania kujumuishwa kikamilifu katika AfCFTA, EAC na SADC, kwa kufikia angalau asilimia 70 ya utekelezaji wa itifaki za biashara za kikanda ifikapo mwaka 2030 | **1.1.** Kukamilisha mahitaji yote ya kuhaulisha sera ya biashara ya kikanda, kuhakikisha mtirirko huru wa bidhaa, huduma na mitaji, na kufikia utekelezaji wa asilimia 100 wa itifaki za biashara za kikanda. |
| | 1.1 Kuhuisha sera za kitaifa za biashara na forodha kulingana na matakwa ya AfCFTA, EAC na SADC |
| | 1.2 Kukamilisha mikataba yote ya biashara ya pande mbili na ya pande nyingi iliyosalia inayohusiana na jumuiya za kikanda. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 1.3 Kuimarisha uwezo wa taasissi zinazoratibu vyombo vinavyohusika na masula ya biashara za kitaifa. |
| | 1.4 Kuzindua mfumo jumuishi wa biashara ya kidijitali unaoendeshwa na AI. |
| 2. Kuimarisha diplomasia ya Tanzania kwa kuingia makubaliano ya ushirikiano wa kimataifa na wadau watatu 3 muhimu, kuongeza matumizi ya Kiswahili katika mashirika 4 ya kimataifa, na kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kazi katika angalau taasisi moja ya kimataifa iliyoendelea ifikapo 2030 | **2.1** Kuimarisha ushawishi wa kidiplomasia wa Tanzania katika kupata ushirikiano wa kimataifa na kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kazi. |
| | i. Kuongeza mtandao wa balozi za Tanzania hadi kufikia nchi 6. |
| | ii. Kukuza diplomasia ya kitamaduni na ubadilishanaji wa elimu na nchi 25 na vyuo vikuu 35–40 |
| | iii. Kuwezesha huduma ya kutafsiri lugha ya kiswahili katika wakati halisi kupitia AI katika mikutano na nyaraka muhimu za AU na UN |
| | iv. Kuzindua jukwaa la diplomasia ya kidijitali linaloendeshwa na AI ili kuongeza ushirikiano wa kimataifa. |
| | v. Kuanzisha Baraza Maalumu la Biashara ya Kimataifa ili kuendeleza malengo ya diplomasia ya kiuchumi ifikapo Juni 2031. |
| 3. Kuifanya Tanzania kawa lango kuu la biashara barani Afrika kwa kufikia TEUs milioni 20 (Twenty-Foot Equivalent Units) za makontena kwa mwaka ifikapo Juni 2031 | **3.1** Kuitangaza Tanzania ili kuwa lango kuu la biashara |
| | i. Kukamilisha uboreshaji bandari za Dar es Salaam, Tanga, na Mtwara na kuzifanya kuwa za kisasa, na kuwezeshaa bandari ya Bagamoyo kufanya kazi kikamilifu. |
| | ii. Kuzindua mfumo wa bandari bora unaoendeshwa na AI ili kuwezesha bandari kuwa na uwezo wa kufikia malengo ya TEUs milioni 20 |
| 4. Kuanzishwa kwa mashirikiano ya uwekezaji kati ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuvutia uwekezaji kutoka nje (FDI's) katika sekta muhimu ifikapo Juni 2031 | 4.1 Kujadiliana na kuanzisha ushirikiano wa uwekezaji wa nchi na nchi, kikanda na wa kimataifa ili kuvutia Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka nje (FDIs) katika sekta muhimu za kimkakati |
| | 4.2 Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kitaifa wa ushirikiano wa uwekezaji wa pande mbili, kikanda na kimataifa. |
| | 4.3 Kuanzisha vitengo vya kukuza ushirikiano wa uwekezaji (IPPUs) ndani ya TISEZA na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuratibu na kufuatilia misheni za uwekezaji. |
| | 4.4 Kujadiliana na kupata makubaliano mapya ya pande mbili, kikanda na kimataifa kwa ajili ya uwekezaji wa Moja kwa Moja (FDI) katika sekta za kimkakati. |
| | 4.5 Kuandaa na kuhifadhi orodha ya miradi ya kibiashara na yenye matokeo makubwa kwa ajili ya kukuza uwekezaji |
| **6. Urasimishaji wa Uchumi na Usimamizi Wake** | |
| **Lengo 1:** Kurasimisha sekta isiyo rasmi ili kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi | |
| 1. Mchango wa Sekta Rasmi katika Pato la Taifa kuongezeka kutoka asilimila 55 had 63 ifikapo Juni 2030 | 1.1 Kuanzisha kitengo maalumu ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) cha kukuza na kuendeleza Biashara Ndogo na za kati (MSMEs). |
| | 1.2 kuzindua jukwaa la kidijitali, eneo moja la uandikishaji na jukwaa la uzingatiwaji wa kodi. |
| | 1.3 Kuanzisha programu maalumu ya kusaidia kurasimisha biashara zisizo rasmi. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 1.4 Kuandaa na kutekeleza motisha mahususi kwa sekta kwa lengo la kuwezesha urasimishaji. |
| | 1.5 Kuingiza biashara zisizo rasmi zilizosajiliwa kwenye minyororo ya ugavi ya sekta rasmi ya serikali na binafsi kupitia programu ya maendeleo ya wasambazaji. |
| 2. Kupunguza ajira katika sekta isiyorasmi kutoka asilimia 29 hadi 22 ifikapo Juni, 2031 | 2.1 Kuandaliwa kwa programu ya kitaifa kwa ajili ya kuongeza ujuzi na mafunzo ya ufundi, programu hii ni mahususi kwa ajili ya kusaidia wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kupata ujuzi wa kuwawezesha kupata ajira katika sekta rasmi zenye ujuzi wa juu. |
| | 2.2 Kutekeleza mpango wa motisha za ajira rasmi kwa biashara zinazochukua na kuhifadhi wafanyakazi wanaohama kutoka sekta isiyo rasmi, kwa kutoa ruzuku za muda wa mishahara au mikopo ya kodi. |
| | 2.3 Kuimarisha ukaguzi wa kazi na mifumo ya utekelezaji ili kuhakikisha viwango vya haki vya kazi, ulinzi wa wafanyakazi, na michango ya usalama wa kijamii, na kufanya ajira rasmi kuwa ya kuvutia zaidi. |
| | 2.4 Kuwezesha kuanzishwa kwa ushirika na vyama vya biashara ili kuwezesha wajasiriamali wadogo wa sekta isiyo rasmi kuunganisha rasilimali, kupata masoko makubwa, na kurasimishwa kwa pamoja. |
| **Nguzo 2: Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii** | |
| 2.1. **Jamii Iliyoelimika Vyema, Yenye Ujuzi na Inayojifunza** | |
| **Lengo 1:** Kufikia jamii iliyoelimika vyema, yenye ujuzi na inayojifunza kwa kuongeza upatikanaji wa elimu bora, kukuza maendeleo endelevu ya ujuzi na kuendeleza utamaduni wa kujifunza. | |
| 1. Kuongeza wasichana na wavulana wanaopata elimu bora na kwa sawa ya maendeleo ya awali ya utoto (asilimia 20) na elimu ya awali ya shule ya msingi GRE kutoka asilimia 88.8 hadi 96.7 ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuongeza upatikanaji na kuboresha miundombinu ya vituo vya maendeleo ya awali ya utoto na elimu ya awali ya shule ya msingi ili kuwaandaa watoto na shule ya msingi |
| | i. kufanya elimu ya awali ya shule ya msingi kuwa ya lazima na kupanua mfumo uandikishwaji kwa watoto kupitia uchambuzi wa kitaifa wa utambuzi wa Watoto katika maeneo yao . |
| | ii. Kuakikisha watoto (asilimia 20) wenye umri wa miaka 3 hadi 4 wanapata huduma ya karibu ya kituo cha Maendeleo ya Awali ya Utoto (ECD). |
| | 1.2. kuhakikisha upatikanaji wa wauguzi, walimu wenye sifa, na miundombinu inayofaa kwa umri hitajika na kwa usawa, na vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji jumuishi, pamoja na huduma za maji, usafi wa mazingira na usafi binafsi (WASH) kwa Maendeleo ya Awali ya Utoto (ECD) na elimu ya awali ya shule ya msingi |
| | i. Kuhakikisha upatikanaji wa walimu wenye sifa na usambazaji wenye usawa wa rasilimali za kufundishia na kujifunzia zinazozingatia umri stahiki katika shule zote za awali. |
| | ii. Kuandaliwa kwa programu maalumu za mafunzo kwa waangalizi na walimu wote katika ngazi ya maendeleo ya awali ya mtoto. |
| | iii. Kuongeza ujuzi wa walimu kupitia uendelezaji wa taaluma zao kwa ajili ya ufundishaji na ujifunzaji bora katika shule za awali kila mwaka |
| | 1.3. Kujumuisha Maendeleo ya Awali ya mtoto katika programu za Elimu, Afya na Lishe |
| | i. Kuimarisha uratibu kati ya wizara katika ngazi ya taifa hadi ngazi ya mitaa kwa lengo la kurahisisha usimamizi wa utekelezaji wa pamoja wa programu za elimu, afya, na lishe. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | ii. Kuboresha na kutekeleza kikamilifu seti ya viwango vya ubora wa utoaji wa huduma za Maendeleo ya awali ya mtoto (ECE), kwa msaada wa vyenzo za kuwezesha utoaji ambao ni rafiki kwa watoto na kuridhisha wazazi. |
| 2. Kuongezeka kwa wasichana na wavulana wanaopata elimu bora na yenye usawa ya shule ya msingi kutoka asilimia 98.2 hadi 100, wakidumu na kukamilisha elimu ya msingi, wakiwa na ujuzi unaohitajika ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuimarisha ubora na upatikanaji wa walimu |
| | i. Kuboresha upatikanaji wa walimu, hasa walimu wa STEM na lugha ya Kiingereza, na kutumia walimu kwa ufanisi katika shule za msingi. |
| | ii. Kuboresha ubora wa walimu kupitia programu za maendeleo endelevu ya kitaaluma (CPD), kwa kuzingatia mbinu na teknolojia za kisasa za ufundishaji |
| | 2.2 Kuboresha ubora wa ufundishaji na mazingira ya kujifunzia |
| | i. Kuimarisha na kuviwezesha vituo vya kuandaa rasilimali walimu kwa lengo la kuendeleza kada ya ualimu. |
| | ii. Kukuza upatikanaji wa elimu bora na yenye usawa ya shule ya msingi, kutokuacha shule, uhitimu, matokeo ya kujifunza, na kuwezesha kuvuka kwenda elimu ya sekondari |
| | iii. Kutoa rasilimali za kutosha za ufundishaji na kujifunzia kila mwaka ili kufikia uwiano wa kitaifa wa mwalimu kwa mwanafunzi wa 1:40 |
| | 2.3 Kukuza elimu jumuishi na ushiriki wa jamii ifikapo. |
| | i. Kuimarisha mfumo wa kutambua na kutathmini mahitaji maalum ya kila mwanafunzi |
| | ii. Kuimarisha uwezo wa walimu wa shule za msingi katika Elimu Maalum (SNE) na Elimu Jumuishi (IE). |
| | iii. Kuimarisha ushiriki wa jamii katika kupanga na kutekeleza shughuli za maendeleo ya shule za msingi. |
| | iv. Kuimarisha msingi wa stadi ikiwemo uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na matokeo ya kujifunza |
| | 3.1 Kukuza mfumo maalumu wa nguvu kazi ya walimu wa sekondari |
| 3. kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata elimu bora na yenye usawa ya shule ya sekondari kutoka asilimia 75.3 hadi 100, na elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (TVET) katika shule za sekondari kutoka asilimia 4 hadi 30 ya wanafunzi waliosajiliwa, wakiwa na ujuzi unaohitajika ifikapo Juni 2031 | i. Kuajiri na kuhakikisha hawaondoki walimu wenye utaalamu wa masomo maalumu, kwa kipaumbele katika fani za STEM na lugha ya Kiingereza kila mwaka. |
| | ii. Kuimarisha mfumo wa utoaji wa vyeti na leseni kwa walimu wa sekondari, kwa kuhuisha utaalamu wa masomo mahususi na utendaji |
| | 3.2 Kuboresha mazingira ya kujifunzia kuwa ya kisasa katika ngazi ya Sekondari |
| | i. Kutoa rasilimali za kufundishia na kujifunzia za kila somo ipasavyo ili kufikia wastani wa kitaifa wa uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi wa 1:30 |
| | ii. Kuimarisha na kuviwezesha vituo vya rasilimali za walimu kwa vifaa na teknolojia inayohitajika kwa maendeleo ya kitaaluma ya ngazi ya sekondari |
| | 3.3 Kupanua na Kuimarisha Mwelekeo wa VET |
| | i. Kuboresha na kuongeza miundombinu ya amali katika shule za sekondari |
| | ii. Kuanzisha ushirikiano rasmi na sekta ya viwanda ili kutoa mafunzo kwa vitendo, uanagenzi na programu za uraghibu kwa wanafunzi wa TVET. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | iii. Kuweka maabara na maeneo maalumu ya ubunifu (maker spaces) yaliyo na vifaa kamili katika shule kwa ajili ya shughuli za STEM na TVET. |
| | 3.4 Kukuza Elimu Jumuishi na Bora ya Sekondari. |
| | i. Kuimarisha mfumo wa kubaini na kutathmini mahitaji maalum ya kila mwanafunzi wa sekondari kila mwaka. |
| | ii. Kuongeza umahiri wa walimu wa sekondari katika elimu ya mahitaji maalum (SNE) na elimu jumuishi (IE). |
| 4. Angalau asilimia 30 ya wanafunzi wa shule za sekondari kuweza kuendelea na masomo katika taasisi za elimu ya juu ifikapo Juni 2031. | 4.1 Kuongeza upatikanaji wa huduma ya Elimu ya Juu pamoja na Miundombinu yake. |
| | i. Kujenga na kuboresha vyuo vikuu, vyuo vya ufundi, na vituo huria vya kujifunzia katika mikoa yote. |
| | ii. Kuongeza upatikanaji wa elimu ya juu kupitia programu zilizoboreshwa za kujifunzia huria, kwa masafa ya mbali, na kupitia mtandao. |
| | 4.2 Kuhusianisha elimu ya juu na mahitaji ya sekta ya viwanda. |
| | i. Kutekeleza utaratibu shirikishi wa mapitio ya mtaala unaojibu mahitaji ya sekta ya viwanda na mwenendo wa teknolojia, pamoja na mashauriano ya wadau. |
| | ii. Kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu na sekta ya viwanda ili kukuza ujifunzaji wa vitendo, mafunzo kwa vitendo (internships), na kutoa ajira kwa wahitimu. |
| | iii. Kusaidia vituo vya ubunifu vya wanafunzi na vituo atamizi vinavyopokea ushauri na ufadhili kutoka kwa washirika wa sekta ya viwanda. |
| | 4.3 Kutumia diplomasia ya uchumi kwa ajili ya Elimu |
| | i. Kutumia diplomasia ya uchumi kufanya majadiliano yanayohusu elimu, yakiwemo programu za udhamini na mifumo ya kubadilishana wanafunzi. |
| 5. kufikia uelewa wa masula ya kidijitali wa asilimia 50 ya nguvu kazi ifikapo Juni 2031 | 5.1 Kuweka mfumo wa kudumu wa kujifunza kupitia mtandao na kujenga ujuzi wa kidijitali. |
| | i. Kuweka mfumo na kuwezesha ujifunzaji wa mtandaoni ili kuimarisha programu za kujifunza kupitia elimu masafa kwa watu wazima. |
| | ii. Kukuza ubunifu katika utengenezaji wa maudhui ya ujifunzaji wa kielektroniki, programu za simu, na suluhisho za ujifunzaji za kidijitali. |
| | 5.2 Kuanzisha na kuwezesha mazingira ya utafiti na usimamizi. |
| | i. Kukubali mazingira ya udhibiti yanayounga mkono kuingizwa kwa haraka kwa teknolojia mpya na kushughulikia ujumuishaji wa kidijitali, faragha, na maadili. |
| | ii. Kuongeza uwezo wa taasisi katika utafiti kuhusu teknolojia zinazoibuka kama AI, bioteknolojia, na sayansi za mazingira kwa kuboresha maabara na kushirikiana na taasisi za kimataifa za utafiti kila mwaka. |
| | 5.3 Kukuza ujifunzaji endelevu na ubunifu |
| | i. Kuongeza kiwango cha vituo vya ujifunzaji kwa watu wazima kote nchini kwa kuzingatia ujuzi wa kusoma na kuandika, hesabu, ujuzi wa kidijitali, na ujuzi laini. |
| **2.2. Nguvu Kazi Yenye Uwezo na Motisha** | |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| **Lengo 1:** Kufanikisha kuwa na nguvu kazi yenye uwezo na motisha, ili kuongeza tija na ubunifu | |
| 1. kuongezeka kwa nguvu kazi yenye ujuzi wa ufundi na utaalamu unaohusiana na ubunifu wa viwandani kufikia asilimia 35 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuhusianisha maendeleo ya ujuzi na viwango vya kimataifa |
| | i. Kuhuisha mitaala yote na programu za mafunzo za TVET ili kuwa na viwango vya kimataifa. |
| | ii. Kuingiza kanuni za kimataifa za ujuzi katika sera za kitaifa za elimu, mafunzo, na ajira. |
| | 1.2 Kuongeza upatikanaji wa uhakika wa huduma za TVET |
| | i. Kuongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za TVET katika maeneo ya vijijini kila mwaka. |
| | 1.3 Kuweka mfumo wa kudumu wa kujifunza na utambuzi wa ujuzi |
| | i. Kuendeleza na kutekeleza mfumo wa utambuzi wa mafunzo ya awali (RPL) ili kuthibitisha uzoefu usio rasmi. |
| | ii. Kuimarisha mfumo wa ujifunzaji kwa watu wazima kupitia programu za kila mwaka zinazokuza njia wazi za kazi na utambuzi wa ujuzi. |
| 2. Uwiano wa nguvu kazi yenye ujuzi wa kidijitali kudumishwa kwa aangalau asilimia 50 ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuboresha miundombinu ya TVET na kuwa ya kisasa pamoja na muundo wa ufadhili |
| | i. Kuzindua ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPPs) kwa ajili ya kuchangia ufadhili wa upanuzi na ubunifu wa TVET kila mwaka. |
| | ii. Kuvipatia vituo vya mafunzo zana za kisasa, maabara, na mazingira ya kujifunzia ya kidijitali |
| | 2.2 Kutoa ujuzi wa msingi wa uchumi wa kidijitali |
| | i. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya kijamii vya ubunifu wa kidijitali vijijini na mijini kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo |
| | ii. Kujumuisha masomo ya umahiri wa kidijitali katika programu zote za TVET, elimu endelevu, na mafunzo ya kuongeza ujuzi. |
| 3. Uwiano wa nguvu kazi yenye ujuzi wa kiteknolojia, hasa katika teknolojia, uhandisi na uchambuzi wa taarifa, kuongezeka kwa asilimia 3 ifikapo Juni 2027 | 3.1 Kuimarisha Programu za Mafunzo kwa Vitendo na Mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi |
| | i. Kuandaa programu za mafunzo kwa vitendo kwa kushirikiana na waajiri katika sekta za ubunifu na viwanda |
| | ii. Kuhalalisha uzoefu wa mafunzo kwa vitendo na programu za uanagenzi kama sehemu inayotambulika katika vyeti na sifa za kitaifa. |
| **2.2.1. Kusimamia na Kuitumia Fursa ya Demografia** | |
| **Lengo la 2:** Kuhakikisha Tanzania inanufaika na fursa ya kidemografia kupitia maendeleo ya rasilimali watu, ajira zenye staha, ujasiriamali, maendeleo ya biashara, na uwezeshaji kiuchumi ili kuwa na ukuaji wa uchumi jumuishi na kuboresha maisha. | |
| 1. Ukosefu wa ajira kwa vijana (miaka 15–34) kupungua kutoka asilimia | 1.1 Kulinganisha elimu na ujuzi na mahitaji ya soko la ajira |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 21.5 hadi 19.3 ifikapo Juni 2027 | i. Kuwashirikisha wataalamu wa viwanda na wachambuzi wa soko la ajira ili kubaini ujuzi wa sasa na ujao unaohitajika katika sekta za uzalishaji, hususan kilimo, madini, viwanda, na teknolojia kama kiwezeshaji |
| | ii. Kujumuisha ujuzi, teknolojia zinazoibuka na ujuzi laini katika mitaala ya kitaifa. |
| | iii. Kukuza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuingiza teknolojia mpya na ujuzi maalum wa sekta katika programu za kukuza ujuzi. |
| | 1.2 Kukuza usawa wa jinsia katika elimu na ajira |
| | i. Kujenga na kuweka vifaa kwenye shule za wasichana katika maeneo ya pembezoni na kuhamasisha ushiriki wa wasichana katika masomo ya STEM na ufundi. |
| | ii. Kuwezesha huduma za malezi ya watoto na kuhamasisha mazingira rafiki kwa familia katika maeneo ya kazi, ikiwa ni pamoja na kuogeza utekelezaji wa sera za usawa kwa wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi na watekelezaji wa shughuli kubwa za uchumi |
| | 1.3 Kukuza Ujasiriamali na Ubunifu kwa Vijana |
| | i. Kuanzisha na kuimarisha vituo vya ubunifu na ukuaji wa biashara za vijana |
| | ii. Kutoa huduma kamili za msaada wa biashara, ikijumuisha upatikanaji wa fedha, ushauri na fursa za masoko. |
| | 1.4 Kukuza Fursa katika Uchumi wa Kidijitali na *Gig Economy* |
| | i. Kukuza huduma za upatanishi wa ajira zinazowaunganisha vijana na kazi za mtandaoni na ajira za masafa |
| | ii. Kuwawezesha vijana kuwa na ujuzi wa kujitangaza mtandaoni, kusimamia bajeti ya kazi za kujitegemea, na kujenga chapa binafsi. |
| | 1.5 Kuwezesha urasimishaji wa shughuli zisizo rasmi |
| | i. Kuweka vivutio vya kutathmini utendaji na kurahisisha mwongozo wa kanuni ili kuchochea urasimishaji wa biashara bila kuongeza mzigo kwa wafanyabiashara |
| | 1.6 Kushirikisha Diaspora Katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo |
| | i. Kutoa vivutio kwa wataalamu wa Kitanzania walioko nje kurejea au kuchangia katika sekta za afya, elimu na teknolojia. |
| | ii. Kuhamasisha ushirikiano kati ya wataalamu wanadiaspora na taasisi za ndani kwa ajili ya mafunzo, utafiti na ubunifu |
| 2. Uwiano wa utegemezi wa umri kupungua kutoka 87.4 hadi 79.4 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuongeza upatikanaji wa huduma rafiki za afya ya uzazi kwa vijana ifikapo Juni 2031 |
| | i. Kuongeza upatikanaji wa huduma rafiki za afya ya uzazi, mafunzo ya stadi za maisha na elimu kwa vijana |
| | ii. Kujumuisha elimu ya kina ya afya ya uzazi program mashuleni na kukuza mazingira rafiki kwa vijana. |
| 3. Angalau asilimia 20 ya | 3.1 Kuimarisha hifadhi ya jamii na uchumi jumuishi. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| wazee (miaka 60+) kufikiwa na mpango kamili wa hifadhi ya jamii ifikapo Juni 2031 | i. Kuongeza mafao ya uzeeni na programu zisizohitaji michango, hususan kwa wazee wenye kipato cha chini katika sekta isiyo rasmi kila mwaka. |
| | ii. Kusaidia ujasiriamali kwa wazee kupitia upatikanaji wa mikopo midogo, mafunzo ya biashara, na mtaji. |
| | 3.2 Kuimarisha mifumo ya malezi ya wazee ya kijamii |
| | i. Kupeleka maafisa ustawi wa jamii katika ngazi ya wilaya na kata kwa ajili ya kuwasaidia wazee na walezi. |
| | ii. Kutambua na kuongeza mbinu bora za jadi/kijamii za kuhudumia wazee na kutoa mafunzo ya utunzaji wa wazee kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii. |
| | 3.3 Kuimarisha utolewaji wa huduma za dharura kwa Wazee |
| | i. Kuanzisha mifumo ya tahadhari za mapema yenye kuzingatia mahitaji ya mawasiliano ya wazee na kuhusisha viongozi wa jamii na maafisa ustawi kusambaza taarifa wakati wa dharura. |
| **2.2.2. Soko la Ajira na Mazingira ya Kazi** | |
| **Lengo la 3:** Kuboresha soko la ajira la Tanzania ili kuongeza nafasi za ajira zenye staha na nguvu kazi iliyo tayari kwa mustakabali wa baadae. | |
| 1. Angalau ajira milioni 8 zenye staha kupatikana kupitia uwekezaji na ubunifu ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuimarisha Mazingira ya *Startup* na *SME* ifikapo Juni 2031 |
| | i. Kuanzisha vituo vya kitaifa vya ubunifu kwa ajili ya vijana vinavyotoa malezi, ufadhili na maeneo ya kufanyia kazi. |
| | ii. Kusaidia R&D, ubadilishanaji wa teknolojia na ushirikiano wa kimataifa unaochochea ubunifu na upatikanaji wa masoko kwa SMEs. |
| | 1.2. Kuvutia uwekezaji mkubwa unaotengeneza ajira |
| | i. Kutekeleza kampeni za uhamasishaji wa uwekezaji zinazolenga makampuni makubwa ya ndani na kimataifa kuanzisha shughuli zinazohitaji nguvu kazi kubwa. |
| | ii. Kuendeleza maeneo maalum ya kiuchumi na viwanda vyenye vibali vilivyokubaliwa kabla na miundombinu iliyotayari kwa ajili ya kufunga kiwanda ili kutengeneza nafasi za ajira kutokana na biashara mpya zitakazoanzishwa |
| | 1.3. Kuimarisha Upanuzi na Urasimishaji wa Biashara |
| | i. Kutoa mtaji ya ukuaji na huduma za kukuza biashara kwa SMEs zenye uwezo wa kukua. |
| | ii. Kutekeleza schimu ya kutoa vivutio vitakavyohamasisha biashara zisizo rasmi kujisajili na kukua. |
| 2. Ajira katika sekta za umma na sekta za viwanda vya thamani ya juu kuongezeka kwa angalau asilimia 10 ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuanzisha na kufungamanisha ujuzi na viwanda vya sekta zenye thamani ya juu |
| | i. Kuanzisha programu za ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi zitakazolenga kupata mafunzo ya teknolojia mpya, nishati safi na viwanda vya juu. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | ii. Kushirikiana na makampuni binafsi kuanzisha vituo vya mafunzo vyenye teknolojia ya kisasa. |
| | 1.2. Kukuza Uwekezaji katika Sekta za viwanda vya thamani ya juu |
| | i. Kutoa vivutio maalum vya kifedha na visivyo vya kifedha ili kuvutia na kushikilia uwekezaji katika sekta zenye thamani ya juu kama vile: teknolojia, viwanda vya dawa, na viwanda vinavyotumia teknolojia ya juu. |
| | ii. Kukuza ushirikiano kati ya makampuni ya kimataifa, *startups* za ndani na SMEs ili kuwaunganisha katika minyororo ya thamani ya kimataifa na kutengeneza ajira zinazohitaji ujuzi wa juu. |
| **2.2.3. Jamii jumuisha na iliyolindwa** | |
| **Lengo la 1:** Kuongeza wigo wa jamii jumuishi iliyolindwa kwa kuongeza wigo wa hifadhi ya jamii ili kupunguza hatari na kuhakikisha usawa wa fursa kwa makundi yote. | |
| 1. Ulinzi wa angalau asilimia 40 ya watu walio katika mazingira hatarishi kufikiwa ifikapo Juni 2031 | 2.1. Kutekeleza sheria za kupinga ubaguzi na usawa wa fursa |
| | i. Kuimarisha uwezo wa taasisi za udhibiti, wakaguzi wa kazi, na mahakama kutekeleza sheria zinazokataza ubaguzi kwa misingi ya jinsia, umri, ulemavu au kabila |
| | ii. Kujumuisha mbinu bora zinazotumika kimataifa katika viwango vya kitaifa. |
| | 2.2. Kuhakikisha upatikanaji sawa wa ardhi kwa makundi yaliyopo kwenye mazingira hatarishi |
| | i. Kutekeleza sera za mageuzi ya ardhi zinazowezesha umiliki sawa wa ardhi kwa wanawake na watu wenye ulemavu. |
| | ii. Kukuza programu za umilikishaji ardhi na kuimarisha vituo vya utoaji huduma ardhi mahali pamoja kwenye maeneo yasiyofikika na yasiyo na huduma ili kuwainua wanachi kiuchumi |
| | 2.3. Kujumuisha sekta isiyo rasmi katika mifumo ya hifadhi ya jamii |
| | i. Kutekeleza mifumo ya usajili wa kidijitali iliyorahisishwa kuandikisha wafanyakazi wa sekta isiyo rasmi kila mwaka. |
| | ii. Kuhuisha mifumo ya kitaifa ya hifadhi ya jamii ili kufikia wafanyakazi wote wa sekta isiyo rasimi. |
| | 2.4. Kuboresha na kuimarisha programu muhimu za hifadhi ya jamii |
| | i. Kupitia na kuboresha TASAF na PSSN ili iweze kutumia daftari la kidijitali la walengwa, kuboresha ufuatiliaji, na kupunguza utegemezi wa wafadhili. |
| | ii. Kujumuisha vipengele vya riziki na ujuzi kwenye hifadhi ya jamii ili kuwawezesha walengwa kujitoa katika umaskini. |
| | iii. Kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia utoaji wa hifadhi ya jamii kwa ufanisi. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | iv. Kushirikisha sekta binafsi kutoa au kuwekeza katika hifadhi ya jamii. |
| | 2.5. Kujumuisha mafunzo ya afya ya akili katika elimu na huduma za jamii |
| | i. Kujumuisha elimu ya afya ya akili katika mitaala yote ya elimu. |
| | ii. Kuongeza moduli za afya ya akili katika mafunzo ya walimu na programu za maendeleo ya kitaaluma. |
| | iii. Kuimarisha mazingira ya shule na jamii yanayokuza ustawi na kupunguza unyanyapaa na kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya ya akili |
| **2.2.4. Kuboresha huduma ya afya kwa wote** | |
| **Lengo la 1:** Kuboresha afya ya wananchi, ili kuongeza tija, na kupunguza tofauti katika huduma za afya. | |
| 1. Vifo vya watoto wachanga kupungua kutoka 43 hadi 27 kwa vizazi hai 1,000 ifikapo Juni 2031 | 1.1. Kuimarisha Huduma za Afya ya mama na mtoto mchanga |
| | i. Kuajiri, kutoa mafunzo na kupeleka wakunga wenye ujuzi ili kufikia asilimia 90 ya upatikanaji katika vituo vyote vya afya |
| | ii. Kuweka vifaa muhimu vya uchunguzi na dawa muhimu katika vituo vya ANC na PNC. |
| | iii. Kuondoa gharama za moja kwa moja za huduma za ANC na PNC kwa wanawake wanaoishi katika maeneo yasiyofikika kirahisi, ya kipoto cha chini na makazi hatarishi. |
| | iv. Kuimarisha kliniki zinazotembea za ANC/PNC kufikia jamii za wafugaji zinazoishi maeneo ya siyofikika. |
| | 1.2. Kutekeleza Programu za kitaifa za Lishe kwa akina mama na watoto |
| | i. Kuongeza upatikanaji wa vyakula vilivyoongezwa virutubisho kwa watoto wenye umri wa miezi 6–24. |
| | ii. Kuhakikisha utoaji wa kirutubisho cha vitamini A na dawa za minyoo kwa watoto chini ya miaka 5. |
| | iii. Kusambaza virutubisho kwa watoto wadogo. |
| | 1.3. Kuimarisha mazoezi ya lishe kwa watoto wachanga |
| | i. Kuwaandaa na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili waweze kutoa msaada wa unyonyeshaji katika ngazi ya jamii. |
| | ii. Kutekeleza utoaji elimu ya unyonyeshaji kwa wanaume ili kuongeza ushiriki wao. |
| | 1.4. Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto ngazi ya jamii |
| | i. Kutoa mafunzo kwa angalau asilimia 50 ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii katika huduma za mama na mtoto, ikilenga msaada wa elimu ya afya ya akili na saikolojia |
| | ii. Kujumuisha uchunguzi wa afya ya akili katika huduma za ujauzito na baada ya kujifungua. |
| 2. Kuongeza wigo wa Bima ya Afya kutoka asilimia 15 hadi | 2.1 Kuongeza Uwigo wa utoaji wa bima ya afya kwa wote (UHC) |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 35 ifikapo Juni 2031 | i. Kutengeneza sera za UHC zinazohakikisha upatikanaji sawa, kwa kuzingatia makundi ya sekta isiyo rasmi, wananchi wa vijijini, wanawake, vijana na makundi maalum. |
| | ii. Kuimarisha uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongoza uandikishaji wa wananchi katika UHC. |
| | 2.2 Kuimarisha Bima ya Afya ya Jamii (CBHI). |
| | i. Kubuni vifurushi vya malipo vyenye gharama nafuu na vinavyobadilishika ili kuendana na mapato ya misimu na hali halisi ya uchumi wa eneo husika |
| | ii. Kuanzisha huduma tembezi za uandikishaji wa Bima ya Afya ya Jamii (CBHI) katika maeneo yasiyofikika kirahisi. |
| | 2.3 Kutumia majukwa ya mtandaoni kuhamasisha bima ya afya na utoaji wa huduma. |
| | i. Kutumia mifumo ya kidijitali kwa ajili ya kurahisisha usajili wa bima ya afya na malipo ya michango ya wateja. |
| | ii. Kutumia nyenzo za kidigitali za nje kuandaa nyenzo za ndani katika lugha mbalimbali na rafiki kwa watu wenye mahitaji maalumu ili kuongeza ujumuishi wa makundi hayo |
| 3. kupungua kwa idadi ya vifo vya akina mama wajawazito kwa kila vizazi hai 100,000 kutoka 104 hadi 85, ifikapo juni 2031. | 3.1 Kuhakikisha huduma bora za afya ya mama na mtoto inapatikana kwa wote ifikapo juni 2031. |
| | i. Kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za upimaji na usimamizi wa wjawazito wote kabla na baada ya kujifungua, ili kubaini na kudhibiti mapema matatizo ya uzazi, ifikapo Juni 2031. |
| 4. Kupunguza kiwango cha jumla cha uzazi (TFR) kutoka 4.8 mwaka 2022 hadi 4.1, ifikapo Juni 2031. | 4.1 Kujumuisha elimu ya afya ya uzazi katika ngazi zote za shule |
| | i. Kuimarisha utoaji wa mitaala ya afya ya uzazi inayoendana na umri, iliyojumuishwa katika programu za shule nchini katika ngazi zote |
| | ii. Kushirikiana na Mashirikayasiyo ya kiserikali (NGOs) na vyombo vya habari ili kukuza elimu ya afya ya uzazi. |
| | 4.2 Kutekeleza Sera zenye motisha ili kuwabakiza wasichana shuleni na kuwalinda dhidi ya vihatarishi vya ujana wakati wa balehe |
| | i. Kuboresha miundombinu ya shule, ikiwemo vyoo kwa ajili ya usafi kwa wasichana, ili kujenga mazingira wezeshi ya kujifunzia. |
| | ii. Kuhusisha wazazi na walezi kupitia warsha ili kushughulikia vikwazo vya kiutamaduni na kiuchumi vinavyokabili elimu ya wasichana |
| | 4.3 Kuongeza programu za afya za jamii zinazohamasisha ushiriki wa wanaume |
| | i. Kuimarisha vikao vya ushauri nasaha vya wanandoa ili kukuza uamuzi wa pamoja katika upangaji uzazi |
| | ii. Kuhimiza waajiri kutoa elimu ya uzazi wa mpango kuwa sehemu ya motisha ya watumishi kwa ajili ya ustawi wa wafanyakazi |
| 5. Kuongezeka kwa Umri wa kuishi kutoka miaka 68.3 hadi 70.4 ifikapo Juni 2031. | 5.1 Kutekeleza Ugunduzi wa Mapema na Kinga dhidi ya Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs) |
| | i. Kujumuisha uchunguzi wa vipengele hatarishi vya magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) ikiwemo shinikizo la damu, Kisukari kwenye damu, na (BMI) katika utoaji wa huduma za msingi za afya za kila siku |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | ii. Kuimarisha mifumo ya rufaa ili kudhibiti kwa wakati na kufuatilia watu waliogunduliwa kuwa na magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) |
| | 5.2 Kutekeleza programu za lishe na chakula bora |
| | i. Kuimarisha huduma za ushauri nasaha wa lishe kwa jamii, kwa kuwalenga wajawazito, watoto wachanga, na watu wenye magonjwa yanayotokana na unene uliopitiliza |
| | ii. Kutumia majukwaa ya mawasiliano hususai simu za mkononi (mHealth) kutoa ushauri na kuikumbusha jamii umuhimu wa lishe |
| | 5.3 Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa sekta mbalimbali wa magonjwa yasiyoambukiza (NCDS) |
| | i. Kujumuisha uratibu wa mfumo wa kitaifa wa sekta mbalimbali wa magonjwa yasiyoambukiza (NCDS), katika mifumo rasmi ya kitaasisi kwa ajili ya kukinga, kudhibiti, na kutibu magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) |
| | ii. Kuimarisha mifumo ya mawasiliano ya sekta mbalimbali katika matumizi ya mara kwa mara ya takwimu za magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) |
| 6. Kupunguza ueneaji wa magonjwa magonjwa Makuu ya Kuambukiza ikiwemo VVU, Malaria, na Kifua Kikuu kwa angalau asilimia 30 kutoka viwango vya sasa, ifikapo Juni 2031. | 6.1 Kupanua Huduma za Kinga na Upimaji wa VVU, kila mwaka. |
| | i. Kuongeza upatikanaji wa kinga kabla ya kuambukizwa (PrEP) na kuongeza huduma za tohara ya hiari kwa wanaume (VMMC) |
| | ii. Kuhakikisha Huduma za Upimaji wa VVU zinapatikana kwa asilimia 100 katika vituo vyote vya afya na programu za kuifikia jamii |
| | 6.2 Kutekeleza programu za udhibiti wa vimelea vya malaria nchi nzima |
| | i. Kutekeleza programu za kudhibiti vimelea vya malaria nchi nzima, ikiwemo vyandarua vyenye viuatilifu, unyunyiziaji wa dawa ndani ya nyumba, na udhibiti wa vyanzo vya mazalia ya mbu. |
| | ii. Kuimarisha usafi wa mazingira kwenye jamii ili kuondoa mazalia ya mbu |
| | 6.3 Kuimarisha hatua za kudhibiti kifua kikuu (TB) |
| | i. Kutekeleza hatua za udhibiti wa maambukizi ya kifua kikuu (TB), ikiwemo kupima watu wengi na kuboresha hewa bora katika maeneo ya umma |
| | ii. Kuanzisha vitengo tembezi vya upimaji wa kifua kikuu (TB) vyenye vifaa vya X-ray na mashine za GeneXpert, katika maeneo ya vijijini na yasiyofikika kirahisi |
| | 6.4 Kuanzisha kampeni za uelimishaji jamii kuhusu uzingatiaji wa kinga ya magonjwa, upimaji, na uzingatiaji wa matibabu |
| | i. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya wa jamii (CHWs), wafanyakazi wa huduma za jamii na wanaojitolea, ili kutoa elimu ya afya kuhusu kinga ya magonjwa, upimaji, na uzingatiaji wa matibabu |
| | ii. Kujenga uwezo wa waandishi wa habari wa ndani na wataalamu wa vyombo vya habari kuhusu utangazaji wa habari za afya ulio sahihi, wa kimaadili, na usio na unyanyapaa. |
| | iii. Kusaidia ujumuishwaji wa jumbe zenye kuelimisha kuhusu magonjwa kupitia majukwaa ya huduma za kifedha kwa njia ya simu za mkononi (mobile money), mifumo ya usafiri na maeneo mengine yanayofanana na hayo |

| Shabaha | Afua |
| --- | --- |
| 7. Kufikiwa kwa asilimia 58.0 ya jumla ya idadi ya watu wanaopata huduma za afya zinazofikika, zinazopatikana kwa ubora na gharama nafuu ifikapo Juni 2031. | 7.1 Kurahisisha kanuni za huduma za afya ili kurahisisha ushiriki wa sekta binafsi |
| | i. Kuimarisha uwezo wa vyombo vya udhibiti (mfano, TMDA) ili viweze kutoa uangalizi wa haraka na wa uwazi |
| | 7.2 Kuunganisha tiba mbadala sambamba na tiba za kisasa |
| | i. Kuimarisha mfumo wa kitaifa kwa waganga wa jadi na wataalamu wa mitishamba, kwa kukuza mifumo ya rufaa mtambuka pamoja na wataalamu wa tiba-biolojia |
| | 7.3 Kuimarisha maadili ya kitaaluma kwa wafanyakazi wa afya |
| | i. Kuimarisha ushirikiano kati ya vyombo vya udhibiti wa huduma za afya na vyombo vya sheria ili kushughulikia utovu mkubwa wa nidhamu wa kitaaluma. |
| | ii. Kujumuisha miongozo ya maadili ya kimataifa katika kanuni za kitaifa za maadili kwa wafanyakazi wote wa afya |
| 8. Kujumuishwa kwa usimamizi wa afya na takwimu za kidijitali ili kutoa huduma za afya kwa ufanisi, ifikapo Juni 2031. | 8.1 Kuhakikisha utendajikazi wa mifumo ya taarifa za afya |
| | i. Kufungamanisha mifumo ya afya katika ngazi zote (msingi, sekondari, na kitaalamu) ya sekta ya umma na sekta binafsi |
| | ii. Kuhakikisha utendajikazi wa kimfumo kati ya mifumo ya kliniki na majukwaa ya vifaa na ugavi, ili kuwa na uratibu mzuri kati ya utoaji wa huduma na upatikanaji wa vifaa |
| 9. Kupunguza uagizaji wa bidhaa muhimu za afya kwa asilimia 20, ifikapo Juni 2031. | 9.1 Kuweka vivutio kwa ajili ya uzalishaji wa ndani wa bidhaa za afya |
| | i. Kuanzisha vivutio vya kodi, sera za fedha, na udhibiti kwa ajili ya viwanda vya ndani vinavyozalisha teknolojia za afya za msingi na za hali ya juu |
| | ii. Kutoa mikopo yenye riba nafuu au dhamana za mikopo kwa kampuni zinazojishughulisha na uzalishaji wa ndani wa teknolojia za afya |
| | 9.2 Kuimarisha minyororo ya ugavi wa dawa zinazozalishwa ndani |
| | i. Kuhakikisha malighafi kwa ajili ya sekta ya dawa zinapatika kwa gharama nafuu kupitia ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) |
| 10. Tanzania kuwa moja ya vituo vikuu viwili (2) vya utalii wa matibabu katika ukanda wa Afrika mashariki na kati, ifikapo Juni 2031. | 10.1 Kuanzisha diplomasia ya afya na ukuzaji. |
| | i. Kuanzisha mahusiano rasmi ya diplomasia ya afya na yaliyohalalishwa kitaasisi na nchi jirani na nchi washirika wapya |
| **2.2.5. Nyumba na Makazi ya Watu.** | |
| **Lengo la 1:** Kuboreshwa kwa nyumba na Makazi ya Watu, ili kuwezesha Maisha bora maendeleo jumuishi ya miji | |
| 1. Kuongezeka kwa asilimia ya idadi ya watu wanaoishi katika maeneo ya makazi yaliyopangwa kutoka asilimia 30 hadi asilimia 50, ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kufanya mageuzi ya kisheria na Kisera kwa ajili ya umiliki za Ardhi. |
| | i. Kutekeleza mageuzi ya kisheria ili Kuhakikisha uwazi katika usimamizi wa haki za ardhi kwa wananchi wote ikiwemo wanawake, vijana, na makundi maalumu. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | ii. Kuwianisha mifumo ya umiliki wa ardhi kisheria, kimila, na kidini ili kuhakikisha ulinzi na utambuzi sawa wa haki za ardhi |
| | iii. kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi yenye haki na ufanisi, kila mwaka. |
| | 1.2 kuboresha mifumo na taratibu za usimamizi wa ardhi kuwa za kisasa. |
| | i. Kuanzisha na Kutumia Mfumo wa Kitaifa wa Taarifa za Ardhi Kidijitali (LIS) unaojumuisha kada, usajili, na takwimu za mipango. |
| | ii. Kurahisisha na Kugatua taratibu za Utoaji wa Hati za Ardhi ili Kupunguza Muda wa Ushughulikiaji, Gharama, na Urasimu, na hivyo Kufanya urasimishaji Kuwa rahisi zaidi. |
| | iii. Kushirikisha sekta binafsi katika Upimaji, Usimamizi wa takwimu, na matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kuharakisha utoaji wa huduma, kila mwaka. |
| | 1.3 Kuzindua Programu Rasmi ya Kitaifa ya Utoaji Hati za Ardhi |
| | i. Utoaji wa hati rasmi za ardhi kwa angalau asilimia 95 ya wamiliki wote wa ardhi mijini na vijijini. |
| | ii. Kutoa Hati rasmi za ardhi kwa angalau asilimia 40 ya wakazi wa sasa katika miji mikuu yenye makazi yasiyo rasmi ya mijini. |
| | iii. Kuwezesha ofisi za ardhi za wilaya kuwa na zana za kidijitali na wafanyakazi waliofunzwa ili waweze kushughulikia taratibu za utoaji wa hati kwa ufanisi katika ngazi ya wilaya, kila mwaka. |
| **2.2.6. Usalama wa Chakula na Lishe** | |
| **Lengo la 1:** Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe, kwa lengo la Kupunguza Njaa na Kuongeza Ubora wa Afya ya Umma. | |
| 1. Idadi ya Watu Wanaopata Chakula Chenye Lishe ya uhakika kwaa Mwaka Mzima kuongezeka hadi asilimia 60, ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Uimarishaji wa Chakula. |
| | i. Kuhamasisha matumizi ya Vyakula Vikuu (kwa Madini ya Chuma na Asidi ya Foliki), Mafuta ya Kula, na Vyakula vya Nyongeza kwa Watoto Wachanga. |
| | ii. Kuhalalisha Kisheria Uwekaji wa madini ya Chumvi ya Iodine (USI) na Kuhakikisha Uzingatiaji wa asilimia 100 kwa Wazalishaji Wote. |
| | iii. Kutoa Vivutio vya kikodi kwa uzalishaji wa Ndani wa Vyakula Vilivyoimarishwa Vya Kutosha na Chumvi Yenye Iodi, kupitia ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). |
| | 1.2 Kuimarisha Mifumo mchanganyiko ya Taifa ya Chakula kwa ajili ya Lishe. |
| | i. kukuza uzalishaji na utumiaji wa mazao yenye wingi wa madini chuma, provitamini A, na mazao mengine yenye virutubisho vingi kupitia huduma za ugani na usaidizi wa kimasoko. |
| | ii. Kujumuisha elimu ya lishe inayozingatia jinsia katika shule za sekondari, programu za vijana, na kampeni za kuelimisha umma kila mwaka. |
| | 1.3 Kujumuisha Huduma za Lishe katika Huduma za Afya ya Msingi na huduma ya Mama na mtoto. |
| | i. Kupachika uchunguzi wa upungufu wa damu (anemia), upimaji wa alama za chuma (iron biomarker testing), na ushauri nasaha wa lishe katika taratibu za kitaifa za huduma kabla ya kujifungua (ANC) |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | ii. Kupanua Mpango wa Hospitali Rafiki kwa Mtoto (BFHI) kwa vituo vyote vya afya vya umma na maeneo ya kunyonyesha mahali pa kazi kila mwaka. |
| | iii. kujumuisha huduma za lishe katika huduma za msingi za afya ili kupunguza idadi ya watu wenye utapiamlo kila mwaka. |
| | 1.4 Kuwezesha Mifumo ya Kitaifa ya Ufuatiliaji na uwezeshaji wa Lishe |
| | i. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kitaifa ya ufuatiliaji wa upungufu wa virutubisho muhimu (Vitamini A, iodini, chuma) kwa wanawake na watoto. |
| | ii. Kujenga uwezo wa wahudumu wa afya wa jamii kwa ajili ya utambuzi wa mapema wa utapiamlo kwa kutumia nyenzo kama vile MUAC na alama za uzito-kwa-urefu kila mwaka.. |
| | i. Kupachika uchunguzi wa upungufu wa damu (anemia), upimaji wa alama za chuma (iron biomarker testing), na ushauri nasaha wa lishe katika taratibu za kitaifa za huduma kabla ya kujifungua (ANC). |
| | 1.5 Kuhakikisha Viwango vya Kitaifa vya Usalama na Ubora wa Chakula vinazingatiwa. |
| | i. Kupanua Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Magonjwa Yatokanayo na Chakula kwa kutumia uchanganuzi wa kijiografia kila mwaka. |
| | ii. Kutoa vivutio kwa ajili ya mifumo ya uidhinishaji inayohusika na uzingatiaji wa sheria kwa wasindikaji wa chakula, biashara ndogo na za kati (SMEs), na biashara za kilimo ili kuhakikisha utiifu wa 100% wa viwango vya kitaifa |
| **2.2.7. Upatikanaji na Uuunganishwaji wa Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira kwa Wote** | |
| **Lengo 1:** Kuwezesha uunganishwaji wa maji safi katika ngazi ya taifa ili kuongeza upatikanaji wa maji safi kwa kaya na jamii. | |
| 1. Kuunganishwa kwa maji safi na salama yenye gharama nafuu na endelevu kwa asilimia 60 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuwezesha Usimamizi Jumuishi wa Rasilimali za Maji na Sera Zinazohimili Mabadiliko ya Tabianchi. |
| | i. Kufanya marekebisho ya Sera ya Taifa ya Maji (2002) ili kujumuisha masuala ya ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, upatikanaji wa maji, na kanuni za ESG (Mazingira, Jamii na Utawala). |
| | ii. Kuimarisha usimamizi wa maeneo ya vyanzo vya maji katika mabonde yote ya mito na kujenga uwezo wa serikali za mitaa katika usimamizi wa maji unaohimili mabadiliko ya tabianchi kila mwaka. |
| | iii. Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika usimamizi endelevu wa rasilimali za maji kila mwaka. |
| | 1.2 Kupanua na kuboresha miundombinu ya usambazaji wa Maji kuwa ya kisasa Kila Mwaka. |
| | i. Kujenga visima vipya na miradi ya maji ya bomba katika vijiji 200 kila mwaka. |
| 2. Matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma za maji na usafi kufikia asilimia 70 mijini na asilimia 40 vijijini ifikapo Juni 2031 | ii. Kuboresha miundombinu ya kusukuma na kusambaza maji katika mikoa na majiji yote kila mwaka. |
| | iii. Kuendelea na ujenzi wa mtandao wa Maji wa Ziwa Victoria/Ziwa Tanganyika na kuanzisha mfumo mzuri wa usimamizi |
| | iv. Kukarabati mitandao iliyopo ya kusambaza maji na kupunguza upotevu wa maji yasiyoingiza mapato kupitia ufungaji wa mita na utambuzi wa uvujaji kila mwaka ili kuongeza mtandao wa mabomba yaliyoounganishwa kutoka asilimia 30% hadi 55%. |
| | 1.3 Kuboresha Ubora wa Maji Kitaifa. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | i. Kuimarisha mifumo ya kijamii ya ufuatiliaji wa ubora wa maji kufikia asilimia 50 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) kila mwaka. |
| | ii. Kufanya Kampeni za uelewa kitaifa kuhusu utupaji salama wa taka na kupunguza utupaji wa kemikali hatarishi kwa mwaka. |
| | 2.1 Kusanifu mifumo janja ya usimamizi wa matumizi ya maji |
| | 2.2 Kuhamasisha matumizi ya mifumo ya maji inayotumia nishati ya jua. |
| | i. Kufunga pampu za maji zinazoendeshwa kwa nishati ya jua kwenye visima vya maji vilivyo maeneo ya vijijini kila mwaka |
| | ii. Kutoa mafunzo kila mwaka kwa mafundi na vyama vya watumiaji maji kuhusu uendeshaji na matengenezo ya pampu za maji zinazotumia nishati ya jua ili kufikia asilimia 30 ya maeneo ya vijijini |
| 3. Upatikanaji wa huduma bora na za kutosha za usafi na usafi wa mazingira na kutokomeza kujisaidia vichakani kufikia asilimia 80 ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuboresha huduma za usafi mijini na pembezoni mwa miji |
| | i. Kuboresha miundombinu ya maji taka katika miji mikubwa kila mwaka |
| | ii. Kuimarisha usimamizi, udhibiti na ufuatiliaji wa huduma za maji taka kila mwaka. |
| | iii. Kuimarisha mfumo wa kutibu majitaka kwa kuhamasisha viwanda kutibu majitaka kabla ya kuyaachia kwenye mazingira na kuhimiza matumizi ya mitambo midogo ya kisasa ya kutibu majitaka |
| | 3.2 Kutokomeza kujisaidia vichakani na kuhamasisha usafi kwa wote |
| | i. Kupanua upatikanaji wa miundombinu ya usafi ya gharama nafuu kwa kuzingatia mahitaji ya wanawake, wasichana na makundi maalumu kila mwaka. |
| | ii. Kuhamasisha matumizi salama ya bidhaa za majitaka kila mwaka (mbolea/umeme) |
| **2.2.8. Jamii Iliyoshikamana, Inayowajibika na Inayoshiriki** | |
| **Lengo Na. 1:** Jamii iliyoshikamana na yenye uwajibikaji, inayochangia umoja wa Kitaifa na mshikamano wa kijamii | |
| 1. Kufikia angalau asilimia 35 ya wanawake katika nafasi za uongozi kwenye biashara, serikali na elimu ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuandaa programu za uhamasishaji wa wanawake kwenye nafasi za uongozi ili kufikia asilimia 40 ya uwakilishi katika serikali kuu na za mitaa |
| | i. Kufanya kampeni za uhamasishaji nchini kila mwaka |
| | ii. Kutoa mafunzo kwa wanawake kuhusu kushiriki kwenye siasa kila mwaka |
| | 1.2 Kuweka miongozo ya jinsia katika uteuzi wa bodi ili kufikia asilimia 35 ya wanawake katika bodi na tume. |
| | i. Kufanya marekebisho ya sheria za uteuzi wa umma ili kujumuisha hitaji la uwiano wa asilimia 35 ya usawa wa kijinsia |
| | ii. Kuhamasisha sekta Binafsi kufuata malengo ya uwiano wa kijinsia kila mwaka |
| | 1.3 Kuhakikisha asilimia 35 ya nafasi za uongozi wa juu katika kampuni za umma zinashikiliwa na wanawake. |
| | i. Kushirikiana na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji – CMSA na Dhamana na Soko la Hisa kutekeleza sera ya jinsia kila mwaka. |
| | ii. Kuwashirikisha vyama vya kisekta kuwa mabalozi wa usawa wa kijinsia kila mwaka. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 2. Kuweka misingi ya Tunu za Taifa (heshima, mshikamano, utambulisho wa kitaifa) kwa asilimia 60 ya wananchi ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuanzisha majukwaa ya mijadala ya Kijamii inayohamasisha umoja, uzalendo na maadili |
| | i. Kuwashirikisha wasanii na washairi kuhamasisha jumbe za umoja kupitia sanaa kila mwaka. |
| | ii. Kuhamasisha vyombo vya habari kutoa habari chanya zenye kuimarisha mshikamano kila mwaka |
| | 2.2 Kuimarisha mafunzo ya uzalendo na uwajibikaji wa kiraia shuleni kila mwaka |
| | i. Kushirikiana na vyombo vya Habari kutoa Taarifa kuhusu jitihada za shule na mafanikio ya wanafunzi katika kukuza maadili na uzalendo kila mwaka |
| | ii. Kujumuisha hadithi na simulizi za asili Katika nyenzo za kujifunzia na kufundishia kila mwaka. |
| **2.2.8.1. Maendeleo Jumuishi Vijijini** | |
| **Lengo Na. 2:** Kuimarisha maendeleo Jumuishi vijijini ili kupunguza tofauti za vijijini na mijini na kuboresha maisha ya vijijini | |
| 1. Asilimia 30 ya vijiji kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi na asilimia 40 ya ardhi kusajiliwa ifikapo 2031. | 1.1 Kuhuisha mifumo ya kisera na kisheria kuhusu usimamizi wa ardhi. |
| | i. Kuhuisha Sheria ya Ardhi, Sheria ya Matumizi ya Ardhi na sheria nyingine za Ardhi. |
| | 1.2 Kuimarisha urasimishaji na mipango ya matumizi ya ardhi vijijini |
| | i. Kuhamasisha jamii kupitia kampeni za uelimishaji kila mwaka kuhusu mipango ya matumizi ya ardhi na urasimishaji |
| | ii. Kuanzisha na kutoa mafunzo kwa kamati za ardhi za vijiji kila mwaka ili kuhakikisha uendelevu na usimamizi wa taarifa za ardhi |
| 2. Kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao kwa asilimia 30 ifikapo mwaka 2031 | 2.1 Kuimarisha usimamizi wa rasilimali maji na miundombinu ya kilimo kila mwaka |
| | i. Kuwekeza na kuimarisha skimu ndogo za umwagiliaji, visima vya maji na uvunaji maji. |
| | ii. Kuhimiza matumizi ya teknolojia zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi kama umwagiliaji wa matone na pampu zinazoendeshwa kupitia nishati ya jua kila mwaka |
| | iii. Kuwekeza katika miundombinu muhimu ikiwemo barabara za mashambani na miundombinu ya kuhifadhi mazao kila mwaka ili kupunguza upotevu wa mavuno |
| | 2.2 Kutoa ruzuku ya pembejeo muhimu kwa wakulima wadogo kila mwaka. |
| | i. Kutoa ruzuku za mbegu bora, mbolea na viuatilifu muhimu. |
| | ii. Kutoa ruzuku kwenye chakula cha mifugo ili kuimarisha ukuaji fungamanishi wa kilimo. |
| 3. Asilimia 60 ya wajasiriamali na wakulima wapate huduma za kifedha ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kupanua wigo wa huduma maalumu za kifedha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya vijijini kila mwaka. |
| | i. Kuanzisha na kutoa bidhaa maalumu za mikopo midogo kwa ajili ya wakulima, vijana, wanawake na kilimo biashara. |
| | ii. Kusambaza na kutumia maafisa ugani kutoa elimu ya fedha kwa wakulima. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| **2.2.8.2. Vyama vya Ushirika vilivyo Imara** | |
| **Objective 3:** Kuimarisha vyama vya ushirika ili kuchochea maendeleo Vijijini na kuwapa nguvu wanachama wa vyama vya ushirika. | |
| 1. Kuanzisha mfumo wa uongozi unaozingatia uwajibikaji, ubunifu na ukuaji endelevu wa vyama vya ushirika ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha sera na mfumo wa kisheria wa vyama vya ushirika ili kuimarisha mfumo wa uongozi wenye uwazi na uwajibikaji. |
| | i. Kuwajengea uwezo Wizara inayohusika na vyama vya ushirika na Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi na usuluhishi wa migogoro |
| | ii. Kuimarisha utoaji wa motisha za kisheria na kisera zinazowezesha vyama vya ushirika kuweka akiba, kupata mikopo na kuwekeza kila mwaka |
| | 1.2 Kuwezesha vyama vya ushirika kupata huduma za kifedha |
| | i. Kutoa mikopo ya muda mrefu yenye riba nafuu kwa ajili ya uwekezaji, ununuzi wa vifaa, huduma za kuhifadhi mazao na uchakataji kila mwaka |
| | ii. Kukuza mikopo ya mtaji wa uendeshaji inayoendana na misimu ya kilimo kila mwaka |
| **2.2.8.3. Tabaka la Kati.** | |
| **Objective 4:** Kuimarisha tabaka la kati ili kuwezesha ukuaji jumuishi, ukuaji wa soko la ndani na ushiriki katika sekta rasmi kila mwaka | |
| 1. Kuongeza kwa tabaka la kati kutoka asilimia 12 hadi asilimia 18 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuanzisha National Digital Livelihoods Programme |
| | i. Kutoa mafunzo ya ujuzi wa masoko ya kidijitali, biashara ya kidigitali na *freelancing* kila mwaka. |
| | ii. Kuweka mfumo rasmi wa utolewaji wa tuzo ya taifa ya ubunifu wa kidijitali kila mwaka |
| | iii. Kuwezesha uanzishwaji wa biashara mpya za mtandaoni kila mwaka. |
| | 1.2 Kuanzisha *Government-Backed Asset Accumulation Programme*s |
| | i. Kutoa hati mpya 100,000 za umiliki wa ardhi kila mwaka |
| | 1.3 Kuanzisha jukwaa la "Chanzo cha Maisha Diaspora". |
| | i. Kuwezesha uwekezaji wa Dola za Marekani milioni 50 kutoka kwa Diaspora |
| | ii. Kuwarejesha wataalamu 500 kutoka Diaspora katika Taasisi za ndani. |
| | iii. Kuanzisha Jukwaa la kidigitali la Diaspora |
| | 1.4 Kuanzisha *Integrated Economic Growth Centres* kwenye miji midogo |
| | i. Kukamilisha *Growth Centres* katika Majiji maalumu. |
| | ii. Kuwezesha urasimishaji wa biashara zisizo rasmi 10,000 na kuzalisha fursa za ajira mpya 5,000 kwenye Majiji kila mwaka |
| | 1.5 Kuzindua Programu za Uchumi wa Buluu na Kijani |
| | i. Kutoa mafunzo ya ujuzi kwa watu 5,000 kwa mwaka kuhusu uchumi wa buluu na Kijani. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | ii. Kutoa ruzuku kwa biashara mpya za uchumi wa kijani/buluu kila mwaka. |
| | iii. Kuzindua Programu husika. |
| **Nguzo 3: Uhifadhi wa Mazingira na Uhimilivu wa Tabianchi** | |
| **3.1. Uhifadhi wa Mazingira** | |
| **Objective 1**: Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa mazingira na kuweka misingi ya uendelevu katika sekta zote ili kuhakikisha usalama na ustawi wa Ikolojia kwa Kizazi cha sasa na Kijacho | |
| 1. Kulinda bioanuai na kusimamia angalau asilimia 60 ya mifumo ya ikolojia ya bahari, maji na ardhi ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuimarisha mifumi ya kisheria ya kupambana na ujangili, biashara haramu ya wanyamapori na uvamizi wa maeneo tengefu |
| | 1.2 Kuanzisha kikosi kazi cha kufuatilia na kutekeleza sheria katika ikolojia ya maeneo ya mipakani |
| | 1.3 Kuandaa na kutekeleza angalau miradi 20 ya kipato mbadala kwa jamii zinazozunguka maeneo muhimu ya ikolojia |
| | 1.4 Kurasimisha makubaliano ya usimamizi shirikishi na jamii 50 zilizo jirani na maeneo tengefu |
| | 1.5 Kurejesha angalau hekta milioni mbili (2) za maeneo yaliyoharibika zaidi (misitu, ardhioevu na matumbawe) kwa kuchukua hatua muhimu ikiwemo kuzuia viumbe na mimea vamizi |
| | 1.6 Kufanya ufuatiliaji wa asilimia 60 ya mifumo ya ikolojia kwa kutumia satelaiti ya Taifa na droni na kutoa taarifa kwa umma kila mwaka |
| | 1.7 Kuimarisha ugharamiaji wa uhifadhi wa bioanuai kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi |
| 2. Kuifanya Tanzania kuwa kati ya nchi 20 bora barani Afrika katika uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuimarisha Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira - NEMC na kuanzisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa ubora wa maji |
| | 2.2 Kuwezesha upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi kupitia hati fungani za kijani, biashara ya hewa ukaa na ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi kila mwaka |
| | 2.3 Kupunguza hewa chafu na kuchochea usafiri na usafirishaji unaohifadhi mazingira kwa kubadili angalau asilimia tano (5) ya mabasi kuanza kutumia nishati ya umeme katika miji mikubwa |
| | 2.4 Kuimarisha uhimilivu wa mazingira kwa kutekeleza Programu ya “Tanzania ya Kijani” kupitia kilimo kinachozingatia hali ya hewa |
| | 2.5 Kufungamanisha masomo ya mazingira katika mitaala na kufanya kampeni za uelimishaji kitaifa kuhusu mazingira |
| | 2.7 Kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za kilimo zinazozingatia hali ya hewa |
| | 2.8 Kutekeleza programu za upandaji miti kupitia “Tanzania ya Kijani”. |
| 3. Kupunguza kasi ya ukataji misitu kutoka asilimia 1.0 mwaka 2025 hadi asilimia 0.85 ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa misitu kwa kutumia satelaiti ili kushughulikia masuala ya uvunaji haramu wa magogo |
| | 3.2 Kutekeleza marufuku ya kitaifa kwa kutumia mbinu za kidigitali kuhusu uvunaji haramu wa magogo yenye thamani kubwa. |
| | 3.3 Kuanzisha na kuendesha miradi mitano (5) ya kijamii ya hewa ukaa (REDD+) ili kuwawezesha wananchi kupata kipato mbadala kwa jamii inayotegemea Misitu. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 4. Kupima na kupanga matumizi ya angalau asilimia 40 ya ardhi yote nchini ifikapo Juni 2031 | 4.1 Kuanzisha mfumo wa kidijitali wa kitaifa wa upangaji wa matumizi ya ardhi na usajili |
| | 4.2 Kutekeleza mipango jumuishi ya matumizi ya ardhi na kupanua umilikishaji rasmi wa ardhi kufikia asilimia 40 ya eneo la kitaifa la ardhi |
| | 4.3 Kufanya tathmini ya kina ya mifumo ikolojia muhimu, ikijumuisha ardhioevu zote za kitaifa. |
| 5. Kuhifadhi na kudhibiti kwa uendelevu asilimia 50 ya ardhioevu ya kitaifa ifikapo Juni 2031. | 5.1 Kuimarisha uwezo wa kitaasisi kwa kutoa mafunzo kwa maafisa wa usimamizi wa ardhioevu angalau 200 na kuanzisha Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Ardhioevu. |
| | 5.3 Kuandaa na kutekeleza angalau programu tano (5) za majaribio za usimamizi wa vyanzo vya maji na ardhioevu na Mamlaka za Serikali za Mitaa. |
| 6. Kuhakikisha ulinzi wa asilimia 60 ya maeneo makuu ya vyanzo vya maji (Kagera, Mara, Ruaha Mkuu, Momba, Lufurio, Ruvu, Wami na Ruvuma) kufikia Juni 2031 | 6.1 Kuandaa na kutekeleza mipango ya urejeshwaji wa ufunikaji wa ardhi kupitia upandaji miti kwa wingi na kuendeleza urejeshwaji wa asili katika mabonde lengwa. |
| | 6.2 Kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya miundombinu fanisi ya matumizi ya maji kwa ajili ya umwagiliaji, ikilenga kuongeza asilimia 20 ya matumizi ya maji yenye tija katika maeneo ya kilimo ndani ya mabonde yaliyoainishwa. |
| | 6.3 Kuongeza uwezo wa Bodi za Mabonde zilizopo kwa kutoa mafunzo kwa angalau maafisa 150 na kutekeleza taratibu za kawaida za uendeshaji (SOPs) za ufuatiliaji wa utekelezaji na usimamizi wa sheria |
| 7. Kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa taka ngumu mijini na huduma za usafi hadi asilimia 60 kufikia Juni 2031. | 7. Kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ya ukusanyaji taka (malori, mapipa, vituo vya kukusanyia taka) na kuongeza huduma kwa maeneo ya mijini yasiyohudumiwa. |
| 8. Kufikia asilimia 40 ya ardhi iliyopangwa kitaifa kufikia Juni 2031 | 8.1 Kuhuisha sera zote za ardhi za taifa na kuingiza masuala ya uhimilivu wa tabianchi katika mfumo wa kisheria wa upangaji matumizi ya ardhi. |
| | 8.2 Kuanzisha na kuendesha vitengo vya upangaji matumizi ya ardhi vilivyogatuliwa katika angalau asilimia 50 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ili kuongoza utekelezaji wa ngazi ya chini. |
| | 8.3 Kuongeza matumizi ya teknolojia za upangaji ardhi kwa njia ya kijiografia na kidijitali kufikia angalau asilimia 60 ya vijiji |
| 9. Kuhakikisha usimamizi na uhifadhi wa angalau asilimia 40 ya rasilimali bainifu za mimea, wanyama na misitu zinazopewa kipaumbele kufikia Juni 2031. | 9.1 Kuanzisha na kuimarisha Kituo cha Taifa cha Rasilimali za Kijenetiki kufikia 2030, chenye jukumu la kujenga mfumo endelevu na imara wa usimamizi wa rasilimali za kijenetiki za mimea, wanyama na misitu. |
| | 9.2 Kuingiza uhifadhi wa rasilimali za kijenetiki katika mifumo ya kitaifa ya usalama wa chakula, lishe na ulinzi wa bioanuai. |
| | 9.3 Kuhifadhi kwa utaratibu anuwai ya nyenzo bainifu za mimea, wanyama na misitu kila mwaka kupitia mbinu za uhifadhi nje ya makazi asilia (ex-situ) na ndani ya makazi asilia (in-situ). |
| | 9.4 Kuanzisha na kudumisha hifadhidata ya kitaifa ya kidijitali ya rasilimali za kijenetiki ili kuhakikisha upatikanaji kwa watafiti na watunga sera |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 9.5 Kuanzisha mfumo wa uwazi na ufanisi wa upatikanaji na ugawaji faida (ABS), unaolingana na itifaki ya Nagoya ili kukuza upatikanaji wa haki na ugawaji wa faida kwa uwazi. |
| | 9.6 Kushiriki kikamilifu katika tafiti na ushirikiano na taasisi za ndani na kimataifa kila mwaka ili kuimarisha uhifadhi na matumizi ya rasilimali za kijenetiki. |
| **3.1.1 Mipango na Usimamizi wa Miji iliyoboresha na endelevu.** | |
| **Lengo la 2:** Kukuza upangaji mzuri wa miji ulio endelevu kwa kuongeza miundombinu ya kisasa, kuboresha ufanisi wa matumizi ya ardhi na kuimarisha usafiri wa mijini unaoruhusu ukuaji wa uchumi wa taifa ifikapo 2050. | |
| 1. Angalau asilimia 50 ya wakazi wapya wa mijini waishi katika makazi yaliyopangwa rasmi, huku mfumo wa kitaifa wa ardhi wa kidijitali ukiwa unafanya kazi kufikia Juni 2031. | i. Kuandaa na kuendesha mfumo wa kitaifa wa upangaji miji na taarifa za Ardhi (NULIS). |
| | ii. Kuimarisha utekelezaji wa sheria za upangaji miji na matumizi ya ardhi ili kudhibiti ukuaji holela wa makazi yasiyo rasmi. |
| 3. Angalau asilimia 20 ya miradi mipya ya miundombinu ya miji kujumuisha usanifu unaozingatia utoaji mdogo wa hewa ukaa na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi na miji mahiri miwili ya majaribio ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kujumuisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na Usimamizi wa Vihatarishi vitokanavyo na Majanga katika maandalizi ya mipango miji mahiri kwa angalau asilimia 70. |
| | 3.2 Kuzindua miji mahiri miwili ya majaribio yenye miundombinu ya kidijitali, utoaji wa huduma za umma zenye tija na makazi yanayostahimili tabianchi. |
| | 3.3 Kuongeza wigo wa programu za makazi nafuu na kuandaa kongani/SEZs moja hadi mbili kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPPs). |
| **3.1.2 Mageuzi na usimamizi endelevu wa ardhi** | |
| **Lengo la 3:** Kuimarisha usimamizi endelevu na wenye tija wa ardhi kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa umiliki wa ardhi, kuboresha upangaji wa matumizi ya ardhi na kukuza ukuaji endelevu wa uchumi. | |
| Kurasimisha ardhi kwa kuimarisha usajiliwa na utoaji haki miliki wa ardhi kutoka asilimia 30 (2023) hadi angalau asilimia 50 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuimarisha mifumo ya kisheria na kanuni zinazoongoza ugawaji endelevu wa ardhi na kuzingatia usawa wa kijinsia katika hati miliki za ardhi. |
| | 1.2 Kuandaa mwongozo wa kitaifa wa kuzuia, kusuluhisha na kutatua migogoro ya ardhi. |
| | 1.3 Kutoa mafunzo kwa angalau asilimia 50 ya maafisa ardhi katika ngazi ya Serikali za Mitaa kuhusu matumizi ya mifumo ya kidijitali, GIS, usuluhishi wa migogoro na usimamizi wa ardhi unaozingatia tabianchi. |
| 3. Kuongeza eneo la ardhi lililotengwa kwa matumizi ya viwanda kutoka asilimia 5 (2023) hadi angalau asilimia 7 ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kuanzisha benki ya kitaifa ya ardhi kwa ajili ya kusimamia na kutenga ardhi kwa matumizi ya kongani za viwanda, SEZs na shoroba kubwa za usafirishaji. |
| | 3.2 Kuandaa na kutekeleza mipango maalum ya matumizi ya ardhi kwa ajili ya ukuaji wa viwanda katika Kanda za Vipaumbele 3 – 5 zinazounganishwa kimkakati na miundombinu ya usafiri na usafirishaji. |
| | 3.3 Kubuni na kujaribu mifumo ya vivutio vya kodi ili kuvutia uwekezaji katika matumizi ya ardhi kwenye shughuli za viwanda na usafirishaji kwa angalau Maeneo Maalumu ya Uwekezaji matatu. |
| **3.2. Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi** | |

| Shabaha | Afua |
| --- | --- |
| **Lengo la 1:** Kuimarisha uhimilivu wa tabianchi unaohifadhi urithi wa asili wa Tanzania kwa ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho**.** | |
| Uhimilivu wa tabianchi kuingizwa katika mifumo yote ya kitaifa ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi katika sekta zote muhimu na Mamlaka za serikali za mitaa, na kuuunganisha katika mipango na bajeti za kila mwaka. |
| 2. Kupunguza uzalishaji wa gesi joto (GHG) kwa asilimia 30–35 na kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika umeme wa taifa kufikia asilimia 75 ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuongeza nishati safi ya kupikia kwa angalau asilimia 50 ya kaya na kutekeleza programu za ubora wa nishati ili kupunguza matumizi kwa asilimia 10 katika sekta muhimu. |
| 3. Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kukabiliana na hasara na uharibifu (Loss and Damage) ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa hasara na uharibifu kwa ajili ya kuratibu maandalizi, urejeshwaji na fedha za kukabiliana na athari za tabianchi zisizoweza kuepukika. |
| **Lengo la 2:** Kuchochea teknolojia na ubunifu katika kilimo, mifugo, uvuvi na misitu ili kujenga minyororo ya thamani yenye uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha ukuaji endelevu wa uchumi ifikapo 2050**.** | |
| Asilimia 30 ya wazalishaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kutumia teknolojia rafiki kwa mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2031 | Kuongeza majukwaa ya ushauri unaotolewa kupitia simu kwa wakulima, wavuvi na wafugaji ili kuwapa taarifa za tabianchi na masoko kwa wakati. |
| Asilimia 20 ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo kutumia nishati jadidifu na kutekeleza mbinu stahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi ifikapo Juni 2031. | Kuwezesha kongani za viwanda vya kilimo zinazoendeshwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi zenye mifumo ya kidijitali kwa ajili ya ufanisi wa matumizi ya rasilimali. |
| Kunapunguzwa upotevu wa mazao baada ya mavuno kwa asilimia 15, na asilimia 40 ya biashara ya mazao ya kilimo kufanyika kupitia majukwaa ya kidijitali ifikapo Juni 2031. | Kuanzisha majukwaa jumuishi ya takwimu yanayounganisha uzalishaji, usafirishaji na mahitaji ya watumiaji ili kuboresha ufanisi wa minyororo ya ugavi. |
| **3.2.1. Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema na Uwezo wa Taasisi** | |
| **Objective 3:** Kuanzisha mfumo jumuishi wa sekta mbalimbali wa utoaji wa tahadhari ya mapema utakaoimarisha uhimilivu wa taifa kupitia taarifa za wakati, za kuaminika na zinazoweza kuchukuliwa hatua katika sekta za mazingira, uchumi, afya na kijamii ifikapo 2050. | |
| 1. Kuongeza uwekezaji na ugharamiaji wa Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema (EWS) kwa angalau asilimia 0.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka, ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuanzisha mifumo ya Ubia baina ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya kufadhili miundombinu ya tahadhari ya mapema. |
| 2. Kutumia teknolojia ya kidigitali kutoa taarifa za tahadhari ya mapema katika kanda zote zenye hatari kubwa ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuanzisha majaribio ya tahadhari za moja kwa moja katika maeneo 2–3 yenye hatari kubwa. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 3. Kuongeza idadi ya watu wanaofikiwa na Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema kutoka asilimia 2 (2023) hadi angalau asilimia 30 ifikapo Juni 2031, kwa kuongeza mifumo jumuishi ya kijamii kwa angalau miji 10. | 3.1 Kuanzisha kampeni za kitaifa za uhamasishaji katika sekta mbalimbali kuhusu Mfumo wa Utoaji wa Tahadhari ya Mapema na kuanzisha mazoezi ya majaribio kwa kila mwaka katika sekta mbalimbali. |
| **3.2.2 Kuimarisha Ushiriki katika Biashara ya Hewaukaa** | |
| **Lengo la 1:** Kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kinara wa kikanda katika biashara ya hewaukaa, kuchochea mapato endelevu, ajira zinazotokanazo na uchumi wa kijani na uhimilivu wa tabianchi. | |
| 1. Kuanzisha sera ya taifa ya biashara ya hewaukaa na mfumo wa utawala ifikapo Juni 2028. | i. Kufanya mapitio na kuhuisha miongozo na kanuni za Biashara ya hewaukaa za kitaifa ili kuendana na mwenendo na viwango vya masoko ya kimataifa. |
| | ii. Kuanzisha mfumo wa ndani wa kupanga bei ya hewaukaa (mfano, kodi ya hewaukaa au mfumo wa biashara) kwa sekta za kipaumbele. |
| 2. Kuanza kufanya kazi kikamilifu kwa mfumo wa kitaifa wa kidijitali wa MRV na usajili wa biashara ya hewaukaa ifikapo Juni 2030. | i. Kuandaa na kuendesha mfumo imara wa kitaifa wa kidijitali wa upimaji, utoaji taarifa na uthibitishaji (MRV) na jukwaa la usajili wa biashara ya hewaukaa. |
| | ii. Kuwekeza katika teknolojia za kisasa, zenye uwazi na zinazotoa taarifa kwa wakati mfano setilaiti ili kuboresha ujumuishaji wa mfumo wa MRV. |
| | iii. Kuanzisha vivutio na mifumo ya kifedha (mfano: punguzo la kodi, hati fungani za kijani) ili kuvutia wawekezaji wa ndani na jamii kushiriki katika miradi ya biashara ya hewaukaa. |
| | iv. Kuwezesha uundaji wa vyama vya ushirika na mashirika ya kijamii ili kushiriki kwa pamoja katika miradi ya biashara ya hewaukaa na kusimamia manufaa yake. |
| **3.3.3 Kuimarisha Manufaa ya Uchumi wa Buluu** | |
| **Lengo la 1:** Kutumia rasilimali za bahari na maji baridi kwa njia endelevu ili kuchochea ukuaji jumuishi wa uchumi, kuzalisha ajira, kulinda mazingira na kuboresha maisha, pamoja na kuchochea ubunifu na kuimarisha usimamizi. | |
| 1. Kuongezeka kwa mchango wa uvuvi na ufugaji samaki katika Pato la Taifa kufikia asilimia 3.5 ifikapo 2030. | 1.1 Kuanzisha maeneo makubwa ya ufugaji samaki yenye vituo vya kuzalisha vifaranga, viwanda vya chakula cha samaki pamoja na miundombinu ya uchakataji ili kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani ya Samaki. |
| | 1.2 Kuwekeza katika mtandao wa kitaifa wa usafirishaji wa bidhaa zinazoharibika na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa kidijitali ili kupunguza upotevu wa samaki baada ya mavuno na kufungua masoko ya nje ya samaki yenye kiwango cha kubwa. |
| | 1.3 Kutoa mikopo nafuu na ruzuku kwa wavuvi na SMEs kwa ajili ya kutumia vifaa vya kisasa, mbinu endelevu na uongezaji thamani. |
| | 1.4 Kutekeleza viwango vya uvunaji vinavyozingatia tafiti za kisayansi na kulinda maeneo muhimu ya kuzaliana samaki ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa sekta. |
| | 1.5 Kuwekeza katika viwanda vikubwa vya uzalishaji wa chakula cha samaki. |
| | 1.6 Kuongeza miundombinu ya usafirishaji wa bidhaa za uvuvi zinazoharibika (cold chain). |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 2. Kuongeza biashara ya majini (maritime trade) hadi tani milioni 35 ifikapo 2030. | i. Kukamilisha maboresho ya kuongeza uwezo wa bandari kuu zote (Dar es Salaam, Mwanza, n.k.) na kuanza kuendesha bandari ya Bagamoyo ili kuongeza uwezo wa kushughulikia mizigo. |
| | ii. Kuweka sharti la kutumia mfumo wa kisasa wa kidijitali uliounganishwa wa forodha na usafirishaji ili kupunguza muda wa meli kukaa bandarini na kurahisisha taratibu zote za biashara. |
| | iii. Kutoa vivutio maalum vya kikodi ili kuvutia wazalishaji wa kimataifa na makampuni ya usafirishaji kuanzisha viwanda vinavyohisiana na bandari. |
| | iv. Kushirikiana na kampuni kubwa za usafirishaji ili kuanzisha njia za meli zenye uzalishaji mdogo wa hewaukaa kwa kutumia nishati mbadala, na hivyo kuifanya nchi kuwa kinara wa biashara endelevu majini. |
| | v. Kuendeleza njia za usafiriji baharini (blue and green shipping corridors) zenye uzalishaji mdogo wa hewaukaa. |
| | vi. Kuunganisha miji ya pwani na visiwa. |
| | vii. Ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya doria na usalama hususan kwenye maeneo ya uvuvi mipakani. |
| 3. Kuongeza mapato ya utalii yatokayo na shughuli za bahari kufikia kiasi cha shilingi bilioni 2,000 ifikapo 2030. | i. Kutoa msamaha wa kodi na vibali kwa wakati kwa wawekezaji wanaowekeza katika mapumziko ya kitalii yenye thamani kubwa, *marinas* na miundombinu ya burudani. |
| | ii. Kuzindua kampeni ya kimataifa ya masoko ili kuhakikisha nchi inatambuliwa kama moja ya maeneo matatu bora duniani kwa utalii wa baharini. |
| | iii. Kuanzisha programu ya ubia wa biashara (franchise) na mafunzo itakayowezesha jamii kuendesha na kumiliki maeneo yenye hadhi ya malazi ya watalii. |
| | iv. Kuanzisha tamasha mahsusi la kitaifa (flagship event) la kuvutia watalii, vyombo vya habari na wawekezaji, ili kuongeza mapato ya kila mwaka pamoja na kuongeza muonekano kimataifa. |
| 4. Kuendelezwa kwa jumla ya MW 400 za nishati jadidifu ya bahari ifikapo mwaka 2030. | i. Kukamilisha na kuchapisha sheria, viwango vya uunganishaji kwenye gridi ya umeme, pamoja na utaratibu wa ushindani wa zabuni kwa miradi ya upepo wa baharini, mawimbi ya bahari na mikondo ya Bahari. |
| | ii. Kuandaa mnada wa ushindani kwa miradi miwili mikubwa ya uzalishaji wa umeme kwa kutumia upepo wa bahari, yenye uwezo wa MW 400. |
| | iii. Kuboresha uwezo wa gridi ya taifa katika kushughulikia nishati jadidifu pamoja na kuwekeza katika mifumo mikubwa ya uhifadhi wa umeme kwa kutumia betri, ili kuhakikisha uimara na uhakika wa upatikanaji wa umeme. |
| 5. Kuongezeka kwa asilimia 5 ya maeneo ya baharini yaliyohifadhiwa ifikapo mwaka 2030. | i. Kutunga sheria za kuteua rasmi maeneo mapya ya baharini yaliyohifadhiwa (MPAs) yanayochukua asilimia 10 ya eneo la mpaka wa bahari na kuhakikisha upatikanaji wa bajeti mahsusi kwa ajili ya usimamizi wake. |
| | ii. Kutumia setilaiti na teknolojia ya droni kufuatilia uvuvi haramu na hali ya ikolojia ndani ya maeneo yote ya baharini yaliyohifadhiwa. |
| 6. Kukusanya mapato kiasi cha dola za Marekani milioni 150 kila mwaka kupitia *blue carbon credit* ifikapo 2030. | i. Kurejesha hekta 150,000 za mikoko na nyasi kwa kutumia nguvu kazi katika jamii na teknolojia ya droni/akili unde kwa ajili ya upandaji sahihi na mauzo ya mikoko na nyasi za bahari. |
| | ii. Kuanzisha chombo maalumu cha serikali kitakachothibitisha, ukusanyaji na uuzaji wa hewa ukaa katika masoko ya kimataifa, na kusimamia mtiririko wa mapato. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | iii. Kutoa mafunzo na vifaa kwa wananchi 50,000 wa maeneo ya pwani ili kusimamia urejeshaji wa miradi na kupata mgao wa moja kwa moja wa mapato kutoka mauzo ya hewaukaa kupitia majukwaa ya kifedha ya kidijitali (fintech). |
| 7. Kukusanya mapato kiasi cha Dola za Marekani milioni 50 kila mwaka kupitia bioteknolojia ya bahari ifikapo 2030. | i. Kuanzisha kituo maalumu cha kukuza kampuni zinazoibukia (startups), kutoa ruzuku za utafiti na maendeleo (R&D grants), na kuwezesha upatikanaji wa mtaji wa uwekezaji (venture capital) ili kuongeza wigo wa miradi ya bioteknolojia ya bahari. |
| | ii. Kushirikiana na kampuni za kimataifa za dawa, vipodozi na lishe (nutraceuticals) ili kuzalisha na kuuza kwa pamoja bidhaa zenye thamani zinazotokana na rasilimali za bahari. |
| | iii. Kuunda mifumo ya ugavi, kanuni na mikataba ya biashara kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa za thamani katika bioteknolojia ya bahari. |
| | iv. Kutoa punguzo la kodi na umiliki wa haki miliki (intellectual property) kwa kampuni zinazowekeza katika uzalishaji wa dawa na vimeng'enyo vya viwandani vinavyotokana na rasilimali za bahari. |
| **1. VICHOCHEO** | |
| **1.1. Nishati** | |
| **Lengo 1:** Sekta ya nishati ya Tanzania kusimamiwa na taasisi za kisasa, zenye uwazi na ufanisi, zikisaidiwa na nguvu kazi yenye ujuzi, inayohakikisha utoaji wa huduma za uhakika, ubunifu na endelevu. | |
| 1. Kuthibitishwa kwa nguvu kazi ya taifa yenye wataalamu 10,000 katika sekta ya nishati ifikapo Juni 2031 | i. Kuandaliwa na kuanza kutekelezwa kwa Programu Jumuishi yaTaifa ya Kuendeleza Ujuzi wa Nishati (NESDP). |
| 2. Uwepo wa usimamizi wa uwazi, ufanisi na uwajibikaji katika sekta ya nishati ya Tanzania ifikapo Juni 2031 | i. Kuimarisha mifumo ya kisheria na udhibiti kwa ajili ya usimamizi madhubuti na wenye ufanisi katika sekta ya nishati. |
| | ii. Kuanzisha Kanuni ya Utawala Bora kwa Mashirika ya umma katika sekta ya nishati, inayoweka wajibu wa kisheria wa kuchapisha hadharani taarifa za utendaji na kifedha. |
| **Lengo 2:** Kufanya mageuzi katika sekta ya nishati kwa kuijengea mfumo wa ushindani, uwazi na uendelevu wa kifedha, ikiwemo kubadilishwa kwa shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuwa shirika la kibiashara lililoganywa katika vitengo vinavyofanya kazi kwa kujitegemea, na linaloendeshwa chini ya mfumo wa udhibiti unaozingatia utendaji (performance-based regulatory framework) utakaowezesha ushiriki wa sekta binafsi na utoaji wa huduma za umeme za uhakika. | |
| 1. Kubadilishwa kwa shirika la TANESCO kuwa shirika la kibiashara na kugawanywa kikamilifu katika idara tofauti za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji wa umeme ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kufanyika kwa maboresho ya muundo wa taasisi na fedha kupitia ukaguzi huru, mpango kazi na uhuishaji wa kanuni za udhibiti. |
| | 1.2 Kutenganisha miundo ya fedha na usimamizi katika shughuli za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme. |
| | 1.3 Kutunga sheria na nyenzo za udhibiti zinazowezesha kuibadilisha TANESCO kuwa kampuni kuu ya kitaifa ya nishati (national energy holding company) na kugawa sekta katika taasisi huru za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji (G, T & D). |
| | 1.4 Kuanzishwa kwa mfumo wa bei zinazoakisi gharama halisi (cost-reflective tariffs) na uwazi ili kupunguza ruzuku na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. |
| | 1.5 Kuanzishwa kwa mikataba ya udhibiti na usimamizi inayozingatia utendaji (performance-based regulation and management contracts) ili kuboresha ufanisi, kupunguza hasara, na kuimarisha utoaji wa huduma. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 2. Kuanzisha na kugharamia Usimamizi Huru wa Mfumo na Soko la Umeme (ISMO) mwenye mamlaka ya upangaji wa uzalishaji (dispatch), upatikanaji wa mfumo (open access), na kuratibu uendeshaji wa soko shindani la umeme ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuandaliwa kwa mfumo wa udhibiti na uendeshaji wa ISMO, kwa kushirikiana na EWURA, TANESCO na wadau wa sekta binafsi. |
| | 2.2 Kukusanya fedha, msaada wa kitaalam na uwezo wa kitaasisi unaohitajika kwa ajili ya kuanzisha ISMO pamoja na kusimamia uendeshaji wake kila mwaka. |
| | 2.3 Kuwezesha uendeshaji wa Usimamizi Huru wa Mfumo na Soko la Umeme (ISMO), utekelezaji wa kanuni za upatikanaji wa mfumo, na uratibu wa shughuli za soko shindani la umeme kwa wazalishaji wa umeme wa umma na binafsi. |
| **Lengo 3:** Kuimarisha uwezo wa Tanzania wa kuwa na miundombinu ya nishati iliyo imara, unganishi na tayari kwa ajili ya uwekezaji pamoja na upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika ndani ya nchi, na mipakani kupitia ushiriki endelevu wa sekta ya binafsi na *green capital*. | |
| 1. Kuwepo kwa angalau kiunganishi kimoja (1) cha kikanda cha umeme wa msongo wa kV 400 pamoja na kuboreshwa kwa mtandao mkuu wa usafirishaji wa umeme ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini na biashara ya umeme ya kikanda ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kujengwa kwa kiunganishi kimoja (1) mpakani cha msongo wa 400kV kinachounganisha Tanzania na Zambia, Uganda na Kenya ili kuimarisha gridi na biashara ya umeme ya kikanda. |
| | 1.2 Kusambaza mifumo ya SCADA na teknolojia bora za gridi katika vituo vyote vya kikanda vya udhibiti wa mfumo kwa asilimiaa 90. |
| | 1.3 Kuboresha gridi ya taifa ya usafirishaji wa umeme kufikia 400kV katika ushorobo wa uliopewa kipaumbele, ili kuhakikisha gridi inaweza kupokea na kusafirisha umeme wenye uwezo mkubwa wa ndani ya nchi na kikanda. |
| | 1.4 Kuhuisha kanuni na taratibu za gridi ili kuendana na viwango vya Mifuko ya Nishati ya Kusini mwa Afrika na Afrika Mashariki (SAPP na EAPP) kwa asilimia 70. |
| 2. Kukusanya kwa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 7 kutoka katika mikopo yenye masharti nafuu ili kufadhili uzalishaji wa nishati safi na usafirishaji wa umeme nchini ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuanzisha na kutumika Mfumo wa ufadhili wa nishati safi ya kupikia - *Clean Energy Blended Finance Facility*. |
| | i. Kuanzishwa kwa mfumo wa ufadhili wa nishati safi ya kupikia - Clean Energy Blended Finance Facility. |
| | ii. Kuanzisha ushirikiano na Benki za Maendeleo za Kimataifa (MDBs) na mifuko ya tabianchi. |
| | iii. Kuandaa mfumo wa upangaji unaozingatia masuala ya mazingira na orodha ya miradi ya kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji. |
| **Lengo 4:** Kuongezeka kwa uwezo wa uzalishaji umeme nchini Tanzania kufikia MW 70,000 ili kukidhi mahitaji ya baadae, kuimarisha uendelezaji wa viwanda na kuhakikisha upatikanaji wa nishati kwa wote. | |
| 1. Kuongeza matumizi ya nishati kwa mtu mmoja mmoja kufikia 600 kWh ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya uzalishaji wa nishati safi (umeme wa maji, jua, upepo, jotoardhi, gesi na nyuklia). |
| | 1.2 Kuandaliwa kwa mpango kabambe jumuishi wa upanuzi wa uzalishaji wa umeme. |
| | 1.3 Kutoa ruzuku kwa kaya ajili ya uunganishaji wa umeme na matumizi ya teknolojia zilizonje ya gridi (off-grid technologies). |
| 2. Kuongeza uwezo wa uzalishaji wa nishati safi kufikia MW 15,000 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuanza kwa uzalishaji wa mitambo mikubwa ya umeme wa maji, jua, upepo na jotoardhi kwa awamu. |
| | 2.2 Kuandaliwa na kuanza kuendesha kiwanda cha majaribio cha nyuklia chenye uwezo wa MW 1,000. |
| | 2.3 Kuanza matumizi ya mifumo ya vivutio na minada ya ushindani kwa wazalishaji binafsi wa umeme (IPPs). |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| **Lengo 5:** Kuongezeka kwa ujumuishaji wa nishati jadidifu katika mchanganyiko wa nishati ya Tanzania kufikia asilimia 50, ili kupunguza uzalishaji wa hewaukaa na kuimarisha ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. | |
| 1. Kuzalisha umeme MW 1,700 kupitia jotoardhi, MW 500 upepo, na MW 715 jua ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kutoa kipaumbele katika utoaji wa leseni za nishati jadidifu (RE) na taratibu za vibali vya kimazingira kwa kurahisisha hatua za udhibiti, kuweka muda maalumu wa utekelezaji na kuimarisha uratibu wa taasisi. |
| | i. Kufanyika kwa mapitio na kufungamanisha mifumo ya udhibiti ya nishati jadidifu (RE). |
| **Lengo 6:** Kuboreshwa kwa mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini Tanzania ili kupunguza hasara za kiufundi na kibiashara kufikia chini ya asilimia 5 pamoja na kuhakikisha uimara wa gridi | |
| 1. Kupunguza upotevu wa umeme katika mfumo wa Taifa kutoka asilimia 14.2 hadi asilimia 12.4 ifikapo Juni 2031. | Kubadilishwa kwa angalau asilimia 70 ya transfoma zilizochakaa na kuboreshwa kwa kilomita 1,000 za njia kongwe za usambazaji wa umeme mijini ili hasara za kiufundi. |
| | i. Kubadilisha transfoma zilizochakaa na kuboresha njia za umeme za mijini. |
| 2. Kujenga vituo vidogo 100 vya kupooza umeme (substations) vijijini na mifumo ya gridi mahiri katika mikoa mikuu ifikapo Juni 2031. | ii. Kuwekeza katika gridi za vijijini na miundombinu ya usambazaji wa umeme yenye teknolojia mahiri. |
| | iii. Kutekeleza uendeshaji wa mtandao wa umeme kwa teknolojia ya "digital twin" na matengenezo ya kutabiri hitilafu (predictive maintenance) kwa njia ya kidijitali. |
| | iv. Kutekeleza matumizi ya mita zenye ubora kwa asilimia 100 kwa wateja wa kibiashara na wa kati (medium customers). |
| | v. Kusimikwa kwa nyaya za chini ya ardhi katika maeneo yenye msongamano mkubwa mijini. |
| | vi. Kuongeza wigo wa ushiriki wa sekta binafsi katika usafirishaji na usambazaji wa umeme kupitia Makampuni Huru ya Usambazaji wa Umeme (IDNOs) kwenye maeneo ya viwanda. |
| Lengo Na. 7: Upatikanaji wa umeme wa uhakika na gharama nafuu katika kaya zote nchini Tanzania kwa asilimia 100. | |
| 1. Kuongeza uunganishaji wa umeme kwa kaya nchini kutoka asilimia 49 hadi asilimia 55.2, na uunganishaji wa umeme vijijini kutoka asilimia 36 hadi asilimia 42.8 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kutekeleza kampeni za kitaifa za uunganishaji wa umeme kwa kuunganisha kaya milioni 4 mpya. |
| | 1.2 Kuanzishwa na kufadhiliwa kwa Mfuko wa Umeme Vijijini wenye thamani ya dola za Marekani milioni 200 |
| | 1.3 Kufanya mapitio na kuboresha taratibu za uunganishaji wa umeme zilizorahisishwa na kupunguza gharama za uunganishaji kwa asilimia 50 kwa kaya zenye kipato cha chini. |
| | 1.4 Kuanzishwa kwa motisha zinazotegemea utendaji (performance-based incentives) kwa wawekezaji binafsi wanaotoa huduma katika maeneo ya vijijini. |
| 2. Kuboresha upatikanaji wa umeme kwa asilimia 80 katika kaya ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kujengwa kwa vituo vidogo 100 vya kupooza umeme (substations) vijijini pamoja na kuboresha transfoma za maeneo ya vijijini. |
| | 2.2 Kusambazwa kwa gridi mahiri na mifumo ya ufuatiliaji katika ya maeneo ya vijijini kwa asilimia 80. |
| | 2.3 Kuanzishwa kwa mikataba ya matengenezo kulingana na utendaji (performance-based maintenance contracts) katika maeneo yote ya vijijini. |
| **Lengo 8:** Kuimarisha usalama wa nishati na uhakika wa upatikanaji wa umeme Tanzania kupitia vyanzo mchanganyiko vya uzalishaji wa umeme, unaojumuisha matumizi ya kimkakati ya akiba ya makaa ya mawe yanayoungwa mkono na teknolojia zenye utoaji mdogo wa hewa chafu, pamoja na ujumuishaji wa vyanzo vya nishati jadidifu. | |
| 1. Kusimikwa mitambo yenye uwezo wa kuzalisha MW 1,000 za umeme kupitia makaa ya mawe kwa | 1.1 Kutambuliwa na kutengwa kwa maeneo yenye makaa ya mawe na kuharakisha utoaji wa leseni kwa ajili ya mitambo ya uzalishaji wa umeme ya MW 3,000 inayotumia makaa ya mawe. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| kuzingatia vigezo vya kimazingira ifikapo Juni 2031 | 1.2 Kuhamasisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi (PPPs) na dhamana za uwekezaji katika matumizi ya teknolojia safi za makaa ya mawe, ikijumuisha mifumo ya kupunguza salfa katika moshi (flue gas desulphurisation) na teknolojia za kunasa hewa ukaa. |
| | 1.3 Kuanzishwa kwa Mfumo Endelevu wa Uzalishaji Umeme unaotokana na Makaa ya Mawe utakaosimamia uibuaji wa miradi na ufuatiliaji wa masuala ya mazingira. |
| 2. Kuwa na akiba ya ziada ya asilimia 20 (reserve margin) ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuongeza uzalishaji wa umeme wa MW 1,500 unaounganishwa na gridi kupitia gesi, umeme wa maji na mifumo ya nishati jadidifu. |
| | 2.2 Kuanzishwa kwa Sera ya Akiba ya Kimkakati ya Nishati (Strategic Energy Reserve Policy) yenye sharti la kuwa na akiba ya ziada isiyopungua asilimia 20 ya umeme. |
| | 2.3 Kutekelezwa kwa mfumo wa maoteo wa wakati halisi (real-time forecasting) wa mahitaji na upatikanaji wa nishati ili kuimarisha usimamizi wa akiba. |
| **1.2. Miundombinu na Usafirishaji** | |
| **Lengo 1:** Kumairisha ufanisi na uunganishaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa kuboresha usafirishaji wa watu, bidhaa na rasilimali ndani ya miji na mikoa ili kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi, maendeleo ya viwanda, na kuboresha upatikanaji wa masoko ya kimataifa | |
| **1.2.1. Usafiri wa Barabara** | |
| 1. Kuanzisha Mfumo jumuishi, endelevu na wa kisasa wa miundombinu ya barabara nchini ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuasili viwango vya usanifu vinavyostahimili mabadiliko ya tabianchi na kutumia zana za kidijitali (AI, GIS) kwa ajili ya matengenezo ya barabara, taa za barabarani zinazoendeshwa kwa nishati itokanayo na jua, na mifumo ya kisasa ya usimamizi wa vyombo vya usafiri barabarani. |
| | 1.2 Kuanza utekelezaji na kuuboresha Mfuko wa Barabara ili kuwezesha matengenezo ya kawaida na ya mara kwa mara kufanyika kwa wakati. |
| | **1.3** Kusambazwa kwa Mifumo Bora ya Usafirishaji (ITS) ikijumuisha ufuatiliaji wa msongamano wa magari, mifumo ya ukusanyaji tozo (smart tolling), mizani ya kidijitali, na udhibiti wa uzito kupita kiasi. |
| | 1.4 Kutengeneza ramani ya kidijitali ya barabara zote za vijijini zisizoorodheshwa kwa kutumia GPS na zana huria ili kusaidia upangaji, matengenezo na kukabiliana na matukio dharura. |
| | 1.5 Kuwekeza katika miundombinu ya mijini ili kupunguza msongamano wa magari katika miji mikuu ikiwemo Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Mbeya. |
| 2. Kuongeza uwiano wa barabara zilizopigwa lami kutoka asilimia 8.6 hadi asilimia 10.58 ifikapo Juni 2031. | **2.1** Kujenga, kukarabati na kufanya matengenezo ya barabara za mikoa na za pembezoni (feeder roads) zinazoziunganisha kanda za kilimo, madini na viwanda. |
| | **2.2** Kuongeza mtandao wa barabara za kisasa na mifumo ya Usafiri wa Mabasi yaendayo Haraka (BRT) katika miji mikuu. |
| | **2.3** Kuendeleza barabara za mipakani zinazoiunganisha Tanzania na nchi jirani za EAC na SADC ili kukuza biashara ya kikanda. |
| | **2.4** Kujenga barabara mpya za mwendokasi (expressways) zinazounganisha miji mikubwa na vituo vya uchumi, zikiwa na spidi bora. |
| | **2.5** Kusanifu na kujenga madaraja ya kisasa yenye hadhi kwa ajili ya kuvuka mito mikubwa na hivyo kuimarisha utambulisho wa kikanda. |
| | **2.6** Kuanzishwa kwa miradi ya majaribio ya barabara kwa ajili ya magari ya umeme (EV) na vituo vya kuchajia magari ya mizigo na abiria katika njia zenye msongamano mkubwa. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 3. Kufikia kiwango cha asilimia 35 cha matengenezo ya barabara ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa miundombinu ya barabara, ikijumuisha Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali za Barabara (RAMS), mifumo ya utunzaji wa taarifa za barabara zinazotumia GIS, na ripoti za kila mwaka za miundombinu ili kujua maendelea, hali na athari zake. |
| | 3.2 Kuongezeka kwa bajeti ya matengenezo ya barabara pamoja na kubuni vyanzo vipya vya ufadhili. |
| | 3.3 Kutenga na kujenga mifumo ya njia za chini ya ardhi (underground ducts) kwa ajili ya maji, umeme, intaneti na mifereji ya maji taka chini ya barabara za mijini ili kupunguza uchimbaji wa mara kwa mara na uharibifu wa miundombinu. |
| **1.2.2. Usafiri wa Anga** | |
| 1. Kuongeza Farihisi ya Uunganishaji wa Usafiri wa Anga (ACI) kutoka asilimia 0.35 mwaka 2025 hadi asilimia 0.85 ifikapo Juni 2031. | **1.1** Kuongeza uwezo wa majengo ya abiria, maeneo ya maegesho ya ndege, njia za kurukia na kutua ndege, pamoja na miundombinu ya shehena katika viwanja vikuu vya kimataifa (JNIA, KIA, Zanzibar, Songwe na Mwanza). |
| | **1.2** Kukarabati na kupanua viwanja vya ndege vya mikoa ya Mbeya, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mtwara, Musoma na Shinyanga. |
| | **1.3** Kutenga vituo vya shehena katika viwanja vya JNIA, Mwanza na Songwe kuwa kitovu cha usafirishaji kwa mazao ya bustani, samaki na biashara ya mtandaoni. |
| | **1.4** Kuweka mifumo ya uangalizi kwa rada na usambazaji kwa satelaiti katika anga lote la Tanzania. |
| | **1.5** Kufungamanisha utoaji wa leseni, usalama wa anga na taratibu za uongozaji ndege na nchi jirani ili kuwezesha usafiri wa kikanda bila vikwazo na kuwa na anga huru. |
| | **1.6** Kujenga kituo cha kitaifa cha mafunzo ya usafiri wa anga kwa ushirikiano na wadau wa kimataifa ili kuzalisha marubani, wahandisi, waongozaji ndege, wahudumu na huduma za droni. |
| | **1.7** Kutumia mifumo ya Kieletroniki ya kuhakiki taarifa kwa kutumia alama za vidole katika milango ya kusafiriia, viza na uthibitisho wa kiafya ili kuboresha usalama, kasi na ufanisi wa huduma za abiria. |
| | **1.8** Kujenga na kuboresha karakana za matengenezo na ukarabati wa ndege (MRO) katika Mwanza, Songwe, Kilimanjaro na Dar es Salaam ili kuhudumia ndege za ukanda wa kikanda. |
| **1.2.3. Usafiri wa Reli** | |
| 1. Kuongeza wigo wa mtandao wa reli kutoka kilomita 4.97 kwa kila kilomita $1{,}000^2$ hadi kilomita 7.98 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kukamilisha ujenzi wa mfumo wa reli wa mizigo na abiria wenye uwezo mkubwa (SGR) unaounganisha Dar es Salaam–Dodoma–Mwanza, Isaka–Kigali, Tabora–Kigoma–DRC, Tabora–Mpanda–Kalemie na Mtwara–Mbambabay–Mchuchuma–Liganga. |
| | 1.2 Kukarabati huduma za reli ya kati (MGR), ikiwemo miunganisho ya matawi kama Dar–Tanga–Arusha. |
| | 1.3 Kujenga njia fupi za reli kutoka njia kuu kwenda maeneo ya migodi (mf. Liganga, Mchuchuma) na maeneo ya viwanda (mf. Bagamoyo, Kisarawe, Mlandizi). |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 1.4 Kuiunganisha reli na huduma za meli katika maziwa makuu (Victoria, Tanganyika, Nyasa) kupitia bandari zenye njia za reli. |
| | 1.5 Kujenga au kuboresha maghala na vituo vya mizigo katika vituo vya reli kama Tabora, Mwanza na Kigoma. |
| | 1.6 Kuboresha miundombinu chakavu (reli, nguzo, mawe) kutoka Dar es Salaam hadi New Kapiri Mposhi. |
| | 1.7 Kufanya maboresho ya kisheria na kiuwekezaji katika shirika la reli la TAZARA ili kuwezesha uashiriki wa sekta binafsi kama waendeshaji na wabia wa usafirishaji. |
| | 1.8 Kujenga na kuendeleza bandari kavu katika miji ya Mbeya, Tunduma na Mpika (Zambia). |
| 2. Kupunguza msongamano wa abiria mijini kwa asilimia 40 ifikapo Juni 2031. | **2.1** Kukamilisha ujenzi wa reli za umeme za abiria zinazounganisha vitongoji vikuu na maeneo ya biashara ya kati ya miji (CBDs). |
| | **2.2** Kujenga miundombinu ya Metro na vituo vya kubadilishia usafiri vinavyounganisha commuter rail, SGR, BRT, mabasi na vituo vya mizigo. |
| | **2.3** Kuweka mfumo wa kidijitali wa tiketi na mnyororo wa usafiri unaounganisha reli, BRT, mabasi ya jiji na mizigo. |
| | **2.4** Kuwekeza kwenye mabehewa ya umeme na miundombinu ya nishati iliyo rafiki kwa mazingira. |
| | **2.5** Kufungamanisha reli ya abiria Dar es Salaam kama mradi wa kielelezo ili kupunguza msongamano kwa angalau asilimia 40. |
| | **2.6** Kujenga mifumo ya reli ya abiria katika Mikoa ya Arusha, Mwanza na Dodoma, ikijumuishwa na miundombinu ya usafiri wa ndani. |
| | **2.7** Kuboresha mafunzo na vyuo vya reli kwa wahandisi, waendeshaji, wahudumu na mameneja wa usafirishaji. |
| | **2.8** Kushirikiana na kampuni za kimataifa (CRRC, Alstom, Siemens Mobility) kwa uhaulishaji wa teknolojia. |
| **1.2.4. Usafiri wa Maji** | |
| 1. Kuongeza wigo wa miundombinu ya usafiri wa maji kutoka km 3.2 hadi km 4.36 kwa kila $km^2$ 1,000 ifikapo Juni 2031 | i. Kujenga Bandari ya Kina Kirefu ya Bagamoyo kama lango la kimataifa. |
| | ii. Kukarabati na kuboresha bandari za maziwa (Mwanza, Bukoba, Musoma, Kigoma, Kasanga, Itungi, Liuli, Mbamba Bay). |
| | iii. Kujenga maeneo maalum ya kiuchumi (SEZs) na viwanda vinavyotumia bandari katika Mwanza, Kigoma, Mtwara, Mbeya, Kilwa na Bagamoyo. |
| | iv. Kusimika mifumo ya kidijitali katika shughuli zote za bandari—tiketi, mizigo, forodha na ufuatiliaji wa meli. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | v. Kuhuisha na kuratibu kanuni za uongozaji ili kuhakikisha uwiano wa utoaji wa leseni za vyombo vya usafirishaji, utozaji wa tozo na taratibu za ukaguzi kwa mujibu wa viwango vya EAC, SADC na COMESA. |
| | vi. Kujenga vituo vya kimataifa vya usafirishaji na bandari kavu zilizounganishwa na bandari kuu na maziwa, ili kuboresha muda wa uhamishaji wa mizigo na kuimarisha minyororo ya thamani ya kikanda. |
| | vii. Kusimika mifumo ya tahadhari ya hali ya hewa katika maziwa na na maeneo ya ukanda wa pwani. |
| | viii. Kujenga vituo vya mafunzo ya usafiri wa maji kwa vyeti vya lazima kwa marubani wa baharini, wahandisi, makanika na wafanyikazi wa kizimbani. |
| **1.2.5. Mabomba ya Mafuta na Gesi** | |
| 1. Kuongeza mtandao wa mabomba kutoka km 1,500 hadi angalau km 2,200 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kukamilisha ujenzi na kuanza uendeshaji wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Uganda hadi Bandari ya Tanga, ili kuiweka Tanzania kama njia kuu ya usafirishaji wa mafuta ghafi Afrika Mashariki na kuchochea shughuli za kiuchumi katika ukanda wa mradi. |
| | 1.2 Kuboresha na kuongeza mtandao wa bomba la gesi asilia uliopo kutoka Mtwara na Songo Songo hadi vituo muhimu vya mijini (k.m. Dodoma, Mwanza, Arusha, Mbeya) na mbuga za viwanda na Maeneo ya Maalum ya uwekezaji (SEZ) ili kuwezesha upatikanaji wa gesi kwa gharama nafuu kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, viwanda na usafiri. |
| | 1.3 Kujenga mabomba ya bidhaa mbalimbali kutoka bandari za pwani (Dar es Salaam, Tanga, Mtwara) hadi kwenye bohari za nchi kavu (Dodoma, Mwanza, Kigoma) ili kupunguza utegemezi wa meli za barabarani, kuboresha usalama na kupunguza gharama za usafiri. |
| | 1.4 Kujenga mifumo ya kuweka gesi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha na Morogoro kwa ajili ya gesi ya kupikia majumbani, taasisi za umma na mabasi ya mijini na viwanda nyepesi. |
| | 1.5 Kusimika mabomba ya gesi katika SEZ na IDZ zilizopangwa (k.m. Bagamoyo, Mtwara, Kibaha) ili kuboresha urahisi wa kufanya biashara na kuvutia wawekezaji wa viwanda. |
| | 1.6 Kuanzisha maabara ya kisasa kwa ajili ya kupima vifaa vya bomba, vali na mita za kupimia maji jijini Dar es Salaam au Dodoma ili kuhakikisha udhibiti wa ubora, viwango vya usalama na usaidizi kwa wazalishaji wa ndani. |
| **1.3. Sayansi, Teknolojia na Ubunifu** | |
| Lengo 1. Kuimarishwa kwa uthabiti, ushirikishwaji na uendelevu wa mfumo wa ikolojia wa sayansi, teknolojia na uvumbuzi (STI), unaochochea ukuaji wa uchumi wa muda mrefu na kuimarisha ushindani wa kimataifa. | |
| 1. Tanzania kuwa kinara wa kikanda katika sayansi, teknolojia na uvumbuzi ifikapo Juni 2031 . | 1.1 Kutoa ufadhili endelevu kwa Utafiti na Maendeleo, uvumbuzi na biashara ya teknolojia kila mwaka |
| | i. Kuanzisha mfumo endelevu wa kitaifa wa ufadhili wa magonjwa ya zinaa ili kuendesha utafiti wa muda mrefu wa R&D, uvumbuzi na biashara ya teknolojia. . |
| | ii. Kulinda na kuendeleza uvumbuzi kupitia mfumo imara wa haki miliki (IP). . |
| | iii. Kujumuisha STEM na umahiri wa kidijitali katika ngazi zote za elimu na kuboresha elimu ya ufundi stadi (TVET) pamoja endelevu, ili kujenga nguvu kazi iliyo tayari kwa uvumbuzi. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | iv. Kuwezesha wafanyakazi kupata ujuzi wa juu wa Kidijitali kila mwaka. |
| | v. Kuboresha upatikanaji wa takwimu za utafiti na ushirikiano wa kitaasisi kila mwaka |
| | vi. Kusaidia Utafiti na Maendeleo katika nishati jadidifu, bioteknolojia, kilimo na uendelezaji taka kila mwaka. |
| | vii. Kukuza mifumo ya ubunifu kwa vijana ili kupanua ushirikishwaji na kujenga uwezo wa uvumbuzi wa kuanzia ngazi ya chini kwenda juu kila mwaka. |
| | viii. Kutumia fursa za mitandao ya kimataifa kwa ajili ya ufadhili, uhuhishaji wa teknolojia na utafiti kila mwaka. |
| 2. Michango ya STI kufikia angalau asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo 2031. | i. Kuimarisha kasi ya intaneti nchi nzima ili kusaidia uvumbuzi wa kidijitali na uchumi wa kidijitali. |
| | ii. Kusimamia utekelezaji wa wa teknolojia za Akili Bandia (AI), *Blockchain*, Mtandao wa Vitu (IoT) na Bioteknolojia katika sekta za kilimo, afya, nishati na viwanda. |
| | iii. Kujenga uwezo wa kitaasisi na rasilimali watu katika utafiti wa maeneo ya muhimu (frontier research), hususan katika nishati jadidifu, afya na kilimo. |
| | iv. Kujenga vituo maalumu vya ubunifu na ujasiriamali katika sekta zenye tija kiuchumi. |
| | v. Kukuza teknolojia za ndani ili kuongeza ushindani katika masoko ya kikanda na kimataifa. |
| | vi. Kutumia teknolojia zinazoibukia (AI, roboti na IoT) katika kuimarisha ukuaji wa viwanda, tija na kuongeza thamani ya uzalishaji viwandani kila mwaka |
| | vii.. Kujenga miji ya kisasa na maeneo ya ubunifu (smart cities). |
| | viii. Kutumia *big data* na ML ili kuongeza tija na kuunda fursa mpya za kiuchumi katika sekta za kimkakati kila mwaka. |
| | ix. Kusaidia ubunifu wa *green technology* (na uendelevu ili kuiweka Tanzania kama kinara wa kikanda katika nishati safi, usimamizi wa taka na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. |
| | x. Kujenga minyororo ya ugavi wa ndani inayowezeshwa na teknolojia inayoimarisha uwezo wa uzalishaji wa ndani katika sekta kama vile kilimo, viwanda na nishati kila mwaka. |
| **1.4. Utafiti na Maendeleo (R&D)** | |
| **Lengo la 1:** Mfumo endelevu wa utafiti na maendeleo unaoendeshwa kidijitali (R&D) ulioanzishwa kufikia 2050, unaoendesha ushindani wa kimataifa na kuleta maboresho yanayoweza kupimika katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika sekta muhimu. | |
| 1. Vijana milioni 1 kuwa na ujuzi wa Akili Unde na teknolojia za juu ifikapo 2031 | 1.1 Kuandaa na Kukamilisha Mkakati Wa Taifa Wa Ujuzi Wa Akili Unde (AI). |
| | 1.2 Kuanzisha mpango maalum wa kukuza ujuzi wa baadaye (Tanzania Future Skills Accelerator (TFSA). |
| | 1.3 Kujumuisha masomo ya coding, roboti na umahiri wa kidijitali katika mfumo wa elimu ya msingi. |
| | 1.4 Kusimika na kuendesha maabara za Akili Unde katika shule na vituo vya TVET. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 1.5 Kufanikisha ushirikiano na makampuni ya kimataifa ya Akili Unde kwa ajili ya kutoa mafunzo yenye ithibati na vyeti vya kimataifa. |
| 2. Kuongeza uwekezaji katika utafiti na maendeleo (R&D) kutoka asilimia 0.56 hadi angalau asilimia 0.8 ya Pato la Taifa ifikapo 2031 | **2.1** Kuandaa Mkakati wa Taifa wa R&D chini ya COSTECH. |
| | **2.2** Kutunga Sheria ya Utafiti na Ufadhili wa Ubunifu (Research and Innovation Finance Act) ili kuhakikisha bajeti endelevu za Utafiti na Bunifu. |
| | **2.3** Kuanza Mfuko wa Uhamishaji Teknolojia kwa Makampuni yanayoibukia (startups) na vyuo vikuu. |
| | **2.4** Kuweka vivutio vya kodi (tax incentives) kwa shughuli za R&D ili kuongeza uwekezaji wa sekta binafsi. |
| | **2.5** Kuwezesha angalau asilimia 50 ya SMEs kutumia teknolojia za viwanda 4.0. |
| | **2.6** Kuanzisha kanda nne za teknolojia (tech parks) katika Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya. |
| | **2.7** Kuanzisha maabara za Taifa za AI na Kituo cha Supercomputing. |
| | **2.8** Kuandaa Mwongozo jumuishi wa kitaifa wa miundombinu ya AI na supercomputing. |
| | **2.9** Kuunda mkakati wa taifa wa kufadhili utafiti kwa sekta kipaumbele, ukiwa na dhamana ya serikali. |
| 3. Kuongeza idadi ya vituo vya ubunifu (innovation hubs) kutoka 5 hadi angalau 10 ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kuimarisha Sera ya Taifa ya Ubunifu (National Innovation Policy). |
| | 3.2 Kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Ubunifu (National Innovation Fund – NIF) pamoja na kituo cha Ubunifu wa utoaji wa Mikopo. |
| | 3.3 Kuanzisha Kituo cha Ubunifu wa AI na Quantum Computing jijini Dar es Salaam. |
| | 3.4 Kujenga angalau vituo vitatu vya sayansi na teknolojia katika kanda. |
| | 3.5 Kuweka mfumo rasmi wa maabara za maarifa asilia (Indigenous Knowledge Labs). |
| | 3.6 Kuingiza programu za incubator za ubunifu katika vyuo vikuu vyote nchini. |
| | 3.7 Kuanzisha incubators za R&D katika innovation hubs zote ili kusaidia startups za utafiti. |
| 4. Kuhakikisha asilimia 100 ya tafiti muhimu zinazohusiana na malengo ya kimkakati zinatumika ifikapo Juni 2031. | 4.1 Kuandaa na kuzindua hazina ya kitaifa ya utafiti yenye upatikanaji wazi (national open-access research repository). |
| | 4.2 Kuanzisha jukwaa la pamoja la sera na utafiti kati ya wizara (inter-ministerial policy–research platform). |
| 5. Kuanzisha Mwongozo wa Kitaifa wa Utafiti wa Agenda (NRA) na kuhakikisha mipango ya taasisi zote inalingana nayo ifikapo Juni 2031. | **5.1** Kufufua Mfumo wa Taifa wa Uratibu wa Utafiti pamoja na kanzidata ya watafiti kitaifa. |
| | **5.2** Kuhakikisha wizara zote zinaoanisha mipango yao na NRA. |
| | **5.3** Kutumia mifumo ya AI kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa NRA. |
| | **5.4** Kuanzisha Baraza la Taifa la Utafiti (National Research Council). |
| | **5.5** Kuunganisha taasisi zote za utafiti kwenye jukwaa la kidijitali la NRA. |
| | **5.6** Kuandaa mkakati wa kufadhili NRA. |
| 6. Kuanzisha mifumo ya AI kwa utabiri wa hali ya hewa | 6.1 Kuunda Mfuko wa Taifa wa Utafiti wa Bioteknolojia. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| na Utafiti na Maendeleo (R&D) ya kilimo ifikapo 2031 | 6.2 Kuanzisha mfumo wa Taifa wa utabiri wa hali ya hewa unaotumia Akili Unde. |
| | 6.3 Kuboresha taasisi ya TARI kuwa Taasisi ya *Smart Agriculture Research*. |
| | 6.4 Kujumuisha teknolojia mpya na za kidijitali katika Sera ya Taifa ya Kilimo. |
| 7. Kuongeza ushirikiano wa kimataifa katika utafiti kwa asilimia 50 ifikapo 2031. | **7.1** Kuandaa mfumo wa ushirikiano wa kimataifa wa utafiti (International Research Cooperation Framework). |
| | **7.2** Kuanzisha *Global Research Mobility Fund*. |
| | **7.3** Kutengeneza mfumo wa kudumu wa ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali katika utafiti wa kimataifa. |
| 8. Kuanzisha National Open Data Repository (NODAR) na Mfumo wa Maadili ya Data ifikapo 2031. | 8.1 Kuanzisha Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Data (National Data Governance Board). |
| | 8.2 Kuunda Hazina ya Taifa ya Takwimu Huria (NODAR). |
| | 8. Kutekeleza mfumo wa maadili ya Akili Unde na ulinzi wa taarifa (AI Ethics and Data Protection Framework). |
| **1.5.Mfumo Ikolojia Unaotegemea Takwimu** | |
| **Lengo 3:** Mfumo ikolojia imara unaotegemea takwimu, wenye mifumo jumuishi ya takwimu bora, uliowekwa ili kuimarisha utoaji wa maamuzi sahihi, ubunifu wa kidigitali na maendeleo ya kijamii na kiuchumi jumuishi ifikapo 2050. | |
| 1. Uoanishaji kamili (asilimia 100) wa mifumo ya takwimu ya ufuatiliaji na tathmini wa Dira 2050 na LTPP 2050 umefikiwa ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuandaa na kupitisha mpango kazi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Takwimu inayooanisha matokeo ya takwimu na malengo ya Dira 2050, ikijumuisha ratiba ya utekelezaji na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini, ifikapo. |
| | 1.2 Kufanya mapitio ya sheria ya Takwimu ili kuingiza mahitaji mapya ya takwimu pamoja na maboresho ya muundo wa usimamizi wa takwimu. |
| | 1.3 Kushirikiana na Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali (MDAs) kuhakikisha kuwa Sekta za Umma na Binafsi zinajumuisha viashiria vinavyoendana na Dira 2050 katika mifumo yao ya utoaji taarifa kwa kuzijengea uwezo na kuzipa msaada wa kitaalamu. |
| | 1.4 Kuhakikisha ulinganifu na muunganiko wa mifumo yote mikuu ya takwimu ndani ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu ili kuwezesha upatikanaji wa takwimu kwa wakati halisi, uchambuzi na maamuzi ya kisera. |
| | 1.5 Kujumuisha makundi muhimu ya takwimu kama vile picha za setelaiti, takwimu za simu za mkononi, taarifa za mitandao ya kijamii, taarifa za tovuti, taarifa za sensa na *big data* katika mifumo ya takwimu ya taifa. |
| | 1.6 Kuboresha na kudumisha mifumo ya wazi ya takwimu na dashibodi shirikishi za umma zinazoonyesha angalau sekta kuu mbili za maendeleo ili kuongeza uwazi na matumizi ya takwimu katika maamuzi. |
| | 1.7 Kuweka mfumo wa kuchapisha viashiria muhimu vya uchumi na kijamii kwa kila robo mwaka ili kuboresha masuala ya mipango na kisera. |
| 2. Ongezeko la bajeti ya Maendeleo ya Takwimu za Kitaifa kufikia kiwango cha angalau asilimia 0.4 ya Pato la Taifa (GDP) ifikapo 2031 | 2.1 Kuanzisha mifumo mitatu ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya kuwekeza kwenye teknolojia za kisasa za ukusanyaji wa takwimu na mifumo ya uchambuzi wa takwimu (ugharamiaji bunifu + teknolojia). |
| | 2.2 Kuweka katika muundo wa kidigitali na kuunganisha mifumo ya usimamizi ya takwimu katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha ulinganifu na utoaji |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | taarifa kwa wakati. |
| | 2.3 Kuongeza bidhaa za takwimu rasmi na kuanzisha bidhaa mpya za takwimu zenye kipaumbele kwa kutumia zana za kidigitali na mbinu bora zilizoboreshwa. |
| | 2.4 Kuhakikisha takribani asilimia 70 ya wataalamu wa takwimu wanapata mafunzo katika matumizi ya *big data, AI* na teknolojia zinazoibukia. |
| 3. Mfumo wa Taifa wa Takwimu ubadilishwe kuwa wa kidigitali kwa angalau asilimia 80 ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kuanzisha miundombinu jumuishi ya kitaifa ya takwimu (uhifadhi wa takwimu kwenye *cloud*, dashibodi za wakati halisi). |
| | 3.2 Kuhamisha asilimia 100 ya ukusanyaji wa takwimu kwenda kwenye mifumo ya kidigitali (CAPI, simu). |
| | 3.3 Kuanzisha programu za utafiti wa *AI* na sayansi ya takwimu katika vyuo vikuu nchini. |
| | 3.4 Kuandaa na kuzindua Mtaala wa Kitaifa wa Mafunzo ya Takwimu unaolenga sayansi ya takwimu, *big data, AI* na utumiaji wa mifumo inayojiendesha na kujisimamia. |
| | 3.5 Kuweka utaratibu wa matumizi ya *AI* na maamuzi yanayotokana na uchambuzi wa takwimu Serikalini, ikiwa ni pamoja na kuanzisha vitengo maalumu vya uchambuzi wa takwimu. |
| 4. Kupunguza muda wa kuchakata data kwa asilimia 50 ifikapo Juni 2031 | 4.1 Kuongeza matumizi ya teknolojia za ukusanyaji takwimu kwa simu *(mobile data collection)* na *remote sensing* katika maeneo lengwa ya takwimu kwa asilimia 100. |
| | 4.2 Kuanzisha vitengo vya *AI* na uhandisi wa takwimu katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara mbalimbali. |
| | 4.3 Kuweka mifumo ya ushirikishaji na uchakataji wa data inayoendeshwa na *AI*. |
| | 4.4 Kuanzisha dashibodi za wakati halisi katika wizara za kisekta. |
| | 4.5 Kutekeleza *machine learning algorithim* katika vitengo muhimu vya takwimu serikalini ili kuharakisha uhakiki, uchambuzi wa takwimu, na maoteo mbalimbali ya takwimu. |
| | 4.6 Kuanzisha kituo cha Taifa cha Utafiti wa *AI* kwa ajili ya Takwimu na matumizi ya *blockchain* katika usalama wa takwimu. |
| 5. Mfumo wa kidigitali wa taarifa za kiintelijensia wa idadi ya watu na makazi (digital population & housing intelligence) unaofanya kazi kwa wakati halisi umeanzishwa umeanzishwa ifikapo Juni 2031 | 5.1 Kuanzisha mfumo jumuishi wa kitaifa wa usajili wa matukio muhimu ya kiraia unaounganisha taarifa za kuzaliwa, vifo, ndoa, uhamaji na kitambulisho cha taifa katika wizara na Taasisi zote. |
| | 5.2 Kuweka mifumo ya kisheria na utawala wa takwimu kwa ajili ya mifumo ya kidijitali ya idadi ya watu imetungwa na kutekelezwa ili kuhakikisha faragha ya takwimu, usalama, ulinganifu wa mifumo na uwajibikaji wa taasisi. |
| | 5.3 Kufanya Sensa za Watu na Makazi kwa kutumia njia za kidigitali kwa kutumia *tablet, GPS* na dashibodi za wakati halisi. |
| | 5.4 Kuweka mfumo wa kufuatilia kwa wakati halisi maendeleo ya sensa, ubora wa takwimu na uendeshaji wa kazi katika mikoa yote, kwa kutumia dashibodi za moja kwa moja zinazoweza kufikiwa na timu za uratibu za ngazi ya kitaifa na kikanda. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 5.5 Kuanzisha Rejesta Jumuishi ya Watu na Makazi kwa kuunganisha CRVS, NIDA na mifumo ya kiutawala. |
| | 5.6 Kuanzisha jukwaa la kitaifa la ushirikishaji wa takwimu za watu kwa wakati halisi likiunganisha CRVS, sensa za kidigitali, mifumo ya kijiografia (GIS) na data za kiutawala. |
| | 5.7 Kuweka mfumo wa kitaifa wa ufuatiliaji wa kidemografia kwa wakati halisi unaojengwa kupitia majukwaa yanayojiendesha yenyewe na ulinganifu wa mifumo kutoka sekta muhimu kama afya, elimu na uhamiaji. |
| | 5.8 Kutumia zana za kijiografia na *AI* kufuatilia mienendo ya idadi ya watu kwa kutumia *satellite imagery, mobility data* na *remote sensing*. |
| | 5.9 Kuanzisha dashibodi salama na jumuishi ya taarifa za watu kwa wakati halisi inayopatikana kwa watumiaji waliothibitishwa kwa ajili ya upangaji, ufuatiliaji na kukabiliana na dharura. |
| **1.6. Mageuzi ya Kidigitali** | |
| **Lengo 1:** Jamii jumuishi iliyounganishwa na yenye ujuzi wa kidijgtali, inayowezeshwa na miundombinu salama itakayosaidia ubunifu, utoaji huduma na mageuzi ya kijamii na kiuchumi katika mikoa yote nchini. | |
| 1. Kufikia angalau asilimia 80 ya uunganishwaji wa kidijitali nchini ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuandaa na kuendesha vituo vya maarifa ya kidigitali katika kila mkoa ili kuongeza uwezo wa kidigitali, ujuzi na ubunifu kwa vijana, wanawake na makundi maalumu. |
| | 1.2 Kutekeleza mkakati wa uratibu wa uwekaji wa miundombinu ya TEHAMA kwa Serikali na Sekta Binafsi ili kuongeza ufanisi katika miundombinu ya *fiber optic* na kuharakisha uunganishwaji wa *broadband* nchi nzima. |
| | 1.3 Kuanzisha jukwaa salama na jumuishi la kubadilishana takwimu na taarifa kati ya sekta ya umma na binafsi. |
| | 1.4 Kutoa msaada wa kifedha na kitaalamu kwa biashara ndogo ndogo, na za kati (MSMEs) ili kuziwezesha kutumia teknolojia za kidigitali, majukwaa ya kidijitali na biashara mtandaoni (e-commerce) kwa lengo la kuongeza tija na kukuza ujumuishaji wa kiuchumi. |
| | 1.5 Kusimamia na kuamuru uanzishaji na utekelezaji wa huduma za kidigitali zinazoweza kufikiwa na kutumika na watu wenye ulemavu ili kuhakikisha usawa wa upatikanaji wa huduma hizi kwa makundi yote ya kijamii ifikapo. |
| | 1.6 Kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kidigitali vya bei nafuu, vilivyotengenezwa ndani au kuingizwa kutoka nje kwa makundi yote ya jamii. |
| **Lengo 2**: Kuimarishwa kwa miundombinu ya kitaifa ya usalama wa mtandao na utawala na matumizi ya kimkakati ya teknolojia zinazoibukia, hivyo kulinda mageuzi ya kidigitali ya Tanzania na kuiweka nchi katika nafasi ya ushindani wa kimataifa. | |
| 1. Upatikanaji matumizi ya teknolojia zinazoibukia kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha vituo maalumu vya utafiti, ubunifu na mafunzo katika *AI, robotics, IoT, blockchain* na teknolojia zingine zinazoibukia. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 1.2 Kuendeleza uwezo wa ndani katika teknolojia za setelaiti, uchunguzi wa anga na matumizi ya takwimu kwa kushirikiana na taasisi za anga za kimataifa. |
| | 1.3 Kukuza matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, vituo vya takwimu vinavyotumia nishati kidogo na mifumo ya kompyuta yenye ufanisi. |
| 2. Kupunguza mashambulizi ya kimtandao kwa asilimia 80 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuanzisha kituo cha kitaifa cha SOC chenye vifaa kamili kwa ajili ya kufuatilia, kugundua na kukabiliana na mashambulizi mtandaoni kwa wakati. |
| | 2.2 Kuanzisha Timu ya Kitaifa ya kukabiliana na matukio ya ulinzi mtandaoni (*Computer Security Incident Response Team (CSIRT))* na Baraza la Utawala wa *Cybersecurity* kwa ajili ya uratibu wa jitihada za kuhakikisha usalama wa mtandao katika sekta binafsi na umma. |
| | 2.3 Kuendesha mazoezi ya kitaifa ya uthibiti wa matukio ya usalama mtandao mara kwa mara. |
| | 2.4 Kuhakikisha taarifa zote za Serikali na sekta muhimu zinahifadhiwa ndani ya mipaka ya nchi chini ya mifumo salama ya *cloud*, ili kuimarisha uhuru wa takwimu, faragha na usalama wa taarifa. |
| **Lengo 3:** Mfumo thabiti, jumuishi na wenye rasilimali za kutosha wa ubunifu na *startups* unaochochea ujasiriamali, utafiti na maendeleo (R&D) na masuluhisho ya kiteknolojia | |
| 1. Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 10 bora Afrika katika kielelezo cha ubunifu (*Global Innovation Index)* ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha utaratibu maalumu kupitia utoaji wa ruzuku, mitaji na usaidizi wa ubia wa kugharamia ubunifu wa kidigitali, utafiti na maendeleo na miradi ya kiteknolojia. |
| | 1.2 Kuanzisha jukwaa la kusaidia biashara za ndani kupata masoko, uwekezaji na kulinda ubunifu ili kuendeleza ukuaji wa uchumi na ujasiriamali. |
| | 1.3 Kuanzisha ushirikiano kati ya vyuo, vituo vya utafiti na sekta binafsi ili kuimarisha utafiti, maendeleo ya ujuzi na uhamishaji wa teknolojia. |
| | 1.4 Kuanzisha mtandao ulioratibiwa wa vituo vya uanzishaji *(incubators)* na vichocheo vya ukuaji *(accelerators)* ili kukuza kampuni changa (*startups)*, kuongeza ukubwa wa biashara za kidigitali zenye uwezekano mkubwa wa ukuaji, na kuwezesha kuingia katika masoko ya ndani na ya kimataifa. |
| **Lengo 4:** Kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa usimamizi wa mageuzi ya kidigitali nchini katika sekta zote. | |
| 1. Kufikia angalau asilimia 80 ya kufungamanisha mifumo ya kidigitali ya sekta ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha taasisi kwa ajili ya kujenga uwezo wa uongozi, uwezo wa kitaalamu na usimamizi wa mageuzi ya kidigitali katika sekta zote, ili kuhakikisha utekelezaji wenye ufanisi na usimamizi madhubuti |
| | 1.2 Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa viwango vya ulinganifu, usalama, faragha na ubora kwa mifumo yote ya kidigitali ya umma na binafsi, ili kuwezesha utoaji wa huduma jumuishi |
| | 1.3 Kujumuisha na kuboresha mifumo ya udhibiti ili kuwezesha biashara ya kidigitali, ulinzi wa taarifa, usalama mtandao na ubunifu. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 1.4 Kuandaa jukwaa jumuishi la serikali kwa ajili ya kuunganisha mifumo ya sekta mbalimbali, kuwezesha utoaji huduma bila usumbufu na kufuatilia maendeleo ya mabadiliko ya kidigitali. |
| **1.7. Miundombinu ya TEHAMA** | |
| **Lengo 1.** Miundombinu dhabiti na jumuishi ya TEHAMA inayohakikisha uunganisho wa kidigitali nchini, kuimarisha ujuzi wa kidigitali kwa makundi yote ya watu na kuwezesha matumizi ya teknolojia zinazoibukia ili kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. | |
| 1. Kuongeza matumizi ya *broadband* kufikia angalau asilimia 80 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano na wasimamizi ili kuhakikisha upatikanaji wa mtandao wa 5G katika miji yote, ili kuwezesha upatikanaji wa huduma ya intaneti ya kasi na ya kuaminika kwa biashara, elimu na huduma za serikali. |
| | 1.2 Kuanzisha maeneo yatakayotoa huduma ya itanenti (Wi-Fi ) ya bure au ya gharama nafuu katika taasisi za umma, maeneo ya wazi na vituo vya jamii ili kuongeza upatikanaji wa huduma za intaneti kwa wananchi, wakiwemo walio katika mazingira magumu. |
| | 1.3 Kutekeleza mifumo ya udhibiti inayochochea uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo yasiyohudumiwa vizuri ili kuhakikisha upatikanaji wa usawa wa huduma za kidigitali katika maeneo ya vijijini. |
| | 1.4 Kuandaa miradi maalumu ya miundombinu kwa kutumia *fiber, wireless* na teknolojia za setelaiti ili kuunganisha jamii za vijijini na maeneo ambayo ni vigumu kufikiwa. |
| | 1.5 Kushirikiana na waendeshaji wa setelaiti kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za kidigitali nchini, hususani katika maeneo ambayo miundombinu ya ardhini haiwezekani ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kidigitali. |
| 2. Uelewa wa kidigitali *(Digital Literacy)* kuongezeka kutoka asilimia 30 hadi angalau asilimia 60 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kuanzisha Taasisi ya Kitaifa ya Mafunzo ya Kidigitali (DTI). |
| | 2.2 Kutoa mafunzo kwa walimu 30,000 juu ya teknolojia zinazoibukia. |
| | 2.3 Kuandaa mifumo ya elimu ya kisasa inayoendeshwa na AI, ikijumuisha majukwaa ya *e-learning* yanayotumia AI. |
| | 2.4 Kujumuisha AI, *blockchain* na usalama mtandao (cybersecurity) katika mitaala ya elimu. |
| | 2.5 Kujumuisha uelewa wa kidigitali katika mtaala wa kitaifa katika ngazi zote, kuhakikisha angalau asilimia 60 ya wanafunzi wanapata ujuzi wa msingi wa TEHAMA. |
| | 2.6 Kutekeleza programu za kitaifa za mafunzo ya ujuzi wa kidigitali katika jamii zinazolenga makundi yaliyo maalum ili kufikia watu angalau milioni 20. |
| | 2.7 Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa uthibitishaji wa ujuzi wa kidigitali na kuhakikisha angalau asilimia 50 ya nguvu kazi inapata cheti/uthibitisho wa kiwango cha awali. |
| 2. Mifumo ya Usalama Mtandao na Ulinzi wa Takwimu kutekelezwa kwa asilimia 100 kila mwaka | 3.1 Kuimarisha mfumo wa kisheria wa Taifa wa Usalama Mtandao na Ulinzi wa Taarifa. |
| | 3.2 Kuhakikisha uimara wa mifumo ya usalama mtandao kwa kufanya tathmini za mara kwa mara za usalama mtandao, majaribio *(penetration testing)* na ukaguzi kila mwaka. |
| | 3.3 Kuanzisha Kituo cha Kitaifa cha Usalama Mtandao (*National Cybersecurity Operations Centre)*. |
| | 3.4 Kutoa mafunzo ya usalama mtandao kwa wataalamu wote wa TEHAMA katika sekta muhimu. |
| 4. Kupanda kutoka kiwango cha chini hadi cha kati cha *AI Adoption Index* ifikapo Juni | 4.1 Kuandaa sera, mfumo wa kisheria na kanuni za Akili mnemba (AI). |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 2031 | 4.2 Kufanya mapitio ya kila mwaka juu ya utekelezaji wa mfumo wa udhibiti wa AI. |
| **1.8. Huduma za Mawasiliano na Usafirishaji wa Vifurushi (Courier Services)** | |
| **Lengo 1.** Kuboresha upatikanaji wa huduma za mawasiliano zenye kuaminika, nafuu na za kasi ya juu, mijini na vijijini, ili kuwezesha ushiriki jumuishi wa kidigitali, ukuaji wa uchumi na ubora wa maisha kwa wananchi wote ifikapo 2050 | |
| 1. Upatikanaji wa huduma za posta kwa wote, muunganisho wa kidigitali na huduma salama za biashara mtandaoni *(e-commerce)* umefikiwa ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kukuza na kuwezesha matumizi ya intaneti inayotumia setelaiti katika maeneo ambayo mitandao ya ardhini haiwezekani kutekelezwa. |
| | 1.2 Kuboresha upatikanaji wa huduma za posta za kisasa na huduma za kusafirisha vifurushi (courier) zinazojumuishwa na mifumo ya fedha ya kidigitali katika maeneo ya mbali ili kuhakikisha upatikanaji wake nchi nzimaa. |
| | 1.3 Kuandaa na kutekeleza mfumo jumuishi (harmonized framework) wa huduma za posta na usafirishaji vifurushi vinavyovuka mipaka. |
| | 1.4 Kuboresha mfumo wa kitaifa wa anwani za makazi, unaounganishwa na majukwaa ya Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS), ili kusaidia utoaji bora na wenye ufanisi wa huduma za usafirishaji hatua ya mwisho (last mile) wa barua na mizigo midogo. |
| | 1.5 Kuiweka Tanzania katika nafasi ya kuwa kitovu cha biashara mtandaoni *(e-commerce)* katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini kwa kutumia miundombinu ya Posta, majukwaa ya kidigitali na huduma za usafirishaji bidhaa mipakani. |
| 2. Kuongeza kiwango cha ushindani wa huduma za kidijitali *(Digital Services Competitiveness Index)* hadi angalau asilimia 50 ifikapo Juni 2031 | 2.1 Kufanya tathmini za mara kwa mara za utoaji wa huduma za kidigitali na miundombinu, na kutumia ubunifu na mbinu bora ili kuhakikisha maboresho endelevu na ushindani. |
| | 2.2 Kuhuisha na kutekeleza mifumo ya kisheria kwa ajili ya kulinda watumiaji wa huduma za kidigitali ili kuhakikisha uaminifu, uwazi na uwajibikaji katika biashara mtandaoni *(e-commerce)*, posta na usafirishaji wa vifurushi. |
| 3.Kuimarishwa kwa usalama wa mtandao na uaminifu wa umma, kwa utekelezaji wa asilimia 100 wa mifumo ya kitaifa ya usalama mtandaoni ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kutoa elimu kwa wananchi, biashara na taasisi za umma kuhusu matumizi salama ya teknolojia za kidigitali, *cyber hygiene* na vitisho vipya vya kimtandao ili kujenga uaminifu katika huduma za kidijitali. |
| | 3.2 Kuwezesha shughuli za kitafiti zinazilenga uibuaji wa teknolojia mpya, zana na suluhisho za kukabiliana na vitisho vya kidigitali, ili kuimarisha ustahimilivu katika mitandao ya mawasiliano. |
| | 3.3 Kuhamasisha ushirikiano kati ya taasisi za kiserikali, kampuni za teknolojia, na wataalamu wa usalama mtandao ili kuendeleza ubunifu, kushirikishana mbinu bora, na kuimarisha uwezo wa taifa wa kujilinda kimtandao. |
| **1.9. Mazingira ya Biashara** | |
| **Lengo 1.** Kuimarisha uhamasishaji wa uwekezaji kupitia uanzishwaji wa mazingira ya ushindani, uwazi, ufanisi na mfumo wa taasisi, unaolingana na kufanikisha hadhi ya nchi yenye uchumi wa kipato cha kati cha juu kufikia mwaka 2050. | |
| 1. Kutoa huduma za serikali kwa njia ya kidigitali kwa angalau asilimia 50 kufikia Juni 2031. | 1.1 Kuandaa mfumo wa sera ya Serikali Mtandao *(e-Government).* |
| | 1.2 Kutekeleza mfumo wa Kitaifa wa utambuzi wakidigitali *(Digital ID).* |
| | 1.3 Kuunda mfumo wa ufuatiliaji wa uzingatiaji wa kodi unaoutumia akili mnembe (AI). |
| 2. Kufungamanisha huduma wezeshi za biashara | 2.1 Kuandaa kanuni fungamanishi za biashara ya kidigitali. |

| Shabaha | Afua |
| --- | --- |
| zitakazowezesha takribani asilimia 50 ya miamala ya biashara kufanyika kidijitali na kuwezesha upatikanaji wa kidijitali kwa wajasiriamali wadogo na kampuni zinazoibukia kufikia Juni 2031. | 2.2 Kuboresha upatikanaji na uwezo wa kidigitali kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na biashara chipukizi kupitia vifaa, mafunzo na majukwaa maalumu ili kuwawezesha kushiriki katika biashara za mtandaoni *(online trade).* |
| | 2.3 Kuhamasisha matumizi ya mifumo salama ya malipo na miamala ya kidigitali katika ikolojia ya biashara ili kuhakikisha kuwa angalau asilimia 60 ya biashara za wajasiriamali wadogo na wakati zinafanyika kwa njia ya kidijitali. |
| 3. Kuongeza mchango wa uwekezaji kutoka nje katika Pato la Taifa kufikia takribani asilimia 10 kila mwaka ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kukamilisha mageuzi ya sera ya uwekezaji. |
| | 3.2 Kuanzisha vituo vya uwekezaji katika mikoa yote nchini. |
| | 3.3 Kuimarisha udhamini wa uwekezaji (Investment Ombudsman). |
| | 3.4 Kuimarisha jukwaa la kidigitali la usajili wa uwekezaji. |
| | 3.5 Kuhamasisha utoaji wa vivutio za uwekezaji katika teknolojia ya hali ya juu. |
| | 3.6 Kuandaa miongozo ya uwekezaji kwa sekta za teknolojia ya hali ya juu. |
| 4. Kuwezesha uwekezaji wa angalau asilimia 5 mpya katika teknolojia ya hali ya juu kwa kufikia Juni 2031. | 4.1 Kuanzisha angalau kanda maalumu tatu za akili mnemba na ubunifu wa kidigitali. |
| | 4.2 Kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Teknolojia ya Hali ya Juu wenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 1. |
| 5. Kuwezesha angalau asilimia 15 ya nguvu kazi kuwa na ujuzi wa kisasa na wa kitaalamu kufikia Juni 2031. | 5.1 Kuandaa programu ya kitaifa ya kujenga ujuzi katika uwekezaji. |
| | 5.2 Kuongeza wigo wa ushirikiano katika mafunzo ya ufundi. |
| 6. Kuongeza miradi ya maendeleo ya miundombinu kupitia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kufikia takribani asilimia 20 ifikapo Juni 2031. | 6.1 Kuwezesha angalau miradi mitano ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuimarisha maendeleo ya miundombinu. |
| 7. Kuwezesha uwekezaji katika teknolojia wenye thamani ya takribani Dola za Marekani Bilioni 2 kufikia Juni 2031. | 7.1 Kuongeza wigo wa vivutio kwa ajili ya sekta za viwanda vya kisasa *(futuristic industries)* ili kufikia jumla ya uwekezaji wa teknolojia wa USD 2B. |
| **Lengo 2:** Kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuiweka Tanzania katika nafasi ya tatu bora miongoni mwa nchi zenye uchumi rafiki wa biashara barani Afrika, kwa lengo la kuongeza kiasi ya uwekezaji na kuharakisha urasimishaji wa biashara katika sekta zote kufikia mwaka 2050. | |
| 1. Tanzania kushika nafasi ya tatu kati ya vituo vinavyovutia zaidi kwa biashara na uwekezaji barani Afrika kufikia Juni 2031. | 1.1 Kutenganisha malengo ya ukusanyaji mapato na majukumu ya udhibiti ili kuhakikisha tozo zinagharamia gharama za utoaji huduma. |
| | 1.2 Kuboresha taasisi za udhibiti ili kuharakisha ukuaji wa biashara na uwekezaji. |
| | 1.3 Kuunganisha kanuni zinazofanana na kuondoa maeneo yanayojirudia ili kupunguza gharama za miamala. |
| | 1.4 Kufanya tathmini ya athari za udhibiti *(Regulatory Impact Assessments – RIAs)* kwa kanuni zote na sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa *(LGA by-laws)* zinazoweza kuathiri biashara. |
| | 1.5 Kuimarisha imani ya wawekezaji kupitia sera za kukabiliana na vihatarishi, dhamana za mapato, na mifumo ya haraka ya utatuzi wa migogoro. |
| 2. Urasimishaji wa biashara | 2.1 Kuanzisha wakala maalum wa kukuza uwekezaji na kampuni za zinazoibukia *(Investment and Startup Promotion Agency – ISPA).* |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| kwa asilimia 80 na kuweka mfumo wa kidigitali wa taratibu za biashara kufikia Juni 2031. | 2.2 Kuwezesha ushiriki wa kampuni zinazoibukia na wafanyabiashara wadogo wadogo wasio rasmi katika ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPPs). |
| | 2.3 Kukuza fursa za soko la Tanzania ndani ya maeneo ya AfCFTA na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). |
| **1. MISINGI** | |
| **3.1. Utawala Bora, Demokrasia, Usalama na Utulivu** | |
| **Lengo 1:** Kuimarishwa kwa uwazi, uwajibikaji, maadili na demokrasia, amani na utulivu kwa ajili ya ushiriki wa ufanisi na usawa wa wanajamii wote katika maendeleo ya taifa. | |
| 1. Kiwango cha Fahirisi ya Ushiriki wa Wananchi na Uwajibikaji *(Voice and Accountability Index)* kimeboreshwa na kufikia - 0.45 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuandaa, kuidhinisha na kutangaza katiba mpya inayojumuisha, kanuni za kijamii na kiuchumi, demokrasia, usimamizi wa rasilimali asili, utawala wa sheria, haki za binadamu na utawala jumuishi. |
| | *i. Kufanya mapitio ya kina ya mifumo ya kikatiba na ya kisheria iliyopo.* |
| | *ii. Kuandaa Rasimu ya Katiba Mpya na kuratibu uthibitishaji, na uidhinishaji.* |
| | *iii. Kufanya marekebisho ya sheria na sera zilizopo ili ziendane na katiba mpya.* |
| | *iv. Kuandaa muundo wa ufuatiliaji na tathmini ya mageuzi ya sheria na utawala baada ya utekelezaji.* |
| | 1.2 Kufanya mageuzi ya mpangilio wa taasisi ili kuhakikisha utawala bora wa rasilimali za taifa na usimamizi endelevu wa mipango ya kijamii na kiuchumi ya muda mrefu. |
| | *i. Kufanyia mageuzi ya mifumo ya taasisi iliyopo ili kuhakikisha kwamba serikali inasimamia rasilimali na uhuru katika usimamizi na maamuzi ya rasilimali za Taifa kwa uhuru bila kuathiri maslahi ya Taifa.* |
| | *ii. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa ushirikishwaji wa kijamii (societal corporatist framework) kwa ajili ya utawala wa rasilimali za taifa.* |
| | *iii. Kuimarisha au kuanzisha taasisi huru ili kuhakikisha manufaa yatokanayo na kupunguza gharama na kuongeza uzalishaji kutokana na rasilimali za taifa zinagawanywa kwa umma kwa usawa kwa lengo la kupunguza ukosefu wa usawa.* |
| | *iv. Kufanya mapitio na mageuzi ya kimuundo ya taasisi muhimu za umma, hususan mashirika na taasisi za udhibiti, ili kuondoa muingiliano wa majukumu, na kuongeza ufanisi.* |
| | 1.3 Kuimarisha mfumo wa kisheria na wa taasisi kwa ajili ya usimamizi wa uchaguzi katika ngazi za kitaifa na za chini za kiutawala. |
| | *i. Kufanya mapitio na kutekeleza mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya usimamizi bora wa uchaguzi katika ngazi za kitaifa na za chini za kiutawala.* |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | *ii. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa uchaguzi kwa ajili ya michakato ya uchaguzi.* |
| | 1.4 Kuhakikisha taasisi huru za uchaguzi zenye majukumu ya kisheria, miundo ya utawala na mifumo ya uwajibikaji. |
| | *i. Kufanya mapitio ya majukumu yaliyopo ya kisheria na miundo ya taasisi za uchaguzi.* |
| | *ii. Kuandaa majukumu ya kisheria, miundo ya utawala na mifumo ya uwajibikaji ya taasisi za uchaguzi.* |
| | 1.5 Kuimarisha mifumo ya haki za uchaguzi ili kuhakikisha utatuzi wa migogoro ya uchaguzi kwa wakati na kwa usawa katika ngazi zote. |
| | *i. Kufanya mapitio na marekebisho ya sheria na kanuni zilizopo za uchaguzi na vyama vya siasa.* |
| | *ii. Kuanzisha mfumo huru wa utatuzi wa migogoro ya uchaguzi na miongozo yake.* |
| | 1.6 Kuandaa na kutekeleza viwango vya uwazi na uadilifu wa uchaguzi ikiwemo rejista za wapiga kura za kidijitali, mifumo ya utoaji matokeo na takwimu za wazi. |
| | i. *Kuandaa miongozo ya viwango vya uwazi na uadilifu.* |
| | ii. *Kubuni, kuandaa na kuweka mfumo wa kidigitali wa kupiga kura, utolewaji wa matokeo na takwimu kwa uwazi.* |
| | iii. *Kutafsiri sheria zote kwa Kiswahili kwa kutumia lugha rafiki kwa raia ili kuongeza uelewa wa umma na kuboresha upatikanaji wa haki.* |
| | 1.7 Kuandaa mikakati ya kuoanisha sheria za kimila na sheria za nchi kuhusu usawa wa kijinsia na haki za binadamu. |
| | i. *Kufanya mapitio ya sheria za kimila ili kubaini maeneo yenye migongano na sheria za nchi.* |
| | ii. *Kuandaa na kutekeleza mikakati ya usawa wa kijinsia na haki za binadamu.* |
| | 1.8 Kukuza ushiriki jumuishi katika uchaguzi unaozingatia jinsia, vijana, na watu wenye ulemavu katika sera na taratibu za uchaguzi. |
| | i. *Kufungamanisha na kuratibu sera za taasisi.* |
| | ii. *Kuandaa miundombinu, zana na majukwaa ya kusaidia ushiriki wa watu wenye mahitaji maalum katika uchaguzi.* |
| | 1.9 Kuandaa na kutekeleza mpango wa kitaifa wa muda mrefu wa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na jamii zenye kipato cha chini, kwa kushirikiana na asasi za kiraia na sekta binafsi. |
| | *i. Kufanya mapitio na kuandaa mpango wa kitaifa wa muda mrefu, jumuishi na wenye uwazi wa utoaji wa huduma za misaada ya kisheria.* |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | *ii. Kuandaa na kutekeleza mfumo wa utoaji elimu ya uraia, utetezi, ufuatiliaji, tathmini na kujifunza.* |
| 2. Kuimarisha fahirisi ya kiashiria cha Rushwa (Corruption Perception Index) kutoka 41/100 (2024) hadi 55/100 kufikia Juni 2031 | 2.1 Kutoa huduma za mahakama na kiutawala kidigitali ili kukuza uwazi katika maamuzi. |
| | 2.2 Kutekeleza mfumo wa mikataba ya wazi *(open contracting)* na ununuzi wa umma kwa njia ya kielektroniki *(e-procurement).* |
| | 2.3 Kuimarisha mifumo ya mrejesho kwa wa raiai na utatuzi wa malalamiko kila mwaka |
| 3. Kuimarisha fahirisi ya kiwango cha utulivu wa kisiasa, amani na usalama kufikia +0.10 ifikapo Juni 2031 | 3.1 Kufunga mifumo ya ulinzi na usalama kwa kutumia teknolojia za kisasa. |
| | 3.2 Kuimarisha mifumo ya amani na upatanisho katika ngazi ya jamii ili kusuluhisha migogoro (kama vile ardhi, siasa, mvutano wa kikabila), kuzuia ghasia na kukuza ustahimilivu. |
| | 3.3 Kufanya maboresho ya kimuundo ya Jeshi la Polisi Tanzania na kulibadili kuwa Huduma ya Polisi ya Taifa. |
| **Lengo 2:** Kuimarishwa kwa utolewaji wa huduma za umma kwa kuboresha mfumo wa utoaji mrejesho, uwajibikaji, uwazi, na maadili ya kiutawala ili kuongeza ufanisi. | |
| 1. Kuboresha fahirisi ya kiwango cha ufanisi wa Serikali kufikia -0.30 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kurekebisha muundo wa Wizara na Taasisi za Serikali kuwa chache zenye wigo mpana wa majukumu kwa ufanisi na urahisi. |
| | *i. Kufanya mapitio ya kina ya majukumu na muundo wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.* |
| | *ii. Kufanya ukaguzi wa viwango vya uwezo kwa watumishi ili kuongeza ufanisi wa ajira, kuhakikisha yanakidhi majukumu na miundo ya wizara na taasisi iliyofanyiwa maboresho pamoja na mahitaji ya mabadiliko ya kidijitali katika utoaji wa huduma.* |
| | 1.2 Kuweka mfumo jumuishi wa Uchumi wa kidigitali kufikia. |
| | *i. Kubuni na kuendeleza mfumo mmoja wa usanifu.* |
| | *ii. Kuunda mfumo wa kidigitali utakaounganisha takwimu zinazozalishwa na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. .* |
| | 1.3 Kuimarisha uwezo wa kitaaluma, kiufundi na uongozi katika sekta ya umma. |
| | *i. Kuandaa na kutekeleza mpango wa mafunzo jumuishi na mpango kazi wa kujenga uwezo.* |
| | 1.4 Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa uwazi wa ajira na uteuzi unaotegemea viwango vya ufaulu katika nafasi zote katika sekta ya umma. |
| | *i. Kuratibu sera, sheria, taratibu na miongozo ya uajiri iliyopo.* |
| | 1.5 Kubadilisha Sekretarieti ya Ajira kuwa taasisi huru kamili ya ajira ya umma. |
| | 1.6 Kuimarisha utayarishaji wa modeli za kiuchumi na maoteo ya mapato. |
| | *i. Kufanya mapitio ya modeli iliyopo ili kuendana na mahitaji ya maendeleo ya baadaye na ubora wa kimataifa.* |
| 2. Kufanikisha angalau asilimia 80 ya taasisi za umma zenye utendaji wa | 2.1 Kuanzisha tathmini ya mara kwa mara ya utendaji kwa watumishi kwa pande zote (360-degree) na mifumo ya mrejesho wa wakati halisi katika taasisi zote za umma. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| kiwango cha juu, kimaadili na uwajibikaji nchini kufikia Juni 2031. | *i. Kuandaa sera na miongozo ya tathmini za pande zote (360-degree) na mrejesho wa wakati halisi.* |
| | *ii. Kufanya mapitio, kuanzisha na kuunganisha zana na majukwaa ya kidijitali kwa ajili ya kusimamia tathmini za utendaji na mrejesho wa wakati halisi.* |
| 3. Kuimarishwa kwa kiwango cha kuridhika na huduma kutoka asilimia 45 (2024) hadi 70 kufikia Juni 2031. | 3.1 Kuweka mikataba ya kupima utendaji wa maafisa waandamizi wa umma. |
| | 3.2 Kukuza maendeleo endelevu ya kitaaluma na kuimarisha mafunzo ya maadili. |
| | 3.3 Kuimarisha ugatuzi wa kifedha ili kuboresha utoaji wa huduma za umma. |
| **Lengo 3:** Kuimarishwa kwa uadilifu na uaminifu wa taasisi zinazosimamia mahusiano na mausala ya wananchi. | |
| 1. Kuimarika kwa fahirisi ya utawala wa sheria *(Rule of Law Index)* kufikia -0.20 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuimarisha ushirikiano na wadau wa kikanda na kimataifa kwa ajili ya kubadilishana maarifa kuhusu mifumo ya kisheria. |
| 2. Kuimarika kwa fahirisi ya kiwango cha uaminifu wa umma kutoka asilimia 52 (2024) hadi 75 kufikia Juni 2031 | 2.1 Kuimarisha taasisi za usimamizi (CAG, PCCB, Kamati za Bunge). |
| | 2.2 Kutekeleza mifumo ya uwazi ya ajira na upandishaji vyeo. |
| | 2.3 Kuimarisha majadiliano ya kitaifa juu ya mageuzi ya utawala. |
| **3.2. Kuimarisha ufanisi na uimara wa Mamlaka na Tawala wa Mitaa** | |
| **Lengo 1:** Uwepo wa Utawala wa Mitaa Imara na wenye Ufanisi. | |
| 1. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimefikia uhuru wa uendeshaji wa asilimia 100 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuimarisha Sera ya Kitaifa ya Ugatuzi na Mfumo wa Kisheria. |
| | 1.2 Kuanzisha majukwaa ya kidigitali ya utoaji wa huduma katika ngazi za mitaa pamoja na mifumo ya mrejesho wa wananchi. |
| | 1.3 Kubuni na kuendeleza majukwaa ya kidigitali ya utoaji wa huduma na mifumo ya mrejesho wa wananchi. |
| | 1.4 Kusambaza, kuanza kutumia na kuyaendesha majukwaa na mifumo husika. |
| | 1.5 Kuandaa na kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na kujifunza (MEL), ili kufikia kiwango cha uhuru wa uendeshaji kwa asilimia iliyokusudiwa. |
| | 1.6 Kuimarisha mifumo ya uhamishaji wa fedha kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa (*Intergovernmental Fiscal Transfers)*. |
| | 1.7 Kuongeza na kuimarisha vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs). |
| | 1.8 Kuimarisha usimamizi wa fedha, uwajibikaji na uwazi. |
| | 1.9 Kukuza Maendeleo ya Uchumi wa Mitaa *(Local Economic Development – LED)* kama kichocheo cha mapato. |
| 2. Kufanya maboresho ya Miundo ya kiutawala ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) na usimamizi wa Serikali Kuu kwa asilimia 100 kufikia Juni 2031. | 2.1 Kupitia muundo wa Tawala zasa Mkoa na Serikali za Mitaa ili kutekeleza kwa ufanisi uratibu wa sera, msaada wa kiufundi na ufuatiliaji wa utendaji ili kuimarisha ugatuzi wa Utawala na uhuru wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. |
| | *i. Kulinganisha, kuoanisha na kuboresha miundo ya kisheria na kitaasisi ya ugatuzi.* |
| | *ii. Kubuni, kuandaa na kuasili matumizi ya zana za kidigitali na majukwaa kwa ajili ya uratibu, uwazi, uwajibikaji na utekelezaji mzuri wa majukumu.* |
| | *iii. Kuoanisha majukumu na kazi za uongozi wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha ushirikiano katika kutoa huduma za umma kwa ufanisi na uwajibikaji.* |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| 3. Kuajiri wa Wakurugenzi wa Halmashauri na watumishi wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia viwango mbalimbali vya uwezo kufikia Juni 2031. | 3.1 Kuweka mfumo wa uajiri wenye ushindani, uwazi na mahsusi kwa ajili ya uongozi wa watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. |
| | *i. Kuandaa miongozo ya viwango vya kuajiri na muundo wa viwango vya umahiri kwa viongozi watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.* |
| | *ii. Kubuni, kuendeleza na kuanzisha mfumo wa kidijitali kwa ajili ya kuajiri na watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.* |
| | *iii. Kuandaa Mfumo wa Kitaifa wa Stadi na Umahiri kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.* |
| | *iv. Kutekeleza mikataba ya utendaji na tathmini ya mwaka kwa wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.* |
| | 3.2 Kushirikisha Vyuo Vikuu pamoja na Taasisi za elimu ya Juu na Tafiti kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ndani. |
| | *i. Kufanya utafiti wa kina ili kubainisha Mahitaji ya ushirikiano.* |
| | *ii. Kuanzisha na kutekeleza mikakati* ya utekelezaji *kwa ajili ya kushirikiana.* |
| | *iii. Kujenga uwezo wa Kitaasisi na Uongozi wa wataalamu wa Serikali za Mitaa.* |
| | 3.3 Kuboresha miongozo ya kiutendaji ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ili kuwianisha viwango vya watumishi na majukumu kuendana na majukumu ya utoaji huduma yaliyogatuliwa. |
| | *i. Kuwianisha hali ya watumishi na majukumu ya watumishi wa umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs).* |
| | *ii. Kuboresha miongozo ya kiutendaji kwa kuzingatia viwango vya watumishi na majukumu.* |
| 4. Kufikiwa asilimia 80 ya ushiriki wa wananchi na uwajibikaji wa jamii kwenye Mamlaka za Serikali za Mtaa ifikapo Juni 2030. | 4.1 Kufanya mapitio ya kisera na kutekelezwa jukumu la kisheria la ushirikishwaji wa kata na vijiji katika kupanga na kuandaa bajeti. |
| | *i. Kufanya Mapitio ya kina ya miundo, miongozo ya Kisheria na mikakati ya utekelezaji iliyopo*. |
| | 4.2 Kuweka mifumo na nyenzo za kuwezesha jamii kufanya tathmini kufikia angalau asilimia 60 ya mamlaka za Serikali za Mitaa ifikapo 2028 na asilimia 100. |
| | *i. Kusanifu na kuweka mifumo na nyezo za kuwezesha jamii kufanya tathmini.* |
| | 4.3 kuanzishwa kwa mifumo ya Kidigitali ya Kurudisha majibu kwa wananchi (ujumbe mfupi, tovuti, programu tumishi ya simu) kwa ajili ya ufuatiliaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote nchini. |
| | *i. Kutoa mafunzo na kuwezesha Taasisi za Serikali za ndani, mabaraza, kamati za maendeleo za kata, halmashauri za vijiji na Asasi za kiraia ili kuwezesha ushiriki wa wananchi na kupata mrejesho.* |
| | 4.4 kuimarishwa kwa mabaraza na kamati za maendeleo za kata na viji kama majukwaa ya utoaji huduma na ubunifu kutoka ngazi za chini. |
| | *i. Kuandaa na kuanzisha jukwaa na programu ya usimamizi wa mageuzi ya ubunifu katika ngazi za chini.* |
| **Lengo 2: Kuboreshwa kwa Mifumo ya Kifedha na Utawala iliyogatuliwa** | |
| 1. Kuongezeka kwa mchango wa mapato ya ndani ya | 1.1 kutoa wigo mpana wa mamlaka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha/kusimamia kodi za ndani. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka asilimia 12 (2024) hadi asilimia 25 ifikapo Juni 2031 | 1.2 Kuanzisha mifumo ya uhamishaji fedha ndani ya mamlaka za Serikali kulingana na utendaji kazi. |
| | 1.3 Kuimarisha uratibu kati ya Tume ya Taifa ya Mipango (NPC), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (PO-RALG), na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs). |
| **Lengo 3: Kuchochea Uwajibikaji na uwazi katika mamlaka za Serikali za Mitaa** | |
| 1. Kuboreshwa kwa kiwango cha kuridhika kwa wananchi na huduma za mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka asilimia 40 (2024) hadi asilimia 65 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuanzisha na kutekeleza majukwaa shirikishi ya kibajeti na mipango. |
| | 1.2 Kuweka mifumo ya kidigitali ya utoaji taarifa za fedha na huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs). |
| | 1.3 Kuanzisha kamati huru za ukaguzi wa mahesabu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs). |
| **Lengo 4: Kuboreshwa kwa uhimilivu wa kitaasisi na kifedha LGAs** | |
| 1. Kuboreshwa kwa mikutano ya mamlaka za Serikali za Mitaa ya utolewaji wa misingi ya utoaji huduma kutoka asilimia 45 (2024) hadi asilimia 75 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuunda mifuko ya maendeleo ya ndani kwa ajili ya sekta muhimu. |
| | 1.2 Kujenga uwezo wa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) katika usimamizi wa miradi na mipango. |
| | 1.3 Kukuza ushirikiano kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), sekta binafsi, na mashirika ya kiraia (CSOs). |
| **3.3. Kuimarisha Matumizi ya Kidigitali na Takwimu Sahihi** | |
| **Lengo 1:** Kuanzishwa kwa Mfumo Salama, Unaotegemea Takwimu na Utawala wa kidigitali ifikapo mwaka 2050. | |
| 1. Kufanya Asilimia 50 ya huduma za Serikali kuwa za kidigitali ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuimarisha sera, miongozo ya kisheria na kitaasisi ili kuimarisha utawala wa kidigitali. |
| | *i. Kufanya mapitio na kuunganisha sera na sheria zinazohusiana na utawala wa kidigitali.* |
| | *ii. Kufanya mapitio na kuanzisha vigezo na miongozo ya uunganishaji wa mifumo na usimamizi wa Takwimu.* |
| | 1.2 Kuhuisha, kuanzisha na kuiimarisha miundombinu inayohusiana na Tehama. |
| | *i. Kuboresha miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za Serikali.* |
| | 1.3 Kuboresha usanifu na taratibu za huduma za tehema. |
| | *i. Kurahisisha na kuunganisha huduma ili kupunguza urasimu.* |
| 2. Kuhakikisha angalau asilimia 90 ya idadi ya watu wanapata kitambulisho cha kidigitali na huduma za kielektroniki ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kuandaa zana na jukwaa salama ya huduma ya kielektroniki. |
| | *i. Kuanzishwa kwa majukwaa rafiki kwa mtumiaji yenye mifumo ya vitambulisho vya kidigitali.* |
| | 2.2 Kuanzisha na kutekeleza programu za kujenga uelewa wa kidigitali. |
| | *i. Kuanzisha na kutekeleza programu na majukwaa ya ushirikiano ili kuunganisha na kuratibu taasisi za umma, asasi za kiraia na sekta binafsi.* |
| 3. Utekelezaji kamili wa mifumo mahiri ya data katika sekta zote kuimarishwa ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kupitisha Sera ya *Open Data.* |
| | *i. Kupitisha na kutekeleza Sera ya open data katika sekta zote.* |
| | *ii. Kuimarisha na kuunganisha mifumo ya data mahiri (smart data systems) ili kuongeza upatikanaji na uaminifu wa huduma pamoja na ubadilishanaji wa taarifa.* |
| 4. Kuhakikisha Fahirisi ya Kitaifa ya Ustahimilivu wa | 4.1 Kuimarisha Sera ya Kitaifa ya Usalama wa Mtandao na mifumo ya kisheria. |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| Usalama wa Mtandao inaendelea kuwa katika kiwango "Imara" ifikapo Juni 2031. | *i. Kufanya mapitio sera na sheria za uhalifu wa mtandao, ulinzi wa data na faragha.* |
| | *ii. Kuandaa miongozo ya uzingatiaji na utekelezaji wa usalama wa mtandao pamoja na mifumo ya uthibitishaji (certification frameworks).* |
| | 4.2 Kuimarisha miundombinu na uwezo wa kiufundi kwa ajili ya kugundua, kuzuia na kukabiliana tishio la Kimtandao. |
| | i. Kuimarisha Timu za Kidigitali za Kukabiliana na Dharura za Mtandaoni (TZ-CERT) Kitaifa na kisekta (sector-specific CERTs). |
| | i. Kuimarisha Kituo cha Kitaifa cha Uendeshaji wa Usalama wa Mtandaoni. |
| | 4.3 Kuboresha uratibu wa kitaasisi na utawala wa kuimarisha masuala ya usalama wa mtandaoni. |
| | i. Kufanya mapitio ya sera na kuimarisha ya sera, miongozo ya kisheria na kitaasisi. |
| | ii. Kufanya ukaguzi wa mifumo wa mara kwa mara. |
| | 4.4 Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa. |
| | i. Kuwianisha sera na miongozo ya kisheria za kitaifa kuendana na mikataba na miongozo ya kikanda na kimataifa kuhusu usalama mtandaoni. |
| | ii. Kufanya mapitio na kutekeleza itifaki za mwitikio wa usalama wa mtandao za pande mbili na za kimataifa . |
| | iii. Kushirikiana katika mikakati ya pamoja ya utafiti na uvumbuzi na washirika wa kikanda na kimataifa. |
| | 4.5 Kuimarisha ushirikiano na taasisi za kibiashara, asasi za kijamii na umma. |
| | i. Kusaidia uwekezaji wa sekta ya umma na binafsi katika kutafuta suluhisho za ndani la usalama wa mtandaoni. |
| | i. Kuandaa na kutekeleza nyenzo na majukwaa ya kidigitali ya wadau mbalimbali kwa ajili ya kubadilishana taarifa. |
| **Lengo 2:** Upatikanaji wa huduma za kidigitali kwa wote | |
| 1. Kuongeza upatikanaji wa intaneti kutoka asilimia 79.3 (mwaka 2024) hadi asilimia 98 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuongeza wigo wa miundombinu ya intaneti katika maeneo ya vijijini. |
| | 1.2 Kutoa ruzuku kwa vifaa vya kidijitali kuwezesha bei kuwa nafuu. |
| | 1.3 Kuzindua kampeni za kitaifa za kujenga uelewa wa masuala ya kidijitali. |
| **Lengo 3:** Kuboreshwa kwa Miongozo ya Kitaasisi na mifumo ya Tehama | |
| 1. Kuongezeka kwa Mifumo inayosomana katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MDAs/LGAs) kutoka asilimia 20 (mwaka 2024) hadi asilimia 80 ifikapo Juni 2031 | 1.1 Kuandaa Miongozo wa Kitaifa wa kuunganisha mifumo. |
| | 1.2 Kuunganisha majukwaa ya Tehama yaliyopo. |
| | 1.3 Kuimarisha miongozo ya usalama na faragha ya Taarifa. |
| **Lengo 4:** Uboreshaji wa Huduma za Jamii Kidigitali | |
| 1. Kuongezeka kwa huduma muhimu zinazotolewa mtandaoni kutoka asilimia 35 (mwaka 2024) hadi asilimia 85 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuweka huduma zenye mahitaji makubwa (kodi, leseni, afya, elimu) kuwa za kidigitali. |
| | 1.2 Kuanzisha majukwaa ya ushirikishwaji wa kidigitali. |
| | 1.3 Kuanzishwa kwa mifumo ya ufuatiliaji wa kielektroniki wa utoaji huduma. |
| **Lengo 5:** Kujengwa Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu ili kujenga Uhimilivu | |
| 1. Kuongezeka kwa Sera zinazotumia uchambuzi wa | 1.1 Kuanzisha Kituo cha taarifa cha Taifa chenye uwezo wa kufanya uchambuzi wa takwimu kubwa (*big data analytics*). |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| Taarifa za muda halisi kutoka asilimia 15 (mwaka 2024) hadi asilimia 70 ifikapo Juni 2031. | 1.2 Kukuza mikakati ya upatikanaji wa taarifa kwa uwazi. |
| | 1.3 Kutoa mafunzo kwa watumishi katika uchambuzi wa taarifa na uandaaji wa sera unaozingatia takwimu. |
| **3.4. Kukuza Mageuzi ya Mtazamo ili Kuimarisha Mageuzi** | |
| **Lengo 1:** Kuimarishwa kwa utekelezaji, uratibu na ufuatiliaji thabiti wa mageuzi muhimu ya kimuundo yaliyoainishwa katika Mpango wa maendeleo wa muda mrefu wa 2050 (LTPP 2050) ili kuchochea mageuzi endelevu. | |
| 1. Kuboreshwa na kuanza kutumika kwa utawala wa kitaasisi kwa angalau asilimia 70 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuimarisha Kitengo cha mageuzi ya hali ya Juu kilichopo Ofisi ya Rais ili kuratibu na kufuatilia mageuzi katika sekta mbalimbali. |
| | i. Kufanya mapitio ya mifumo ya sasa ya vitengo ili iendane na mahitaji ya maendeleo ya baadaye. |
| | 1.2 Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa utekelezaji wa mageuzi, mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na uwajibikaji unaozingatia matokeo, pamoja na mfumo wa viashiria vya kimkakati vya utendaji kazi ili kutekeleza kwa ufanisi 4Rs. |
| | *i. Kuanzisha na kutekeleza mkakati wa usimamizi wa mabadiliko na mawasiliano ili kuwaunganisha wadau katika ngazi zote za jamii.* |
| | *ii. Kuanzisha na kuunganisha viashiria vya kimkakati vya utendaji kazi vya kimkakati kuwa nguzo kuu ya mageuzi.* |
| | *iii. Kufanya mapitio ya utendaji kazi ya mara kwa mara ili kuhakikisha uwajibikaji na usimamizi thabiti wa 4Rs.* |
| | *iv. Kuanzisha Taasisi Jumuishi ya Kitaifa au kikosi kazi cha kusimamia mageuzi ili kuongoza utekelezaji wa mageuzi yanayohusiana na 4Rs.* |
| | *v. Kujenga Uwezo wa Wizara, Idara na Taasisi kwa kutoa mafunzo maalumu na usaidizi wa kiufundi ili kuwianisha mikakati ya kitaasisi na vipaumbele vya LTPP 2050.* |
| 2. Kuanzishwa na kufanyiwa majaribio kwa mfumo wa kidigitali wa ufuatiliaji na tathmini kwa angalau asilimia 30 ya Wizara na Idara Zinazojitegemea ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kusanifu na kuanzisha jukwaa la kitaifa la kidjgitali la RBMEA&L ili kufuatilia matokeo ya mageuzi. |
| | *i. Kufanya tathmini ya mahitaji na mashauriano ya watumiaji katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali zote.* |
| **Lengo 2:** Kuchochea mageuzi ya mitazamo ya kitaifa kwa kuhusisha maadili ya ujasiriamali, uwazi, uvumbuzi, usawa na ushirikishwaji wa kiraia kupitia majukwaa jumuishi. | |
| 1. Kurasimisha dhamira ya uongozi katika utekelezaji wa mageuzi na kuhakikisha utoaji wa huduma bora katika kila sekta ifikapo Juni 2028 | 1.1 Kuandaa majukwaa ya uongozi wa ngazi ya juu, programu na mafunzo maalumu ya kutoa mwelekeo kuhusu maadili ya uongozi. |
| | i. *Kuanzisha na kutekeleza mwongozo wa kitaifa wa maadili ya uongozi ulioundwa kwa ushirikiano wa viongozi wa umma, sekta binafsi na asasi za kiraia ili kuongoza maendeleo ya uongozi.* |
| | 1.2 Kuimarisha vitengo/sehemu za utafiti na uvumbuzi ili kuratibu na kuharakisha mikakati ya mageuzi. |
| | *i. Kuanzisha na kutekeleza programu za kujenga uwezo ili kuongeza ujuzi katika utafiti, uvumbuzi na usimamizi wa mageuzi katika Wizara, Idara na Taasisi (MDAs) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) zote.* |

| Shabaha | Afua |
| --- | --- |
| | *ii. Kuchochea programu za kubadilishana maarifa na taasisi za utafiti na uvumbuzi za ndani, kikanda na kimataifa.* |
| | 1.3 Kutoa mafunzo kwa viongozi wa dini, kimila na mitaa ili waweze kujenga hoja za mageuzi ya mtazamo, wakitumia jumbe zinazokubalika na tamaduni husika. |
| | 1.4 Kuanzisha na kuendesha vyuo vya uongozi vya kitaifa na kikanda, klabu na ushirika kwa ajili ya kuimarisha uongozi katika sekta mbalimbali. |
| | *i. Kuimarisha, kuanzisha na kuendesha Taasisi ya Taifa ya Uongozi kwa ajili ya kuimarisha viongozi wa umma na binafsi.* |
| | 1.5 Kuimarisha programu za usimamizi wa urithishaji wa uongozi kwa ajili ya uendelevu wa utoaji huduma. |
| | i. *Kufanya utambuzi wa vipaji vya kisekta ili kubainisha viongozi watarajiwa wa baadaye.* |
| | 1.6 Kuandaa na kutekeleza programu maalumu za mafunzo kwa viongozi. |
| | *i. Kuandaa miongozo, nyenzo na majukwaa ya kutoa mafunzo na ushauri kwa uongozi katika sekta zote.* |
| | *ii. Kuunganisha watendaji waandamizi na wataalamu wa kati kwa ajili ya ukuzaji wa uongozi.* |
| | 1.7 Kuanzisha na kutekeleza programu za kubadilishana maarifa baina ya viongozi wa rika moja (peer-to-peer) kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa viongozi. |
| | *i. Kuanzisha majukwaa ya ngazi za juu kwa viongozi ili kubadilishana mbinu bora za utawala na uzoefu.* |
| | *ii. Kuandaa na kutekeleza mwongozo wa mafunzo kwa uongozi na ubadilishanaji wa maarifa baina ya sekta mbalimbali.* |
| | 1.8 Kuandaa programu ya uibuaji vipaji vya vijana katika sekta mbalimbali na uimaarishaji uongozi kwa kuzingatia mahitaji ya maendeleo ya baadaye. |
| | i. Kuanzisha programu maalumu za mafunzo kwa viongozi waandamizi na viongozi wapya katika sekta mbalimbali |
| | 1.9 Kuimarisha mikakati ya utekelezaji wa maadili na uadilifu katika sekta mbalimbali |
| | i. Kufanya mapitio na kuimarisha miongozo ya lazima ya tamko la mali kwa viongozi wa ngazi ya juu na waandamizi |
| | ii. Kuendesha majukwaa ya maadili ya kila mara kwa kuhusisha wananchi ili kujenga uaminifu na kukubalika kwa uongozi |
| | iii. Kufanya utambuzi wa vinara wa uadilifu katika uongozi na utoaji huduma |
| | 1.10 Kuandaa na kutekeleza mifumo ya mawasiliano ya mageuzi ya mtazamo, tabia na mienendo ili kuimarisha mbinu za uongozi katika sekta mbalimbali |
| | i. Kuanzisha na kuendesha kampeni za kiwango cha juu za kisekta zinazokuza kaulimbiu ya "Huduma Kwanza Katika Uongozi" |
| | ii. Kuwezesha viongozi katika sekta mbalimbali ili wawe mfano wa kuigwa katika kutumia mbinu bora za uongozi |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| | 1.11 Kuchochea mageuzi ya kitamaduni ili kuimarisha mitazamo, tabia na mienendo |
| | i. Kuunganisha kanuni za maadili ya uongozi na maadili ya kijamii kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya maendeleo ya baadaye |
| | ii. Kufanya utoaji wa huduma kwa jamii kuwa kanuni kuu ya uteuzi na upandishaji vyeo kwa viongozi |
| | ii. Kuweka mifumo ya kutoa mrejesho kwa wananchi ambapo viongozi wanakubali maadili na kuchukua hatua kulingana na maoni ya wananchi |
| 1. kubadilishwa kwa Utamaduni wa utawala na mtazamo wa sekta ya umma ifikapo Juni 2031. | 2.1 Kufanya mapitio na kufuta sheria na miongozo iliyopitwa na wakati kwa utumishi wa umma ili kuondoa majukumu yanayolenga udhibiti |
| | i. Kufanya ukaguzi wa miongozo ya kisera na kisheria katika huduma za kijamii |
| 3. Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi kupitia majukwaa ya majadiliano ya mara kwa mara na kuanzishwa kwa mikakati ya ushirikiano wa kisera ifikapo Juni 2031. | 3.1 Kuimarisha majukwaa ya kitaasisi ya Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika ngazi ya kitaifa na kisekta |
| | i. Kufanya mapitio ya kiutendaji ya majukwaa yaliyopo ya Midahalo kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| | 3.2 Kuanzisha kituo cha mafunzo ya utawala wa masoko kwa watumishi wa umma |
| | Kusanifu na kuandaa miongozo na mitaala ya mafunzo ya utawala wa masoko kwa kushirikiana na wataatalmu kutoka taasisi za elimu, sekta binafsi na wataalamu wa kimataifa |
| 4. Kuimarishwa kwa Ushiriki na uwajibikaji wananchi ifikapo Juni 2031. | 4.1 Kuzingatia masuala ya ujasiriamali, uelewa wa kidijitali, usawa wa kijinsia, na uwajibikaji wa kiraia katika mitaala ya elimu ya kitaifa kutoka ngazi ya elimu ya msingi hadi elimu ya juu |
| | i. Kufanya mapitio ya mitaala iliyopo ili kuingiza na kuzingatia masuala ya ujasiriamali, uvumbuzi, uelewa wa kidijitali, usawa wa kijinsia, na uwajibikaji wa jamii katika masomo na ngazi zote |
| | 4.2 Kuandaliwa kwa majukwaa ya ndani kwa ajili ya kupata mrejesho wa bajeti na masuala ya kiutawala |
| | i. Kuanzishwa kwa Majukwaa ya Mipango Shirikishi kufikia angalau asilimia 70 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) |
| | 4.3 Kukuza programu za kijamii za uvumbuzi zinazowalenga vijana |
| | i. Kuanzisha angalau kituo kimoja cha uvumbuzi cha vijana katika kila kanda ambapo vijana wanaweza kushirikiana kutafuta suluhisho kwa changamoto za eneo husika |
| | 4.4 Kuanzisha tuzo za kitaifa za uzalendo ili kukuza umuhimu wa uzalendo na uwajibikaji kwa wananchi |
| | Kuandaa programu yenye vigezo na muundo wa tuzo kwa ajili ya Tuzo za kitaifa za Uzalendo kwa taifa |
| **Lengo 3:** Kuimarishwa kwa uadilifu, tija na uwajibikaji | |
| 1. Kuboresha kiwango cha farihisi ya maadili ya kitaifa kutoka asilimia 50 hadi asilimia 75 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuanzishwa kwa kampeni za elimu ya uraia ifikapo Juni 2028. |
| | 1.2 Kukuza majukwaa ya majadiliano baina ya Serikali, sekta binafsi, na Asasi za kiraia kila mwaka. |
| | 1.3 Kutoa motisha kwa watu maarufu wa kuigwa na waadilifu ifikapo Juni 2031. |
| **Lengo 4:** Kuboresha mifumo ya elimu na uongozi | |
| 1. Kuongeza mitaala inayozingatia | 1.1 Kufanya mapitio ya mitaala ili kuzingatia masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM), maadili na ubunifu |

| Shabaha | Afua |
|---|---|
| uvumbuzi/maendeleo ya viwanda kutoka asilimia 30 hadi asilimia 70 ifikapo Juni 2031. | 1.2 Kuanzisha vyuo vya uongozi na programu za kujenga uwezo |
| | 1.3 Kushirikiana na sekta binafsi kutoa mafunzo kwa vitendo na uanagenzi |
| **Lengo 5:** Kuboresha Taasisi za Umma kwa kuzingatia wananchi na matokeo | |
| 1. Kuboresha farihisi ya ufanisi wa utoaji wa huduma za Umma kutoka asilimia 48 (2024) hadi 72 ifikapo juni 2031 | 1.1 Kuanzisha hati za huduma kwa raia na kadi za alama za kupima utendaji |
| | 1.2 Kutumia mifumo ya usimamizi wa utendaji unaozingatia matokeo |
| | 1.3 Kuimarisha mikakati ya kutoa taarifa za kupinga rushwa |
| **Lengo 6:** Kujengwa kwa utamaduni wa uhimilivu wa uvumbuzi na kuendana na mazingira | |
| 1. Kuongezeka kwa Kiwango cha uvumbuzi baina ya taasisi kutoka asilimia 25 (mwaka 2024) hadi asilimia 60 ifikapo Juni 2031. | 1.1 Kuanzisha vituo vya uvumbuzi na ukuzaji vipaji |
| | 1.2 Kuimarisha kampeni za kitaifa kuhusu matumizi ya teknolojia na uongezaji tija |
| | 1.3 Kuweka mifumo ya ufundishaji ya muda mrefu na ya uendelezaji utaalamu |

TUME YA TAIFA YA MIPANGO

NPC

Ustawi wa Pamoja